YA PADRI NA MUTAWA
SOFRONIOS MIKAILIDIS

# ORTHODOKSIA
## NA WASHUHUDA YA YEHOVA

CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE
KOLWEZI KONGO
2000

# YALIYOMO

**UTANGULIZI YA MUANDISHI**
**HADISI KIFUPI YA KUNDI YA WASHUHUDA YA YEHOVA**
**MA SHINA YA IMANI WA KRISTU**
**KANISA-MAPOKEO KIMUNGU-MADIKO TAKATIFU**
**KANISA**
**MAPOKEO KIMUNGU**
**MADIKO TAKATIFU**
**UFANANISHO YA AGANO LA KALE NA JIPYA**
**MUNGU WA MA USO TATU**
**MASHUHUDA TOKA AGANO LA KALE JUU YA UTATU MUTAKATIFU**
**AGANO JIPYA: UFUNUO MUZIMA YA UTATU MUTAKATIFU**
**MAFUNDISHO-BUNDUKI YA WASHUHUDA YA YEHOVA KUPINGANA YA UTATU MUTAKATIFU**
**«JINA» WA MUNGU**
**MUNGU ANALAZIMISHWA JINA?**
**MA «JINA» YA MUNGU NI MENGI**
**JINA WA KWELI NI YAKHVE NA HAPANA YEHOVA**
**KWA AJILI YA «JINA» WANAKATAA KAZI YA KRISTU**
**JINA YA YEHOVA HAKUNA NDANI YA AGANO JIPYA**
**JINA MUPYA YA MUNGU MU AGANO JIPYA**
**WASHUHUDA YA KRISTU, «WAKRISTU» NA HAPANA «WASHUHUDA YA YEHOVA»**
**PAKA JINA YA YESU KRISTU INAOKOA**
**MITUME NA WATUMISHI WENGINE YA EVANGELION WALITOA YOYOTE NA UZIMA WAO, HAPANA KWA JINA YA «YEHOVA», LAKINI KWA JINA YA KRISTU**
**KUHUBIRI YA MITUME HAIKUKUWE KWA YEHOVA, LAKINI ILIKUWA KWA JINA YA BWANA WETU YESU KRISTU**
**MA SAUTI KUPIGANA YA WASHUHUDA YA YEHOVA**
**YAKHVE NI MUNGU WA UTATU MUTAKATIFU**
**UMUNGU WA KRISTU**
**KRISTU NI MUNGU MUKAMILIFU NA MUTU MUKAMILIFU**
**KRISTU NI MUNGU WA MILELE BILA MWANZO NA MUUMBA YA ULIMWENGU**
**MWANA NI ASIYE MWANZO, WA MILELE NA ASIYE UHARIBIFU, SAWA MUNGU-BABA**
**KRISTU NI MUNGU WA KWELI**
**KRISTU NI SAWA-SAWA NA MUNGU-BABA**
**KRISTU NI WA ASILI MOJA NA MUNGU-BABA**
**KRISTU NI KWELI KAMILI, UZIMA NA NURU**
**KRISTU ANAJUA ROHO YA MTU, NI PA FASI YOTE, NI «MTAKATIFU» NA «MWENYE HAKI»**
**KRISTU NI MUNGU MUKAMILIFU NA MUTU MUKAMILIFU**
**ROHO MUTAKATIFU NI ROHO NA WA BABA NA WA MWANA**
**KRISTU NI MUNGU YAKHVE YA AGANO LA KALE**
**TUNAMWABUDU KRISTU SAWA VILE TUNAMWABUDU BABA**
**MASHUHUDA YA WASHUHUDA YA YEHOVA KUPIGANA HALI KIMUNGU YA KRISTU**
**ROHO MUTAKAITFU NI MUNGU WA KWELI**

**ROHO MUTAKATIFU NI USO WA KWELI, KWA SABABU ANA MAFANANISHO YOTE YA USO MOJA NA WA AKILI**
**ROHO MUTAKATIFU NI MUNGU WA KWELI**
**ROHO MUTAKATIFU NI MUNGU-YAKHVE YA AGANO LA KALE**
**MUNGU NI MA FASI YOTE YA DUNIA**
**UFUFUO WA KRISTU KATIKA MWILI MWAKE**
**MADIKO TAKATIFU INAANDIKA JUU YA UFUFUO WA KRISTU**
**MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA YA YEHOVA KUPINGANA UFUFUO YA KRISTU KATIKA MWILI MWAKE**
**K A N I S A**
**MAFANANISHO YA KANISA YA KRISTU**
**MA FUMBO TAKATIFU YA KANISA**
**UBATIZO**
**UBATIZO MU KIPIMO KIDOGO**
**UPADIRISHO**
**JINA YA: «BABA (PADRI»**
**MAMBO YA MALIPO YA WAPADRI YA KANISA YETU**
**EUKARISTIA KIMUNGU (KOMUNYO TAKATIFU)**
**MATENDO YENYE YATAKUJA - YA KUJA WA MBILI YA KRISTU DUNIANI- «UFALME WA MIAKA ELFU»**
**NAMNA GANI WALIFIKA MU MWAKA 1914?**
**YA KUJA KRISTU MARA YA MBILI- MWISHO YA DUNIA-UHUKUMU WA MWISHO-MWANZO YA UZIMA WA MILELE WANASHARIKIWA KATIKA WAKATI MOJA**
**NI NANI UFALME WA MIAKA ELFU (1000)**
**UFUNUO, SEHEMU 20**
**UFALME WA MUNGU ILIKUJA TANGU HILE WAKATI ALIKUJA KRISTU DUNIANI**
**KRISTU ALIKUWA MUFALME TANGU HILE WAKATI ALIISHI**
**«KWA KUFUNGWA» SHETANI ILIKUWA TANGU HILE WAKATI ALIISHI KRISTU DUNIANI**
**UFALME WA MUNGU NI UMOJA**
**UFALME WA MUNGU NI WA MBINGU**
**UFALME WA MUNGU NI WA ROHO NA HAPANA WA MWILI**
**UHARIBIFU YA INCHI NA MBINGU**
**MA NENO YA WAKATI**
**ISIYO KUFA YA NAFSI**
**MAANA YA NENO «NAFSI»**
**NAFSI UBINADAMU NI ISIYO KUFA**
**HADEZE NI FASI YA NAFSI YASIYOOKOLEWA NA KUSHUKA KULE KRISTU**
**«NAFSI» NA «ROHO» YANASHARIKIWA**
**MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA**
**UFUFUO YA WAFU WOTE**
**MADIKO TAKATIFU INAANDIKA JUU YA UFUFUO YA WAFU**
**MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA**
**UZIMA WA MILELE MU GEHENA**
**MADIKO TAKATIFU INASEMA NINI JUU YA GEHENA WA MILELE**
**MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA**
**MUZAZI-MUNGU MARIA**
**MADIKO TAKATIFU JUU YA MUTAKATIFU KAMILI MUZAZI-MUNGU**
**MA SHAIRI- MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA**

**WATAKATIFU YA KANISA YETU NA MAOMBEZI YAO**
**WATAKATIFU NI WATUMISHI WA KWELI YA MUNGU**
**MAOMBEZI YA WATAKATIFU**
**MIUJIZA YA WATAKATIFU**
**MA PICHA (IKONE) MATAKATIFU NA USUJUDU KATIKA SIFA YAO**
**USUJUDU HESHIMIWA YA MA IKONE (MA PICHA)**
**MIFUPA MATAKATIFU YA WATAKATIFU**
**MUSALABA MWESHIMIWA**
**FUNDISHO YA MAKUMBUSHO**
**JUU YA NVITA**
**UBADILISHO YA MADIKO TAKATIFU KU WASHUHUDA WA YEHOVA**

# UTANGULIZI YA MUANDISHI

Yesu Kristu, mwana wa Mungu na Mwokozi wa dunia, yeye eko Mungu wa kweli, alikuja na mwili wake duniani na alikufa kwa mapenzi yake pa Msalaba kusuudi atuokoe ku minyororo ya lufu na ku utumwa ya shetani. Ma siku dogo mbele ya lufu yake, alisema kwa wanafunzi wake hii sauti wa unabii: **«Angalieni musidanganyiwe na mutu.. . Na manabii wengi ya uwongo watasimama na kudanganya watu wengi.. . Na manabii ya uwongo wao, nao wataonyesha alama kubwa na maajabu wapate kudanganya kama ikiwezekana, hata wachaguliwa»** (Matayo 24, 4, 22 na 24). Lakini na Mtume Petro anajulisha wakristu ya kama **«manabii wa uwongo walisimama katikati ya watu, kama katikati yenu vilevile watakavyokuwa walimu wa uwongo watakaoingiza mafundisho ya imani ya uwongo kwa siri, wakikana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea wenyewe uharibifu usiokawia»** (Barua wa pili ya Petro 2, 1). Mtume Paulo alifunua ya kama walimu wa uwongo walionekana toka wakati ya Mitume (Matendo ya Mitume 20, 29-30) na, ya kama wataendelea kuonekana mpaka wakati wa mwisho ya dunia (barua wa kwanza ya Timotheo 4, 1). Mtume Yoano hawa walimu wa uwongo anawaita «wapinga Kristu» (Barua wa kwanza 2, 18) na anashauria waaminifu wasimame wenye nguvu kufatana fundisho ya Kristu na wakatale kutembea na kuzungumuza pamoja na wale «wapinga Kristu» (ona barua wa pili ya Yoano 10, 11).

Wakati hii tukona yo, pempeni ya mafundisho ingine wa uwongo na walimu wingi wa uwongo waliongezekwa na Washuhuda wa Yehova. Hawa ni kundi mbaya kuliko kundi ya uwongo ingine. Hii fitina ni jambo ya mafundisho yetu.

Fitina ya Washuhuda ya Yehova ilionekana ku mwisho ya milele wa mukongo, karibu mu mwaka 1870. Mkubwa na muumba ya hii kundi ya uwongo alikuwa mtu moja mwenye biashara toka inchi ya Ebrania, jina lake Karolo Roseli. Huyu alihubiri ya kama «alipokea neno kimungu ya kunyioloka toka kinywa ya Mungu»! Huyu mtu wa Ebrania na wanafunzi wake walipokelea mafundisho yoyote hile ilionekana katika milele yote na walifanya kundi-fitina moja mupya. Hii fitina ilipokea ndani yake mafundisho yote ya uwongo katika milele yote, tangu mwanzo ya Kanisa wa Kristu mpaka sasa. Washuhuda wa Yehova waliharabisha kabisa fundisho ya Dini ya Kristu na sasa hakuna fundisho hata moja katikati ya Kanisa ya Kristu na kundi ya wa Yehova. Na hawa Washuhuda wa Yehova wanafanya sawa vile walifanya **«Waandishi na Wafarisayo** zamani, **walizunguka bahari na inchi kufanya mutu mumoja kuwa mugeuzi; na akikwisha kufanyiwa, munamufanya kuwa mwana wa gehena mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe»** (Matayo 23, 15). Kwani weko na makuta mingi, wanazambalisha ma fasi yote vitabu na karatasi yao na wanakankamana kutandaza mafundisho ya uwongo wao na kwarabisha usingi ya Kanisa Orthodokse. Sawa vile anasema padri na mutawa moja, hawa Washuhuda wa Yehova wanahubiri hapana paka fundisho moja, lakini mafundisho ya wongo mingi pamoja. Kwa mfano wanakataa asili kimungu ya Bwana Yesu Kristu, wanakataa ya kama Roho Mtakatifu ni Mungu kweli, wanaamini ya kama nafsi ya watu inakufa pamoja na mwili; wanaamini ya kama Yesu Kristu atakuja wakati ya miaka elfu moja (1000) na ataweka pa inchi makutano kubwa ya wa patriarki wakubwa ya Agano la Kale, wanakataa ya kusujudu ma Picha (Ikone) ya Watakatifu na mafundisho ingine mengi.. . Ni kusema haina paka fundisho moja ya wongo, lakini mafundisho mingi pamoja.

Bwana Yesu Kristu anatufundisha tupate kusopoka mzuri mu uzima yetu kwa ajili ya walimu wa wongo: **«Angalieni kwa manabii ya uwongo wanaokuja kwenu wakivaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani wao ni imbwa wakali za mwitu»** (Matayo 7, 15). Kweli hawa watu wana fundisho wongo wanakuja na mavazi ya kondoo, lakini ya kweli wanarabisha ma nafsi ya waaminifu wetu, kama wataanguka ndani ya makila maovu wao. Basi, pasopo mingi! Musisuburie na hawa walimu wa wongo, kama hamujue muzuri Madiko Takatifu. Munapaswa

kuwa Mitume na Washuhuda wa Kristu.. . Tena sisi tunapashwa kuomba kwa Mungu awaangazie wapate kurudia ku fundisho ya kweli na tena sisi tunapaswa kuishi katika amri ya Bwana wetu Yesu Kristu, kwani Kwake ni utukufu «katika Kanisa» ( Wa Efeso 3, 21) kwa milele.

Mafundisho ya wongo yao ni mengi, lakini hapa sasa tutaandika kidogo:

-Wanafundisha ya kama juu ya kuokolewa mtu moja anapashwa kuita Mungu «Yehova».

-Wanakataa Utatu Mtakatifu (Baba, Mwana na Roho Mtakatifu) aliye Mungu moja kweli. Katika fundisho yao Mwana wa Mungu ni kiumbe ya Mungu (wanasema ya kama Huyu eko uso mumoja na malaika Mikaeli). Tena wanaamini ya kama Roho Mtakatifu haina Mungu, lakini ni paka nguvu moja ya Mungu isiyo na uso.

-Wanakataa Mapokeo Takatifu sawa chemchem ya Ufunuo Kimungu.

-Wanakataa ufufuo katika mwili ya Bwana Yesu Kristu.

-Wanakataa Kanisa na ma Fumbo yake yote.

-Wanakataa imani ya kama nafsi inabakia kwa milele.

-Wanafundisha ya kama Ufikisho wa Pili ilifanyika mu mwaka 1914 na Yesu Kristu atakuja na haraka pa inchi, juu ya kutengeneza Ufalme wake ya wakati miaka 1000.

-Wanafundisha ya kama Paradizo itakuwa pa inchi yetu na uzima wa milele itakuwa uzima kufurahi na bintu ya chakula pa hii ulimwengu.

-Wanakataa gehena wa milele na wanafundisha ya kama, hawa wasiyookolewa, watarudia ku sifuru (0).

-Wanakataa Bikira Maria Mzazi-Mungu na uzima ubikira wake.

-Wanakataa Watakatifu na maombezi yao.

-Wanakataa Msalaba Mweshimiwa na ma Picha ya Watakatifu wetu na ingine mafundisho ya wongo.

Kwa hivyo, waaminifu wote wetu wanaona, ya kama hawa walimu ya wongo waliharabisha ao walikataa mafundisho Dini ya Kristu. Kwa hivi hatari ni mnene kwa wale waaminifu imani yao ilishuka.

Tena mambo yao ingine ni hii: Zamani walisadiki fundisho ingine na wakati ingine wanabadilisha hii imani yao na wanasadiki fundisho ingine. Hawa wenyewe wanasema ya kama hii mambo inafanyika hivi kwani nuru inaonekana pole-pole mu akili yao. Wanaitika ya kama mwendo ya mafundisho yao haina ya kunyoloka.

Sisi tutakankamana na saidio ya Mungu kufunua mafundisho yao ya wongo kusudi ya kwanza kwa kusaidia waaminifu wetu waorthodoksi wabaki na imara pa imani Orthodokse, imani ya Mitume na Watakatifu wetu na ya pili kusudi kuangazie Mungu akili ya wale wakosefu kwa imani warudie imani ya kweli.

## HADISI KIFUPI YA KUNDI YA WASHUHUDA YA YEHOVA

Hadisi ya kundi ya Washuhuda ya Yehova inaanza mu mwaka 1870. Tangu hile mwaka mwenye wa ebrania mtu wa biashara, jina lake Karolo Roseli alianza kusanyika watu kwa somo na Madiko Takatifu.

Karolo Roseli alizaliwa mu 1852 mu muji Pichburg ya Pensilvania ya inchi Amerika. Tangu kipimo ya umri yake miaka 11 a; itumika pamoja na baba yake mu biashara na alikuwana maendeleo munene kwa ajili ya zawadi yake mu kazi ya biashara. Tangu kipimo ujana wake alianza kutumika na mafundisho ya Mungu, lakini alipotesha imani ya Mungu na aliweka yulu mu uzima yake paka neno ya akili yake. Ku mwanzo ya uzima yake alifata kundi ya «kanisa ya waProtestanti inaitwa Kongregasionali». Kisha miaka kidogo alisoma mafundisho ya Guiliam Miler, aliyekuwa muumba ya kundi ingine ya Waprotestanti na katika hii mafundisho ya bwana Miler, alifanya mafundisho yake. Tangu hile wakati alianza kusadiki ya kama huyu wa pekee ni

nabii kweli ya Mungu. Alipokelea mafundisho ya wongo wote tangu mwnazo ya Kanisa ya Kristu mpaka hile wakati na aliandika wakati gani itakuja mwisho ya hii dunia, wakati gani atakuja Yesu Kristu mara ya pili, wakati gani itaanza ufalme ya miaka 1000 ya Kristu pa hii inchi na ingine.. .

Mu mwaka 1872 Karolo Roseli aliumba kundi, jina lake «Wanafunji ya Madiko», ao na jina ingine: «Wafwasi ya alfajiri mapema ya wakati wa miaka 1000» na hii kundi tangu mwaka 1931 alibadilisha jina na inaitwa «Washuhuda ya Yehova». Mu mwaka 1881 aliumba kundi ingine jina lake Kundi Ulinzi (Skopia) na alisadiki ya kama hii kundi yake ni chemchem wa pekee wa Mungu na toka hii inapita duniani chakula ya roho kwa watu wote. Tangu mwezi ya saba ya mwaka 1879 alianza kuandika na kuzambalala kitabu-Reviste jina lake Ulinzi ao (Skopia). Hii kitabu inaendela andiko na kuzambalala yake mpaka leo. Tena huyu bwana Karolo aliandika na vitabu sita minene na jina yao: «Ma somo wa Madiko» (1886-1904).

Mu mwaka 1909 utawalo ya hii Kundi yao ilihamishwa toka Pensilvania mu muji Mbruklin ya Amerika, pahali inabaki mpaka sasa. Bwana Karolo Roseli alikufa mu mwaka 1916.

Mu utawalo ya hii Kundi alimufuata Yosefu Roderfod, mtu wa jivuno na katika kiburi, aliyezaliwa mu muji Misuri mu mwaka 1869. Huyu bwana Yosefu alibadilisha Kundi Ulinzi sawa Kundi moja na desturi ya Diktature ya roho. Mu mwaka 1919 pempeni na hii kitabu Skopia ao Ulinzi, aliandika na kitabu ingine jina lake «Milele wa zahabu» na kisha wakati kidogo ilibadilishwa jina lake na sasa inaitwa «Lamuka»(Amka) na hii kitabu inaendelea kujizambalala ma fasi yote ya dunia mpaka sasa.

Yosefu Roderford aliongeza na mafundisho yake ingine yulu ya hile ilikuwa zamani na aliendelesha kazi yake kwa kutangaza ma fundisho yake pa fasi yote. Mu mwaka 1931 aligeuza jina ya kundi yake Ulinzi (Skopia) na jina ingine mupya, hii: «Washuhuda ya Yehova». Tanfu hile mwaka wafwasi ya bwana Roderford wanaitwa Washuhuda ya Yehova, lakini wafwasi ya Karolo Roseli walichunga jina yao wa zamani, nikusema jina hii: «Wanafunji ya Madiko».

Bwana Roderford alikufa ku mwanzo ya mwaka 1942 na alimufuata bwana Nathan Nori na huyu alimufuata ku mwaka 1977 bwana Frideriko Fransi. Kisha lufu yake alimufuata bwana Milton Khenseli, na huyu sasa ni mutawalo ya hii Kundi.

Kila mutawalo aliongeza na mafundisho yake mapya. Lakini hule aliyeweka nguvu chapo yake pa hii Kundi alikuwa Yosefu Roderford. Katika wakati ya Nathan Nori maendeleo ya hii fitina ilitengenezwa kabisa muzuri na kwa ufungulio ya Masomo moja juu ya kufundishwa wale watu watatumika ndani ya hii Kundi.

Hawa wenye zamani waliitwa «Wanafunji ya Madiko» na sasa wanaitwa «Washuhuda ya Yehova», tangu ku mwaka 1922 walianza kufundisha juu ya ufalme wao wa wongo na wanakombana kufundisha watu wote ya dunia. Hawa Washuhuda ya Yehova weko walimu wa wongo wakubwa, kupita ya walimu wote tangu mwanzo ya Kanisa ya Kristu mpaka sasa.

# 1

# MA SHINA YA IMANI WA KRISTU

## KANISA-MAPOKEO KIMUNGU-MADIKO TAKATIFU

Kizungumuzo moja iko namna kufanya watu wa wili kama weko na usingiu moja. Kwa mfano, kwa kizungumuzo ya wakristu, usingi umoja juu ya kusimama na kutafuta mafundisho yote ni ma shina ya Imani wa Kristu. Hii Ma Shina inafai kuwa na mwanzo juu ya kupata hawa wanazungumuza yeyuko ya kila mambo yao.

Lakini, kama kizungumuzo inafai kujifanya pamoja na Washuhuda ya Yehova ao na wakubwa ya ma Fitina ingine ya Wa Protestani mambo ni munene, kwa sababu hawa walimu wa wongo wanasuburia paka na Kitabu ya Madiko Takatifu na wanakataa Mapokeo Kimungu. Lakini Madiko Takatifu haina paka hii wa pekee. Tunaweza kuisoma paka katika nuru ya Mapokeo Takatifu.

Kwa hivyo na sisi tunalazimishwa ndani ya hii Kitabu kutumia sawa usingi paka na Madiko Takatifu na tunasadiki ya kama, hata huu Kitabu wa pekee, Madiko Takatifu, bila Mapokeo Takatifu itaweza kujibu ku mbele ya mafundisho ya wongo ya Washuhuda ya Yehova.

Kwa kuendelea tutajibu juu ya nini Madiko Takatifu haiweze hii wenyewe kuwa shina ya Imani wa Kristu na juu ya nini inalazimishwa na ushuhuda ya Kanisa na mapokeo Takatifu.

## 1. KANISA

Huku sisi tutaandika mafundisho kidogo juu ya Kanisa ya Kristu, kusudi kusaidia kila mtu kwa usikio ya fundisho yetu ya Mapokeo Kimungu na Madiko Takatifu. (Fundisho ya kanisa tutafundisha mu ukurasa ingine mu sura ingine).

Hadisi ya Kanisa inaanza ku zamani sana, tangu wakati ya watu wa kwanza, Adamu na Eva. Na kweli, kama tutarudia ku mukongo, tutaona ya kama Adamu na bibi yake Eva waliishi mu Paradizo katika amani na furaha, kwani waliishi pamoja na Mungu. Makadaza yao ilikuwa wafike katika utii na moyo yao kwa mapenzi kitakatifu ya Mungu kwa uzima kimungu. Ni kusema wafate uzima takatifu ya Mungu katika neema Yake. Lakini ilikuja unyanganyi ya utii yao, uharibifu na ondokeo yao ku Paradizo. Matunda ya hii kosa yao ilikuwa wa matata: Kwa ajili ya zambi zao ilipasuka ushirika yao pamoja na Mungu na mtu alifanyika adui ya Mungu, mutumwa ya shetani ya ya zambi na mutumwa mu uharibifu na mu lufu. Milele kwa milele mtu mupotevu aliishi mu dunia na aliomba ukombozi. Wakati fulani, ilikuja utimizo ya wakati. Huyu Mukombozi walimuongojea kizazi ya kizazi alikuja. Huyu alikuwa Mwana na Neno wa Mungu (Uso wa mbili ya Utatu Mutakatifu), aliyefanyika mtu bila kusimama kuwa na mtu pamoja. (Yoano 1, 14**), «aliyetolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki»** Wa Roma 4, 25), **«Akakuwa mwenye kutii hata mauti, ndiyo mauti ya musalaba»** (Wafilipo 2, 8). Sandaka wa musalaba na Ufufuo ya Mukombozi wetu walikuwa kwa sisi shina ya uzima mupya na uzima isiyo kwarabika. Vile, Mwana wa Mungu alitakasa na tendo Yake asili wa uharibifu yetu na aliiuhuru toka utumwa ya shetani na minyororo ya lufu. (Wa Ebrania 2, 14-15 na Barua wa Pili ya Timotheo 1, 10). Yesu Kristu alikuwa Adamu wa mbili na alifanya uzalio wa mbili na uzima mupya ya asili ubinadamu, utakaso yake na ushirika yake mu uzima ya Neema Takatifu, mu ushirika na ungano pamoja na Mungu wa Uso Tatu. Niku sema Yesu Kristu alikuwa Muzazi wa kwanza ya ubinadamu mupya, iliyeokolewa na ilitakazwa katika Neema Yake.

Hii Ubinadamu Mupya ni Kanisa Yake. Madiko Takatifu inaiita Mwili ya Kristu na Kichwa yake ni huyu mumoja Muzazi na Mukombozi yake, Yesu Kristu. Tangu hile wakati watu wote waliitwa toka Kristu na Mitume wake juu ya kukataa mutu wao wa zamani, «Adamu wa kwanza», na kukuwa mateule ya hii Mwili Mupya ya «Adamu wa Mbili», nikusema Yesu Kristu, na ndani ya hii Mwili yake (Kanisa yake) ni namna wote ya wokovu wao. Hii Mwili ni Bibi-Arusi ya Kristu, ni Safina ya wokovu, ni sanduku ya Neema na Mulinzi ya fundisho ukweli, iliyeonekana kwa sisi.

Ushirika hii mupya katika Neema takatifu, hii desturi mupya alitengeneza na alileta Kristu hapa duniani, Kanisa Yake, haina kintu ingine, paka Ufalme wa Mungu pa inchi yetu. (Nikusema ni utawalo ya ufalme wa mbingu pa inchi yetu). Vile waliiona ma Nabii, vile, aliihubiri Mt. Yoano Mutangulizi, vile aliionyesha Yesu Kristu.

Hii Kanisa ya Kristu ni wa milele na isiyo uharibifu (Matayo 16, 18) na mulinzi ya fundisho kweli, kwani inaongozwa ku Roho Mtakatifu (Yoano 16, 13), kwa hivyo inaitwa **«Nguzo na musingi wa kweli»** (Barua wa kwanza ya Timotheo 3, 15).

## 2. MAPOKEO KIMUNGU

Hile amri aliipatia Yesu Kristu kwa Wanafunji wake, mbele ya kupanda mbinguni ilikuwa hii: **«Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu; mukiwafundisha kushika maneno yote niliyowaamuru ninyi; »** (Matayo 28, 19-20).

Lakini ku mbele aliwaambia hivi: «**Musaidizi, Roho Mutakatifu, Baba atakayemutuma kwa jina langu, yeye atawafundisha ninyi yote, na kuwakumbusha ninyi yote niliyowaambia ninyi»** (Yoano 14, 26). Na tena aliwaambia: «**Ninganli na maneno mengi ya kuwaambia ninyi, lakini hamuwezi kuyabeba sasa; lakini wakati anapokuja yule Roho ya kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli.. . »** (Yoano 16, 12-13).

Kweli, hile siku ya Pentikoste (masiku makumi tano, kisha Ufufuo ya Kristu) Wanafunji ya Kristu na wengine (wote walikuwa watu 120) walikuwa mu muji Yerusalema ndani ya nyumba moja na alishuka Roho Mutakatifu na aliangazie wote (Matendo ya Mitume 2, 1-4). Hile siku ilikuwa na kuhubiri wa kwanza ya Mtume Petro ku mbele ya taifa wa Yudea, na walisadiki watu ma elfu tatu (3000) (Matendo ya Mitume 2, 41). Tangu hile siku Kanisa, yenye mpaka hile siku alikuwa na paka wafwasi ya Kristu, ilianza kunenepa na kutawala ma fasi yote ya dunia.

Uzima ya Kanisa katika Roho Mutakatifu na Kuhubiri ya Habari Njema (Evangelio) ilitawala mu ulimwengu yote (Wa Kolosayo 1, 23) na hivi ilikuwa Mapokeo Takatifu.

Washuhuda ya Yehova kwani walikataa utakaso na isiyo kosa na isiyoharibifu ya Kanisa ya Kristu, walikataa na Mapokeo Takatifu. Hivi wanapokea sawa shina (chemchem) ya Ufufnuo Kimungu paka Madiko Takatifu. Ma fundisho ingine, wanasema, ni «mafundisho na ma shauria na mawazo ya watu na ufumbuo ya shetani». Kwa hivyo, wanasema, ma kanisa ya waaminifu, wapadri, ma Fumbo Matakatifu na uzima ya Liturgia, Watakatifu ya imani wa Kristu, Wapadri Wakubwa ya Kanisa ni hawa wote watumishi ya shetani. Kwa hivyo Washuhuda ya Yehova si wana wala ma kanisa, wala uzima wa ma Fumbo na Liturgia kimungu, wala Watakatifu, wala ufwasi ya Mitume, hata ushirika ya imani pamoja na Kanisa ya Mitume, yenye aliiumba Mungu hile siku ya Pentikosti. Nikusema, ya kusema na sauti kidogo, walipasukwa toka Kanisa ya Kristu na toka uzima katika Neema ya Roho Mutakatifu.

Kwa sababu, tunapashwa kujua sisi, ya kama Mapokeo Takatifu haina kintu kingine, paka uzima ya Kanisa katika Roho Mutakatifu, katikati ya ma milele yote. Kwa hivi, maonyesho yote ya hii uzima katika Roho Mutakatifu, nikusema, utawalo ya fundisho wa kweli, ufwasi ya Mitume, uzima katika ma Fumbo na Liturgia Kimungu, fundisho wa kweli na ufafanusho ya fundisho ya Evangelio toka Wapadri Watakatifu, maharifa ya uzima ya waaminifu wetu, katika

Neema takatifu na maonyesho yote ya uzima «mupya», yenye anaipatia kwa watu Yesu Kristu, katika Kanisa Yake ni Mapokeo Takatifu.

Kwa sababu hii ni hali na asili ya mapokeo Takatifu, ni mambo ya kusikia mbio kila mtu ya kama Kanisa na Mapokeo Takatifu ni ma fasi wa wili ya feza moja, bila kuwa moja bila ingine.. Kwa hivyo, tangu mwanzo iko Kanisa, tangu hile wakati ni na Mapokeo Takatifu. Lakini, Agano Jipya, yenye Washuhuda ya Yehova, wanaifamia sawa china wa pekee ya Mafundisho wa kweli ya Kristu, iliandikwa wakati ingine ku mbele, mu mwaka 52, kisha uzalio ya Kristu, ni kusema miaka makumi mbili (20), kisha kiumbe na mwanzo ya Kanisa, iliandikwa kitabu yake wa kwanza: Barua wa kwanza kwa WaTesalonika; lakini vitabu vingine ya Agano Jipya iliandikwa tena ku mbele na kitabu wa mwisho: Evangelio ya Yoano iliandikwa karibu mu mwaka 98, kisha uzalio ya Kristu. Hivi, basi, Kanisa iliumbwa, ilijitawala na ilianza kazi ya kuhubiri kwa watu katika Mapokeo Takatifu miaka mengi mbele ya kuonekanana Agano Jipya.

Mapokeo Takatifu, basi, hile wakati ya Mitume, ilikuwa shina wa pekee ya fundisho wa kweli ya Kristu na ilibaki na ilijichunga ku Mitume na waaminifu sawa moja «amana uliyewekewa akiba.. . » (Barua ya kwanza ya Timotheo 6, 20 na barua wa mbili 1, 14), na katika hii kitu kile kizuri ilifanyika mapokeo ya imani ya Kristu, inayeitwa: «Namna ya mafundisho» (Wa Roma 6, 17). Hivi Dini wa Kristu (Kristianisme) ilijitawala na kinywa kwa kinywa sawa mapokeo moja muzima na isiyoandikwa na ilifika pa masikio ya waaminifu. (Wa Roma 10, 17 na Barua wa kwanza ya Watesalonika 2, 13). Tena, na Mitume, wakati walianza kuandika, walipenda kabisa kusema kinywa kwa kinywa (barua wa mbili ya Yoano, shairi 12) na barua wa tatu ya Yoano shairi 14 na barua wa kwanza ya wa Korinto 11, 34), kwa sababu, kama walipenda kuandika mafundisho yote, **«.. . ninazania hata dunia yote haiwezi kutosha kwa vitabu vyote vitakavyoandikwa»** (Yoano 21, 25).

Hii Mapokeo Takatifu, yenye alichunga mafundisho yoyote ya Mitume, haikuwe mafundisho makosefu na «ma amri ya watu», sawa vile wanasema Washuhuda ya Yehova, lakini ilikuwa fundisho ya Kanisa ya Kristu, yenye katika makutano yake alitengeneza katika Roho Mutakatifu matendo yote ya imani na uzima ya waaminifu wake: **«Kwa maana inapendeza Roho Mutakatifu na sisi.. . »(**Matendo ya Mitume 15, 28). Basi, watumishi ya Evangelio hawakuhubiri mafundisho yao, lakini «**walipokuwa wakipita katika miji ile, wakawafundisha kushika amri zilizoamriwa na Mitume na wazee wa Yerusalema»** (Matendo ya Mitume 16, 4). Tena na huyu Mtume Paulo, aliyefundishwa Evangelio katika ufunuo ya Mungu (Wa Galatia 1, 11-12), alisadiki ya kama ilikuwa lazima kusema kuhubiri yake mbele ya masikio ya Mitume weingine juu ya kukikishwa ya kama hasitembee kwa bure (Wa Galatia 2, 1-2).

Ukweli ya Mapokeo Takatifu inaikaa pa usingi ya endeleo isiyo kupasuka ya kuhubiri wa Evangelio ya Kristu na uzima wa Roho Mutakatifu, sawa vile inatembea kwa kizazi ya kizazi, tangu wakati ya Mitume mpaka sasa; **«Kama walivyotuletea wale waliokuwa tangu mwanzo washuhuda na watumishi wa lile neno»** (Luka 1, 2).

Agano Jipya alitosha mafundisho yake toka mali ya mafundisho ya Mapokeo Takatifu, bila kupokea Mapokeo Takatifu muzima. Iko lazima ya kusema ya kama, wakati iliandikwa Vitabu ya Agano Jipya, Kanisa wa Mitume aliiona sawa uteule moja ya Mapokeo Takatifu. Kwa mfano, mukuandika Mtume Paulo kwa waaminifu ya muji Tesalonika: **«Ndugu, simameni kwa nguvu, mushike mafundisho muliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa barua yetu»** (Barua ya mbili wa Tesalonika 2, 15), anaita Mapokeo na mafundisho katika kinywa, «kwa maneno» na katika barua yake. Na, kweli, alikuwa na haki, kwa sababu alitosha toka Mapokeo Takatifu juu ya kuandika ma barua yake.

Kama hii ma neno yote tunaijua muzuri, tunasikia ya kama Madiko Takatifu, bila Mapokeo Takatifu, ni kitabu moja wa lufu na ya kuipasukwa toka uzima ya Kanisa wa Kristu.

Basi, paka Madiko Takatifu wa pekee, haiwezi kujitumia sawa shina (chemchem) muzima ya ufamio wa Kristu. Iko namna kuwa muzima, kama tunaisoma katika nuru ya Mapokeo

Takatifu. Na kweli, mukusoma Agano Jipya tunasikia ya kama inalazimishwa na Mapokeo Takatifu, kwani Huu Mapokeo ni usingi wake:

1)**Basi, walipokuwa wakipita katika miji ile, wakawafundisha (kwa waaminifu) kushika amri zilizoamriwa na Mitume na wazee wa Yerusalema»** (Matendo ya Mitume 16, 4).

**2)Ninawasifu ninyi kwa sababu munanikumbuka mimi katika maneno yote, na munashika mafundisho kama nilivyowaletea ninyi»** Barua wa kwanza ya Wa Korinto 11, 2)

3) «Fanyeni maneno muliyojifundisha na kuyapokea na kuyasikia na kuyaona ndani yangu, na Mungu wa salama atakuwa pamoja nanyi» (Wa Filipi 4, 9).

4) **Ndugu, simameni kwa nguvu, mushike mafundisho muliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa barua yetu»** (Barua ya mbili wa Tesalonika 2, 15).

5) **«Tunawaagiza ninyi, ndugu, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristu, mujitenge na kila ndugu anayetembea pasipo utaratibu, wala si kwa kufuata mafundisho muliyopokea kwetu»** (Barua wa mbili ya Watesalonika 3, 6).

6) **«Shika mufano wa maneno ya kweli uliyosikia kwangu, katika imani na mapendo yaliyo Kristu Yesu»** (Barua wa mbili ya Timotheo 1, 13).

7) « Na maneno yale uliyoyasikia kwangu kwa wahuhuda wengi, maneno haya uwekee watu waaminifu watakaofaa kufundisha wengine vile» (Barua wa mbili ya Timotheo 2, 2).

8)« **Kwa kuwa nina mambo mengi, lakini sitaki kuyaandika kwa karatasi na wino»** (Barua ya mbili ya Yoano shairi 12), **na «Nilikuwa na mambo mengi ya kukuandikia, lakini sipendi kukuandikia kwa wino, lakini ninatataji kukuona karibu, nasi tutasemezana uso kwa uso»** (barua ya tatu ya Yoano, shairi 13-14).

8) **«Na maneno yanayobaki, nitayatengeneza wakati nitakapokuja»,** anasema ku mwisho Mtume Paulo juu ya tendo ya kumaliza Fumbo ya Komunyo Takatifu )Barua wa kwanza kwa Wakorinto 11, 34).

9) **«.. . nayo yakiandikwa moja moja, ninazania hata dunia yote haiwezi kutosha kwa vitabu vyote vitakavyoandikwa»** (Yoano 21, 25).

10) Ku mwisho tuko na na maneno matakatifu, yenye wanaandika Wandishi ya Agano Jipya, haina ndani ya Agano la kale, lakini walibakia na walijiubiri katika Mapokeo Takatifu: Kwa mufano **a)** «.. . Ili litimie neno lililosemwa na manabii: Ataitwa Munazareti» (Matayo 2, 23). **b)** Unabii ya Enoka, hile anaiandika Mtume Yuda mu barua yake: «Na Enoka, mutu wa saba tangu Adamu, alitabiri juu ya hawa, akisema: Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, elfu elfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote.. . » (Yuda 14-15). **c)** Hadisi ya mazungumuzo katikati ya Mikaeli malaika na shetani juu ya mwili ya Musa, yenye anatuelejea mara ingine na MtumeYuda (Yuda, 9) na hii haipate kuandikwa mu Agano la Kale. **d)** Hivi inakuwa na kwa maneno ya Kristu «Heri ya kutoa inapita heri ya kupokea» (Matendo ya Mitume 20, 35) na hii neno haina kuandikwa mu Evangelio fulani, lakini anaiandika Mtume Paulo toka Mapokeo Takatifu.

Kama wanataka na Washuhuda ya Yehova wanapokea ya kama Madiko Takatifu haienee hii wa pekee na inalazimishwa na vitabu ya kuisaidia; kwa hivyo wanaandika na wanazambalala vitabu na vipindi mengi. Tena wanaandika hii maneno ya ajabu: « Kipindi jina lake Ulinzi (Skopia) ni chakula kwa kila wakati ya mwaminifu na mwenye akili mutumwa (nikusema kwa utawalo ya Matengeneo). Hii chakula wa roho, wanaandika, ni kitu kizuri sana. Bila hii chakula wa roho kondoo hawaweze kukomea katika roho yao» Basi, kitu kinene kabisa juu ya Washuhuda ya Yehova haina Madiko Takatifu, lakini ni hii mafundisho hawa wanaandika ndani ya Vitabu vyao na kabisa mu kipindi Ulinzi.

Ku mwisho tunapashwa kuandika sisi ya kama, kupatana na matengenezo ya Mungu Ufunuo iliyapatia Kristu Mwokozi, haitakuwe kuandikwa pa jiwe ya kupanga, sawa iliandikwa

Sheria ya Agano la kale, lakini iliandikwa toka Roho Mtakatifu pa jiwa wa mwili, ni kusema ndani ya ma roho ya waaminifu: **«Maana hili ni agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli, nyuma ya siku zile, anasema Bwana; nitatia amri zangu katika nia zao, na katika mioyo yao nitaziandika: Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu» (Wa Ebrania 8, 10** na 10, 16 Barua wa mpili ya Korinto 3, 3 na Yeremia 31, 31-33). Katika hii neno « Nyumba ya Israeli» maana yake ni Israeli mupya ya Neema ya Kristu, nikusema Waaminifu wa Yesu Kristu.

Andiko ya hii sheria wa Kristu, hapana ndani ya vitabu, lakini ndani ya akili na roho ya waaminifu iko Mapokeo Takatifu, kwani ni maarifa katika Roho Mutakatifu.

Kama sheria ya Mungu iliandikwa na ndani ya vitabu, ilifanyikwa hivi kwa ajili ya kosa ya watu, wenye hawaweze kuchunga ndani ya ma roho na akili yao hii sheria ya Munguna wekona lazima kusoma katika vitabu sauti ya Mungu.

Sauti ya mwisho ni hii: Ya kama Kanisa katika Mapokeo yake Takatifu, yenye inapokea tena na Madiko Takatifu ni shina wa pekee ya Imani wa Kristu.

Wa shuhuda ya Yehova wanatumia hii shairi kupigana ya Mapokeo Takatifu: **«Watu hawa wananiheshimu kwa midomo, lakini mioyo yao iko mbali nami. Wananiabudu bule wakifundisha mafundisho yaliyo amri za watu» (Marko 7, 6-7).**

Lakini hii ma neno haina na mapatano moja na Mapokeo Takatifu ya Kanisa wa Kristu, kwa sababu waliandikwa juu ya Wafarisayo ya hile nyakati na walitengeneza tena na mafundisho wa watu: **«(Yesu) Akawaambia: Isaya alitabiri vema juu yenu, wadanganyifu, kama ilivyoandikwa: . . . . Munaacha amri ya Mungu, munafuata desturi ya watu (Kama kuosha vikombe, na vyungu, na vyombo vya shaba) (Mark. 7, 4).** Akawaambia: **Kweli, munakataa amri ya Mungu, mupate kutii desturi yenu. Maana Musa alisema: . . . Lakini ninyi munasema.. . Mulitangua Neno la Mungu kwa desturi yenu muliyopokeleza. Tena munafanya maneno mengi sawasawa na maneno haya» (Marko 7, 6-13).** Basi, sauti hii ya Washuhuda ya Yehova haina na mapatanao moja na Mapokeo Takatifu. Hivi tunaweza kusema na kwa shairi ya (Wa Galatia 2, 8).

Kwa kusema sasa na sauti kifupi, tunasema mara ingine ya kama Mapokeo Takatifu ni maarifa (Tendo) isiyo kusimama ya Roho Mutakatifu ndani ya Kanisa. Ni uzima ya Kanisa katika Roho Mutakatifu, kwani Kanisa ni Mwili ya Kristu. Ni maarifa isiyosimama kutoka siku ya Pentikosti mpaka mwisho ya milele. Hii endeleo isiyo kusimama ya mapokeo wa Mitume ni ufananisho ya kanisa wa kweli ya Kristu. Kwa hivyo, ninyi wote walipasuka hii endeleo ao waliumba ma «Kanisa» ingine, kisha Siku Kuu ya Pentikosti (sawa walifanya Washuhuda ya Yehova), hawakuwa na hata mapatano moja na Yesu Kristu na Kanisa Yake.

## 3. MADIKO TAKATIFU

Sawa vile sisi tulisema, Washuhuda ya Yehova (tena na ma kundi ya Waprotestanti wote), wanasadiki ya kama shina (chemchem) ya imani wa Kristu ni paka moja: Madiko Takatifu na kabisa» Agano Jipya. Mukuwa na usingi hii Kitabu, wanakankamana kupata ao kuonyesha inafai kuwa nani kanisa wa kweli ya Kristu na imani ukweli.

Hii sauti yao ni ukosefu kabisa kwa sababu:

1) Madiko Takatifu na kabisa Agano Jipya, kwa sababu tunasema juu ya Kanisa wa Kristu, haiweze kuwa paka hii wa pekee shina ya imani wa Kristu, wala msaada kwa kanisa ukweli, kwa sababu imani wa Kristu na Kanisa wa Kristu walikuwa zamani ku mbele ya Agano Jipya. Kanisa, katika mwangaza ya Roho Mtakatifu «alizala» Agano Jipya na hapana Agano jipya «alizala» Kanisa.

2) Tunda ya hii jambo ni ya kama fundisho ya Agano Jipya ni ya kweli, kwani inatokea ya ushuhuda ya Kanisa. Nikusema Kanisa ni Hile inatukikisha ya kama Agano Jipya iliandikwa

katika pumuzi kimungu ya Roho Mutakatifu (na vitabu vyote ya Madiko Takatifu). Kama tutakataa hii ushuhuda ya Kanisa, hasitaweze hata mutu moja kutuonyesha ya kama Agano Jipya iliandikwa katika pumuzi kimungu.

3) Sawa vile tunajua sisi, Agano Jipya inaikaa na vitabu makumi saba (27). Hii vitabu walichaguliwa toka Kanisa katikati ya vitabu vingine (yenye walikuwa na walitawala hile wakati ya Mitume na jina yao) juu ya kufanya Kundi ya vitabu wa kweli ya Agano Jipya.

Sisi tunajua ya kama katikati ya milele wa wili ya Kanisa wa Kristu walitawala «Evangelia» mengi na vitabu vingine na walikuwa na jina ya Mitume, sawa vile Evangelio wa kwanza ya Yakobo, Evangelion ya Mtume Petro, ya Mtume Thomas, ya wa Ebrania, Evangelion ya Mitume kumi na mbili, Matendo wa siri ya Mitume, Kuhubiri ya Petro na vitavu vingine.. . Katikati yao walikuwa na Evangelia hile tukona yo ndani ya Agano Jipya (Katika Matayo, Marko, Luka na Yoano) na Barua yao.

Kanisa yetu katikati ya hii Evangelia mengi kwa saidio ya Wapadri Watakatifu na Makutano matakatifu wetu alichagua paka vitabu makumi saba (27) na alisema ya kama hii Vitabu waliandikwa katika pumuzi ya Roho Mtakatifu. Tena mambo ingine wa ajabu ni hii: Ya kama Kanisa yetu aliitika kupokea na Evangelia, waliiandika hapana Wanafunji ya Kristu, lakini watoto wa roho yao, nikusema Marko na Luka. Lakini Evangelia ingine alikataa, sawa Evangelio ya Yakobo, ya Thomas, ya Petro na ya Mitume kumi na mbili. Tena, vitabu ya watoto wa roho ya Mitume, sawa Marko na Luka, Kanisa yetu aliipokea, lakini vitabu ya watoto wa roho wengine ya Mitume, sawa askofu ya Roma Klimis na askofu ya muji Smirni, jina lake Pilikarpos, Kanisa alikataa kuipokea na alikamata mpango ya kama hii vitabu yao haikuandikwe na pumuzi ya Roho Mutakatifu.

Basi, ilikuwa nani kintu ya kufamia na nani anatukikisha ya kama Marko na Luka ao Yuda (ndugu ya Yakobo) waliandika katika pumuzi ya Roho Mutakatifu na wengine hapana?

Toka Hadisi ya Kanisa tunafunda ya kama ulazimisho juu ya kutengeneza vitabu vya nani walikuwa wa kweli ilionekana ku mwisho ya milele wa mbili. Hile wakati walimu wa wongo (sawa Markioni) walikombana kutengeneza mustari ya vitabu vyao ya Agano Jipya. Kwa hivyo Wapadri Watakatifu wengine ya Kanisa yetu, sawa Irineos, askofu ya muji Lugduno ya Fransa. Ipolitos, askofu ya Roma, Tertilianos wa muji Karkidona ya Afrika, Klimis wa muji Aleksandria, Origenis, Efsevios na wengine walianza kusema na kutengeneza Mustari ya vitabu wa nani walikuwa wa kweli na waliandikwa katika nuru ya Roho Mutakatifu.

Hii mambo ya kutengeneza vitabu ya Agano Jipya iliisha katikati ya milele wa inne, hile wakati Kanisa alipokea sauti ya Athanasios Mkubwa, patriarki ya Aleksandria wa Misri. Huyu mu mwaka 367, kisha uzalio ya Kristu, alioleta mara ya kwanza mu Hadisi ya Kanisa yetu mustari moja muzima na Vitabu ya Agano Jipya. Hii Vitabu ni mpaka sasa bile Vitabu Kanisa yetu anayapokea. Hii Mustari ya Vitabu makumi mbili na Saba ilifamiwa na mu Kanisa ya Magaribi (Kanisa wa Roma) mu mwaka 397 katika Baraza ya muji Karthageni ya Livii wa Afrika.

Mpango wa mwiho ilikuwa tunda ya mazungumuzo wingi, ma shaka na mawazo ya mbalimbali. Paka toka mfalme wa Konstantinopoli jina lake Yustinianos ilisimamisha kila shaka na mabishano juu ya vitabu ya Agano Jipya.

Pa hile fasi tunaweka ulizo moja ukubwa: Namna gani Wapadri ya Kanisa yetu na makutano walikamata mpango na walisema vitabu wa nani na wa ngapi waliandikwa katika nuru ya Mungu na wingine hapana? Jibu ni paka moja: Msaada ilikuwa Mapokeo Takatifu. Nikusema bile vitabu walipatana katika ukadiri na mafundisho yao pamoja na Mapokeo Takatifu ya Kanisa yetu (nikusema walikuwa pamoja na imani, fundisho, desturi ya ma Fumbo ya kanisa na uzima ya Kanisa katika Roho Mtakatifu) walipokelewa sawa vitabu wa mwangaza ya Roho Mtakatifu. Lakini, ninyi wote hawakupatane pamoja na Mapokeo Takatifu ya Kanisa yetu, waliacha inje ya Mustari ya vitabu ya Agano Jipya.

Hii yote niliandika yulu ni hadisi ya kanisa yetu na Washuhuda ya Yehova hawaweze kukataa. Kupindua! ndani ya kitabu yao kubwa na jina: «Madiko yote limepewa kwa maongozi ya Mungu na linafaa kwa mafundisho» (Ukurasa 175-262). Kule wanaandika na wanafafanusha kila kitabu ya Madiko Takatifu. Mambo ya ajabu nhi hii: Juu ya kuonyesha nguvu na ustahli ya kila Kitabu wanaita Wakubwa wapadri ya milele wa wili mpaka wa inne. Nikusema wanaandika wapadri wetu Watakatifu sawa: Papias askofu ya Ierapolis. Iustinos, mushahidi na mwenye akili, Origenis mwenye akili, Klimis askofu ya Roma, Irineos askofu ya Lugduno ya Fransa. Polikarpos, askofu ya Smirni, Ignatio, askofu ya Antiokhia, Efsevios, Ermas, Varnava, Yeronimos. Mt. Athanasios na wengine. Hawa wapadri Watakatifu ya Kanisa yetu Washuhuda ya Yehova wanawaita pa fasi ingine ya vitabu vyao watumishi ya shetani. Lakini sasa, hawa «Watumishi ya shetani» wanawaita, nikusema Mapokeo Takatifu muzima ya Kanisa yetu, juu ya kuonyesha ya kama Madiko Takatifu iliandikwa katika pumuzi na mwangaza ya Mungu!

Ndani ya hii kitabu umoja yao, mu ukurasa 303 wanaandika: «Hii matengenezo (ya Mustari ya Vitabu ya Agano Jipya toka mtu moja Markion, mukosefu kwa imani) pamoja na vitabu mengi, yenye walitawala hile wakati mu dunia muzima, ililazimishwa kuhamakia kila kitabu nani ilikuwa toka pumuzi ya Mungu na nani hapana». Hapa, Washuhuda ya Yehova, ao wanataka ao hawatake, wanapokea ya kama ndani ya ma milele wa wili ya Dini ya Kristu, haikukuwe Agano Jipya, kwa sababu mpaka hile wakati bado kukamata mpango Wapadri Watakatifu wetu vitabu wa nani walikuwa toka Mungu na ingine hapana. Na sawa vile anasema Yesu Kristu: **«Kwa kinywa chako nitakuhukumu, ewe mutumwa mubaya»** (Luka 19, 22).

Sauti ya mwisho ni ya kama, bila Mapokeo ya Wapadri ya Kanisa yetu hile wakati ya milele wa kwanza, hasitaweze hata mtu moja kutukikisha jju ya maongozi ya Mungu ya Vitabu ya Agano Jipya. Bila ufamio kubwa ya Kanisa juu ya fundisho ukweli yao hatutaweze kuwa na ukikisho ya kama hii Kitabu inayeitwa madiko Takatifu ni kweli Madiko Takatifu. Washuhuda ya Yehova, basi, mukukataa Mapokeo Takatifu na Wapadri ya Kanisa yetu, walipashwa kusadiki hile walisadiki, nikusema walipashwa kukataa Agano Jipya, kwa sababu Agano Jipya ni pa msaada ya Kanisa na Wataaktifu wake na pa Mapokeo Takatifu.

Hii sauti orhodokse haipunguke hata kidogo Agano Jipya, lakini, kupindua, inaipatia nguvu kwake, kwa sababu inaonyesha kabisa nguvu na ukweli yake na inaleta ushuhuda juu ya maongozi yake toka Mungu.

Washuhuda ya Yehova wanakankamana kukataa hii sauti nguvu yetu hivi: Wanasema Maongozi ya Agano Jipya toka Mungu inaonyeshwa toka mashuhuda inatupatia huu Agano Jipya umoja. Kwa mfano:

1)**«Madiko yote limepewa kwa maongozi ya Mungu na linafaa kwa mafundisho»** (barua mbili ya Timotheo 3, 16), anaandika Mtume Paulo kwa Timotheo. Lakini hii sura haiseme safi vitabu yenye ni ndani ya madiko Takatifu ni wa nani na wangapi. Tena katika hii sura wa yulu inasikiliwa paka Agano la Kale, kwa sababu hile wakati haikukuwe Agano Jipya na tena, kwa sababu, mu mustari ingine ya mukongo, Paulo anaandika kwa Timotheo: **«Na ya kuwa tangu utoto umejua maandiko matakatifu.. . »** (shairi 15). Lakini inaonekana safi kabisa ya kama hile wakati Timotheos alikuwa mtoto, paka ilikuwa Agano la Kale.

2) **«Ninashuhudia kila mutu anayesikia maneno ya unabii wa kitabu hiki, mutu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongeza mapigo haya yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mutu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamuondolea sehemu yake katika ule muti wa uzima.. . » (Ufunuo 22, 18-19).** Hii ushuhuda wanasema Washuhuda ya Yehova ni upumbafu, kwa sababu hapa wanatangazwa ninyi wote wanataka kuongeza ao kutosha ya hii Kitabu ya Ufunuo, watalipizwa. Haiseme hata sauti moja juu ya vitabu ya Agano Jipya ni wa nani na wangapi.

3) **«.. . Kama vile ndugu yetu mupenzi Paulo alivyoandika kwa hekima aliyopewa; kama vilevile katika barua zake zote.. . » (Barua mbili ya Petro 3, 15-16).** Lakini ndani ya hii mustari hasiandike Mtume Petro Vitabu vya Agano Jipya ni wa nani na wa ngapi. Mt. Petro

anaandika ya kama hii mafundisho yeye aliandika, aliandika na Mtume Paulo ndani ya barua yake. Ingine usafisho hakuna.

## Ufananisho ya Agano la Kale na Jipya

Tunatimiza fundisho juu ya Madiko Takatifu na sasa tunafananisha Agano la kale na Agano Jipya juu ya kusema ya kama Agano Jipya ni kupita kubwa.

Ni mambo moja ya kweli ya kama Washuhuda wa Yehova juu ya kusingi mafundisho yao, wanakimbilia mara mengi mu Kitabu Agano la Kale. Na, kwa kusikia ya kama wekona haki, wanakataa hii uchanisho ni katikati ya Agano la Kale na Agano Jipya, kwa sababu hawatake kuweka Agano la Kale pa fasi kidogo chini ku mbele ya Agano Jipya na hivi ma andiko yao itakuwa ya bure. Wanaachana paka Madiko wa Ebrania na Madiko wa Grekia (Wayunani).

lakini ni uchanisho kubwa ya bile sehemu wa wili ya madiko Takatifu na Agano Jipya ni kuliko mu fasi yulu ya Agano la Kale. Musa ni «Agano la Kale» (Ona barua ya mbili ya Wakorinto 3, 14-15), lakini Yesu Kristu na Sandaka yake ni «Agano Jipya» (Matayo 26, 26-28) (Marko 14, 22-24) (Luka 22, 19-20) (Barua mbili ya Wakorinto 3, 6). Sheria ya Agano la Kale ni «hali ya zamani», lakini Agano Jipya ni « Hali mupya ya roho» (Wa Roma 7, 6). Sheria wa zamani ni hali, hile inaua roho, lakini Agano Jipya inaleta uzima wa milele. Ma amri ya Agano la Kale ni «kivuli», lakini Kristu, nikusema Agano Jipya, ni «Mwili» (Wa Kolosayo 2, 16-17 na Wa Ebrania10, 1). Kwa kusema na sauti kifupi, sheria (nikusema Agano la Kale) ni kivuli ya vitu vema ya Agano Jipya na hapana picha (ikone) ya matendo ya Agano Jipya (Wa Ebrania 10, 1).

Agano la Kale ni matayarisho juu ya kufika kwetu Mwokozi Yesu Kristu. Haina Agano la Kale ufunuo muzima ya fundisho ukweli ya Mungu. Ni ndani yake paka ma alama na mafundisho ya kutayarisha dunia kwa kupokelea Kristu. Hii yote mafundisho na alama ya Agano la Kale iko namna kupata maana na ufafanusho yao kama tutaiangalia katika nuru wa roho ya Agano Jipya.
Agano Jipya, kupindua, ni ufunuo muzima ya fundisho kweli ya Mungu na inaitwa «Na kwa ajili yangu, nipewe usemi kwa kufungua kinywa changu, ili nihubiri kwa uhodari siri ya Habari Njema» (Wa Efeso 6, 19 na Wa Kolosayo 1, 27), «Lakini tunasema akili ya Mungu katika siri, akili inayofichwa» (Barua ya kwanza wa Korinto 2, 7), «ya kwamba kwa ufunuo nilijulishwa siri hii, kama nilivyoandika mbele kwa maneno machache» (Wa Efeso 3, 3-5, 9) (Wakolosayo 1, 26), na «Wapate kujua siri ya Mungu, ndiye Kristu, ndani yake hazina zote za hekima na kujua zinafichwa» (Wakolosayi 2, 2-3).

Basi, hawa hazina ya hekima na ufamio zinafichwa hile wakati ya Agano la kale. Walionekana katika Yesu Kristu mu wakati ya Agano Jipya. Tazama, juu ya nini Agano Jipya ni kupita pa fasi yulu ya Agano la Kale na mafundisho yote toka Agano la Kale wanapata maana na ukadiri yao paka katika nuru ya Agano Jipya. Kwa hivyo Agano la Kale haipashwe kufafanushwa hii wa pekee, paka na maungo yake, lakini inapashwa kufafanushwa katika nuru ya Agano Jipya.

# 2

# MUNGU WA MA USO TATU

## UTANGULIZI

Fundisho ya Utatu Mutakatifu ni «usingi ya imani», anasema mtakatifu Grigorio Mtheologo, kwa sababu mafundisho yote ya Dini ya Kristu inatokea ya hii fundisho ya Utatu Mutakatifu. Madiko Takatifu na kabisa Agano Jipya, yenye inatufundisha neno ya Mungu, inatufunua ya kama Mungu ni mumoja katika asili yake, lakini ni Tatu katika ma uso yake, nikusema Baba, Mwana na Roho Mutakatifu. Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu na Roho Mtakatifu ni Mungu, lakini hapana wa Mungu tatu, paka Mungfu moja, kwa sababu asili ya kimungu yao ni Umoja kwa ma Uso tatu na isiyo kuachana. Nikusema Hawa ma Uso tatu si weko vipande tatu ya kitu kimoja, nikusema vipande tatu ya umungu, lakini kila Uso ana asili kimungu muzima ndani yake na hivi hii asili kimungu inabakia umoja na isiyo kuachana, kama Umungu moja, Mungu moja.

Hii Fumbo kubwa ya Utatu Mutakatifu inabaki isiyo karibisha kwa uwazo ubinadamu na inajikaribisha kwa imani kabisa na hapana kwa akili. Hii fundisho sisi tunajua ni hii: Ya kama Mungu-Baba ni shina (chemchem) ya Umungu muzima, ya kama Mwana wake wa pekee alizaliwa bila mwanzo toka asili ya Baba-Mungu, na Roho Mutakatifu inatokea, bila mwanzo, toka Mungu-Baba. Hii neno: «bila mwanzo» maana yake ni ya kama haikukuwe wakati, pahali Mungu-Baba alikuwa huyu wa pekee, nikusema wakati pahali Mwana wa Mungu hasikuzaliwe na Roho Mutakaitfu hasikutokee toka Baba-Mungu, na huu inafanyika hivi kwani Mungu anaishi yulu ya wakati. Kwa hivyo hakuna mambo ya wakati katikati ya ma Uso ya Utatu Mutakatifu, nikusema, ya kama wakati fulani alionekana Baba-Mungu na wakati ingine alionekana Mwana wa pekee na Roho Mutakaitfu alitokea toka Baba-Mungu tangu wakati fulani. Hapana! Ma Uso Tatu ya Utatu Mtakatifu walikuwa pamoja kwa wakati moja. Kama tunasema juu ya Mwana Yesu ya kama alizaliwa toka Baba-Mungu na Roho Mutakatifu alitokea toka Baba-Mungu aipashwe kuwaza ya kama hii uzalio ni umoja na uzalio ya watu. Ni ufananisho moja juu ya kujua sisi namna gani weko Hawa ma Uso wa wili toka Asili ya Baba-Mungu. Kwa hivi na ma Uso Tatu ya Utatu Mutakatifu ni wa asili moja, ni na mwanzo moja, ni wa milele na weko na sifu moja na weko Mungu kweli wa pekee. Fumbo kubwa ya Mungu na isiyo kusikia inatufundisha Madiko Takatifu, wakati inasema: **«Tazama, Mungu ni mukubwa, nasi hatumujui; Hesabu ya miaka yake haiwezi kutafutiwa» « Hatuwezi kufahamu Mwenyezi» (Yobu 36, 26 na 37, 23).**

Washuhuda ya Yehova wanakataa hii fundisho ya Utatu Mutakatifu na wanafundisha ya kama Munguni paka Baba, anayeitwa Yehova, ya kama Mwana wa Mungu Yesu Kristu ni kiumbe wa kwanza ya Mungu na ya kama Roho Mutakatifu ni paka nguvu moja unyofu ya Mungu, bila uso. Kwa hawa, Yesu Kristu hasina wala Mungu, wala wa milele pamoja na Mungu-Baba, wala wa asili moja na Yeye. Tena wanasema ya kama Roho Mutakatifu hasina wala Uso, wala Mungu. Basi, sisi tutaanza kufunua makosa ya mafundisho yao na tutaonyesha katika usingi ya Madiko Takatifu ya kama Mungu ni kweli wa ma Uso Tatu.

## MASHUHUDA TOKA AGANO LA KALE JUU YA UTATU MUTAKATIFU

Agano la Kale ni «Kivuli», lakini Agano Jipya ni «Mwili»:

Sawa vile tulisema, Agano la Kale ni tayarisho moja pole-pole na imara na juu yake Mungu alitayarisha kila mtu apokee Mwokozi na Mukombozi, hile wakati atakuja duniani.

Agano la Kale haiko ufunuo nzima ya Mungu ku mutu. Paka inatwaambia ma alama na mifano ya fundisho ya Ukweli, kwa sababu fundisho kweli na muzima alikuja duniani katika Bwana Yesu Kristu.

Basi, ni kitu ya kuonekana nzuri ya kama Agano la Kale ni «Kivuli», lakini Agano Jipya (Kristu) ni «Mwili» (Wa Kolosayi 2, 16-17). Kwa sababu kikomo na mwisho ya sheria, ni Yesu Kristu (Wa Roma 10, 4). Agano la Kale wa pekee ni kitabu moja «kufungwa» na isiyo fafanusho na kwa kujaza na «mavuli» na ma alama. Kupindua Agano Jipya ni ufunuo nzima ya fundisho kweli wa Mungu. Ni «mwili», ni wa kweli. Kwa hivi Agano la Kale hakuna namna kuisoma hii wa pekee, kwani haina chemchem (shina) ya kuenea ya neno kimungu. Hii Kitabu inasomwa katika nuru ya Agano Jipya, kwa sababu paka vile inachukua maana yake yote na matendo yake wa siri wanafunuliwa. Neno ya Mungu inatukikisha mara ingine ya kama «.. . wakati wanaposoma Agano la Kale, kitambaa kile kile kinabaki.. . » (Barua wa mbili wa Korinto 3, 14). Na hii «kitambaa» inatoshwa paka «katika Kristu», nikusema kwa Evangelio yake, katika Agano Jipya.

Hivi, basi, na kwa fundisho ya Mungu Agano la Kale hasiseme safi juu ya ya ma Uso Tatu ya Umungu, sawa vile inatufundisha Agano Jipya, (pahali tunapata fundisho safi juu ya Utatu Mutakatifu). Agano la Kale inafundisha juu ya Mungu moja na anamupatia ma jina ya mbalimbali, sawa: Bwana, Yahve, Sabaothi, Adonayi, Elohim na ingine. Juu ya Mungu moja fundisho mu Agano la Kale ni ukali sana, lakini tunapata na ndani yake na mistari na maonyesho juu ya ma Uso Tatu ya Utatu Mutakatifu. Juu ya nini ndani ya Agano la Kale fundisho ya Utatu Mutakatifu haionekane sawa alionekana mu Agano Jipya? Kwa sababu hile wakati aliishi taifa ya Israeli, pempeni yao waliishi ma taifa mapagano na hawa waliabudu ma sanamu na wa mungu wingi. Basi, itakuwa mambo munene mu taifa ya Israeli, kama Mungu aliwafunua ya kama eko na ma Uso Tatu, kwa sababu ilikuwa namna teketeke taifa ya Israeli kutelemuka na wafate mafundisho ya wapagano, kwani na mapagano wanasadiki kwa wa mungu wingi. Tena namna ya kufunua Mungu mafundisho yake duniani alifanya hii tendo pole-pole, kwa sababu hakuna namna watu kupokea na kusikia hii mafundisho kimungu mara moja.

Maonyesho inatwaambia juu ya Utatu Mutakatifu toka Kitabu ya Agano la Kale, ni hii:

1) Onyesho ya kwanza: Agano la Kale ingawa ni fundisho ukali juu ya Mungu moja, lakini neno Mungu (mu lugha kiebrania El na Eloah) inaonekana ku mwisho yake na hesabu Pruriel, nikusema (Elohim= Wa Mungu). Vile inatuelejea juu ya Utatu Mutakatifu.

**2)** Onyesho ya mbili: Agano la Kale inasema juu ya Mungu, hile wakati ya kiumba ya ulimwengu na kisha mu jengo ya mnara babeli, kusuburia na maungo yake sawa weko ma uso mengi: **a)** Mungu akasema: **Tufanye mutu kwa mufano wetu, mwenye sura yetu.. . » (Mwanzo 1, 26). «Mungu akaumba mutu kwa mufano wake mwenyewe, kwa mufano wa Mungu akamwumba» (Mwanzo 1, 27).** Neno « kwa mufano wetu», mwenye sura yetu» tunaona ya kama inasharikiwa na «kwa mufano Yake, kwa mufano ya Mungu». Basi, hakuna namna kusadiki ya kama alisuburia kwa malaika. Ni sauti inayeonekana nzuri ya kama ma Uso Tatu ya Umungu wanasuburia katikati yao.

**b)** «Bwana Mungu akasema**: Tazama, mutu amekuwa kama mumoja wetu.. . » (Mwanzo 3, 22).** Na hapa hakuna namna kusadiki sisi ya kama Mungu alisuburia na malaika, kwani hii neno: «kama mumoja wetu» inatuaambia ma uso wa sifa moja na asili moja.

c) «Bwana akasema: .. . Tushuke tuwachaganyie usemi wao, wasikilizane lugha. Hivi Bwana akawasambaza toka kule juu ya uso wa dunia nzima; .. . » (Mwanzo 11, 7-8).

Ni ya kuonekana nzuri ya kama ndani ya hii mistari Umungu hana paka Uso moja, lakini ni mengi na wanaonekana sawa kwa kusuburia katikati yao.

3) Onyesho tatu: **«Na Bwana alionekana kwake kwa mielo ya Mamure, wakati alipokaa mulangoni mwa hema wakati jua lilipokuwa kali; akanyanyua macho yake, akaangalia, na tazama, watu watatu walisimama mbele yake; na wakati alipowaona, alikimbia kukutana nao toka mulango wa hema.. » (Mwanzo 18, 1-33).** Hawa ma Uso Tatu mu

mazungumuzo yao pamoja na Abrahamu wanaonyesha ungano na usawa moja katikati yao: walikuwa kweli ma Uso tatu ya Umungu moja. (Kisha Abrahamu hawa ma Uso wa wili walienda kama «malaika» mu muji Sodomka kusudi «waaambie», kwa Loti uharibifu ya muji kisha wakati kidogo).

Uwazo ya Washuhuda ya Yehova ya kama «malaika tatu ya Yehova, walichukua mwili na walionekana kwa Abrahamu (Ona kitabu yao: Kikomo wa milele ya Mungu inashinda sasa» hakuna namna kuwa ya kweli, kwa sababu Madiko Takatifu anasema ya kama, «Bwana alionekana.. . na tazama watu wa tatu.. . ».

4)Onyesho wa inne: **«Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu ni Bwana wa majeshi: dunia nzima imejaa utukufa wake» (Isaya 6, 3).** Hii neno mara tatu: «Mutakatifu» ni onyesho kubwa juu ya ma Uso tatu ya Utatu Mutakatifu.

5) Mashuhuda toka Agano la kale juu ya Mwana wa pekee Yesu Kristu:

Ila tu maonyeso wa yulu, tunapata na mashuhuda safi toka Agano la Kale juu ya Mwana na Roho Mutakatifu, lakini bila masafisho na mafafanusho mengi, kwa sababu, sawa tulisema, ufunuo nzima ya Mungu na Uso Tatu itakuwa mu Agano Jipya. Mashuhuda kwa Uso ya Mwana wa pekee ni hii:

**a)** «**Wewe ni Mwana wangu; leo nimekuzaa»** anasema Baba-Mungu kwa Mwana wake. Na Nabii Daudi anatushauria **«Busuni (mupendeni) Mwana asikasirike, nanyi munapotea njiani.. . » (Zaburi 2, 7, 12).**

**b) «Bwana anamwambia bwana yangu: Uketi kwa mukono wangu wa kuume, hata nifanye adui zako kuwa kiti cha miguu yako» (Zaburi 110, 1).** Kupatana na Luka 20, 41-44) na (Matendo 2, 34-36), Bwana wa kwanza ni Mungu-Baba na Bwana wa mbili ni Mwana, kama Mwokozi Kristu.

**c) «Kiti chako cha ufalme, ee Mungu, ni cha milele na milele; fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki.. . » (Zaburi 45, 6).** Hapa Mungu ni Mwana, katika shairi na kwa WaEbrania 1, 8).

**d)** Mu Kitabu ya Mezali, Solomono anasema juu ya Hekima (anayekuja katika mwili) ya Mungu, nikusema Mwana wake (Mwana Yesu ni Hekima ya Baba katika shairi ya barua ya kwanza ya Korinto 1, 24, 30), mwenye anaumba pamoja na Baba wake ulimwengu: **«Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, mbele ya kazi zake za zamani. Nimesimamishwa tangu milele, tangu mwanzo, wakati dunia isipokuwa bado. Wakati visipokuwa vilindi, nilizaliwa; wakati zisipokuwa chemchemi zinazojaa maji. wakati milima isipowekwa bado, mbele ya vilima nilizaliwa» (Mezali 8, 22-25).**

**e)** Mu Sura 30, ya kitabu Mezali ni na hii ushuhuda nzuri kabisa: «Ni nani aliyepanda mbinguni na kushuka chini? ». Eko Mwana wa Mungu, Yesu Kristu, katika sauti ya Mtume Yoano 3, 13 mu Agano Jipya. **«Ni nani aliyekusanya upepo ndani ya makonzi yake? (Ni paka Mungu).. .. «Ni nani aliyefunga maji ndani ya vazi lake? (Ni paka Mungu). «Aliyesimamisha miisho yote ya inchi? Jina lake ni nani, na jina la mwana wake ni nani kama unajua? (Mezali 30, 4).**

**f)** Ku mwisho, kwani daima mu ulimwengu muzima «Mungu ni mapendo» (Barua ya kwanza ya Yonao 4, 8, 16), hakuna namna kuwa paka Uso moja, kwa sababu mapendo ni fazila wa ushirika na inapashwa kuwa ma uso yulu ya moja. Hii ma uso tatu ndani ya Utatu Mutakatifu wanapendana kwa milele. Ndani ya Mezali, sura 8 tunasoma: **«Halafu nilikuwa pamoja naye, kama fundi la kazi: Nikakuwa furaha yake kila siku, nikifurahi siku zote mbele yake» (Mezali 8, 30).** Hii funja inatufunua mapendo wa milele ni katikati ya Baba na Mwana: Mwana ni «furaha yake (ya Baba) kila siku»; mara moja na Baba-Mungu ni furaha wa Mwana.

Kama Mwana alikuwa kiumbe na Roho Mtakatifu alikuwa nguvu moja isiyona Uso, sawa vile wanasadiki Washuhuda ya Yehova, basi, mbele ya kiumba, Baba, kwani alikuwa paka uso moja, haitakuwa namna kuwa «mapendo». Lakini Mungu «hasibadilishwe» na kwa hivyo ni daima «mapendo». Basi, alikuwa daima ku[ita ma Uso mengi na hapana paka moja. Hapa ni

fundisho ya kama mapendo inaonekana paka na uso kupita moja, ao mbili ao tatu. Sasa tunaona hapa Fundisho ya Utatu Mutakatifu mu Agano la Kale.

6) Mashuhuda toka Agano la Kale juu ya Roho Mutakatifu:

Sawa vile Kristu alitufunua, Roho Mutakatifu hana moja nguvu ya Mungu, bila uso (sawa vile wanachabula Washuhuda ya Yehova), lakini ni Uso wa Tatu ya Umungu moja, ni Mufariji (Musaidizi) (Yoano 14, 26, 15, 26-27). Agano la Kale inajaza na mistari ya mafundisho juu ya Roho Mutakatifu, lakini bila mafafanusho mengi.

a) **«Roho yako ni mwema; uniongoze inchi ya haki» (Zaburi 143, 10).**

**b) «Niende wapi mbali na roho yako? ao nikimbie wapi toka uso wako? (Zaburi 139, 7).** Hapa tunasikia ya kama Baba ni mwingine na sisi tusiweze kukimbia toka uso yake, na Mwingine ni Roho yake na toka huyu sisi tusiweze kukimbia. Ma fasi yote ni moja, ma fasi yote ya dunia ni na mwingine.

Tutaacha sasa maonyesho na ma shairi ingine ya Agano la Kale juu ya Roho Mutakaitfu na tuende mu Agano Jipya kuona ufunuo muzima ya Utatu Mutakatifu.

## 2. AGANO JIPYA: UFUNUO MUZIMA YA UTATU MUTAKATIFU

Mu Agano Jipya tusina na paka maonyesho manyofu juu ya Umungu na ma Uso Tatu, lakini tukona ufunuo muzima ya Utatu Mutakatifu:

1) **«Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na laq Mwana na la Roho Mutakatifu» (Matayo 28, 19),** anaambia Kristu kwa Wanafunzi wake.

Hakuna namna kuonekana mustari ingine kuliko safi sawa hii mustari, pahali tunaona ya kama Mungu ni na ma Uso tatu: Baba, Mwana na Roho Mutakatifu. Hakuna namna kusadiki sisi ya kama Baba-Mungu anaweka mu usawa umoja Mwana wake, kama Huyu Mwana wake ni kiumbe, sawa vile wanasema Washuhuda ya Yehova; wala kuweka Maungo Yake pempeni na sifa umoja na Roho Mutakatifu, kama Huyu Roho eko nguvu ya Mungu, sawa vile wanachabula Washuhuda ya Yehova. Ufananisho munene pa hii mustari ni hii: Hasiseme: «kwa ma jina» lakini aliandika: «kwa jina», nikusema hapa tunasikia ya kama Mungu Utatu Mutakatifu eko na asili moja ya ma Uso Tatu. Nikusema kwa jina ya Utatu Mutakatifu.

2) **«Neema ya Bwana Yesu Kristu, na mapendo ya Mungu, na ushirika wa Roho Mutakatifu ukae pamoja nanyi wote» (barua ya mbili ya Korinbto 13, 14).** Hapa inaonekana safi ya kama Mutume Paulo anaandika kwa jina ya Utatu Mutakatifu.

3) Uhushuda munene ya Utatu Mutakaitfu ilikuwa kwa Ubatizo na Ugeuzo ya Sura ya Bwana Yesu Kristu (Matayo 3, 16-17 na Matayo 17, 1-7). pale pamoja na Kristu ilisikiwa na sauti ya Baba, lakini Roho Mutakatifu alionekana na mfano ya ndege mu Ubatizo ya Kristu na mavazi ya Kristu walikuwa meupe sawa nuru, kwa Mageuzo ya Sura ya Kristu.

4) **«Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi» (Ufunuo 4, 8).** Na hii mwimbo Mtume Yoano anasikia mu Ufunuo atukuzwe Mungu. Ulazimisho nini ilikuwa jina ya Mutakatifu mara tatu, kama Mungu hasikukuwe na ma Uso tatu?

5) Wokovu ya kizazi ubinadamu ni tendo umoja ya Utatu Mutakatifu. Kwa hivyo ni daima ungano moja pa matendo na maarifa ya ma Uso Matakatifu tatu. Hivi:

**a)** Hata mtu moja hasiweze kusadiki ya kama Kristu ni Mungu na Mwokozi, kama hasitaangaziwa ku Roho Mutakatifu: **«Wala hakuna mutu anayeweza kusema Yesu ni Bwana, ila katika Roho Mutakatifu» (Barua ya kwanza kwa WaKorinto 12, 3).**

**b)** Hata mutu moja hasiweze kukaribisha Baba-Mungu, ila kama ataongozwa Kwake ku Yesu Kristu: **«Mutu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi» (Yoano 14, 6).**

**c)** Hata mutu moja hasiweze akuje kwa Kristu ila kama atamuongoza Baba: «Hakuna mutu anayeweza kuja kwangu ila Baba aliyenituma amuvute; nami nitamufufua siku ya mwisho» (Yoano 6, 44).

Kwa hivyo tuliokolewa **«Kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua ninyi katika utakaso wa Roho, kwa kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristu» (Barua ya kwanza ya Petro 1, 2).**

6) «Kwa maana watatu ni washuhuda mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mutakaitfu, na watatu hawa ni umoja» (barua wa kwanza ya Yoano 5, 7). Washuhuda ya Yehova wanakataa hii shairi kwani, wanasema, hainawa zamani, lakini mwandishi Tertilianos (155-240), kisha uzalio ya Kristu, askofu Kiprianos (258) na Wapadri wakubwa wengine ya Kanisa wa zamani ya Kristu walijua ya kama hii shairi ilikuwa ndani ya Agano Jipya.

## 3. MAFUNDISHO-BUNDUKI YA WASHUHUDA YA YEHOVA KUPINGANA YA UTATU MUTAKATIFU

Washuhuda ya Yehova wanaleta ma shairi ingine juu ya kukataa fundisho ya Utatu Mutakatifu:

1) **«Lakini kwetu kuna Mungu mumoja, yeye Baba na vitu vyote vimetoke kwake.. . » (barua ya kwanza wa Korinto 8, 6).**
2) **«Mungu mumoja, naye ni Baba ya wote.. . » (Wa Efeso 4, 6).**
3) **«Kwa sababu MUngu ni mumoja tu, na mupatanishi katikati ya Mungu na watu ni mumoja, yule Kristu Yesu» (Barua ya kwanza kwa Timotheo 2, 5).**
4) «Na huu ni uzima wa milele wakujue wewe, Mungu pekee wa kweli, na Yesu Kristu, aliyemutuma» (Yoano 17, 3).

Sisi tunawajibu hivi: Mungu ya Ufunuo wa Kristu ni Hali moja, Asili moja, umingu moja katika ma Uso Tatu. Chemchem (shina) ya Umungu ni Baba na toka Yake «anazaliwa» Mwana na «anatokea» Roho Mutakatifu. Kwa ajili ya hii mufano Yake Mungu-Baba anafananishwa sawa «Mungu mumoja», Mungu mumoja kweli» na toka Yake wanatokea ma Uso wengine wa Wili, wenye ni na Asili moja na sifa moja. Sawa vile nitamionyesha chini kidogo, Madiko Takatifu inaonyesha safi kabisa Umungu na ma uso wengine wa Wili, wenye wanatoka toka Mungu-Baba.

Tena, mukusema Madiko Takatifu «Lakini kwetu kuna Mungu mumoja.. » kisha inaongeza, **«Na kuna Bwana mumoja Yesu Kristu, kwa Yeye vitu vyote vimekuwa, na sisi kwa Yeye» (Barua wa kwanza kwa WaKorinto 8, 6).** Lakini hii ma jina « Mungu» na «Bwana» wanatumiwa na pa fasi ingine ya Madiko Takatifu na kwa Mungu-Baba na kwa Yesu Kristu na wanasharikwa kabisa: Nikusema «Mungu» ni na «Bwana» katika maana muzima, na «Bwana» ni «Mungu» katika maana muzima. Sawa vile, basi, Mungu-Baba anaitwa na namna unyofu «Bwana» (Matayo 22, 44), vile na «Bwana mumoja Yesu Kristu» anaitwa pa fasi ingine (sawa tutasema mu sura ingine) «Mungu», na tena «Aliye juu ya maneno yote, Mungu mubarikiwa kwa milele» (Wa Roma 9, 5). Basi, Utatu Mutakatifu haiharabikwa katika ma sauti-bunduki ya Washuhuda ya Yehova, lakini paka anaonekana Mungu mumoja kweli sawa chemchem (shina) ya Umungu muzima, mbele ya wa mungu ya mataifa wasanamu.

Ni lazima kuandika hapa na hii sauti, pempeni ya shairi wa inne (4). Madiko Takatifu inaita Mwana wa Mungu Yesu Kristu na ma neno umoja, sawa anasema hapa juu ya Mungu-Baba. Kwa mfano: «Nasi tunajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa sisi akili ili tumujue yeye aliye kweli, nasi tuko ndani yake yeye aliye wa kweli, ndani ya Mwana wake Yesu Kristu» (barua wa kwanza ya Yoano 5, 20). Basi, «Mungu wa kweli» ni Baba (Yoano 17, 3), «Mungu wa kweli» ni na Kristu (barua wa kwanza ya Yoano 5, 20). « Uzima wa milele ni Baba (Yoano 17, 3), «Uzima wa milele» ni na Kristu (Barua wa kwanza ya Yoano 1, 1-2, 5, 11-12, 20).

5) Bunduki-sauti ingine ya Washuhuda ya Yehova ni ya kama Jina «Utatu Mutakatifu» hakuna pa fasi moja ndani ya Madiko Takatifu. Ni kweli ya kama hakuna. Lakini haina na mambo munene ya kama hakuna jina hii. Mambo munene ni juu ya kuwa maana ya Utatu Mutakatifu. Ni kusema, (sawa tutaonyesha na kidogo chini), Mwana na Roho Mutakatifu ni ma Uso wa asili moja pamoja na Baba, ni Mungu wa kweli, sawa ni Baba; hivi mara moja inaonyeshwa ukweli ya Utatu Mutakatifu, hata kama ndani ya Madiko hakuna jina ya Utatu Mutakatifu. Maana wa kwanza ni hali ya kama Hawa ma Uso Tatu ni Mungu moja wa kweli. Mu wakati ya Mitume jina ya «Utatu» haikutumiwa, kwa sababu Waaminifu walichunga mu roho yao hii maana yake; Lakini, wakati walianza walimu wa uongo kushaka mafundisho ya Imani ya Kristu, tangu hile wakati kanisa alitumia na ma sauti na jina ingine ya imani, sawa «Utatu Mutakatifu», juu ya kulinzi fundisho ya imani ya Kristu.

6) Ku mwisho, Washuhuda ya Yehova wanachekelea sisi Wakristu, kwani tunakikisha ya kama fundisho ya Utatu Mutakatifu ni Fumbo urefu na isiyo kufafanusha, na wanazania ya kama hii imani yetu mbele ya fundisho-Fumbo wa siri ni imani ya bure. Halafu, Mungu wa kweli, kwani ni asiye na mupaka, Mwenyezi na wa milele, hasiweze paka kwa kuwa asiye sikilizo kwa akili ya ubinadamu. Juu ya kuweze tusikie na namna ukamili Mungu, tunapashwa kuwana na sisi wa mungu katika hali kimungu, sawa vile Yeye eko. Tena neno ya Mungu inatwaambia ya kama Mungu ni fumbo wa siri: **«Tazameni namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazivumbulikani, na njia zake hazitafutikani! Maana ni nani aliyejua nia ya Bwana? Ao ni nani aliyekuwa mushauri wake? (Wa Roma 11, 33-34), na «Siri ya utawani kubwa» (Barua ya kwanza kwa Timotheo 3, 16). Angalia na Yobu 36, 26 na 37, 23).**

7) Hana paka Mungu mumoja siri, lakini na Evangelio Yake, hile paka katika mwangaza ya Roho Mutakatifu tunaweza kuisikia: (Wa Efeso 1, 17-19, 3, 8-9, 14-19) nma pa fasi ingine. Basi, inapashwa kusopoka hii sauti yetu Washuhuda ya Yehova, wenye walishusha kabisa Mungu pa fasi ya akili wa ubinadamu na wanasadiki ya kama hii Siri (Fumbo) ni wa bure (Barua wa kwanza ya Wakorinto 1, 17), na walikuwa watumwa ya akili wa ubinadamu, sawa vile wakosefu wote kwa imani ya Kristu.

Sasa, kwani tuliisha kuandika ma shairi yote juu ya Fundisho ya Utatu Mutakatifu, tutaenbdelesha kuandika ma shairi ingine juu ya Umungu ya Mwana wa pekee na Roho Mutakatifu, lakini mbele nitamifundisha juu ya «jina» ya Mungu.

# 3

# «JINA» WA MUNGU

## MWANZO

Mu Kitabu wa kwanza Agano la Kale ya lugha kiebrania, Mungu anaitwa na ma «jina» ya mbali-mbali. Lakini hata moja «jina» haina «jina» yake. Washuhuda ya Yehova wanapokea paka «jina» Yake moja; mu lugha kiebrania ni hii: «Yakhve» (na waliiharabisha kidogo na waliifanyisia Yehova, kwa hii jina inatokea na jina yao), na wanafundisha ya kama, kama tunakataa kuabudu Mungu paka na hii «Jina» tusikuwe «kwa wale watu Mungu aliwachanisha kwa kuwa taifa yake kwa jina Yake», na hivi, hakuna namna kuokolewa. Wanaandika: «Itajikula mwili ya wale watu hawatake kufunda ya kama Mungu wa muzima na wa kweli anaitwa paka Yehova! Watalekea, pa hile fasi wanasimama pa miguu yao! (Angalia Kitabu yao: Toka paradizo isiyoharibiwa, ukurasa 209 (Lugha kigreki: ’Από τόν Απολεσθέντα παράδεισο.. . σελις 209).

Na majivuno mingi wanasema nguvu ya kama hii jina inandikwa mu Kitabu ya Agano la Kale toka lugha kiebrania wa zamani mara ma elfu saba (7000). Lakini, kwa sikitiko munene yao, hii jina hakuna mu Agano Jipya, hata mara moja, hile waliandika Mitume ya Kristu mu lugha wa kwanza kigreki na wanaandika ma jina ingine kwa Mungu!

Kwa hii neno, sisi wa Orthodoksi, hatukatae hii jina Yakhve, toka lugha kiebrania, lakini tunasikia ya mwisho ya kama-sawa vile na Madiko Takatifu inatuonyesha-utumio yake inakuwa mu mupaka ya taifa wa Ebrania ya Agano la Kale. Mu wakati mbele ya Kristu, Mungu alikuwa na ushirika paka na taifa ya Ebrania na ilikuwa na haki Mungu atumie ma jina toka lugha kiebrania juu ya kufamia maungu yao kwao. Kama Taifa yake, mbele ya Kristu, ilikuwa mwingine, kwa mufano, wa Yunani (taifa wa Grekia (Hellas), Mungu bila shaka ilikuwa namna kutumia jina Yake, toka lugha kigreki na hapana jina «Yakhve». Hii mambo inaonekana muzuri kabisa mu wakati ya Agano Jipya. Mungu anahubiri mbele ya ma taifa yote ya dunia na anapatia jina yake mu lugha kigreki, kwani ile wakati yake lugha ya kuzungumuza na kuandika watu ilikuwa kigreki na kilatina.

## 1. MUNGU ANALAZIMISHWA JINA?

Washuhuda ya yehova wanaandika ndani ya vitabu vyao: «Malaika, watu, ma nyama, tena na manyota na vitu isiyo nafsi, wekona ma jina. Iko namna Muumba yao kuwa bila jina? ». Wanajibu wenye wa pekee pa hii ulizo yao ya kama jina Yakhve ni jina wa miele na umoja ya Mungu na paka katika hii jina sisi wote tunapashwa kumuita. Sauti-bunduki yao ni hii: **«Bwana akamwambia Musa: Utaona sasa nitakayotendea Farao; kwa maana kwa mukono wa nguvu atawaacha kwenda, na kwa mukono wa nguvu atawafukuza toka inchi yake. Na Mungu alisema na Musa, akamwambia: Mimi ni Yehova; » (Kutoka 6, 1-3).** Hawa Washuhuda ya Yehova wanasema ya kama na maneno ya Kristu wanawaza hii jina: **«Nilionyesha jina lako kwa watu wale ulionipa katika dunia» (Yoano 17, 6, 26),** tena na ma neno ya Sala wa Kristu: Baba yetu uliye mbinguni.. . jina lako litukuzwe» (Matayo 6, 9) na pa fasi ingine tutaandika chini kidogo.

Paka na usingi ya hii fundisho yao, walifika pa hile kosa kwa kuabudu jina ya Mungu na wanasadiki ya kama wokovu ya watu inatokea paka, kama mtu anaabudu Mungu katika jina Yake «Yehova». Lakini, sisi twende kuangalia hii fundisho yao na pasopo mingi:

Ku mwanzo, hii sauti yao, ya kama ma nyama, malaika na ma nyota wekona jina, inapashwa na Mungu kuwa na jina Lake, ni sauti wa bure. Hii vitu na ma nyama ni wingi na

inapaswa kuwachanisha na jina yao kila moja, lakini Mungu ni Mumoja na ya mambo gani tunapashwa kumuachana ya wa mungu wengine? Ni na wa mungu wengine wa kweli? Hapana!

Kisha, Mungu ni asiye na mupaka na asiye kusikilizwa na asiyekuandikwa; maana Yake hakuna namna kuiweka ndani ya «jina» moja, inaileta akili ubinadamu. Kwa hivyo, kama na Mungu anapatia kila wakati «jina» yoyote kwa maungo Yake, ni moja alama, moja sauti isiyo kamilifu kwa ajili ya hii «jina» anataka Mungu atupatie tangazo moja.

Ni mambo ya ajabu ingine ya kama pa fasi ingine Mungu anakataa apatie jina kwa maungo Yake na anaitwa Yeye wa pekee «Mwenye kuwa», nikusema Huyu anaye eko wakati yoyote (Kutoka 3, 13-15). Hii «jina» inatushuhuda kabisa ya kama Mungu asiye mupaka ni kwa sisi watu wa milele, asiye kusikilikwa na asiye kuwa na jina.

Kwa kutumia jina unyofu « Mungu», haishushe uwezo na nguvu Yake. Hii fundisho wanaipokea na Washuhuda ya Yehova. Mu Kitabu yao: «Mukufasiri jina Mungu» wanaitika ya kama Mtume Paulo, hile wakati alihubiri kwa watu wa muji Athina, hasikutumie jina «Yakhve» lakini jina « Mungu». Hapa iko na nguvu hii sauti ya Bwana Yesu Kristu: «Kewa kinywa chako nitakuhukumu, wewe mutumwa mubaya» (Luka 19, 22).

## 2. MA «JINA» YA MUNGU NI MENGI

Mukusoma sisi Agano la Kale tunaona ya kama Mungu alipata kwa maungo Yake ma «jina» mengi na hapana paka moja, jina: «Yakhve». Sawa ma «jina»: Ekhiek, Kana, Kantosh=Mutakatifu, Goel=Mukombozi, Mwenyezi, Adonai. Elokhim, El Santai, Yakhve, Savaothi na ingine.

1) **«Musa akamwambia Mungu: Tazama wakati, ninapokuja kwa wana wa Israeli, nakuwaambia: Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wataniambia: Jina lake nani? nitawaambia nini? Mungu akamwambia Musa: Ndimi Niliye; akasema: Utasema hivi na wana wa Israeli: MIMI NIKO aliyenituma kwenu» (Kutoka 3, 13-14).**

**2) «Na Bwana akasema kwa Musa: maana hatuabudu mungu mwingine, kwa kuwa Bwana, jina lake ni mwenye wivu, ni Mungu mwenye wivu» (kutoka 34, 14).**

**3) «Maana yeye aliye juu na kutukuka, anayekaa kwa milele, na jina lake ni Mutakatifu.. . » (Isaya 57, 15).**

**4) «.. . Wewe Bwana ni Baba yetu, Mukombozi wetu, toka milele ni jina lako» (Isaya 63, 16).**

**5) Mu Zaburi 132, 2 Mungu anaitwa Avir.**

6) **Mu Zaburi 16, 2, Mungu anaitwa mu lugha kiebrania Adonayi.**

7) **Mu Kitabu Nehemia 10, 29 anaitwa Elohim.**

8) **Mu Kitabu Kutoka 6, 3 anaitwa Mungu El Santayi (Mungu Mwenyezi) na Yakhve).**

9) Mu Kitabu ya Isaya 6, 3 anaitwa Yakhve Sabaothi. Tena ni lazima sisi kusopoka ya kama Mitume Paulo na Yakobo, wenye wanatumia hii jina wa mbili kwa Mungu mu Agano Jipya wanafasiri jina= Yakhve kwa jina Bwana na wanaacha jina Sabaothi bila kuifasiri: Nikusema «Bwana Sabaothi» (Wa Roma 9, 29 na Yakobo 5, 4). Kama, basi, Mitume ya Kristu wanafasiri jina ya Mungu Yakhve kwa jina Bwana, sisi juu ya nini hatuweze kuifasiri?

Kwa sababu, basi, Madiko Takatifu inatupatia ma jina mengi ya Mungu, juu ya nini Washuhuda wa Yehova wanataka paka kutumia jina moja ya Mungu? Paka jina Yehova? Na namna gani paka hii jina Yehova inaokoa watu na ma jina ingine ya Mungu hawaokoe? Kwa hii ulizo yetu Washuhuda ya Yehova wanajibu katika zoezo yao, ya kama ma jina ingine haina jina ya Mungu, lakini ni jina ya kufananisha hali ya Mungu.

Tunawajibu: Ndivyo, ni ma jina ya kufananisha hali ya Mungu, lakini Madiko Takatifu inaandika «Jina». Tena tunaangalia ya kama jina Yakhve (ao Yehova) haina jina na hii maana kabisa.

Kupatana na Washuhuda ya Yehova hii Jina «ni mfano moja ya verb Havah, maana yake «Huyu anayekuwa». (Ona Kitabu yao: JIna kimungu itabaki kwa milele, ukurasa 6. Na mu kitabu yao: Mungu ni kweli, ukurasa 28). Pa fasi ingine wanafasiri hii jina: «Hule anayetengeneza».

Basi, kama jina Yakhve (ao Yehova) haina jina na maana yake kabisa, iko namna sisi kuifasiri na ma lugha ingine. Kweli, ufasiri ya Agano la Kale inatumia jina «Bwana» pa fasi ya jinaYakve. Vile wanafanya na Mitume ya Kristu mu Agano Jipya.

## 3. JINA WA KWELI NI YAKHVE NA HAPANA YEHOVA

Sisi tunapashwa kujua ya kama lugha wa zamani Kiebrania haikukuwe na ma herufi a, e, o, u, i, y. Kwa hivi jina ya Mungu watu wa Ebrania waliiandika GHVH. Kwa ajili ya heshima kwa hii jina ya Mungu wanaiita GHVH, lakini kisha miaka mingi walisahabu ma herufi na sauti nguvu walikuwa katikati ya hii maherufi GHVH. Kisha miaka mingi, mu mwaka 750, kisha uzalio ya Kristu walianza kutumia na ma herufi a, e, o, u, i, y, lakini hawakujue ma herufi ma nani walipashwa kuitumia. Walikamata mpango kutumia ma herufi wa na sauti nguvu ya jina ingine ya Mungu, jina=Adonayi (Nikusema ma herufi: a, o, a). Vile walifanyaka jina Ga Ho Va H na hii jina pole-pole ilifanyika Yehova. Basi, jina Yehova haina hata hile Jina Mungu aliisema kwa Nabii Musa katika sura ya kitabu Kutoka 6, 3, lakini ni ufundi ya wakubwa wa Ebrania mu mwaka 750-1000 kisha uzalio ya Kristu. Leo watu wenye akili wale wanatumika ma mambo ya lugha ya wa Ebrania wanaitika wote ya kama jina GHVH iliitwa Yahve. Jina Yehova, hile wekona yo Washuhuda ya Yehova haionekane ma fasi yote ya Madiko Takatifu.

## 4. KWA AJILI YA «JINA» WANAKATAA KAZI YA KRISTU

Agano Jipya muzima inahubiri fundisho moja kweli ya kama Mungu-Baba kwa mapendo yake mbele ya viumbe vyake (watu wote ya dunia), alituma Mwana wake duniani aokoe uzazi ubinadamu toka lufu na uharibifu; auhuru toka utumwa ya shetani; kwa kutupatia uhaki na kwa kutufanyisia wakaa ya ufalme Wake (Yoano 1, 12, 3, 16. WaGalatia 4, 4-5. WaEbrania 2, 14-15. Barua ya kwanza ya Yoano 4, 14).

Washuhuda ya Yehova wanaharabisha hii kazi ya Kristu na wanafundisha ya kama wokovu ya uzazi ubinadamu ni kikomo wa mbili ya Mungu na hile kazi Mungu anaonyesha mafaa Yake ni onyesho ya jina Lake! Hapa tutaandika mafundisho ya Washuhuda ya Yehova juu ya kujua waaminifu Waorthodoksi ni nini sauti yao mubaya. Wanaandika: «Kikomo wa kwanza yake (Ya Yesu Kristu), wakati alikuja duniani haikukuwe wokovu ya watu. Wokovu ya watu ni kintu kinene kwa wale wanataka kuokolewa, lakini fasi yake ni ya pili ndani ya akili ya Mungu. Uwazo ya Yehova (Mungu) ni kujenga utawalo uhaki, utawalo katika uwezo ya Mungu na kwa hii utawalo ataonyesha jina lake mbele ya viumbe vya ulimwengu». Pa fasi ingine wanaandika: «Onyesho ya jina ya Yehova ni kupita munene ya wokovu ya watu» (Soma mu Kitabu Yao: Mungu ni kweli».

Fundisho mubaya yao ingine ni hii ndani ya Kipindi yao: Ulinzi (mu lugha kigreki Skopia 15-3-1985, ukurasa 32): Jabo kubwa mu Hadisi ya watu ni nani? Lufu ya Yesu Kristu. Juu ya nini? Kwa sababu ilitumiwa kwa uhaki ya jina wa Mungu». Basi, Kristu hasisulubiwe kwa wokovu wetu, lakini paka kwa uhaki ya jina Lake, jina= Yehova! Tunasikia, basi, ya kama hawa washuhuda ya yehova ni wapingu ya Kristu na wanaharabisha ufafanusho kweli ya Madiko Takatifu. Wanaharabisha Evangelio ya Kristu na wanafundisha «Evangelio» ingine na hivi wanaanguka kwa mafigo ya Mtume Paulo (Wa Galatia 1, 8).

## 5. JINA YA YEHOVA HAKUNA NDANI YA AGANO JIPYA

Jina ya Mungu wa ebrania haiandikwe ndani ya Agano Jipya. Mitume ndani ya mandiko yao, wakati ilizimishwa kuandika mafundisho vipande-vipande toka Agano la Kale mu Agano Jipya, walifasiri jina Yakhve kwa jina Bwana ao Mungu. Hii sauti yetu inatuelejea na jina wa mbili Yakhve Sabaothi toka Agano la Kale (Isaya 6, 3), iliitumia Mitume Paulo na Yakobo juu ya kufasiri jina Yakhve kwa jina Bwana, lakini waliacha jina Sabaothi paka hivi (Wa Roma 9, 29 na Yakobo 5, 4).

Washuhuda ya Yehova, kwa makankamano yao juu ya kutuelejea juu ya nini inalofa jina Yakhve toka Agano Jipya, wanasema ya kama hii jina ilikuwa ndani ya Agano Jipya, lakini.. . . waliitosha wapadri!

Lakini sisi tutachukua vitabu vyao juu ya kuonyesha ma sauti yao ya wogo. Sawa vile hawa washuhuda ya Yehova wanasema ndani ya vitabu vyao, hata kitabu moja wa kwanza toka vitabu ya Agano Jipya haikuokolewa toka mwanzo yake. Lakini ni leo, wanaandika, kundi moja ya vitabu wa zamani ya Agano Jipya, iko yoyote 13. 600 vitabu ya Agano Jipya, waliiandikwa na mukono na wakati yao ni toka milele wa mbili mpaka milele wa kumi.

Ndani ya hii Vitabu wa zamani ya Agano Jipya hakuna jina Yehova. Kutoka kitabu ya Muevangelizaji Matayo mpaka kitabu ya Ufufuno hakuna jina Yehova! Vile wanaandika na Washuhuda ya Yehova ndani ya vitabu yao. Namna gani, basi, wanaandika ya kama jina Yehova ilikuwa ndani lakini waliitosha wapadri?

Tena na hawa Washuhuda ya Yehova wanasema ya kama wanazania ya kama jina Yehova ilikuwa ndani ya Agano Jipya. Hakuna shairi moja toka vitabu yao ya kutuonyesha ya kama Waevangelizaji walitumia jina Yehova ndani ya Vitabu vyao.

Washuhuda ya Yehova wanasema ya kama jina Aliluya mu kitabu Ufunuo inatuonyesha jina ya Yehova mu Agano Jipya (Ufunuo 19, 1-4).

Ni kweli ya kama jina Alilu-yah ni jina toka lugha kiebrania na maana yake: Musifuni Yah=Mungu. Lakini hii sauti yao inapiga hawa wenyewe. Kwa sababu, hii jina ni mu lugha kiebrania, lakini Mtume Yoano ao kusema kupita nzuri, neno ya Mungu inafasiri kwa Yoano mu lugha kigreki hivi: Musifuni Mungu: «Na wale wazee makimi mbili na wane, na wale nyama wane wenye uhai wakaanguka na kuabudu Mungu anayeketi katika kile kiti cha ufalme, wakisema: Amina, Haleluya. Sauti ikatoka katika kiti cha ufalme ikisema: Sifuni Mungu wetu.. . » (Ufunuo 19, 4-5).

Kama huu neno ya Mungu (sauti toka Kiti ya Mungu) inafasiri jina Yakhe kwa jina Mungu, juu ya nini Washuhuda ya Yehova wanasadiki nguvu kwa jina Yakhve, iliyetoka ya lugha kiebrania? Tena ni lazima kusema ya kama jina Aliluya ni sauti wa mwisho ya zaburi na wimbo ingine toka Kitabu ya Zaburi ya Agano la Kale; sawa vile tunasema sisi mu lugha kigreki: Bwana hurumia, iliitumiwa bila ufasiri ya ma Kanisa ingine ya Kristu.

## 6. JINA MUPYA YA MUNGU MU AGANO JIPYA

Mungu anapatia kwa maungo Yake ma jina ya mbali-mbali mu Agano la Kale na Agano Jipya katika hile tangazo Yeye anataka kutuonyesha. Mu Agano la Kale anataka kuonyesha kwa watu ya kama ni Muumba, Anayekuwa, Mwenyezi, Yakhve (Muumba).

Mu Agano Jipya tangazo ya Mungu kwa mutu inatimizwa na anachukua hali yake nzima na jina mupya, hile Yeye mwenyewe anapatia kwa maungo Yake: Ni jina Mungu-Baba.

Sawa vile tuliandika na ku mukongo, mu sura ingine, kikomo wa pekee kwa ajili yake Mungu aliumba mtu ilikuwa kwa kumufanyishia mwana wake katika neema Yake na kwa kufurahi mu uzima kimungu. Kwa hivyo Mungu hasiache kosa ya mtu wa kwanza kuharabisha hii kikomo, lakini katika mapendo isiyo na mupaka juu ya kiumba Yake, anatengeneza namna

moja juu ya wokovu wake (ya mutu) na hii namna anaitimiza katika Mwana wake wa pekee. Wakati ilikuja utimizo ya wakati, Mwana wa Mungu alikuwa na mutu juu ya kutufanyishia sisi wana wa Mungu katika neema Yake (Yoano 1, 14, 12 na Wagalatia 4, 4-5). Mungu katika Mwana wake wa pekee anatupokea sawa wana wake na Yeye anakuwa B a b a wetu. Hii ni tangazo kubwa, inayetupatia Mungu mu Agano Jipya.

Jina Baba-Mungu inatuonyesha hii tendo kubwa ya upenzi-ubinadamu ya Mungu kwa sisi. Mungu ya Wakristu ni Mungu wa mapendo, na hana na kintu kimoja na «mungu» ya Washuhuda ya Yehova, kwani huyu «mungu» yao hana na mafaa ingine paka kuonyesha uwezo ya jina yake duniani!

Agano Jipya inatuwaambia safi kabisa kwa hii mambo ya jina mupya ya Mungu, tangu nyakati wa zamani ya Wakristu.

1). Mtume Paulo anaweka mbele ya wamungu wa uwongo, Mungu kweli na anamuita Baba na hapana Yehova: «.. . Lakini kwetu kuna Mungu mumoja, yeye Baba, na vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake, na kuna Bwana mumoja Yesu Kristu, kwa yeye vitu vyote vimekuwa na sisi kwa yeye» (Barua ya kwanza ya waKorinto 8, 5-6). Mtume Paulo hasiseme: «Mungu mumoja, Yehova», sawa vile ilipashwa kusema, kama jina yake wa ebrania ilizimishwa. Hii sauti-bunduki yetu ni munene kupigana Washuhuda ya Yehova.

2) Kwa sababu Mungu mu Agano Jipya anaitwa B a b a, Yesu Kristu mumoja anatuhamuru kumuita na hii jina mu sala yetu: **«Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe.. . » (Matayo 6, 9).** Nikusema, jina yako (Baba) litukuzwe. Hasiseme: «Yehova yetu uliye mbinguni.. . » sawa vile ilipashwa kuandika kama Mungu alitaka kabisa sisi kumuita na jina Yehova!

Lakini namna gani inatakasha jina ya Mungu? Jina ya Mungu «inatakaswa» kama sisi, wenye tunasema ya kama tuko watoto wake, tunakuwa sababu katika uzima ufazili yetu kutukuzwa na kusifiwa Mungu, sawa vile mtoto moja, anayeishi nzuri, anasifu baba yake. Basi, mukristu moja anatakasa jina ya Baba-Mungu, kama anatii amri yote ya Mungu. Vile wanaandika na Washuhuda ya Yehova. Kupindua, kama sisi hatuishi katika amri Wake, hivi tunafanya kibego ao tunachabula ao tunazarau jina ya Mungu. Ya kusema na ma sauti kidogo, Mungu «anatakaswa» (anasifiwa ao anatukuzwa) ao anajichabula, kama sisi tunaishi ao hatuishi katika mapenzi Yake. (Soma mu Matayo 5, 16. Yoano 15, 8 na Barua ya kwanza ya Petro 2, 12 na wa Roma 2, 24) na ma fasi ingine.

Hii shairi» Jina lako litukuzwe» inasharikiwa na shairi: **«Lakini takaseni Kristu kuwa Bwana mioyoni mwenu, mukiwa tayari wakati wote kujibu kila mutu anayeuliza habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole nakuogopa» (barua ya kwanza ya Petro 3, 15).**

3) Onyesho nguvu kabisa ya kama Mungu anataka sisi tumuite B a b a tangu wakati ya kwanza ya dini ya Kristu ni ya kama Roho Mutakatifu mumoja anatufundisha ndani ya ma roho yetu chini kabisa, tusali kwa Mungu na hii jina: **«Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho ya Mungu, hawa ndio wana wa Mungu. Kwa maana hamupokea tena roho ya utumwa inayoleta woga, lakini mulipokea roho ya kufanywa wana, kwa sababu hii tunalia: Aba, Baba» (Wa Roma 8, 14-15). «Lakini kwa sababu ninyi ni wana, Mungu alituma Roho ya Mwana wake katika mioyo yetu, anayelia: Aba, Baba» (Wa Galatia 4, 6).** Basi, hapana Aba (baba) Yehova, lakini Aba, Baba.

4)Agano Jipya inasadiki ya kama iliandikwa daima jina: «Baba»: **«Nina maneno mengi ya kusema na kuhukumu juu yenu; lakini yeye aliyenituma ni mwenye kweli; nami ninasema katika dunia maneno yale niliyoyasikia kwake. Hawakujua ya kama aliwaambia maneno ya Baba» (Yoano 8, 26-27).** Lakini, kama Mungu aliendelea kuitwa Yehova, Mtume Yoano ilipashwa kuandika: « Hawakujua ya kama aliwaambia maneno ya Yehova».

5) Ku mwisho, tunaweza kusema ya kama mu Agano Jipya ilitupatiwa na jina ingine kuliko muzima na ukamilifu na ya kutimizwa: Ni jina: «Baba, Mwana na Roho Mutakatifu». Kwa hii jina nzima, jina ya Mungu wa kweli, Kristu alihamuru wabatizwe waaminifu: **«Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakaitfu.. . » (Matayo 28, 19).**

Basi, sisi tusiitwe kusadiki na kubatizwa kwa jina ya Yehova, lakini kwa jina wa Baba na wa Mwana na wa Roho Mutakatifu. Sasa, Washuhuda ya Yehova, wanataka nini juu ya kusadiki mu imani yetu Waorthodoksi?

## 7. PAKA JINA YA YESU KRISTU INAOKOA

Kisha hii mafundisho yote tuliandika mpaka sasa, inaonekana safi ya kama jina Yakhve hailazimishwe hata kidogo juu ya wokovu wetu. Ao, tunaweza kusema ya kama ustahilivu ya hii jina ni paka ndani ya mafundisho ya Agano la Kale. Kisha ufikisho ya Kristu duniani, paka jina moja inaokoa watu: Ni jina ya Bwana wetu Yesu Kristu na Mwokozi wetu:

1) **«Wala hakuna wokovu katika mwingine (ila tu jina ya Yesu Kristu) kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu waliopewa watu tupate kuokolewa nalo» (Matendo ya Mitume 4, 12).** Na paka hii shairi inenea kuarabisha safi kabisa ma sauti yoyote ya Washuhuda ya Yehova.

2) **«Na kwa jina lake (ya Yesu Kristu) mataifa watatumaini (wokovu wao) (Matayo 12, 21).**

3) **«Anayemwamini hakukumiwi, asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuamini jina la Mwana wa pekee wa Mungu». (Yoano 3, 18) «Anayeamini Mwana ana uzima wa milele; na asiyetii Mwana uzima, lakini gazabu ya Mungu inakaa juu yake» (Yoano 3, 36). «Kweli, kweli, ninawaambia ninyi, Yeye mwenye kuniamini mimi ana uzima wa milele» (Yoano 6, 47) na «Mimi ni mulango; kama mutu ataingia kwa mimi, ataokolewa, na ataingia na kutoka, naye atapata chakula» (Yoano 10, 9).**

**4) «Lakini hizi zimeandikwa mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristu, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake» (Yoano 20, 31) na barua wa kwanza ya Yoano 3, 23).**

**5) «.. . Na ndivyo ilivyopasa Kristu kuteswa na kufufuka toka wafu siku ya tatu. Na maneno ya toba na kusamehe zambi yahubiriwe kwa jina lake katika mataifa yote, kwanza kutoka Yerusalema» (Luka 24, 46-47 na barua ya kwanza ya Yoano 2, 12).**

6) Utakaso na uhaki ya mutu katika neema ya Mungu inakuwa paka «kwa jina» ya Kristu: **«.. . lakini mulioshwa, (toka ma zambi zenu) lakini mulitakashwa, lakini mulihesabiwa kuwa na haki katika j i n a l a B w a n a Y e s u, na katika Roho ya Mungu wetu» (Barua ya kwanza ya waKorinto 6, 11).**

**7) «Yeye aliye na Mwana ni mwenye uzima; lakini yeye asiye na mwana wa Mungu hana uzima» (Barua ya kwanza ya Yoano 5, 12-13).**

**8) Basi, kwa sababu Kristu ni Mwokozi wa pekee, Mtume Paulo anatwaambia: «Na kila kitu munachofanya, katika neno ao katika tendo, fanyeni yote kwa jina la Bwana Yesu, mukishukuru Mungu Baba kwa yeye» (Wa Kolosayi 3, 17).**

## 8. WASHUHUDA YA KRISTU, «WAKRISTU» NA HAPANA «WASHUHUDA YA YEHOVA»

Sauti-bunduki wa kwanza ya Washuhuda ya Yehova, kama watawauliza juu ya jina yao, wanasema ni maneno ya Mungu kwa Watu wa Ebrania, miaka 700 mbele ya Kristu «Ninyi ni washuhuda wangu, Bwana (Yakhve) anasema» (Isaya 43, 10 na 44, 8).

Hii shairi wanasingi Washuhuda ya Yehova ni ya bure kwa sababu, kama toka hii shairi ilitokea jina ya kundi yao, ilipashwa hii jina kubeba watu wa Ebrania ya hile wakati ya Isaya. Lakini taifa wa Ebrania hawakubebe hii jina. Ilipashwa kupitisha wakati ya miaka 2. 650

mupaka kufika mu dunia Yosefu Roderfont (mutawalo wa mbili ya kundi ya Washuhuda ya Yehova) juu ya kuvumbua, mu mwaka 1931, hii jina na ataipatia kwa wafwasi wake.

Kweli, hii jina «Washuhuda ya Yehova», mara ya kwanza iliingia mu Kundi yao mu mwaka 1931, ile wakati walikuwa na makutano moja wakubwa wao mu muji Okhayo ya Amerika. Hii jina inafanishwa ku hawa wenyewe kama «Jina moja mupya».

Lakini, Agano Jipya, inayekuwa na fundisho muzima na ukamilifu ya mapenzi ya Mungu, inasema ma sauti ingine. Kwa sababu Mwokozi wa pekee ni Yesu Kristu na kwa sababu hakuna jina ingine kwa ajili yake tunaweza kuokolewa paka jina ya Yesu Kristu, mwana wa Mungu, kwa hivyo Madiko Takatifu inatuita kuwa na «Washuhuda» ya Kristu na ya Ufufuo wake, na hapana kwa mwingine:

1). Ya kwanza Kristu mumoja aliita waaminifu wote kuwana «washuhuda» Wake: **«Lakini mutapokea nguvu waakti Roho Mutakatifu anapokuja juu yenu, nanyi mutakuwa washuhuda wangu katika Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria hata mupaka wa dunia» (Matendo 1, 8).**

Tusisahau ya kama Mungu-Baba alishuhuda juu ya Mwana wake na alisema kwa watu wote amutii Kwake: «Huyu ni Mwana wangu, mupendwa wangu, ninayependezwa naye; sikieni yeye» (Matayo 17, 5). Basi, sisi tuliitwa kuwa washuhuda ya Kristu na hapana washuhuda ya Yehova. Hivi, hawa watu wanayeitwa «Washuhuda ya Yehova» wanafanya zambi mara wa wili, kwa sababu wanakanyanga amri na ya Baba-Mungu na ya Mwana Wake. Tena, **«Anayeamini Mwana ana uzima wa milele; na asiyetii Mwana uzima, lakini gazabu ya Mungu inakaa juu yake» (Yoano 3, 36).**

2) Kufatana mapenzi ya Mungu Mitume wake wanaita maungo wao «Washuhuda» ya Kristu. (Ona Matendo 2, 32. 3, 15. 5, 30-32. 10, 39-41. 13, 30-31 na barua ya kwanza ya Petro 5, 1). Zamani Kristu amewaita «Washuhuda» ya ma jabo ya Mateso na Ufufuo Wake (Luka 24, 45-48).

Ufananishwa sana ni na mfano ya Mtume Paulo, aliyemuita Kristu kuwa na «mushuhuda wake kwa watu wote. (Matendo 22, 15 na 26, 16).

3) Kuhubiri ya Mitume inaitwa «Ushuhuda ya Yesu Kristu»:

a) Kwa kuhubiri ya Mitume, «Ushuhuda wa Kristu ulivyosibitishwa ndani yenu» (barua ya kwanza ya wa Korinto 1, 6).

b) Mtume Paulo anaandika kwa Timotheo «Usione haya kwa ushuhuda wa Bwana wetu» (Barua ya mbili kwa Timotheo 1, 8).

**c)** Muevangelizaji Yoano alitumwa sawa mutumwa mu Kisanga Patemo ya Grekia: «Nilikuwa katika kisanga kinachoitwa Patemo kwa ajili ya Neno la Mungu na kwa ushuhuda wa Yesu Kristu» (Ufunuo 1, 9).

4) Wale wanakufa kwa imani wanaitwa «Washuhuda» ya Kristu ao wale wanachunga «ushuhuda»=fundisho ya imani ya Yesu. Kwa mfano: Yesu Kristu anatukuza «malaika»=muchungaji ya roho ya Kanisa ya muji Pergamo kumusema kwake: **«.. nawe unashika sana jina langu, wala hukukana imani yangu, hata katika siku za Antipa mushuhuda wangu waminifu, aliyeuawa kati yenu, pahali.. . » (Ufunuo 2, 13). «Nikaona yule mwanamuke amelewa kwa damu ya watakatifu na kwa damu ya washuhuda wa yesu» (Ufunuo 17, 6. T**ena angalia mu sura 6, 9. 12, 17 na 20, 4).

5) Kwa ajili yao inatokea sauti ya mwisho ya kama sisi tuliitwa kuwa na Washuhuda ya Kristu na hapana ya mwingine: **«Basi kila mutu anayenikiri mbele ya watu, nitamukikiri vilevilembele ya Baba yangu aliye mbinguni. Lakini kila mutu atakayenikana mbele ya watu, nitamukana vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni» Na; «Naye anayeona uzima wake ataupoteza; naye anayepoteza uzima wake kwa ajili yangu, atauona» (Matayo 10, 32-33, 39).** 6) «Wakristu»:

Basi, waaminifu hawakuitwa kuwana «Washuhuda ya Yehova», lakini washuhuda ya kristu na Ufufuo Wake. Kwa hivyo, hata mara moja waliitwa «Washuhuda ya Yehova». Toka Madiko Takatifu tunaona ya kama waliitwa «wanafunzi» (Matendo 6, 1), «wenye

waliokolewa»(Matendo 2, 47), «Watakatifu» (matendo 9, 41), «wenye waliitwa» (Wa Roma 1, 7)na barua ya kwanza ya Korinto 1, 2, 24), «Waaminifu»» (Matendo 10, 45) na barua ya mbili ya wa Korinto 6, 15, WaEfeso 1, 1), «Wandugu» (Barua ya kwanza ya wa Korinto 7, 12 na, ku mwisho «Wakristu ao Wakristiani» (Matendo 11, 26 na hii jina ku mwisho ilibakia daima.

Tena hii jina «Wakristu ao Wakristiani». ilibakia tangu wakati ya Mitume tunajua na ma shuhuda ingine:

**a)** Wakati Mtume Paulo alijibu mbele ya mutawalo Filika na mfalme Agripa mu muji Kesaria ya Palestini, ku mwisho mfalme Agripa alisema kwa Paulo: **«Na Agripa alimwaambia Paulo: Kwa maneno machache unazani kunishahishi kuwa Mukristu» (Matendo 26, 28).**

**b)** Mtume Petro alishauria kwa waaminifu hapana kuteswa hata mtu moja katikati yao sawa mwuaji, mwizi ao mutenda mabaya.. . na anasema ku mwisho: **«lakini mutu akiteswa kwa sababu yeye ni Mukristu, asione haya; lakini atukuze Mungu katika jina hili» (Barua ya kwanza ya Petro 4, 15-16).**

«Wakristu», basi, ilikuwa tangu hile waakati wa kwanza jina ya waaminifu na hapana «Washuhuda ya Yehova».

## 9. MITUME NA WATUMISHI WENGINE YA EVANGELION WALITOA YOYOTE NA UZIMA WAO, HAPANA KWA JINA YA «YEHOVA», LAKINI KWA JINA YA KRISTU

Halafu Petro akajibu, akamwambia: **Tazama, sisi tumeacha yote, na kukufuata, sisi tutapata nini basi? Yesu akawaambia: . . . Na kila mutu aliyeacha nyumba, ao ndugu, ao dada wake, ao baba, ao mama, ao watoto, ao mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapewa mara mia na atariti uzima wa milele» (Matayo 19, 27-29).**

2) **«Kama wakinitesa mimi-**anasema Kristu kwa wanafunzi wake-watawatesa ninyi vilevile.. . **lakini maneno haya yote watawafanyia ninyi kwa ajili ya jina langu.. . » (Yoano 15, 20-21).**

3) **«Lakini mbele ya maneno haya yote, watawakamata ninyi na kuwatesa, watawapeleka ninyi mbele ya masunagogi na katika vifungo, mutapelekwa mbele ya wafalme, na maliwali kwa ajili ya jina langu. Lakini yatakuwa ushuhuda kwenu» (Luka 21, 12). «Na mutachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu» (Luka 21, 17).**

4) **Mitume Paulo na Varnava wanaitwa watu wenye kuhatarisha maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana yetu Yesu Kristu» (Matendo 15, 26).** Tena ufananisho ingine ni ya kama, wakati Kristu aliita Mtume Ananias kwa kumukuta mufukuzi wa zamani Paulo (kisha ono mu niia ya muji Damasiki) alimwaambia: **«Kwenda zako; kwa maana mutu huyu ni chombo kichagulifu kwangu, achukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha mambo makubwa mangapi atakayoteswa kwa ajili ya Jina langu. (Matendo 9, 15-16).** Wakati ingine, saa ya hatari Paulo atasema: «Kwani mimi ni tayari si kufungwa tu, lakini kufa katika Yerusalema kwa ajili ya jina la Bwana Yesu» (Matendo 21, 13).

5) Mwisho, wakati Mitume waliteswa na walifukuzwa kwa ajili ya kuhubiri ya Evangelion, **«Wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kama wamestahili kupata mateso kwa ajili ya Jina lake Yesu» (Matendo 5, 41)**. Tazama ilikuwa nani furaha ya Mitume: Ya kama walifukuzwa kwa ajili ya Jina ya Kristu na hapana kwa jina ya Yehova. Basi, Washuhuda ya Yehova haipashwe kujivuna, kama Waaminifu waorthodoksi wanawafukuza toka nyumba yao, wanasadiki ya kama wanafukuzwa sawa vile zamani Mitume ya Kristu.

## 10. KUHUBIRI YA MITUME HAIKUKUWE KWA YEHOVA, LAKINI ILIKUWA KWA JINA YA BWANA WETU YESU KRISTU

Kweli, sawa vile tunaona mu Madiko Takatifu. Mitume na mahubiri wote ya Evangelio walihubiri Bwana Yesu na hapana Yehova (Matendo 2, 14-36. 5, 28, 40-42. 8, 35. 9, 19-22 na 27-28. 11, 20. 17, 2-3 na 18. 18, 5), (Waroma 10, 8-10. barua ya kwanza ya wa Korinto 15, 1-8, barua ya mbili ya wa Korinto 4, 5 na Wagalatia 3, 1) na pa fasi ingine.

1) Mitume, **«na kila siku, ndani ya hekalu, na katika nyumba zao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri Habari Njema ya Yesu Kristu» (Matendo 5, 42).**

2) Tena Mtume Paulo anaandika hivi safi: **«Lakini tunahubiri Kristu aliyesulibiwa, kwa Wayuda na kikwazo, na kwa kwa Wayunani ni upumbafu; lakini kwao wanaoitwa, Wayuda na Wayunani vilevile, ni Kristu nguvu ya Mungu na akili ya Mungu.. . ». «Maana nilikusudia nisijue neno moja katikati yenu, ila Yesu Kristu, naye amesulibiwa» (Barua ya kwanza ya Wakorinto 1, 23-24 na 2, 1-2). «Kwa sababu hatujihubiri sisi wenyewe, lakini Kristu Yesu Bwana.. . » (Barua ya mbili ya wa Korinto 4, 5).**

3) Mtume Paulo anaandika kwa Timotheo**: «Mukumbuke Yesu Kristu, aliyefufuka toka wafu, wa uzao wa Daudi.. . »** kupatana na kuhubiri ya Wamitume kwa ajili yake «katika ile ninapata mateso, hata kufungwa, kama mutenda mabaya.. . ». (Barua ya mbili kwa Timotheo 2, 8).

4) **«Basi ndugu zangu, ninawajulisha ninyi Habari Njema niliyowahubiri ninyi, muliyopokea vilevile, katika hii munasimama, na kwa hii munaokolewa kama ikiwa munashika sana maneno niliyowahubiri, kama isipokuwa muliamini bule. Kwa sababu kwanza niliwapasha ninyi habari za maneno niliyopokea vilevile: ya kwamba Kristu alikufa kwa sababu ya zambi zetu kama maandiko yanayosema.. . » (Barua ya kwanza ya wa Koritno 15, 1-4).**

5) Tena Mitume na kwa kuhubiri yao ya mbali-mbali hawakuhubiri kwa jina ya Yehova. Ona kwa mfano kuhubiri ya Mtume Paulo mu muji Listra ya Likaonia (Matendo 14, 15-17) na mu muji Atene (Matendo 17, 22-31).

6) Mwisho, ni lazima kuandika sisi ya kama hapana paka kuhubiri ilifanyikwa kwa jina ya Yesu Kristu, lakini na miujiza ya Mitume, kwa mfano: Kwa tunzo ya hule mtu wa kilema ya muji Yerusalema Petro alisema kwake: **«Kwa Jina la yesu Kristu wa nazareti, simama utembee» (matendo 3, 6).** Na kwa wale walishangaa kwa tunzo ya mwenye kilema, alisema Petro: **«Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemutia nguvu mutu huyu munayemwona na kumujua: ndiyo imani iliyo katika yeye imemupatia huyu uzima huu mukamilifu mbele yenu yote» (Matendo 3, 16).**

Kisha hii fundisho kwa mambo ya Jina ya Mungu inaonekana safi ya kama jina ya Yehova haikutumiwa hile wakati ya Mitume na Agano Jipya.

## 11. MA SAUTI KUPIGANA YA WASHUHUDA YA YEHOVA

1) Mungu anaonekana kwa Nabii Musa sawa Yakhve (Kutoka 6, 1-3). Nilijibu ku mukongo.

2) «Anasema Yakhve kwa taifa wa Ebrania**: «Ninyi ni washuhuda wangu.. . » (Isaya 43, 10 na 44, 8).** Nilijibu ku mukongo.

3) «Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe» (Matayo 6, 9). Nilijibu ku mukongo.

4) **«Baba.. . nilionyesha jina lako kwa watu wale ulionipa katika dunia.. . Nami niliwajulisha jina lako, na nitalijulisha.. . »; hivi Yesu Kristu anaomba usiku ya utoaji wake (Yoano 17, 6, 26).**

Hii maneno ya Kristu wanaitumia Washuhuda ya Yehova juu ya kusema ya kama kuhubiri ya Kristu ilikuwa juu ya kuonekana jina ya «Yehova». Hii sauti yao ni ya bure, kwa sababu wale walimusikia kuhubiri ya Kristu, walikuwa watu wa Ebrania na walijua tangu zamani «jina» Yakhve. Vile na Washuhuda ya Yehova wanaitika na wanaandika hivi: «Hile wakati Yesu alikuwa pa inchi, jina yake «Yakhve» ilifamiwa». Tena hii «jina», sawa vile na hawa wanasema, iliandikwa ndani ya Madiko yao Matakatifu (Agano la Kale) mara 7000! Hii «jina» ya Mungu Yesu Kristu aliionyesnha kwa watu na namna ya kuachana ilikuwa jina «Baba». Sawa vile inatufundisha Madiko Takatifu, kama sisi tunapokea tendo wa wokovu ya Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, tunakuwa na sisi katika neema «watoto wa Mungu» (Yoano 1, 12 na Wagalatia 4, 5 na Waefeso 1, 5) na Mungu anakuwa Baba wetu. Kwa hivyo Mutume Paulo anasema ya kama Roho Mutakaitfu anatuangaza kwa kumuita Mungu na jina «Baba» (Waroma 8, 14-15 na Wagalatia 4, 6). Hii jina ilikuwa mupya kwa watu wa Ebrania hile wakati.

Ila tu, neno «jina» inaonyesha tena hali ya mtu moja. Kwa mfano:

**a)** Kristu anaonekana Kitabu Ufunuo hivi: «Na ye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, **Mufalme wa wafalme na bwana wa wabwana»** (Ufunuo 19, 16). Ni kweli ya kama haina jina na maana yake kamili, lakini kwa kuonyesha hali Yake sawa Mfalme na Bwana ya ulimwengu.

**b) «Yeye anayepokea nabii kwa sababu ni nabii atapokea zawabu ya nabii, naye anayepokea mwenye haki kwa sababu ni mwenye haki, atapokea zawabu ya mwenye haki. Naye atakayekunywesha mumoja wa hawa wadogo kikombe cha maji tu, hatapoteza zawabu yake hata kidogo» (Matayo 10, 41-42).** Sawa inaonekana huku «jina» haina maana ya jina, lakini inaonyesha hali ya hule mutu (nabii, mwenye haki, mwanafunzi). Paka na hii namna onekano ya «jina» ya Mungu ni maana yake kwa kuonyesha hali Yake ya kama ni Mungu wa pekee kweli na Baba ya watu wote.

Tena «jina» mara mingi inakaa na maana ya utukufu. Kwa mfano:

**a) « Na tujifanyie jina», hii ilikuwa kikomo yao, hile wakati walijenga munara wa Babeli (Mwanzo 11, 4).**

**b) «Daudi akajipatia jina wakati aliporudi toka kupiga Wasuria.. . » (Kitabu ya mbili ya Samweli 8, 13).**

c) **«Ukaonyesha alama ya maajabu juu ya Farao na juu ya watumishi wake.. . » (Nehemia 9, 9-10).**

d) **«Litakuwa kwa Bwana kwa jina, litakuwa alama ya milele isiyokatiliwa mbali» (Isaya 55, 13 na 63, 11-14).**

Ku mwisho, na «jina» tunawaza masheria, matakio, mamlaka na ingine maana na kwa ajili yao inafanyika kitu kimoja. Kwa mfano: «Kwa jina ya sheria ya serkali yetu, mufungulieni; atasema mtu jemadari ya muji moja. Kwa jina ya dini walikuwa ma nvita» ao «kwa jina ya serkali walikuwa.. . », atasema mtu moja.

5). «Yakobo akisema: **Ndugu zangu, munisikilize. Simeoni ametuelezea namna gani Mungu alivyoangalia Mataifa kusudi achagua toka kwao watu kwa jina lake.. . kama ilivyoandikwa.. . ili wana wa watu waliobaki watafute Bwana, na Mataifa yote walioitwa kwa jina langu; anasema Bwana anayefanya maneno haya yote» (Matendo 15, 13-17).** Washuhuda ya Yehova wanajivuna na wanasadiki ya kama hawa ni huu taifa iliyechagua Mungu kusudi alete jina Yake.

Halafu, sawa vile tuliona na ku mukongo, taifa ya Mungu haikuitwe hata mara moja «Washuhuda ya Yehova», lakini iliitwa «Wakristu ao Wakristiani» (Matendo 11, 26) na hii jina ilibakia mpaka sasa. Basi, Wakristu ni mataifa «waliitwa kwa jina langu» na hapana kwa Washuhuda ya yehova. Hii fundisho tena inatuonyesha umungu ya Kristu kwa sababu Kristu

anasharikiwa na Baba-Mungu, «alivyoangalia Mataifa kusudi achagua toka kwao watu kwa jina lake».

Hii sauti anatukikiri na Mtume Paulo mukusema ya kama huyu atachagua taifa kwa jina lake ni Kristu: **«Tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mkubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristu: aliyejitoa mwenyewe kwa ajili yetu atukomboe toka uovu wote, na kujisafishia watu wawe mali yake mwenyewe, wenye bidii sana katika kazi njema» (Tito 2, 13-14).**

Kupindua, jina « Washuhuda ya Yehova» ilikuja duniani mara ya kwanza mu mwaka 1931 ku Yosefu Roderfont na ilijipatia mu kundi yao, lakini mpaka mu mwkaa 1931 walikuwa na jina: «Wasomaji ya Madiko».

6) **«Na itakuwa kila mutu atakayeomba kwa jina la Bwana (Yakhve), ataokolewa» (Yoeli 2, 32 na Matendo 2, 14-21 na wa Roma 10, 13).**

Sawa vile nitaonyesha na kwa sura ya umungu ya Kristu, Wakristu wa kwanza walifata hii unabii, bila kuita jina Yakhve, lakini Jina ya Yesu Kristu; na hii sauti inatuonyesha, ya kama Kristu ni Mungu Yakhve ya Agano la Kale (Matendo 7, 59. 9, 14, 21 na Barua ya kwanza ya wa Korinto 1, 2).

7) Washuhuda ya Yehova wanasingi pa hii shairi: **«Maneno haya anasema yeye Amina, aliye Mushuhuda mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa viumbe vya Mungu» (Ufunuo 3, 14)** wanaambia ya kama Kristu alikuwa «Mushuhuda» wa Yehova.

Lakini Madiko Takatifu inatupatia fundisho ingine sana. Yesu Kristu alipatia ushuhuda kwa Mungu wa kweli: Kwa Baba, kwa Maungo Yake na kwa Roho Mutakatifu. (Ona Yoano 17, 3-4. 14, 6. 8, 12, 18. 14, 26. 15, 26. 16, 13. Matayo 28, 19) Na ma fasi ingine. Hii ufunuo ya Mungu wa kweli sawa Baba, Mwana na Roho Mutakatifu na kazi yote ya Kristu Madiko Takatifu inafananisha «kukiri kwema» aliyeshuhuda Yesu Kristu mbele ya Pontio Pilato. (Barua ya kwanza ya Timotheo 6, 13).

Tena, ila tu, Madiko Takatifu inasema ya kama na Baba mumoja na Roho Mutakatifu mumoja ni «washuhuda» ya Kristu:

**a)** Baba-Mungu ni mushuhuda ya Kristu: «Matayo 3, 17. 17, 5. Barua ya kwanza ya Yoano 5, 9-12 na Yoano 8, 18).

**b)** Roho Mutakatifu ni mushuhuda ya Kristu: «Yoano 15, 26, Matendo 5, 32 na barua ya kwanza ya Yoano 5, 6).

c) Yesu Kristu ni mushuhuda ya maungo yake: (Yoano 8, 14, 18. 11, 25. 14, 6 na 18, 37).

Ni na ma shairi ingine mengi toka Madiko Takatifu inatuonyesha «jina» ya Mungu. Lakini hii fundisho tuliandika mpaka sasa inenea kujibu kwa Washuhuda ya Yehova.

## 12. YAKHVE NI MUNGU WA UTATU MUTAKATIFU

Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama na jina Yakhve Madiko Takatifu inawaza paka Baba-Mungu na hapana Yesu Kristu, (wanamusadiki kiumbe ya Yakhve) na Roho Mutakatifu (wanamusadiki sawa nfuvu moja ya Yakhve). Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama ndani ya Madiko Takatifu ni maonyesha mengi ya kama Yakhve ya Agano la Kale haina paka Baba-Mungu, lakini na Mwana na Roho Mutakatifu; nikusema ni pamoja Utatu Mutakatifu. Lakini ma sehemu ya Umungu ya Yesu Kristu na ya Roho Mutakatifu, kisha hii fundisho nitaandika maonyesho mengi.

Mungu Yakhve, basi, ya Agano la Kale haina paka Mungu, lakini ni na Mwana na Roho Mutakatifu, Utatu Mutakatifu asiyekuachana na aliye na asili moja, Mungu wa kweli mumoja na wa pekee. Mu Agano Jipya Kristu alikombola hii jina (Yakhve) na jina: **«Baba, Mwana na Roho Mutakatifu» (Matayo 28, 19),** kwani huu jina na ma uso tatu inatuonyesha safi kabisa

Utatu Mutakatifu, aliyekuwa na namna siri ndani ya mafundisho ya Agano la Kale na alionekana na nuru kimungu ya Agano Jipya katika Yesu Kristu (Barua ya mbili kwa wa Korinto 3, 14). Kwa hii jina ya Utatu Mutakatifu alihamuru Kristu wanafunzi Wake kuhubiri na kubatiza mataifa yote na hapana kwa jina ya Yehova (Matayo 28, 19).

# 4

# UMUNGU WA KRISTU

## KRISTU NI MUNGU MUKAMILIFU NA MUTU MUKAMILIFU

### MWANZO

Sawa tulisema mpaka sasa Washuhuda ya Yehova wanakataa Mungu ya ma Uso Tatu. Juu ya kufika pale, ililazimishwa wakatale ku mbele umungu ya Yesu Kristu na Roho Mutakatifu. Juu ya Yesu Kristu wanafundisha ya kama alikuwa kiumbe wa kwanza ya Mungu na kwa ajili yake aliumba Mungu viumba vyote. Tena wanasadiki ya kama Yesu Kristu ni malaika Mikhaeli. Kwa sababu wanaona mafundisho yote ya Kristu katika akili ugonjwa wao, hawakusikie Fumbo kubwa ya Ufikisho ya Yesu Kristu duniani na wanachekelea wakritu waorthodoksi sawa wafwasi ya wamungu wingi. Mbele ya kuonyesha umungu ya Yesu Kristu, nitaandika sasa mafundisho ya Yesu Kristu katika theologia orthodokse na theologia wa wokovu:

Sawa vile tunajua, Mungu aliumba mutu «kwa mufano» Wake na makadaza ya mwisho kwa kuwa «katika sura» Yake, nikusema kila mutu eko na makadaza kufika kwa uzima kitakatifu katika neema ya Mungu. Lakini mutu wa kwanza alikanyanga amri ya Mungu na alifukuzwa inje ya paradizo. Matunda ya zambi ya Adamu ilikuwa mabaya, kwa sababu ilikuja uharibifu moja munene ndani ya uzima na akili yake: Ilisimamishwa ushirika katikati ya mutu na Mungu Muumba yake. Tunda ingine mara moja ilikuwa «lufu» ya mutu na utumwa wake kwa shetani na ufwasi wake kwa sheria ya zambi na lufu (Wa Roma 7, 15-24 na Yoano 8, 34 na Mwanzo 2, 17 na 3, 19). Hivi lufu katika zambi ilitawala kwa watu wote (Wa Roma 5, 12) na shetani alikuwa «mkubwa ya hii dunia» (Wa Efeso 6, 12 na Yoano 14, 30).

Ndani ya hii hali ya «kivuli ya lufu» alikuwa mutu miaka ma elfu mengi mukuongojea Mukombozi, aliyeisha kumulaka Mungu kwa Adamu ya kama siku fulani atamutuma (Mwanzo 3, 15). Lakini matunda ya kosa ya watu wa kwanza, ilikuwa munene sana na hakuna mtu mwingine aliweza kumaliza kazi ya wokovu ya watu, paka Mungu mumoja. Kwa hivyo, **«wakati alipomalizwa, Mungu alituma Mwana wake, aliyezaliwa na mwanamuke, aliyezaliwa chini ya sheria, ili awakomboe waliokuwa chini ya sheria, tupate kupokea hali ya wana» (Wa Galatia 4, 4-**5). Mwana wake wa pekee mwenye eko na asili moja na mwanzo moja, ni Uso wa mbili ya Utatu Mutakatifu, chemchem (shina) ya Uzima (Yoano 11, 25. 14, 6). Huyu alikamata mpango kuleta uzima mupya kwa mutu aliyeisha kufa na kutengeneza «sura ya Mungu» aliyeisha kuharibifu na amupatie sura yake wa kwanza.

Kwa sababu watu weko na mwili na damu, kw ahivyo na Mwana wa Mungu, juu ya kumaliza tendo Yake wa wokovu, alichukua na Yeye mwili na damu, bila kusimama kuwa mara moja na Mungu wa kweli: **«Katika mwanzo alikuwa Neno (Yesu Kristu).. na Neno alikuwa Mungu.. . Na Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu» (Yoano 1, 1, 14).** Alifanyika mutu bila kusimama kuwa mara moja na Mungu, juu ya kuweza kufa, **«hata kwa njia ya kufa apate kuharibu yeye aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye Shetani» (Wa Ebrania 2, 14-15). «Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alionekana, ili avunje kazi za Shetani» (Barua ya kwanza ya Yoano 3, 8),** na alivunja matendo ya shetani katika Musalaba na Ufufuo Wake. Kweli, hii uvunjo ya shetani ilimalizwa, wakati Mwana wa Mungu, alifanyika mutu na alikamata mpango

kama **«Kondoo wa Mungu»,** ya kunyanyua zambi zote ya dunia muzima (Yoano 1, 29. Barua ya kwanza ya Petro 2, 24 na barua ya kwanza ya Yoano 3, 5) na kisha alitoa maungo Yake sandaka kwa Baba-Mungu (Wa Efeso 5, 2) **«kwa ajili ya uzima wa dunia» (Yoano 6, 51**. Barua ya kwanza ya Yoano 4, 9). Katika hii sandaka **«alihukumu zambi (ndani yake ilikuwa nguvu ya shetani) katika mwili» (Wa Roma 2, 14),** na katika Damu yake kimungu, **«Yesu, Mwana wake, inatusafisha zambi zote» (Barua ya kwanza ya Yoano 1, 7.** Ufunuo 1, 5 na barua ya kwanza ya Petro 1, 18-19) na hivi alitakasa hali ubinadamu. Tena, katika Ufufuo Wake alishinda lufu, aliharabisha mamlaka na nguvu ya shetani na malaika wake na **«akizishangilia katika musalaba huu» (Wa Kolosayi 2, 15).** Hivi, Kristu, katika Musalaba na Ufufuo Wake alivunja kichwa ya nyoka (shetani) (Mwanzo 3, 15) **na «imenifanyiza huru kwa sheria ya zambi na kufa» (Wa Roma 8, 2).** Ufufuo ya Kristu ni tangu hile wakati mwanzo ya ufufuo ya watu wote ya dunia na itafanyika kwa Ufikisho ya Mbili ya Yesu Kristu. (Barua ya kwanza ya wa Korinto 15, 20).

Katika Musalaba na Ufufuo ya Kristu mutu alikobozwa (Tito 2, 14) na alitakaswa (barua ya kwanza ya wa Korinto 6, 11), alizaliwa mara ya mbili katika roho (Yoano 3, 3-5), alikuwa «kiumbe kipya» (barua ya mbili ya wa Korinto 5, 17), alipata ushirika pamoja na Mungu. (Barua ya mbili ya wa Korinto 13, 13), alikuwa «wenyeji pamoja na watakatifu na watu wa nyumba ya Mungu» (Wa Efeso 2, 19), «na alitufufua pamoja naye na kutukalisha pamoja naye katika pahali pa mbingu, katika Kristu Yesu» (Wa Efeso 2, 6**), «tupate kupokea hali ya wana» toka Mungu (Wa Galatia 4, 5),** tena mutu alikuwa mushiriki wa tabia ya Mungu» (barua ya mbili ya Petro 1, 4) na alifanana na Mungu. (Bartua ya kwanza ya Yoano 3, 2). Tena aliikaa pa hii kiti aliikaa na Yesu Kristu (Ufunuo 3, 21) na atawala pamoja na Yeye kwa milele. Hivi Yesu Kristu katika ufikisho yake duniani katika mwili alikuwa Adamu wa mbili, alimaliza tendo ya Mungu kwa kiumba ya mutu **«kwa mufano na kwa sura»** Wake. Yesu alikuwa mutu wa kweli, mufano mukamilifu na kufatana na sisi,  Mungu katika Ufikisho wake wa mbili atatutukuza na tutakuwa kwa kufanana katika sura ya Mwana Wake. (Wa Roma 8, 29). Hile kitu hasikuweze kuipata Adamu wa kwanza, aliipata Adamu wa Mbili, Yesu Kristu. Hile kitu aliharabisha Adamu wa kwanza kwa ajili ya kosa na majivuno yake, aliitengeneza Adamu wa Mbili Yesu Kristu, katika unyenyekevu na utii wake mpaka lufu Yake. Huyu Adamu wa Mbili, Yesu Kristu, alikuwa mufano ya mutu wa kweli. Kwani Yesu ni pamoja Mungu mukamilifu na mutu mukamilifu anatupatia Mufano mukamilifu ya Baba-Mungu wetu. (Wa Kolosayi 1, 15) na mara moja anatupatia na mufano ya mutu wa kweli. Yesu Kristu pa Uso Yake aliungana hali kimungu na kimutu na alipeleka mutu kwa kifuo ya  Umungu. Huyu alikuwa Mungu katika mwili wetu, bila zambi zetu, juu ya kukuwa sisi watu wabebaji Mungu.

Hii tendo paka Mungu moja ataweza kuimaliza. Paka Mungu ni Uzima na hii Uzima ni dawa ya kufa lufu. Hii unyenyekevu ya Mwana wa Mungu aliyekuja kuchukua mwili mu dunia yetu, bila kusimama kuwapamoja na Mungu, alivumilia matusi, mateso, tena na mauti toka mikono ya watu, wenye Huyu aliwaumba, inaitwa mu lugha ya Madiko **Takatifu «Kuwa hana utukufu» (Wa Filipi 2, 5-8).** Hapana, kwa sababu ilishuka ao ilipotea utukufu ya hali kimungu Yake, lakini, kwani hali kimutu alipokea hii unyenyekevu ukamilifu na hii hali ilikuwa hali kimutu ya Mwana wa Mungu Yesu Kristu. Vile, huyu aliyekufa pa Musalaba na alifufuka kwa wokovu wetu alikuwa Mungu. Pa Musalaba alikufa katika hali kimutu yake, kwa sababu hali kimungu  isiyo na mauti. Kisha Yesu Kristu, katika hali kimutu Yake alipanda, kisha Ufufuo wake, mbinguni, aliingia mu «Vitakatifu ya Watakatifu» ya mbingu, pahali ni Musaidizi katikati ya Mungu na watu, ni **«askofu katika Sheria ya Melkisedeki»** anaomba kwa Baba-Mungu kwa sisi na anatoa wokovu kwa wale wanakuja katika Huyu kwa Mungu. (Wa Ebrania 4, 14. 6, 20. 7, 25. 8, 1-2. 9, 24-26 na ma fasi ingine).

Hii Tendo kubwa ya Yesu Kristu kwa wokovu ya watu wanaivunja Washuhuda ya Yehova, kwa sababu wanakataa hali kimungu ya Mwokozi wetu na wanafundisha ya kama Huyu Mwokozi yetu ni kiumbe ya Mungu, ni mutumwa moja ya Mungu, sawa viumbe vyote vya dunia.

Lakini, kupita nzuri sasa ni lazima kuacha Madiko Takatifu atuonyeshe ni nini Fundisho ya Bwana wetu Yesu Kristu. Washuhuda wa Yehova watasikia ya kama Huyu Yesu Kristu ni Mungu mukamilifu na mutu mukamilifu.

## 1. KRISTU NI MUNGU WA MILELE BILA MWANZO NA MUUMBA YA ULIMWENGU

1) **«Katika mwanzo alikuwa Neno, (Yesu Kristu) na Neno alikuwa pamoja na Mungu na Neno alikuwa Mungu.. . Vitu vyote vilifanyika kwa huyu; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja» (Yoano 1, 1-3).**

**b)** ««Katika mwanzo alikuwa Neno»: Nikusema, wakati ilikuwa mwanzo ya kuumba, Neno «alikuwa». Basi, alikuwa na mbele ya kila wakati na mbele ya kila kuumba. Kwa hivyo Neno-Mungu ( nikusema, Mwana wa Mungu) ni asiyemwanzo, sawa vile ni na Baba-Mungu. Haikukuwe wakati na Neno hasikukuwe. Basi, pasopo mingi: Haipashwe kusema: «katika mwanzo alifanyikwa Neno» sawa vile wanafafanusha Washuhuda ya yehova, lakini tunapashwa kusema: «katika mwanzo ya kuumba Neno alikuwa». Mwana wa Mungu, basi, hasina kiumbe, hasikufanyike, lakini alikuwa. Kupindua, kwa kusema Madiko Takaitfu juu ya viumbe vyote, inatumia sauti: «Kuumba», kwa mufano: «Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia» (Mwanzo 1, 1) na wakati ingine anatumia sauti: Kuzaliwa» kwa mufano: «Mbele Abrahamu hajaliwa, mimi niko» (Yoano 8, 58) anasema Kristu kwa WaYudea. Anatumia sauti «kujaliwa» juu ya Abrahamu, mwenye ni kiumbe, lakini juu ya maungo Yake anatumia sauti «niko», maana yake ni kwa milele.

**b) «Na Neno alikuwa pamoja na Mungu»:** Hii sauti inatuonyesha ya kama Neno ni Uso sawa vile ni na Mungu na alikuwa pamoja na Mungu mbele ya mwanzo.

**c) «Na Neno alikuwa Mungu»:** Nikusema Neno alikuwa na yeye Mungu, sawa vile Baba. Washuhuda ya Yehova wanafafanusha jina: «Mungu» huku na maana hapana ya Mungu wa pekee na wa kweli, lakini na maana ya Mungu wa nguvu, lakini haina hivi. Kwa sababu tunapata ma shairi ingine na maana ya Mungu ni paka maana ya Mungu wa kweli na wa pekee. Kwa mufano: **«Hakuna mutu aliyeona Mungu wakati wo wote» (Yoano 1, 18) na barua ya kwanza ya Yoano 4, 12). «Ni neno la kuogopa kuanguka katrika mikono ya Mungu aliye hai» (Wa Ebrania 10, 31).** Kupindua tunapata ma shairi pahali Kristu anaitwa Mungu sawa: Bwana yangu na Mungu wangu» (Yoano 20, 28), **«Tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mukubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristu» (Tito 2, 13), «Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele» (barua ya kwanza ya Yoano 5, 20).**

**d)** Vitu vyote vilifanyika kwa huyu; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja» : Nikusema vitu vyote hakikufanyika kwa ajili yake na bila Huyu hasikufanyike kiumbe kimoja. Basi, Huyu (Yesu Kristu» hasina kiumbe, hasikuumbwa. Kwa hivyo Huyu ni asiye na mwanzo na hasiye kuumbwa na wa milele pamoja na Mungu-Baba.

Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama Neno ya Mungu (Yesu Kristu) ni kidogo cheni mbele Yake (Mungu-Baba) kwa sababu Madiko Takatifu anaandika: «kwa huyu», nikusema, katika ufafanusho ya Washuhuda ya Yehova, Yesu Kristu ni chombo moja pa mikono ya Mungu-Baba juu ya kuumba «kwa Huyu» dunia. Halafu neno: «Kwa» hakuna namna kushusha Neno (Yesu Kristu) mbele ya Mungu-Baba, kwa sababu hii neno inatumiwa na kwa jina ya Mungu-Baba. Kwa mufano: **«Mungu ni mwaminifu muliyeitwa naye katika ushirika wa mwana wake Yesu Kristu Bwana wetu» (Barua ya kwanza ya WaKorinto 1, 9).** Hapa Mungu-Baba ni kidogo chini mbele ya Mwana wake na anaonekana sawa chombo moja pa mikono ya Mwana wake? Hapana, hapana! Kupindua ni na ma shairi ingine pahali Madiko Takatifu inasema juu ya Neno Muumba

bila neno «Kwa ao katika». Kwa mufano: **«Wewe Bwana, katika mwanzo umeweka misingi ya inchi, na mbingu ni kazi za mikono yako» (Wa Ebrania 1, 10).** Mtume Paulo anasema huku juu ya Mwana. Hasiseme, basi, «Uliweka misingi ya inchi», lakini «wewe umeweka misingi ya inchi».

**e)** Ku mwisho Mwana wa Mungu anaitwa «Neno» kwa sababu alizaliwa bila mwanzo na bila zambi toka asili ya Mungu-Baba (sawa vile inazaliwa neno toka akili ya mutu) na kwa sababu anatuwambia mapenzi ya Baba, mwenye ni Chemchem (shina)ya Utatu Mutakatifu.

2) Kristu ni **«Mufano wa Mungu asiyeonakana, muzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo duniani, vitu vinavyoonekana na visivyoonekana, .. . vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake.. . Naye ni mbele ya vitu vyote.. . » (Wa Kolosayi 1, 15-17).**

Pasopo: Madiko inasema: «Muzaliwa wa kwanza» na hapana «Kiumba wa kwanza», sawa vile wanataka kufafanusha hivi Washuhuda ya Yehova. Uchanisho ni munene. Muzaliwa wa kwanza anaitwa huyu anayezaliwa toka asili ya Muzazi. Lakini **«Kiumba wa kwanza ni kiumbe inayeumbwa ya kwanza. Kama Muzaliwa wa kwanza ni maana yake kiumbe wa kwanza, kisha vile viumbe wanafata inapashwa kuitwa «wazaliwa wa mbili», «wazaliwa wa tatu» wana wa Mungu, lakini sisi tunajua ya kama «Muzaliwa wa kwanza» Mwana wa Mungu (Wa Ebrania 1, 6) ni pamoja na «Wa pekee» (Yoano 1, 18.** 3, 16). Basi, maana ya neno «muzaliwa wa kwanza» haina na ungano na neno «kiumba wa kwanza». Sauti: «**Muzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote»** ni maana yake: Aliyezaliwa (toka Mungu -Baba) mbele ya viumbe vyote. Huyu ni Muzaliwa wa kwanza ya viumbe vyote kwa sababu Huyu aliumba vitu vyote na Huyu ni mbele ya vitu vyote, asiye na mwanzo na wa milele pamoja na Baba.

3) **«Wewe Bwana, katika mwanzo umeweka misingi ya inchi, na mbingu ni kazi za mikono yako. Hizi zitaharibika, lakini wewe unabaki; na hizi zote zitachakaa kama nguo, na kama mavazi utabadilika; lakini wewe ni sawasawa saa zote, na miaka yako haitakoma» (Wa Ebrania 1, 10-12**). Paka Mungu Muumba anabaki asiye harabika na wa milele kupatana na shairi ya «Malaki 3, 6 na Yakobo 1, 17). Kwa hivyo na Neno-Mungu kwa huyu inaandikwa hii maneno, ni Mungu wa kweli.

4) Mu Kitabu Mezali, «Hekima» wa Mungu ni Mwana wa Mungu (Barua ya kwanza ya Wa Koritno 1, 24), na anasema juu ya maungo Yake: **«Bwana (Baba Mungu) alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, mbele ya kazi zake za zamani.. . wakati alipoweka mbingu nilikuwa pale.. . halafu nilikuwa pamoja naye, kama fundi la kazi.. . » (Mezali 22-30).**

Mwana-Hekima wa Mungu, basi, alikuwa «mbele za kazi zake wa zamani». «Katika mwanzo wa njia yake» (nikusema ku mwanzo ya Kuumba) alikuwa pamoja na Mungu. (Ona na Yoano 1, 1).

## 2. MWANA NI ASIYE MWANZO, WA MILELE NA ASIYE UHARIBIFU, SAWA MUNGU-BABA

1) Asiye na mwanzo:

**a) «Katika mwanzo alikuwa Neno» (Yoano 1, 1).** Nikusema, wakati ilikuwa mwanzo ya kuumba, Neno alikuwa wa zamani. Basi, alikuwa mbele ya kila mwanzo,

nikusema Huyu ni asiye mwanzo. «Naye ni mbele ya vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake» (Wa Kolosayi 1, 17).

**b)** Malkisedeki ni mufano-alama ya Askofu mkubwa Yesu Kristu na anaandikwa mu Madiko Takatifu kuwa «hana baba, wala mama, wala wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, lakini anafananishwa na Mwana wa Mungu» (Wa Ebrania 7, 3). Hii tangazo ni safi kabisa: Mwana wa Mungu hana na mwanzo, wala mwisho ya uzima zake, nikusema yeye ni asiye mwanzo na wa milele.

**c)** Kupatana na Mungu-Baba Madiko Takatifu haiandike ya kama ni pasipo mwanzo. Lakini sisi tunapata na namna wa pempeni. Sawa kwa mfano: «Mungu atasikia na kuwajibu, hata yeye anayekaa tangu milele. watu wasiogeuka, wala wasioogopa Mungu» na: **«Mbele ya kuzaliwa kwa milima, wala hujaumba bado inchi na ulimwengu, tangu milele hata milele wewe ni Mungu» (Zaburi 55, 19 na zaburi 90, 2).**

Hii fundisho tunapashwa sisi kutosha na kwa Mwana Yesu. Nikusema, kama Mungu-Baba ni asiye mwanzo, kwa sababu ni mbele ya milele, vile na Mwana **«kwa yeye alimufanya ulimwengu» (Wa Ebrania 1, 20) na tena Huyu «ni mbele ya vitu vyote» (Wa Kolosayi 1, 17) inapashwa kuwa asiye na mwanzo.**

2) Wa milele na asiye uharibifu:

a) **«Bwana (Baba Mungu) alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, mbele ya kazi zake za zamani.. . » (Mezali 8, 22).**

b) **« Lakini wewe ni sawasawa saa zote, na miaka yako haitakoma» (Wa Ebrania 1, 12).**

c) **«Yesu Kristu ni sawasawa, jana, leo na hata milele» (Wa Ebrania 13, 8). Lakini asiye uharibifu ni paka Mungu (Yakobo 1, 17. Wa Malaki 3, 6 na WaRoma 1, 23).**

## 3. KRISTU NI MUNGU WA KWELI

1) **« Bwana yangu na Mungu wangu»,** anasema Toma kwa Kristu aliyefufua, wakati alimuita kwa kupapasa mikono na ugambo Yake kusudi kuamini ya kama alifufuka toka wafu (Yoano 20, 28). Lakini **«Bwana na Mungu wetu» ni paka moja na wa pekee Mungu wa kweli (Kumbukumbu la Torati 6, 4-5 na Matayo 22, 37).**

Kama Kristu alikuwa kiumbe, haipashwe kupokea hii sauti ya Toma, kwani hii sauti inaikaa paka kwa Mungu. Lakini, kwa sababu Yesu alipokea hii sauti ya mtume Toma «Bwana yangu na Mungu wangu», inatuonyesha ya kama Yesu Kristu alikuwa kweli Bwana na Mungu wetu. Lakini Washuhuda ya Yehova watafuata siku fulani Mtume Toma na watakikiri Yesu Kristu sawa Mungu wao?

2) Kwa sababu Kristu alihubiri maungo Yake Bwana na Mungu, kwa hivyo taifa ya Yuda walitafuta kumuua na mawe mukusema kwake: **«Kwa kazi njema hatukupigi kwa mawe, ila kwa matukano, na kwa sababu wewe uliye mutu, unajifanyiza mwenyewe kuwa Mungu» (Yoano 10, 33).**

3) Mtume Paulo mu barua yake kwa Waroma anasema kwa WaIsraeli toka yao alizaliwa **«katika hawa alitoka Kristu kwa namna ya mwili, aliye juu ya maneno yote, Mungu mubarikiwa kwa milele» (Wa Roma 9, 4-5).**

Kristu ni **«aliye juu ya maneno yote, Mungu mubarikiwa kwa milele», na hapana «aliyekuwa juu ya maneno yote Mungu.. . »** kama alikuwa kiumbe. Hii sauti: **«aliye juu ya maneno yote.. . »** inashariki Mwana katika hali kimungu pamoja na Mungu-Baba, kwani na Huyu anasharikwa na hii sauti (na mu wa Efeso 4, 6). Lakini na sauti: «Mubarikiwa kwa milele» inamushariki tena na kwa kimungu yake pamoja na Mungu-

Baba, anayefananishwa mara ingine na hii namna (Barua wa mbili ya wa Korinto 11, 31. Wa Roma 1, 25 na Marko 14, 61).

Hii shairi inatuonyesha ya kama Kristu ni Mungu na mutu pamoja. Huyu «aliye juu ya maneno yote, Mungu mubarikiwa kwa milele», alizaliwa toka uzao ya Wa Izraeli katika mwili, nikusema katika hali kimutu Yake. Ya kwanza ni «aliye juu ya maneno yote» na ya mbili Huyu alizaliwa kama mutu toka uzao ya WaIsraeli.

4) **«Hata mumoja wa watawala wa dunia hii hakuijua: kwa sababu kama wangalijua wasingasulibisha Bwana wa utukufu» (Barua ya mbili kwa Wa Korinto 2, 8).** Lakini «Bwana wa utukufu» ni paka Mungu wa kweli (Matendo 7, 2: **«Ili Mungu wa Baba wetu Yesu Kristu, Baba ya utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufufuo katika kumujua yeye» (Wa Efeso 1, 17. Zaburi 24, 7-10).** Kwa hivyo, «Bwana wa utukufu» waliyemusulibisha hasikukuwe mwingine paka Mungu wa kweli.

5) **«Tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mkubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristu» (Tito 2, 13).** Kweli, paka moja ni Mungu mukubwa na hapa anasharikiwa na Yesu Kristu.

6) **«Nasi tunajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa sisi ili tumujue yeye aliye wa kweli, nasi tuko ndani yake yeye aliye wa kweli, ndani ya Mwana wake Yesu Kristu. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele». (Barua ya kwanza ya Yoano 5, 20).**

Basi, Mwana wa Mungu, ni hapana paka : Mungu wa kweli», lakini na «uzima wa milele» na hii sauti inaandika mara mingi Madiko Takatifu (barua ya kwanza ya Yoano 1, 1-2. 5, 11-12). Lakini paka Mungu wa kweli ni Chemchem ya Uzima.

**7) «Maana katika yeye unakaa, utimilifu wote wa Mungu kwa mwili» (Wa Kolosayi 2, 9).** Nikusema, ndani ya Kristu inakaa kweli umungu muzima ndani ya mwili yake. Lakini namna gani iko namna Mungu asiye mupaka aikae muzima ndani ya mwili ya mutu-Kristu? Hii iko namna kufanyika kama Mungu, (bila kusimama kuwa Mungu) atachukua tena na hali kimutu. Kweli, hii tendo ilifanyika. Neno-Mungu alikuwa mwili, nikusema mutu (Yoano 1, 14), sawa vile inatwaambia Madiko Takatifu. Hii inatuonyesha ya kama hii mwili (nikusema mutu-Kristu) haikukuwe uso ingine, lakini ilikuwa Huyu Neno-Mungu mumoja katika mwili. Kwa hivyo, hali kimungu ya Neno Yesu Kristu ilikuwa na hali kimungu ya mutu-Kristu. Paka katika hii maana iko namna kuikaa ndani ya mutu-Kristu na kutumika pamoja na hali kimungu muzima.

Lakini na Mtume Paulo anatimiza: **«Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kupatanisha vitu vyote kwake, akiwa amefanya salama kwa njia ya damu ya musalaba wake, kwa yeye, kama ni vitu duniani ao vitu mbinguni» (Wa Kolosayi 1, 19-20). Nikusema** Mungu aliyekuwa katika Kristu alipatanisha vitu vyote na Maungo Yake. (Hapa maana yake ni hii upatanisho ilifanyika katikati ya Mungu na mutu, iliyemalizwa kwa sandaka pa Musalaba ya Kristu). Lakini, kwa sababu Kristu hasikukuwe Uso moja ingine, lakini alikuwa Neno-Mungu katika mwili, hii sauti: «alipatanisha vitu vyote kwake» inaonyesha ya kama Neno-Mungu anasharikiwa pamoja na Mungu katika hali kimungu. Kwa sababu, juu ya kupatanisha watu pamoja na maugo Yake, inatuonyesha ya kama Huyu alikuwa mumoja Mungu na sisi mbele yake tulikuwa wakosefu. (Sawa vile tunajua, sisi tulikosa hapana mbele ya kiumbe moja ya dunia, lakini kupigana ya Mungu mumoja na Muumba wetu). Basi, Kristu kwani ni Neno-Mungu, ni pamoja na wa asili moja pamoja na Mungu-Baba, Mungu mukamilifu na mutu mukamilifu. (Ona tena na barua ya mbili ya wa Korinto 5, 19): «Mungu alikuwa ndani ya Kristu, akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe»).

Pa hii fasi tunaweza kuandika na maneno ya Mwandishi ya Kitabu Mezali, anayeandika ya kama: **«Fundisha mwenye hekima (nikusema Mwana wa Mungu), naye atazidi kuwa na hekima» (Mezali 9, 9),** maana ni mwili ubinadamu iliyechukua, wakati alikuja duniani juu ya kuikaa ndani ya hii mwili. Basi, **«utimilifu wote wa Mungu»** (Wa Kolosayi 2, 9) aliyeikaa ndani ya mwili ubinadamu ya Kristu, haina kitu kingine paka Hekima-Mwana wa Mungu. Basi, Hekima-Kristu= «utimilifu wote wa Mungu». Nikusema Kristu anasharikiwa na umungu muzima.

8) Maneno ingine ya Kristu mu kitabu Ufunuo wanaandika, bila shaka, ya kama Huyu ni Mungu wa kweli: **a) «Tazama anakuja (Kristu) na mawingu; na kila jicho litamwona, nawale waliomuchoma; na mataifa yote ya dunia wataomboleza kwa aili yake. Ndiyo. Amina. Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, anasema Bwana Mungu, yeye aliye sasa, na aliyekuwa na atakayekuja, Mwenyezi» (Ufunuo 1, 7-8).**

b) **«Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho» (Ufunuo 21, 6).**

**c) «Tazama, ninakuja upesi na mushahara wangu ni pamoja nami, kulipa kila mutu kama ilivyo kazi yake. Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho» (Ufunuo 22, 12-13).**

**d) «Usiogope, mimi ni wa kwanza na wa mwisho; na aliye hai; nami nilikuwa nimekufa, na tazama, mimi ni hai hata milele na milele. Nami nina funguo za mauti, na za Hadeze» (Ufunuo 1, 17-18).**

Ma sauti «(Huyu) atakayekuja», «Tazama ninakuja upesi», na «nami nilikuwa nimekufa» wanatuonyesha ya kama hii ma shairi wanasema juu ya Bwana Yesu Kristu. Basi, Kristu ni Huyu mumoja «Bwana Mungu, Mwenyezi».

Tena, **«Maneno haya anasema yeye aliye mutakatifu, aliye wa kweli.. . » (Ufunuo 3, 7), lakini «Mutakatifu na aliye wa kweli» ni paka Mungu «Ufunuo 6, 9-10).**

9) Ufunuo inamuita tena: «**Bwana wa bwana na mufalme wa wafalme» (17, 14 na 19, 16). Lakini Bwana wabwana ni paka Mungu (Danieli 2, 47 na barua ya kwanza kwa Timotheo 6, 15).**

10) Mu Kitabu Ufunuo ya mtume Yoano iko na ushuhuda ingine nguvu: «Akaniambia (malaika): Maneno haya ni amini na kweli. Na Bwana Mungu, wa manabii watakatifu alituma malaika yake kuonyesha watumishi wake mambo yaliyopaswa kuwa upesi.. . Mimi, Yesu nimetuma malaika yangu kuwashuhudia ninyi mambo haya katrika makanisa.. . » (22, 6 na 16). Yesu anasharikiwa pamoja na «Bwana Mungu wa manabii watakatifu», na Yehova-Mungu.

11) «Mujiangalie wenyewe, na kundi lote, Roho Mutakatifu alilowapa ninyi kuwa wasimamishi ndani yake mupate kulisha kanisa la Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe (nikusema Hii Kanisa Mungu alijenga na Damu Yake) » (Matendo 20, 28). Basi, damu iliyemwangishwa pa Musalaba ilikuwa Damu ya Mungu mumoja. Mutu-Kristu, basi, alikuwa Mungu «katika mwili».

12) **«Na pasipo shaka, siri ya utawa ni kubwa: Mungu alionekana katika mwili.. . » (Barua ya kwanza kwa Timotheo 3, 16).** Washuhuda ya Yehova wanakataa hii shairi.

13) Ku mwisho, kupatana na madiko Takatifu, Muhukumu mu Ufikisho wa Mbili atakuwa Kristu na hapana Baba-Mungu: **a) «Maana Baba hamuhukumu, hata mutu mumoja, lakini amemupa Bwana hukumu yote» (Yoano 5, 22). b)** Evangelio ya Hukumu wa

Mwisho (Matayo 25, 31-46). **c) «Kwa sababu sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu» (Wa Roma 14, 10).**

Pempeni lakini, anaandika ya kama: **«Basi, kwa hii mumoja wetu atatoa habari zake mwenyewe mbele ya Mungu» (Wa Roma 14, 12).** Nikusema, Mungu-Muhukumu anasharikiwa na Kristu-Muhukumu.

## 4. KRISTU NI SAWA-SAWA NA MUNGU-BABA

1) «Filipo akamwambia (kwa Kristu): **Bwana, utuonyeshe Baba, basi inatufaa. Yesu akamwambia: Nimekuwa pamoja nanyi wakati gani unasema: Utuonyesha Baba? (Yoano 14, 8-9).** Nikusema, hule aliyeniona mimi, aliona Baba-Mungu.

Hii ushuhuda juu ya kutuonyesha sawasawa katikati ya Mwana wa Mungu na Baba-Mungu ni nguvu kabisa. Kwa sababu, paka kama Kristu ni Mungu sawasawa na wa asili moja na Baba-Mungu hii ma shairi ni wa kweli sana. Kama Kristu hasikukuwe sawasawa pamoja na Baba-Mungu, hii shairi itakuwa chabula kupigana ya Mungu, kwa sababu namna gani kiumbe moja atashariki maungo yake na Mungu wa milele na asiye mupaka?

2) **«Basi kwa sababu hii Wayuda wakazidi kutaka kumwua (Kristu), si kwa sababu alivunja sabato tu, lakini tena kwa sababu aliita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu» (Yoano 5, 18).**

Vile, Kristu alihubiri safi ya kama alikuwa sawasawa na Baba-Mungu na hii mambo ilileta kisilani ya Wayuda. Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama hii maneno ni mashuhuda ya wogo ya Wayuda juu ya kumuhukumu Kristu. Lakini, kama ni vile, juu ya nini Kristu alipokea ma sauti yao ya kumushitaki?

3) Kwa ajili ya hii usawa katikati ya Mungu-Baba na Mwana wake, Mungu-Baba anasema **«Ili watu wote waheshimu Mwana kama wanavyoheshimu Baba» (Yoano 5, 23).** Lakini paka kama Kristu ni Mungu wa asili moja pamoja na Baba iko namna kuheshimiwa na usawa moja pamoja Naye. Viumbe hakuna namna kuheshimiwa sawa anaheshimiwa Baba.

4) «Mimi ni Baba yangu ni mumoja.. . Baba ni ndani yangu, nami ni ndani ya Baba» (Yoano 10, 30, 38). Washuhuda ya Yehova wanakataa ya kama Kristu aliwaza usawa na ushariki pamoja na Mungu-Baba na na wanafafanusha na namna ingine hii shairi. Lakini, sawa vile sisi tunaona watu wa Ebrania walisadiki maana ya hii shairi na walikamata mawe kwa kumupiga Kristu sawa mutu mubaya, bila Kristu kuwaelejea maneno Yake.

5) **«Lakini wakati anapokuja yule Roho ya Kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli: kwa sababu hatasema kwa mamlaka yake mwenyewe; lakini maneno yote anayosikia atayasema; naye atawatangazia ninyi habari za maneno yatakayokuja. Atanitukuza mimi, kwa sababu atatwaa katika yaliyo yangu na kuwaambia ninyi. Yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa sababu ya maneno haya nilisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu na kuwaambia ninyi» (Yoano 16, 13-15).**

Hii ushuhuda ya Kristu ni bunduki wa nguvu kupigana ya Washuhuda ya Yehova. Hapa Kristu anatuonyesha ya kama kila kitu ni kwa Baba na na Yake; hii inatuonyesha ya kama katikati yao ni usawa umoja. Tena na Roho Mutakatifu juu ya kusema na kufundisha watu anachukua, (sawa inasema andiko) toka Kristu. Na, kama, kupatana na Imani Orthodokse, Roho Mutakatifu ni Uso wa tatu ya Utatu Mutakatifu, maneno ya Kristu

inatuonyesha ushariki na umoja usawa kwa hali kimungu, katikati ya Baba, Bwana na Roho Mutakatifu. Lakini, kama Kristu ni kiumbe na Roho Mutakatifu ni «nguvu ya Mungu» sawa vile hivi wanasadiki Washuhuda ya Yehova, namna gani iko namna Mungu atachukua matangazo toka kiumbe moja juu ya kusema na kufundisha watu? Hii haina matusi mbele ya Mungu? Washuhuda ya Yehova wanasema nini? Ao, wanapashwa kuamini hali kimungu na wa asili moja katikati ya Baba, Mwana na Roho Mutakatifu ao inapashwa kuitika ya kama Mungu anachukua ma tangazo toka kiumbe kimoja kwa kusema na kufundisha watu. Wakati ingine Kristu anasema mara ingine: «Na wote walio wangu ni wako, naalio eako ni wangu, nami nimetukuzwa ndani yao» (Yoano 17, 10). Basi, yote ni yaliyo na wao katikati Baba na mwana, basi na hali kimungu. Basi, katikati yao ni usawa umoja.

6) **«Muwe na nia hii ndani yenu iliyokuwa ndani ya Kristu Yesu vilevile; ndiye aliyekuwa na namna ya Mungu, hakuona kuwa sawa na Mungu kuwa kitu kushikamana nacho, lakini alijifanya mwenyewe kuwa hana utukufu, akitwaa namna ya mutumwa, akakuwa na mufano wa mutu; na akionekana na sura ya mutu, alijinyenyekeza mwenyewe, akakuwa mwenye kutii hata mauti, ndidyo mauti ya musalaba» (Wafilipi 2, 5-8).**

Nikusema, katikati yenu ninamitakia, kuwa unyenyekevu sawa vile ilikuwa na kwa Kristu, aliyekuwa pa fasi moja ya utukufu na Mungu-Baba wake, lakini hasikushake kwa wokovu wetu kuwa hana utukufu na alikuwa mutu na alikufa pa Musalaba kwa ajili yetu. Washuhuda ya Yehova, wanafafanusha hii shairi na namna ingine na wanasema: Hasikutakie kuwa sawasawa na Mungu-Baba kuwa kitu kushikamana nacho». Lakini hivi ilipashwa kusema shairi: «.. . Hakuona (kufanyika) sawa Mungu», lakini shairi wa kweli ni: «hakuona kuwa sawa na Mungu.. »

Tena Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama Hii sauti ya shairi: Kuwa sawa na Mungu.. » haina maana yake ya kama alikuwa Mungu wa kweli, lakini ya kama alichukua mufano kimungu. Kama ni vile, katika akili ya Washuhuda ya Yehova, na hii sauti: «akitwaa namna ya mutumwa» haipashwe kuwa na maana ya kama Kristu alichukua mwili kweli ya mutu. Halafu, sawa hii sauti: «akitwaa namna ya mutumwa» inaonyesha maana ya kama alikuwa mutu wa kweli, vile na hii shairi: «kuwa sawa na Mungu» inapashwa kuonyesha maana ya kama alikuwa Mungu wa kweli.

7) **«Nimepewa vitu vyote na baba yangu, wala hakuna mutu anayejua Mwana, ila Baba; . . » (Matayo 11, 27).** Kwani ni wa pekee anayejua Baba-Mungu hii inatuonyesha maana ya kama ni na Huyu Mwana, Mungu wa kweli, sawa vile Baba ni sawasawa Naye. Kwa sababu paka Mungu moja mukamilifu, na usawa moja na Baba-Mungu, anaweza kujua baba-Mungu.

Hivi inasemwa na ya Roho Mutakatifu: **«Kwa sababu nani katikati ya watu anayejua maneno ya mutu, ila roho ya mutu iliyo ndani yake? Hivi kwa maneno ya Mungu hakuna mutu anayeyafahamu ila Roho ya Mungu» (barua ya kwanza ya wa Korinto 2, 11).** Sawa vile Roho Mutakatifu anamufamia Mungu, vile na Mwana anamufamia. Lakini paka, kama ni ma Uso matakatifu na wa asili moja na usawa moja iko namna kufamiana.

Tena umoja hii na hii shairi: «Si kwamba mutu aliona Baba ila yeye aliyetoka kwa Mungu, yeye ndiye aliyeona Baba» (Yoano 6, 46). Paka Mungu moja anaweza kuona Mungu. Kristu, kwani ni wa pekee anayemuona kamili katika hali kimungu Yake, anapashwa kuwa sawasawa na Ye na asili umoja na Ye.

## 5. KRISTU NI WA ASILI MOJA NA MUNGU-BABA

1) **«Wewe ndiwe Mwana wangu, mimi leo nimekuzaa», anasema Baba kwa Mwana (Wa Ebrania 2, 5 na Zaburi 2, 7).** Neno: «Nimekuzaa» inaonyesha asili umoja ya Baba na ya Mwana, lakini neno: «leo» inaonyesha ya kama uzalio yake ilikuwa bila na inje ya wakati na uzalio Yake ni wa milele. Mungu anaishi yulu na inje ya nyakati, kwa hivyo neno «leo»
kwa Kungu inaonyesha ya kama Mungu ni na wa zamani na wa sasa na ku mbele Mumoja, kwani ni inje ya wakati. Nikusema, kwa sababu Mungu-Baba ni wa milele na uzalio ya Mwana toka Baba ni bila mwanzo na bila wakati. Nikusema tangu hile wakati eko Mungu-Baba, eko na Mwana mwake aliyezaliwa toka Baba na namna bila kuisikia na bila wakati ya hii dunia.

2) **Hakuna mutu aliyeona Mungu wakati wo wote; Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemufunua» (Yoano 1, 18).** Shairi hii: «Mwana wa pekee» inaonyesha safi asili umoja pamoja na Baba na Mwana. Kwa sababu, kama Mwana alikuwa kiumbe, hakuna namna kuwa «wa pekee», kwa sababu viumbe vyote ilikuwa namna kuwa «wana» wa Mungu. Lakini, ni kweli ya kama malaika na waaminifu wanaitwa wana wa Mungu, lakini ni wana katika neema, « tupate kupokea hali ya wana» (Wa Galatia 4, 5). Paka Kristu ni Mwana wa kweli ya Mungu, na kwa hivyo ni «wa pekee». Ku mwisho, neno: «aliye katika kifuo cha Baba» inatuonyesha uzima wa milele ya Mwana wa Mungu, kwani haikukuwe wakati na Mwana wa Mungu hasikukuwe ndani ya kifua ya Mungu-Baba wake.

3). Kristu tena anaitwa: **«Yeye akiwa kungaa kwa utukufu wake(ya Mungu), na chapa ya nafsi yake mwenyewe.. . » (Wa Ebrania 1, 3).** Nikusema, (Mwana) ni kungaa wa milele ya utukufu ya Mungu na chapa nzima ya asili ya Baba-Mungu.

Sawa vile nuru ya jua inazaliwa toka asili ya sahani ya jua na iko pamoja na Jua, vile na Mwana Yesu anazaliwa toka asili ya Baba wake inje ya wakati (kwani Mungu ni asiye na wakati) na ni pamoja na Mungu kwa milele. Sawa «chapa ya nafsi yake mwenyewe» ya Mungu, Kristu ni chapa muzima, bila uchanisho na bila geuza, ya Mungu-Baba, basi, ni Mungu mukamilifu, sawa na Baba-Mungu ni mukamilifu.

4) **«Mimi na Baba yangu ni mumoja» (Yoano 10, 30). «Aliyeniona mimi, ameona Baba» (Yoano 14, 9)** sawa vile tulisema ku mukongo. Hii maneno yote inatuonyesha asili umoja katikati ya Baba na Mwana wake wa pekee.

## 6. KRISTU NI KWELI KAMILI, UZIMA NA NURU

**1) «Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima» (Yoano 14, 6) «Mimi ni ufufuko na uzima» (Yoano 11, 25); «Neno lililokuwa tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama na kulipapasa kwa mikono yetu, kwa habari za Neno la uzima; na uzima ulifunuliwa, nasi tumeona, na tukashuhudia, tukahubiri kwenu ule uzima wa milele, uliokuwa kwa baba, ukaonekana kwetu; » (barua ya kwanza ya Yoano 1, 1-2)** (Ona na barua ya kwanza ya Yoano 3, 20, pahali Kristu anaitwa «Mungu wa kweli», na Ufufnuo 3, 7 na 19, 11 pahali Kristu anaitwa «wa kweli».

Ma neno «kweli» na «uzima» iko nayo maana ukamilifu. Hakuna namna kiumbe moja kuwa uzima na wa kweli, lakini paka Mungu (Yoano 7, 28. 17, 3. Ufunuo 6, 10) na

pa fasi ingine. Tena hakuna namna kiumbe moja kuwa uzima, lakini ni paka Mungu (Ufunuo 4, 9, 10).

**2) «Mimi ni nuru ya dunia; yeye anayenifuata hatakwenda kwa giza kabisa, lakini atakuwa na nuru ya uzima» (Yoano 8, 12). Kristu «ilikuwa nuru ya kweli inayotia nuru kila mutu anayekuja katika ulimwengu» (Yoano 1, 9).**

Lakini Madiko Takatifu inatufunua pa fasi ingine ya kama, «Mungu ni nuru, wala giza si ndani yake kabisa» (barua ya kwanza ya Yoano 1, 5) na barua ya kwanza kwa Timotheo6, 16). Basi, Kristu-Nuru anasharikiwa mara ingine na Mungu-Nuru.

## 7. KRISTU ANAJUA ROHO YA MTU, NI PA FASI YOTE, NI «MTAKATIFU» NA «MWENYE HAKI»

1) Anajua roho ya mtu:

a) **«Na kwa sababu hakuhitaji mutu hata mumoja kushuhudia habari za mutu; kwa sababu yeye mwenyewe alijua yaliyo ndani ya watu» (Yoano 2, 25).**

b) **«Yesu akijua mafikili yao akasema: .. . » (Matayo 9, 4. Yoano 6, 61, 64. Matayo 16, 8. Marko 2, 60) na ma fasi ingine.**

**c) «Na ma kanisa yote watajua ya kuwa mimi ndiye anayetafuta viuno na mioyo» (Ufunuo 2, 23).** Lakini paka Mungu anajua mioyo ya watu. (Zaburi 7, 9. Yeremia 17, 10. Matendo 15, 8. Wa Roma 8, 27).

2) Ni pa fasi yote ya ulimwengu:

a) Hile wakati alikuwa pa inchi yetu «Mwana wa mutu», mara moja alikuwa na mbinguni. (Yoano 3, 13).

**b) «Kwa kuwa pahali watu wawili ao watatu wanapokusanyika kwa jina langu, mimi ni pale katikati yao» (Matayo 18, 20).** Kristu ni mara moja pamoja na ma kundi wote ya waaminifu wake mu dunia muzima.

**c) «Kama mutu akinipenda, atatii neno langu, na Baba yangu atamupenda, nasi tutakuja kwake, na tutafanya makao (nyumba) yetu kwake» (Yoano 14, 23**).

Lakini ma fasi yetu ni paka Mungu: **«Si mimi ninayejaza mbingu na inchi? anasema Bwana» (Yeremia 23, 24)** Tena ona Zaburi 139, 7-10. Matendo 17, 28. Wa Efeso 4, 6).

3) Ni Mutakatifu kamili na mwenye haki kamili:

**a)** Baba-Mungu ni mutakatifu kamili na mwenye Haki kamili: **«.. . Baba Mutakatifu, uwalinde kwa jina lako wale ulionipa, wawe mumoja kama sisi» «Bwba mwenye haki, dunia haikukujua, lakini mimi nilikujua» (Yoano 17, 11, 25). «Muwe Watakatifu kwa kuwa mimi ni mutakatifu» (Barua ya kwanza ya Petro 1, 16).**

**b)** Vile ni na Kristu: **«Lakini ninyi mulikana yule Mutakaitfu.. », alisema Petro kwa watu wa Yuda (matendo 3, 14). «Mungu wa baba zetu amekwisha kukuchagua upate kujua mapenzi yake, na kuona Mwenye Haki, na kusikia sauti iliyotoka kinywa chake» alisema Anania kwa Paulo (Matendo 22, 14). «Maneno haya anasema yeye aliye Mutakatifu aliye wa kweli.. . » (Ufunuo 3, 7).**

## 8. KRISTU NI MUNGU MUKAMILIFU NA MUTU MUKAMILIFU

Kwa ajili ya hii mashuhuda tuliandika mpaka sasa tunaona ya kama, bila shaka, inaonyeshwa ya kama Kristu ni MUTU NA MUNGU.

1) **«Katika mwanzo alikuwa Neno.. . na Neno alikuwa Mungu.. . Na Neno alifanyika mwili (Mutu)» (Yoano 1, 1, 14).**

2) Hile wakati Kristu alikuwa pa inchi yetu (Mwana wa mutu»), mara moja alikuwa na mbinguni kama Mungu Neno («Na hapana mutu aliyepanda mbinguni ila yeye aliyeshuka toka mbinguni») (Yoano 3, 13 na Yoano 1, 18).

3) Kristu alikuwa ya kwanza «aliye juu ya maneno yote, Mungu mubarikiwa kwa milele» na, mara moja, alikuwa mutu Yesu Kristu, aliyekuja «kwa namna ya mwili» toka kabila ya Wayuda. (Wa Roma 9, 5).

4) «Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili», **«Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae» (Wa Kolosayi 2, 9. 1, 19).** Na **«Mungu alikuwa ndani ya Kristu, akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe.. . » (Barua ya mbili kwa Wakorinto 5, 19).**

5)Namna gani Kristu alikuwa mara moja Mungu na Mutu, hii ni Fumbo kubwa ya Utawa wetu na sisi tunapashwa paka kuisujudu: **«Na pasipo shaka, siri (fumbo) ya utawa ni kubwa: Mungu alionekana katika mwili, alihesabiwa kuwa na haki katika Roho, alionekana na malaika, alihubiriwa katika mataifa, aliaminiwa katika ulimwengu, alipokewa katika utukufu» (Barua ya kwanza kwa Timotheo 3, 16).**

## 9. ROHO MUTAKATIFU NI ROHO NA WA BABA NA WA MWANA

Onyesho ingine kubwa ya hali kimungu ya yesu Kristu na usawa wake pamoja na Mungu-Baba ni jabo ya kama Roho Mutakatifu wakati ingine anaitwa «Roho wa Mungu» ao «Roho wa Baba», na wakati ingine anaitwa «Roho wa Kristu» ao «Roho wa Mwana». Kwa sababu Roho Mutakatifu, wala ni Uso anayetoka toka Mungu-Baba (Yoano 15, 26), sawa vile sisi waorthodoksi tunaamini, wala ni «nguvu moja» ya Mungu-Baba, sawa vile hivi wanaamini Washuhuda ya Yehova, hakuna namna kuwa na kwa Mungu-Baba na kwa Mwana mwake, kama Mwana Yesu Kristu alikuwa kiumbe.

1) (**a)** Roho Mutakatifu anaitwa «Roho wa Mungu»» (matayo 3, 16. 12, 28. WaRoma 8, 9, 14. Barua ya mbili ya WaKorinto 2, 11. 3, 16 na pa fasi ingine) ao «Roho wa Baba» (Matayo 10, 20).

**b)** Roho Mutakatifu anaitwa «Roho wa Mwana» (Wa Galatia 4, 6) ao «Roho wa Yesu Kristu» (Wa Filipi 1, 19. barua ya kwanza ya Petro 1, 11).

**c)** Roho ya Mungu na Roho ya Mwana anasharikiwa: (Wa Roma 8, 9).

2). Usawa na usharikiwa katikati ya Baba na Mwana inaonekana safi na kwa sababu Roho Mutakatifu anatumwa duniani na toka Baba na toka Mwana: Anatumwa toka Baba (Ona shairi 14, 26) na toka Mwana: (Yoano 15, 26 na 16, 7).

## 10. KRISTU NI MUNGU YAKHVE YA AGANO LA KALE

Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama Yakhve (Mungu ya Agano la Kale) ni Mungu-Baba na paka yeye wa pekee (lakini Mwana mwake ni kiumbe ya Yakhve). Lakini Madiko Takatifu inatuonyesha ya kama na Mwana ni Mungu Yakhve. Tena na Roho Mutakatifu ni Mungu Yakhve. Nikusema Yakhve anasharikiwa pamoja na Utatu Mutakatifu ya Agano Jipya. Sasa tutaangalia mashuhuda mengi toka Madiko Takatifu, yenye wanatuonyesha ya kama Kristu ni Mungu-Yakhve. Hii mashuhuda ni onyesho nguvu kabisa juu ya hali kimungu ya Kristu:

1). Ushuhuda wa kwanza tunaandika unabii ya malaika kwa Nabii Zakaria kwa mambo ya mwana wake Yoano Mutangulizi: **«Maana atakuwa mukubwa mbele ya Bwana (Yakhve inaandika Madiko Takatifu), .. . na wengi wa wana wa Israeli arawageuza kwa Bwana Mungu wao (Yakhve); naye (Yoano) atatangulia mbele yake (Ya Bwana Mungu wa Israeli, nikusema Yakhve) mwenye roho na nguvu za Elia, kugeuza mioyo ya baba kwa watoto wao.. . » (Luka 1, 15-17).**

Sisi wote tunajua ya kama Yoano alikuwa «Mutangulizi» ya Kristu na hapana ya Baba. Kwa hivyo, Huyu anayeandikwa pa hii shairi yulu «Bwana Mungu ya wa wana ya Israeli», nikusema Yakhve, kwake alikuwa «mutangulizi» Yoano, hakuna mwingine paka Yesu Kristu, kwani paka kwake alikuwa mutangulizi Yoano.

Lakini na Nabii Zakaria alisema unabii moja: **«Atukuzwe Bwana Mungu wa Israeli; kwani amekuja kwa watu wake, na kuwakumboa.. . Nawe, Mutoto, utaitwa nabii lake Mungu aliye juu; kwa maana utatangulia mbele ya uso wake Bwana (Yakhve), kutengeneza njia zake; (Luka 1, 68, 76).**

Ma «Jina» «Bwana» na «aliye juu» ni «jina ya Yakhve, aliyekuwa «Mungu wa Israeli», sawa vile hivi wanasadiki Washuhuda ya Yehova. Na, kwani Yoano alikuwa mutangulizi ya Kristu na hapana ya Baba wake, inaonekana safi ya kama na huku, «Bwana» na «aliye juu» hana mwingine paka Yesu Kristu.

Umoja na hii ushuhuda ni na unabii kubwa ya Isaya juu ya Yoano Mutangulizi: **«Sauti ya Mutu anayelia katika jangwa, tengenezeni njia ya Bwana (Yakhve katika andiko ya Wa Ebrania)Nyosheni mapito katika jangwa kwa Mungu wetu! (Isaya 40, 3).**

Kupatana na Agano Jipya (Marko 1, 2-3), Bwana (Yakhve), njia Yake Yoano «anatayarisha» hana mwingine paka Yesu Kristu. Lakini na huyu mumoja Isaya inatuelejea ya kama Hule, mapito yake atanyolosha Yoano mu jangwa, nikusema Mwokozi Kristu, ni mumoja «Mungu wetu».

Lakini na kwa nabii malaki Yakhve anaandika juu ya Yoano na hii maana, mukusema hivi: «Tazameni, ninatuma mujumbe wangu, naye atatayarisha njia mbnele yangu» (Malaki 3, 1). Inaonekana huku ya kama Yakhve anayesema huku anasharikiwa pamoja na Kristu.

2) Kwa Nabii Isaya Mungu Yakhve anahubiri: «Mimi, mimi ni Bwana; na pasipo mimi hapana mwokozi mwingine» (Isaya 43, 11). Mu Agano Jipya, Huyu Mungu wa pekee anasharikiwa na Kristu:

**a) «Yosefu, mwana wa Daudi, usiogope kuchukua Maria muke wako, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mutakatifu. Naye atazaa mwana; nawe utamwita jina lake Yesu= Yekhosua (maana yake: Yakhve (Mungu) anaokoa), kwa sababu ndiye atakayeokoa watu wake toka zambi zao.. . Nao watamwita jina lake Emanueli; maana yake Mungu pamoja nasi» (Matayo 1, 20-23).**

**b) «Kwa sababu leo amezaliwa kwenu katika muji wa Daudi, Mwokozi, ndiye Kristu Bwana» (Luka 2, 10-11).**

c) **«Sasa tunaamini.. na tunajua kweli huyu ni Mwokozi wa ulimwengu» (Yoano 4, 42).**

**d)** Mutume Paulo anashariki Mungu-Mwokozi (toka andiko ya Isaya) pamoja na Kristu: **«Tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mkubwa, Mwokozi wetu Yewu Kristu» (Tito 2, 13).**

**e)** Hii anakikiri na Mutume Petro wakati anahubiri ya kama: **«Wala hakuna wokovu katika mwingine, kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu waliopewa watu tupate kuokolewa nalo» (Matendo 4, 12).**

Yakhve, basi, anayesema ya kama ila yake Mwokozi mwingine hakuna, anasharikiwa na Mwokozi-Kristu.

3). Nabii Isaya mu sura 6 (sita) ya Kitabu yake anaandika ya kama aliona utukufu kubwa wa Mungu Yakhve, aliyemwambia: **«Kwenda; na utawaambia watu hawa: Kusikia mutasikia, lakini hamutafahamu; na kuona mutaona lakini hamutajua. Ufanyize moyo wa watu hawa kuona, na ufanyize masikio yao mazito, na ufunge macho yao; hata wasione na macho yao, na kusikia na masikio yao, na kufahamu na moyo wao, na kugeuka na kupona» (Isaya 6, 9-10).**

Mwevangelizaji Yoano anatumia hii unabii kwa Uso ya Kristu na anashariki Yakhve pamoja na Kristu: **«Lakini hata alikuwa amefanya (Kristu) alama nyingi mbele yao, hawakumwamini: .. . kwa sababu Isaya alisema tena: Amepofusha macho yao, na amefanya migumu mioyo yao, wasije wakaona kwa macho yao, wakafahamu kwa mioyo yao, wakageuka, nikawaponyesha. Maneno haya aliyasema Isaya, kwa sababu. a l i o n a u t u k u f u w a k e (Kristu) na alisema habari zake» (Yoano 12, 37-41).** Basi, Yakhve, utukufu yake aliiona Isaya hasikukuwe mwingine paka Mwana wa Mungu. Kwa hivyo Kristu alisema ya kama, « Mimi na Baba tuko pamoja» na «Huyu aliyeniona aliona Baba».

4) Mu Sura 35 ya Kitabu ya Isaya inaandikwa hadishi ya kurudia Wayuda kwao toka utumwa ya muji Babeloni; hii tendo yao ya kurudia kwao ni maana ya kama hivi watarudia watu kwa Mwokozi ya dunia. Anasema: **«jangwa na inchi kavu zitafurahi; na jangwa litashangilia na kutoa maua kama waridi.. . Wataona (Palestini) utukufu wa Bwana, enzi ya Mungu wetu. Mutie nguvu mikono iliyo zaifu, musimamishe magoti yaliyolegea. Muwaambie walio na moyo wa woga: Mukae na nguvu, musiogope; tazama, Mungu wenu atakuja na kisasi, na malipo ya Mungu. atakuja yeye (Mungu) mwenyewe nakuwaokoa ninyi. Ndipo macho ya vipofu yatafunguliwa, na masikio ya viziwi yatafunguliwa. Ndipo kiwete atarukaruka kama ayala, na ulimi wa bubu utaimba; .. . » (Isaya 35, 1-6).**

Maneno haya wanatuwaambia juu ya wakati wa Mwokozi. Kwa hivyo Kristu aliitimiza kwa Maugo yake: **«Na wakati Yoane (mutangulizi) aliposikia katika kifungo matendo ya Kristu, alituma wanafunzi wake akamwambia: Wewe ni yeye anayekuja, ao tutazamie mwingine? Yesu akajibu, akawaambia: Kwendeni zenu mumwambie Yoane maneno muliyosikia na kuona; vipofu wanapata kuona kwao, na viwete wanatembea, wakoma wanasafishwa, na viziwi wanasikia, na wafu wanafufuliwa, na masikini wanahubiriwa Habari Njema. Abarikiwe yeye asiyechukizwa nami» (Matayo 11, 2-6).**

Katika hii jibu Kristu alikikisha Yoano ya kama Huyu alikuwa «aliyekuja», Mungu (Yakhve), aliye pashwa kuja katika Isaya aokoe taifa lake na hivi watatunzwa vipofu, wa bubu, wenye vilema. Hile wakati «Ndipo macho ya vipofu yatafunguliwa, na masikio ya viziwi yatafunguliwa». Kwa kusema na maneno madogo Kristu alikuwa «aliyekuja Mungu». Tena hii shairi: «Abarikiwe yeye asiyechukizwa nami» iko na mafaa mingi. Kama Kristu hasikukuwe Yakhve na alikuwa kiumbe moja, hakuna mambo kama mtu moja atachukizwa kwa ajili Yake. Tena shairi ingine inayetuonyesha ya kama unabii ya nabii Isaya inaonyesha nyakati ya Mwokozi, ni na hii sauti anasema Mtume Paulo kwa Wakristu ya wakati wake: «Kwa sababu hii nyosheni mikono iliyolejea, na magoti yenye kupooza» (Wa Ebrania 12, 12).

5) Nabii Daudi mu Zaburi 78 anaandika maneno ya Mungu Yakhve na hii maneno yake inatuonyesha wakati ya Mwokozi Yesu: **«Sikilizeni, ee watu wangu, sheria yangu:**

**Tegeni masikio kwa maneno ya kinywa changu. Nitafungua kinywa changu kwa mezali; nitasema mafumbo ya kale: » (Zaburi 78, 1-2).**

Hii Unabii alitimiza Kristu kwa maugo Yake: **«Maneno haya yote Yesu akawaambia kwa mifano, wala hakuwaambia kitu pasipo mufano; litimizwe lililosemwa na nabii, akisema: Nitafungua kinywa changu kwa mifano; nitasema maneno yaliyo siri tangu mwanzo wa dunia» (Matayo 13, 34-35).** Basi, Mungu Yakhve atayefungula kwa mifano kinywa Yake hakuna mwingine paka Yesu Kristu mumoja.

6) Nabii Daudi mu Zaburi 8 anasema kwa Mungu Yakhve: «**Ee Bwana, Bwana wetu, jina lako ni lenye utukufu duniani mwote! Wewe uliyeweka utukufu wako juu ya mbingu. Vinywani mwa watoto wachanga nao wanaonyonya umesimamisha nguvu, kwa sababu ya adui zako» (Zaburi 8, 1-2).**

Hii unabii alitimiza kabisa Kristu kwa Maugo yake: **«Lakini wakati wakubwa wa makuhani na waandishi walipoona maajabu aliyoyafanya, na watoto wakilia hekaluni wakisema: .. . Husikii maneno hawa wanayoyasema? Yesu akawaambia: Ndiyo, hamukusoma: Toka vinywa vya watoto wachanga nao wanaonyonya umepata sifa ya kutimia? (Matayo 21, 15-16).** Hii unabii inanyoloka kabisa kwa uso ya Yakhve: Toka vinywa vya watoto atachanga wimbo kwa maugo Yake. Kwa utimizo ya hii unabii tunaona ya kama hii wimbo ya «watoto» ilinyolokwa kabisa kwa uso ya Kristu. Basi, Yakhve ya hii unabii ni Kristu mumoja.

7) Mu Zaburi 68 Nabii Daudi anaimba Bwana (Yakhve Mungu) na anasema hivi: «Imbeni kwa Mungu.. . Jina lake ni JA=Bwana (Yakhve).. . Umepanda (ewe Yakhve) juu, umefunga utumwa wako, umepokea zawadi katikati ya watu, ndiyo, katikati ya waasi vilevile, hata Bwana Mungu akae pamoja nao» (Zaburi 68, 4 na 18).

Mutume Paulo anatuelejea ya kama Yakhve Mungu, kwa huyu anasema Nabii Daudi ni Kristu «wakati alipopanda juu, alifunga kifungo, akawapa watu zawadi», lakini zamani kwa lufu yake «alishuka vilevile mupaka pande za chini za inchi (nikusema mu Hadeze) na ku mwisho anasema: **«Yeye aliyeshuka ndiye aliyepanda vilevile juu sana kupita mbingu zote ili ajaze vitu vyote». (Wa Efeso 4, 7-10).**

8) Mu Zaburi 102 Nabii Daudi anasema taabu yake mbele ya Yakhve Mungu na katikati ya maneno ingine anasema: **«Tangu mwanzo uliweka musingi wa inchi; na mbingu ni kazi ya mikono yako. Hizi zitaharabika, lakini wewe utadumu: ndiyo, hizi zote zitachakaa kama nguo; na kama vazi utazibadilisha, nazo zitabadilishwa; lakini wewe ni sawasawa, na miaka yako haina mwisho» (Zaburi 102, 25-27).**

Na mara ingine Mutume Paulo anatimiza hii maneno kwa Kristu (Wa Ebrania 1, 10-12) na anatuelejea ya kama Yakhve Mungu kwa huyu mwenye aliomba Mwimbaji Daudi ni Kristu mumoja.

9) Nabii Yoeli aliyeandika manabii juu ya ma siku wa mwisho anasema ya kama, **«Na itakuwa kila mutu atakayeomba kwa jina la Bwana (Yakhve), ataokolewa» Yoeli 2, 32).**

Mutume Petro anatimiza hii unabii mu wakati ya dini ya Kristu (Matendo 2, 14-21). Basi, masiku wa mwisho ni wakati ya dini ya Kristu na hapana mwisho ya dunia, sawa vile wanasadiki Washuhuda ya Yehova. tena mara moja Mtume Paulo anaelejea safi ya kama jina ya Bwana, katika hii kila mutu anaokolewa ni jina ya Kristu: **«Kwa sababu kama ukikiri kwa kinywa chako ya kuwa Yesu ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimufufua toka wafu, utaokolewa: kwa maana kwa moyo mutu anaamini hata kupata haki; na kwa kinywa anakiri hata kupata wokovu. Kwa**

**sababu maandiko yanasema: mutu gani anayemwamini, hatapata haya.. . kwa sababu kila mutu anayeitia jina la Bwana ataokolewa» (Wa Roma 10, 9-13).**

Kweli, tunaona wakristu wa kwanza wenye walitimiza hii unabii na walitumia jina ya Kristu na hapana jina ya Yakhve:

**a) «Wakapiga Stefano kwa mawe, naye aliomba, akisema: Bwana Yesu, pokea roho yangu» (Matendo 7, 59).**

**b) «Bwana-anasema Anania kwa Kristu, wakati alionekana kwake na alimuhamuru amukute na Paulo-nimesikia habari za mutu huyu kwa watu wengi, namna alivyotenda mabaya mengi kwa watakatifu wako katika Yerusalema: hata hapa ana mamlaka toka wakubwa wa makuhani awafunge wote wanaoitia Jina lako».** Wakati Paulo alianza kuhubiri Kristu, **«wote waliosikia wakashangaa wakasema: Siye huyu aliyewaharibu walioitia Jina lili katika Yerusalema? » (Matendo 9, 14, 21).**

**c) «Paulo.. . kwa kanisa la Mungu lililo katika Korinto, wale waliotakaswa katika Yesu Kristu, walioitwa kuwa watakatifu pamoja na wote wanaoitia jina la Bwana wetu Kristu katika kila pahali, Bwana wao na Bwana wetu». (barua ya kwanza kwa Wakorinto 1, 2).**

Kw ahivyo Yakhve Mungu, jina lake wataoitia hawa wataokolewa mu wakati ya kwanza ya dini ya Kristu, hana mwingine paka Bwana wetu Yesu Kristu.

10) Mu Nabii Isaya Mungu anasema maneno haya: **«Bwana, mufalme wa Israeli, na Mukombozi wake, Bwana wa majeshi anasema hivi: Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho, na zaidi yangu hakuna hivi» (Isaya 44, 6) na 48, 12).**

Maneno haya ya Yakhve kristu anatimiza kabisa kwa Maugo yake: **«Mimi ni wa kwanza na wa mwisho; na aliye hai; nami nilikuwa nimekufa, na tazama, mimi ni hai hata milele na milele. Nami nina funguo za mauti, na za Hadeze» (Ufunuo 22, 13 na 21, 6).**

11) Kwa Nabii Zakaria Mungu Yakhve anasuburia na anasema: **«Nami nitamwanga juu ya nyumba ya Daudi, na juu ya wenyeji wa Yerusalema, roho ya neema na ya maombi, nao watamutazama waliyemuchoma.. . » (Zakaria 12, 10).**

Mwevangelizaji Yoano anatwaambia ya kama Hule waliyemuchoma (nikusema walimupiga na mukuki) ni Kristu (Yoano 19, 34) na anatimizwa hii unabii ya Zakaria kwa Kristu: «Kwa maana maneno haya yalifanyika, ili andiko litimWatamutazama yeye waliyemuchoma» (Yoano 19, 34-37); na, **«Tazama anakuja na mawingu; na kila jicho litamwona, na wale waliomuchona» (Ufunuo 1, 7).** Ninazania ya kama watu wote wanasikia na wasomaji wote wanaitika ya kama Huyu Yakhve, waliyemuchoma (Zakaria 12, 10) hana Baba Mungu, lakini ni Yesu Kristu.

Kweli, Huyu uso waliyemuchoma ni Mungu Yakhve mumoja.

12) Mu Agano la Kale inaandikwa ya kama Yakhve kwa kufundisha wenye wasiyoimani watu wa Ebrania, hile wakati walikuwa mu jangwa, **«alituma nyoka za moto katik ya watu, wakauma watu; watu wengi katika Israeli wakakufa» (Hesabu 21, 4-6).**

Mu Agano Jipya Mutume Paulo anaelejea ya kama Yakhve walimujaribu watu wa Ebrania mu jangwa, hasikukuwe mwingine ila tu Yesu Kristu: **«Wala tusijaribu Kristu, kama wengine wao walivyonungunika, wakaharabiwa na Muharibishaji» (barua ya kwanza kwa Korinto 10, 9).**

Hii andiko iko ndani ya mandiko wa zamani ya Agano Jipya. Lakini ndani ya maandiko iongine pahali ya maneno: «wala tusijaribu Kristu», ni andiko».. . Bwana». Lakini, kwa sababu maandiko».. . Kristu», ni ya kweli, inaonyeshwa kidogo yulu pahali inaandikwa Kristu (sawa Mungu Neno)aliyekuwa pamoja na watu wa Ebrania mu jangwa na aliwasidikiza na aliwasaidia: **«Wote wakakunywa kinyweo kile cha roho, kwa**

**sababu walikunywa katika mwamba ule wa roho uliowafuata, na mwamba ule ni Kristu» (barua ya kwanza ya Korinto 10, 4).**

Basi, Yakhve Mungu, jina Yake wale wanataka kuokolewa tangu wakati ya dini ya Kristu tangu mwanzo haina ingine paka jina ya Yesu Kristu.

13) Mu Agano la Kale, (Kutoka 3, 14-16) Yakhve mukusuburia na Musa, anaita Maugo Yake «Mimi ni». Hii Jina Yake inaonyesha ya kama Huyu Mungu ni wa milele na hapana sawa wamungu wengine ya wapagano.

Lakini hii sauti ya Yakhve: «Mimi ni», tunaona kuitumia na kristu kwa Maugo Yake:

**a) «Basi ninawaambia ninyi: Mutakufa katika zambi zenu; kwa sababu musipoamini ya kama mimi ndiye, mutakufa katika zambi zenu» (Yoano 8, 24).**

**b)** Halafu Yesu akawaambia: Wakati mutakaponyanyua Mwana wa watu, mutafahamu ya kuwa mimi ndiye, na sifanyi neno kwa mimi mwenyewe; lakini sawa Baba yangu alivyonifundisha, ninavyosema» (Yoano 8, 28). Ndani ya hii maneno ya Kristu ni tena na maana ya ma hali wa wili ya Kristu, kwa sababu katika neno»Mwana wa mutu» inaonyeshwa hali kimutu Yake na katika neno: «Kuwa mimi ndiye» inaonyeshwa hali kimungu Yake.

**c)** Yesu akawaambia: Kweli, kweli ninawaambia ninyi, mbele Abrahamu hajazaliwa, mimi niko» (Yoano 8, 58). Hapa tunaona ufananisho moja ya kama kwa Abrahamu anatumia neno «hajazaliwa», lakini juu ya Maugo Yake neno: «Mimi niko», juu ya kuonyesha uzima wake wa milele kama Yakhve. Inaonekana nzuri ya kama watu wa Ebrania walisikia alitaka Kristu kuwaambia nini, wakati alisema: «Mimi niko» na walikamata mawe kumupiga (Yoano 8, 59).

**d)** Tangu sasa ninawaambia ninyi mbele hayajatokea, ili wakati yatakapotokea, mwamini ya kama mimi ndiye» (Yoano 13, 19).

Basi Kristu anasharikiwa na Mungu ya Agano la Kale, kwa sababu na Huyu Mungu ya Agano la kale alipatia Jina: «Mimi niko» ao «aliyekuwa».

Tunazania, ya kama haina lazima kuandika na mashairi-maonyesho ingine juu ya kusandiki kila mutu ya kama Kristu ni huyu Munngu mumoja Yakhve ya Agano la Kale, aliye wakati ilikuja utimilifu ya wakati alichukua mwili na alikuja katikati yetu. Kwa sababu na Mungu ni Yakhve (na hii sauti hakuna shaka ku kila mutu) iko kweli ya kama Baba na Mwana (Na Roho Mutakatifu sawa tutaonyesha kidogo chini) ni wa asili moja na wekona umungu umoja. Kwa hivyo, basi: **«Ni nani aliye muwongo ila yeye anayekana Yesu ni Kristu? Huyu ndiye mupinga Kristu, yeye anayekana Baba na Mwana. Kila mutu anayekana Mwana ana Baba; anayekiri Mwana ana Baba vilevile». (Barua ya kwanza ya Yoano 2, 22-23).**

## 11. TUNAMWABUDU KRISTU SAWA VILE TUNAMWABUDU BABA

Kwa sababu, basi, Kristu ni Mungu wa kweli, anapokea pamoja na Mungu-Baba usujudu umoja ya kumwabudu:

1) **«Bwana yangu na Mungu wangu» (Yoano 20, 28),** anasema Tomasi wakati alimusujudu Kristu.

2) **«Na malaika zote za Mungu wamwabudu» (Wa Ebrania 1, 6).**

3) **«Na kila kiumbe kilicho mbinguni na juu ya dunia na chini ya dunia na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyo ndani yake, nilivisikia, vikisema: Baraka na heshima na utukufu na uwezo kwa yeye anayeketi juu ya kiti cha Ufalme (Mungu), na yeye Mwana-Kondoo (Yesu Kristu) hata milele na milele.. . na wale wazee makumi mbili**

**na wane wakaanguka wakamwabudu yeye aliye hai milele na milele» (Ufunuo 5, 13-14).**

Ushuhuda ya Madiko Takatifu ni usafi kabisa. Ndani ya maandiko yake Kristu anaonekana «Mungu wa kweli toka Mungu wa Kweli, aliyezaliwa mbele ya wakati na bila uharibifu toka asili ya Mungu-Baba, sawa vile inazaliwa neno toka akili ao moto nuru toka moto. Basi, ni wa mwanzo umoja pamoja na Baba na wa milele na wa asili moja, asiye uharibifu, aliyejua wowote, ma fasi wote. Eko na hali umoja na Mungu-Baba lakini si weko wa mungu wa wili, lakini ni Mungu moja. Hawa watu wanakataa hii mafundisho na wanafundisha Habari Njema (Evangelio) ingine wanapashwa kusoma ma sauti ya Mutume Paulo, anasema kwa barua ya Wagalatia 1, 8.

Mbele ya kufunga hii sura ya Bwana Yesu, iko nzuri kuandika na ushuhuda ingine toka Mapokeo Takatifu juu ya Mwana na Neno ya Mungu. Hii fundisho inatokea ya Makutano wa Ine Kubwa:

«Kufatana na sisi Wapadri Watakatifu wetu, tunaamini kwa Mwana na Bwana wetu Yesu Kristu sawa vile sisi wote tunafundisha ya kama Huyu ni Mungu mukamilifu na mutu mukamilifu, Mungu wa kweli na mutu wa kweli, kwani eko na na nafsi na mwili ya mutu; tena ni wa asili moja na Baba katika umungu na wa asili moja katika kimutu, bila zambi. Aliyezaliwa mbele ya wakati katika hali kimungu, lakini kwa masiku haya alikuja kwetu kwa wokovu wetu toka Maria Bikira na Mzazi-Mungu sawa mutu na alikuwa pamoja na hali kimungu bila ma hali wa wili kuwa na kuchanga, bila kuwa mbali, bila kuharabika, bila kuachana. Hii ma hali wake wa wili walikuwa pa Uso moja bila kuachanishwa ao kupasukwa, lakini alikuwa moja Mwana wa pekee, Neno Mungu, Bwana Yesu Kristu, sawa vile na Manabii walisema kwake na Huyu Bwana Yesu Kristu alitufundisha.

## 12. MASHUHUDA YA WASHUHUDA YA YEHOVA KUPIGANA HALI KIMUNGU YA KRISTU

Sisi, tunasadiki, ya kama tuliandika mashuhuda yote juu ya kuonyesha hali kimungu ya Bwana Yesu Kristu, lakini sasa tutaandika na mashuhuda ya Washuhuda ya Yehova na tutaonyesha ya kama ma shairi yao ni ya bure:

1) **«Maneno haya anasema yeye Amina, aliye Mushuhuda mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa viumbe vya Mungu» (Ufunuo 3, 14);** anaandika Yoano juu ya Kristu mu Ufunuo. Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama hii neno: «mwanzo wa viumbe vya Mungu» maana yake ni «kiumbe wa kwanza».

**a) Sisi tunajibu ya kama hii shairi ni umoja na shairi ingine ya huyu Mwandishi: «Katika mwanzo alikuwa Neno» (Yoano 1, 1),** (nikusema katika mwanzo ya kiumba Neno alikuwa) pahali Neno Mungu anaonyeshwa asiye na mwanzo na wa milele, kwani alikuwa mbele ya kila kiumbe «na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyika» (Yoano 1, 3). Hakuna namna kusadiki sisi ya kama «mwanzo wa viumbe vya Mungu» kuwa na maana: «kiumbe wa kwanza».

**b)** Jina «Amina» (nikusema wa kweli kabisa) ni kwa Mungu na hapana kwa kiumbe kimoja: Kwa Nabii Isaya (65, 16) inaandikwa ya kama hile wakati ya Mwokozi waaminifu «atajibariki kwa Mungu wa kweli; naye anayeapa duniani ataapa kwa Mungu wa kweli». Andiko ya waEbrania inaandika pa neno: «Mungu wa kweli», inaandika: «Mungu wa Amina». Kwa sababu, basi, katika Nabii Isaya «Mungu wa Amina» (Mungu wa kweli) ni Yakhve, inaonekana safi ya kama Kristu ni «Amina» ya Ufunuo na anasharikiwa na Yakhve. Basi, hakuna namna kuwa kiumbe.

**c)** Neno «mwanzo» mu lugha kigreki maana yake haina paka ya wakati, lakini mara mingi iko na maana na hivi:

-Mamlaka (Luka 12, 11 na 20, 20. Wa Efeso 1, 21 na Wakolosayi 2, 10) na pa fasi ingine.

-Tendo, hali: **«Hata malaika wasiolinda enzi yao wenyewe, lakini wakaacha makao yao, .. . kwa hukumu ya siku ile kubwa» (Yuda, 6).**

-Sababu ya huyu anayeleta mwanzo.

Kama tunajua hii mafafanusho yote juu, tunaweza kuelejea hivi hii shairi ya Ufunuo: **«Maneno haya anasema yeye Amina, aliye Mushuhuda mwaminifu na wa kweli, chemchem (shina), sababu na mwanzo ya kiumba, mkubwa na mwenye mamlaka ya kiumbe ya Mungu».**

2) **«Kwa sababu ninakwenda kwa Baba, kwa maana Baba yangu ni mukubwa kuliko mimi» (Yoano 14, 28),** alisema Kristu kwa wanafunzi wake hile usiku ya utoaji yake.

Tunajibu ya kama Kristu, sawa vile inaonyesha Madiko Takatifu, alikuwa Mungu mukamilifu na mutu mukamilifu. Sawa Mungu ni sawasawa na wa asili moja pamoja na Baba, sawa vile ilionyeshwa. Sawa mutu, lakini, alikuwa wa chini ku Baba. Hapa Kristu anasuburia sawa mutu, sawa mwokozi na musaidizi ya watu, aliye pashwa kutembea kwa Baba, katika Mateso, Ufufuo na Kupanda mbinguni (Marko 16, 19). Hapa Neno Mungu, alikuwa daima pamoja na Baba «Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemufunua» (Yoano 1, 18).

Tena tunaweza kuelejea ya kama Mwana alikuwa mudogo mbele ya Baba wake hapaka katika hali kimungu, lakini katika fasi yake, kwa sababu Baba alikuwa Muzazi yake, chemchem ya Umungu na toka Yake wanazaliwa ma uso ingine ya Utatu Mutakatifu. Ya kusema na ma sauti ingine: Baba, kwani ni chemchem ya Umungu ni mu fasi wa kwanza katikati ya ma Uso wengine, bila lakini kuharabika usawa wao wa tatu.

3) **«Lakini kwenda kwa ndugu zangu, ukawaambie: Ninapanda kwa Baba yangu na Baba yenu; na kwa Baba wangu na Mungu wenu» (Yoano 20, 17**) anasema mwenye Ufufuo Kristu kwa Maria Magdalena.

Ni usafi huku ya kama anasuburia Kristu sawa «mwana wa mutu», katika hali kimutu yake. Ni Mwokozi ya watu aliyekufa na alifufuka kwa wokovu wetu na atasimama kama mutu mbele ya Baba wake kuwa musaidizi ya watu katika maombi yake mbele ya Baba-Mungu. Kristu sawa mutu mukamilifu ni kiumbe na kwani ni kiumbe na yeye eko na Mungu-Baba, Mungu Yake, sawa wekona yo viumbe vyote. Sauti yake: «Ninapanda kwa Baba» inatukikiri bila hata shaka kidogo ya kama anasuburia mutu-Kristu, kwa maana, sawa Mungu-Neno ni pamoja masiko yote na Baba ««Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemufunua» (Yoano 1, 18). Hii ni ufafanusho na mu shairi: «Ufufnuo 3, 12).

4). **«Na huu ni uzima wa milele, wakujue wewe Mungu pekee wa kweli, na yesu Kristu, uliyemutuma» (Yoano 17, 3).** Aliomba Kristu kwa Mungu-Baba hile usiku ya utoaji.

Ni kweli ya kama na huku Kristu anaomba sawa mutu, sawa Mwokozi, sawa Musaidizi katika ya Mungu na watu, sawa Kuhani wa tayari ya kutoa sandaka kubwa yake, sandaka ya Maugo Yake kwa wokovu ya dunia. Basi, sawa Musaidizi anaomba kwa Mungu-Baba, «Mungu wa kweli wa pekee» na maana ya kama Huyu ni chemchem ya umungu, kwa maana toka Yake anazaliwa Mwana na anatokea Roho Mutakatifu. Mungu-Baba kama chemchem ya Umungu na Muzazi ya ma Uso Matakatifu wengine wa wili wenye wa asili moja na wa milele, kama Umungu muzima ni Mungu wa pekee wa kweli. Hii haishushe Mwana na Roho Mutakatifu, wenye wanasharikiwa na Baba katika Umungu.

5) «Maana sharti atawale hata atakapoweka adui zote chini ya miguu yake.. . Basi vitu vyote vikikwisha kuwekwa chini yake, wakati ule Mwana mwenyewe vilevile atawekwa chini yake yeye aliyeweka vitu vyote chini yake, (Kwa Baba) hata Mungu awe yote katika yote».

Ni kweli ya kama na huku hii shairi inanyoloka kwa Mutu-Kristu, kwa sababu ma shairi yote wa juu ya sura 15 (1-22) wananyolokwa kwa Mutu-Kristu, kwa Mwokozi, aliyekuwa «Adamu wa mbili» na alikufa kwa zambi zetu na alifufuka na atawala kama Mwokozi mpaka ataisha tendo yake: Hile wakati Mutu-Kristu atatoa Ufalme Wake kwa Baba na atajitii. Lakini, kama Neno-Mungu ataendelea kutawala pamoja na Baba kwa milele na milele.

Kweli, pempeni ya hii fundisho ya yulu, ni na ma shairi ingine toka Madiko Takatifu na wananyolokwa mu Ufalme wa Mwana wa milele:

**a) «Atamiliki nyumba ya Yakobo (Israeli ya roho, Kanisa ya Kristu) hata milele; na ufalme wake hautakuwa na mwisho» (Luka 1, 33).**

**b) «Kiti chako cha ufalme, ee Mungu, ni cha milele na milele»,** wanasema ma Zaburi juu ya Mwana wa Mungu (Zaburi 45, 6 na Wa Ebrania 1, 8).

c) **«Kwa Yeye (Kristu) utukufu na uwezo hata milele na milele» (Ufunuo 1, 6).**

d) **«.. . kwa Yeye (Mungu) anayeketi juu ya kiti cha ufalme, na yeye Mwana-Kondoo (Kristu) hata milele na milele» (Ufunuo 5, 13).**

Ku mwisho, ni lazima kusopoka ya kama na hii shairi: «Lakini Kristu ni yote, na katika yote» unapata utimizo kwa Kristu: **«Kwa kuwa mumeondosha kabisa mutu wa zamani na matendo yake, na mumevaa mutu mupya anayefanywa mupya apate ufahamu sawasawa na mufano wake yeye aliyemwumba. Hapa hapana Muyunani wala Muyuda, . . . lakini Kristu ni yote, na katika yote» (Wa Kolosayi 3, 9-11).** Na hii shairi ni onyesho ingine ya kama Mwana na Mungu-Baba wanasharikiwa katika hali kimungu yao.

6) **«Kichwa cha kila mwanamume ni Kristu na kichwa cha mwanamuke ni mwanamume; na kichwa cha Kristu ni Mungu» (Barua ya kwanza ya wa Korinto 11, 3).** Hule ni «kichwa» ni daima mukubwa; basi, Mungu-Baba, kama kichwa ya Kristu ni kuliko mkubwa, wanasema Washuhuda ya Yehova.

Ni kweli ya kama na hii sauti inanyolokwa kwa mutu-Kristu, kwa maana na yeye kama kiumbe eko na kichwa yake, Mungu Muumba.

7) **«Lakini habari za siku ile na saa, hakuna mutu anayejua wala malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba tu» (Marko 13, 32).**

Ni usafi na hapa ya kama na Yesu Kristu sawa mutu asijue. Haipashwe tusahabu sisi ya kama Kristu ni mutu mukamilifu na ufananisho moja ya hali ubinadamu ni ya kama asijue. Kristu sawa mutu **«alizidi na aliendela katika akili na kimo» (Luka 2, 52**) na alijua paka hii mafamio Neno-Mungu (nikusema maugo kimungu yake) alimufunulia. Sawa Neno-Mungu anajua yoyote, kwa maana **«Hakuna mutu anayejua Mwana, ila Baba; wala hakuna mutu anayejua Baba ila Mwana, naye Mwana anapendezwa kumufunulia» (Matayo 11, 27).** Ufamio ya Mwana sawa Neno-Mungu inapashwa kuwa muzima, sawa muzima ni na ufamio ya Mungu-Baba, kwa sababu hii ma sauti wa wili: «nayejua-anayejua» ni pa kipimo moja.

Ila tu **«Ndani yake hazina zote za hekima na kujua zinafichwa» (Wa Kolosayi 2, 3).** Mwana wa Mungu ni mwenye kufamia yoyote.

Lakini na mu Nabi Zakaria ni jibu wa mwisho: **«Na Bwana Mungu wangu, atakuja na watakatifu wote pamoja naye. Na itakuwa siku hile nuru haitakuwa na kungaa, wala na giza, lakini itakuwa siku moja iliyojulikana kwa Bwana, si muchana, wala usiku; lakini itakuwa wakati wa mangaribi, nuru itakuwa» (Zakaria 14, 5-7).** Ni kweli ya kama Bwana aliye atakuja pamoja na Watakatifu wake siku ya muchana moja ni

Kristu wakati atakuja mara ya Mbili. Kama tutaweka hii shairi pempeni na shairi ya Matayo 24, 29-30) na 25, 31), atasikia ya kama Huyu Uso ni Yesu Kristu na hii siku ya mwisho na hukumu anaijua Bwana Yesu Kristu sawa Neno-Mungu.

8) **«Ee Baba yangu kama ikiwezekana kikombe hiki kinipitie; lakini si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka» (Matayo 26, 39),** na: **«Eloi, Eloi, lama sabaktani; maana yake: Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? » anapaza sauti Kristu pa Musalaba Yake (Matayo 27, 46).**

Na huku hii maneno ya Kristu Yeye anasema sawa mutu mukamilifu, aliyesikia uchungu, alitesa na hali kimungu Yake alimuacha bila kumusaidia juu ya kuvumilia sandaka pa Musalaba yake na namna muzima kwa ajili ya wokovu ya watu (Wa Ebrania 2, 10, 14). Halafu, kama Mungu-Neno alibakia bila uharibifu, kwa sababu hali kimungu yake wala anatesa, wala anauwwa.

9) Pa fasi mengi ya Agani Jipya anaonekana ya kama Mungu ao Baba-Mungu alimufufulia Kristu toka wafu. Kwa mufano Matendo 2, 24, 32. Wa Galatia 1, 1 na pa fasi ingine. Hivi, wanasema Washuhuda wa Yehova Huyu Kristu hasikukuwe Mungu.

Lakini na pa fasi ingine Kristu alisema kwa watu wa Yuda: **«Vunjeni hekalu hili, nami nitalisimamisha kwa siku tatu.. .  Lakini yeye alisema juu ya hekalu la mwili wake» (Yoano 2, 19-21).** Nikusema: **«Mimi kisha ma siku tatu nitafufua mwili yangu».** Basi, hii uwezo kimungu ya Mungu-Baba iliyefufulia mwili-maiti ya Kristu ni mara moja na uwezo ya Kristu. Hii inatuonyesha usharikisho muzima katikati ya Baba na Mwana mwake.

10) **«Naye ni mufano wa Mungu asiyeonekana, muzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote» (Wa Kolosayi 1, 15).** Angalia ufafanusho ya hii shairi mu ukurasa: (31-32).

11) **«Kwa sababu Mungu ni mumoja tu, na mupatanishi katikati ya Mungu na watu ni mumoja, yule Mutu-Kristu, aliyejitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote; » (Barua ya kwanza kwa Timotheo 2, 5).** Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama «ukombozi» ni ustahili umoja pamoja na vile vitu anataka kunuua mutu moja. Hivi, wanasema, Kristu aliyepatia maugo yake na alitununua toka lauma, anapashwa kuwa na ustahili kimoja  na hile ustahili weko na hawa watu Yeye aliwanunua. Vile wanasema kwa sababu wanataka kukataa hali kimungu ya Kristu, ustahili yake ni bila mupaka.

Kwa hivyo wanafundisha ya kama **«Mwana Yesu alifika kwa mufano ya Adamu juu ya kusamehe zambi za Adamu. Alikuwa paka mutu mukamilifu na hakuna kintu kingine (Wa Roma 5, 15).**

Lakini haina kweli fundisho yao, kwa sababu Madiko Takatifu inawajibu hivi: **«Na Neno alifanyika mwili (mutu), akakaa kwetu,,  tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli» (Yoano 1, 14).** Mutu wa kwanza, Adamu, hasikukuwa na wala **«utukufu kama wa mwana pekee akitoka kwa Baba», wala «amejaa neema na kweli». Lakini Mutu-Kristu alikuwa na utimilifu muzima ya Neema ya Roho Mutakatifu (Yoano 3, 34),,  na «utimilifu wote wa Mungu» (Wa Kolosayi 2, 9).**

Kwa hivyo pa hii jabo ya kununua na wokovu ya watu, ukombozi, nikusema Kristu hasikukuwe na ustahili umoja na wale aliwanunua, lakini alikuwa Kristu na ustahili munene, bila mupaka. Kwa hivyo neema wa wokovu ya Mungu haikukuwe pa kipimo umoja na zambi za watu, lakini ilikuwa kupita mingi (Ona wa Roma 5, 15-21), kwa sababu neema ya Bwana Yesu Kristu ilikuwa kuliko mingi (Ona barua ya kwanza kwa Timotheo 1, 14).

12) Kristu **«Lakini alijifanya  mwenyewe kuwa hana utukufu, akitwaa namna ya mutumwa, akakuwa na mufano wa mutu.. .  » (Wa Filipi 2, 7).** Kristu kwa ajili yetu

**«alikuwa masikini, hata ninyi mupate kuwa matajiri» (barua ya mbili kwa wa Korinto 8, 9).** Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama, kupatana na hii maneno, Kristu, wakati alikuwa mutu, alisimama kuwa sawa alikuwa zamani, nikusema aligeuzwa na hivi hana Mungu, kwani Mungu hasigeuzwe.

Kristu, wakati alikuwa mutu, hasikusimame kuwa sawa alikuwa na zamani. Nikusema Neno Mungu, wakati alichukua mwili, hasikusimame kuwa na Neno Mungu. Kristu, wakati alikuwa mutu, alikuwa na Mungu: **«Na hapana mutu aliyepanda mbinguni ila yeye aliyeshuka toka mbinguni, ndiye Mwana wa mutu» (Yoano 3, 13**). Alikuwa duniani, alikuwa na mbinguni mara moja. Tena «Hakuna mutu aliyeona Mungu wakati wowote; Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemufunua» (Yoano 1, 18). Nikusema, hile wakati Kristu alikuwa mutu pa inchi yetu na alituelejea ma siri yote ya Mungu asiyeonekana, mara moja alikuwa na ndani ya kifua ya Baba, sawa vile alikuwa na mbele ya kuchukua mwili na kufika kwetu. Basi, hasikugeuzwa Neno-Mungu, wakati alikuwa mutu. Paka alichukua hali kimutu, bila kusimama kuwa sawa alikuwa na zamani. Umasikini ya Neno Mungu ilikuwa unyenyekevu Yake, kwa sababu alipokea kuchukua hali kimutu. Mutu Kristu hasikukuwe uso moja mwingine, lakini alikuwa Neno Mungu katika mwili, bila zambi; kwa hivyo kila mateso na matusi alivumilia Mutu Kristu ilikuwa unyenyekevu ya Neno-Mungu.

**13) «Nikasema: Ninyi ni miugu, na ninyi wote wana wake aliye juu» (Zaburi 82, 6),** anasema Mwimbaji Daudi na anasema hii sauti yake kwa wakubwa Wahukumu ya Israeli. Mutume Paulo anaita shetani **«mungu wa dunia» (Barua ya mbili ya Wakorinto 4, 4). Na Musa aliitwa «mungu» ya Faraoni (Kutoka 7, 1**). Sawa vile hawa wanaitwa «wamungu» hapana na maana ukamilifu, lakini na maana ya mwenye nguvu na mamlaka, hivi, wanasema Washuhuda ya Yehova, anaitwa na Kristu «mungu» na maana ya mwenye nguvu.

Lakini Kristu anaitwa «Mungu» na maana ukamilifu ya hii neno, nikuse aya kama Huyu ni Mungu wa pekee na moja. «Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele» (barua ya kwanza ya Yoano 5, 20), **«Mungu mubarikiwa kwa milele» (Wa Roma 9, 5), «Bwana yangu na Mungu wangu» (Yoano 20, 28), «Bwana Mungu, yeye aliye sasa, na aliyekuwa, na atakayekuja, Mwenyezi» (Ufunuo 1, 8). Kwa jina «wana» tunatazama ya kama wana wengine wote ni «wana» katika neema (Wa galatia 4, 5), lakini Kristu ni «wa pekee» katika hali yake, ni Mwana wa Mungu (Yoano 1, 18 na 3, 16). Basi, hakuna ufananisho na hata hakuna usawa katikati ya «wamungu» wengine na «Mungu wa pekee» Yesu Kristu.**

14) **«Hakuna mutu aliyeona Mungu wakati wowote» (Yoano 1, 18 na barua ya kwanza ya Yoano 4, 12).** Kristu hakuna namna kuwa Mungu-wanasema Washuhuda ya Yehova- kwa sababu hata mutu moja hasiweze kumuona Mungu.

Kweli, hakuna mutu hata moja hasiweze kuona Mungu katika hali kimungu Yake na utukufu ukubwa Yake. Lakini Kristu hana paka Mungu. Ni na Mutu mukamilifu na sawa Mutu tunamuona. Kwa sababu Mutu Kristu ni mumoja Neno Mungu katika mwili, vile mukuona Mutu Kristu, tunaona mumoja Neno-Mungu (hapana katika hali kimungu Yake, lakini katika hali kimutu Yake).

Ila tu, hii shairi wa yulu ni maana ya kuona Mungu katika namna ukamilifu. Lakini katika hii namna ukamilifu ni kweli ya kama hasikumuone Mungu hata mutu moja, wala ataweza kumuona. Lakina na namna ingine, watu wengine waliona Mungu: Kwa mufano Abrahamu na bibi yake Sara waliona Mungu katika mufano ya malaika wa tatu (Mwanzo 18, 1-3). Nabii Isaya na Manabii wengine waliona maono ya mbalimbali (Isaya 6, 1-10. Kitabu ya kwanza ya Wafalme 22, 19-21). Nabii Musa aliona utukufu wa Mungu mu Kilima Sinaya (Kutoka 24, 9-11. 15-18. 33, 18-23. Hesabu 12, 6-8). Malaika daima

wanaona uso ya Baba wetu aliye mbinguni (Matayo 18, 10). Hawa wote, kama viumbe, wanaona Mungu na namna hapana ukamilifu.

Kupindua Madiko Takatifu inasema ya kama paka Kristu anaona na maana ukamilifu Mungu-Baba mwake: **«Si kwamba mutu aliona Baba ila yeye aliyetoka kwa Mungu, yeye ndiye aliyeona Baba» (Yoano 6, 46).** Na huku mara ingine Kristu anaonyeshwa Mungu wa kweli, kwa sababu Huyu ni wa pekee, anayeona Mungu-Baba katika maana ukamilifu. Ya kama Kristu «anaona» Mungu-Baba mwake katika maana ukamilifu ni kweli: Kwa sababu Madiko Takatifu inasema wa kwanza ya kama wingi «waliona» Mungu (sawa Abrahamu, Musa, Isaya), ya mbili ya kama paka Kristu «aliona» Mungu (Yoano 6, 46). Kwani Kristu ni wa pekee aliyeona Mungu-Baba hii inatuonyesha ya kama anamuona na namna ingine. Wale watu (Abrahamu, Isaya, Musa.. )walimuona Mungu hapana na namna ukamilifu, lakini Kristu aliona Mungu-Baba yake na namna ukamilifu.

15) Washuhuda ya Yehova wanasema ya kama haipashwe Kristu kupokea hii jina «Mwema» alimupatia hule kijana mutajiri, wakati aliuliza Kristu: **«Mwalimu mwema, nifanye nini lililo jema nipate uzima wa milele? Kwa nini unaniuliza juu ya maneno mema? Ni mumoja aliye mwema, lakini kama ukitaka kuingia katika uzima, ushike amri» (Matayo 19, 16-17).**

Inaonekana safi ya kama Kristu alijibu na hii namna, kwa sababu hule kijana mutajiri alimukaribia Kristu sawa mutu mupole; sawa mwalimu mkubwa, lakini alimuona paka sawa mutu mupole na hapana sawa Mungu. Basi, hule kijana mutajiri alikosa, kwa sababu aliita mutu moja mupole, sawa hivi yeye alimuona Kristu na jina «mwema». Hii jina inapashwa kuipatia paka kwa Mungu.

16) Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama Kristu hana wa asili moja na Mungu-Baba Yake na Mwana wa milele wa Mungu, lakini, wanasema ni.. . . Malaika mkubwa Mikaeli, aliyeshuka toka mbingu, alikuwa mutu, sawa Yesu Kristu na kisha alipanda mbinguni na alikuwa mara ingine malaika Mikaeli!!! Juu ya kuonyesha ya kama hii fundisho yao ni wa kweli, wanaleta hii mistari:

**a) «Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, na sauti kubwa, na sauti ya malaika mukubwa, na pamoja na baragumu ya Mungu», hile wakati Kristu atakuja mara ya Mbili duniani (Barua ya kwanza kwa Watesalonika 4, 16).**

**b) «Lakini Mikaeli, malaika mukubwa, wakati aliposhindana na Shetani na kubishana naye kwa ajili ya mwili wa Musa, hakusubutu kumushitaki kwa kumutukana, lakini alisema: Bwana akukemee» (Yuda, 9).**

**c) «Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka; yule joka akapigana nao na malaika zake, nao hawakushinda, wala pahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mukubwa, nyoka ya zamani anayeitwa Diabolo, na shetani, anayedanganya dunia yote; akatupwa hata dunia, na malaika zake wakatupwa pamoja naye» (Ufunuo 12, 7-9).**

Hata kama musomaji ya Madiko Takatifu ni mumbafu, ataweza kusikia ya kama hakuna fasi moja ya kusema ya kama malaika Mikaeli ni Kristu. Hii imani yao ni mambo ya kucheka na haina lazima kuwajibu. Lakini, kwa sababu katikati yetu ni na watu wasiyoakili na wanafuata kundi yao, tutawajibu, hivi:

Hakuna mustari moja ndani ya Madiko Takatifu inayetuonyesha ya kama malaika Mikaeli anasharikiwa na Yesu Kristu. Lakini ni mistari ingine pahali tunaona ya kama hakuna ufananisho na uchanisho katikati ya hawa ma uso wa wili ni munene:

«Amepata kuwa muzuri kupita malaika, kwa sababu ameriti jina lenye utukufu kuliko lao. Kwa maana Mungu alimwambia malaika gani wakati wo wote: Wewe ndiwe Mwana

wangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena, Mimi nitakuwa kwake Baba, na yeye atakuwa kwangu Mwana? Na tena, wakati alipoleta muzaliwa wa kwanza katika dunia, anasema: Na malaika zote za Mungu wamwabudu. Na juu ya malaika anasema: Anayefanya malaika zake kuwa pepo, nawatumihsi wake ndimi za moto. Lakini juu ya Mwana, anasema: Kiti chako cha ufalme, Mungu, ni cha milele na milele, na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki.. . . Na tena: Wewe Bwana katika mwanzo umeweka misingi ya inchi, na mbingu ni kazi za mikono yako. Hizi zitaharibika, lakini wewe unabaki; na hizi zote zitachakaa kama nguo, na kama mavazi utazikunja, nazo zitabadilika; Lakini wewe ni sawasawa saa zote, na miaka yako haitakoma. Lakini kwa malaika gani amekwisha kusema hata mara moja: **Uketi kwa mukono wangu wa kuume hata nitakapoweka adui zako chini ya miguu yako? Hawa wote si roho za kutumikia, waliotumwa kutumikia wale watakaoriti wokovu? (Wa Ebrania 1, 4-14).**

Basi, kupatana na Madiko Takatifu, Kristu ni Mwana wa Mungu, aliyemuzala Mungu-Baba (basi ni wa asili moja na Baba) bila mwanzo na bila wakati na wa milele ya Mungu. Huyu ni Muumba na inchi na mbingu na malaika wote wanamusujudu sawa Mungu wa kweli na Kiti yake, nikusema mamlaka yake kimungu ni wa milele. Lakini malaika wote ni viumbe vya Mungu, ni ma roho ya kutumika kazi na amri ya Mungu na wokovu ya watu. Basi, hakuna ufananisho na usawa katikati ya Kristu na malaika wote.

Na sauti ingine kusema: Malaika moja mukubwa ni paka mkubwa wa kwanza ya kundi ya malaika yake. Juu ya malaika Mikaeli Madiko Takatifu inaandika ya kama huyu alikuwa mkubwa moja katikati ya wakubwa wengine na mulinzi ya taifa ya Israeli, hile wakati ilikuwa taifa ya Mungu (Danieli 10, 13, 21. 12, 1).

Lakini kupindua, Kristu ni Mwana wa Mungu wa pekee na moja (YOano 1, 18. 3, 16). Ni **«Bwana wa bwana na Mufalme wa wafalme» (Ufunuo 17, 14. 19, 16. Ni «Bwana na Mungu wetu» (Yoano 20, 28). Ni «Bwana wa utukufu» (barua ya kwanza ya wa Korinto 2, 8). Ni «Bwana ya vitu vyote» (Matendo 10, 36).**

Basi, hakuna ungano moja katikati ya Kristu na malaika Mikaeli mukubwa. Kwa ajili ya mistari wa tatu wa yulu, yenye wanaleta Washuhuda ya Yehova, tunajibu hivi:

**a)** Kwa mustari ya kwanza tunajibu ya kama, wakati atakuja Kristu mara ya Mbili duniani, atakuja kama Mufalme mutukufu na hazina ya malaika wake wote. Hasiseme ya kama Kristu mumoja ataita sawa malaika mukubwa, wakati atashuka toka mbingi. Lakini, ila «sauti ya malaika mukubwa» itasikiwa na «amri» na «baragumu ya Mungu». Nani atahamuru na atapika na baragumu? Yesu Kristu? Hapana! Hawapike baragumu wafalme, lakini wafwasi na wasaidizi wao. Vile na huku, Kristu kama Mufalme atashuka toka mbingu na atasidikizwa na malaika wingi, wenye watapika baragumu na wataita kwa baraka ya mufalme Kristu.

**b)** Mu mustari yao ya mbili, tunaona ya kama malaika Mikaeli na diabolo wanakombana katikati yao juu ya mwili-maiti ya nabii Musa. Lakini mu Evangelio tunaona shetani-diabolo kutetemeka mbele ya Kristu na anajitii kwake kabisa (Tazama Matayo 8, 29. Marko 1, 23-26, 34. Luka 9, 1. 10, 17-18).

**c)** Mustari wa tatu ni toka Ufunuo. Kule mwanamuke moja «aliyevikwa jua», naye alikuwa mimba, akilia, akiwa katika uchungu wa kuzaa.. . Naye akazaa mutoto mwanamume atakayetawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma» (Ufunuo 12, 1-5). Shetani alikankamana kumukula, lakini hakuna namna. Kisha inafanyika vita kwa mbingu, na malaika mukubwa Mikaeli na malaika wake wanamushinda shetani na malaika wake na wanawatupa pa inchi.

Washuhuda ya Yehova wanasadiki ya kama huyu aliyezaliwa toka Mwanamuke ni ufalme ya Kristu iliyejengwa mu. . . . . mwaka 1914 mu mbinguni na Mikaeli ni Kristu, aliyefanya nvita mu mwaka 1914 na alifukuza shetani toka mbingu!

Mbele ya hii mafafanusho yao wa bure sisi tunajibu ya kama Huyu aliyezaliwa «mutoto mwanamume» ni Yesu Kristu, mwenye atawala mataifa yote katika fimbo ya chuma. Hii uwezo eko nayo paka Mungu na Mwokozi (Zaburi 2, 8-9. Ufunuo 19, 15). Basi, kwani Kristu ni «Mutoto mwanamume» aliyezaliwa, hakuna namna kuwa Mikaeli Malaika. Malaika Mikaeli wapi inasema Madiko Takatifu ya kama alizaliwa? Hakuna hata mustari moja!

Mbele ya majibu haya yetu Washuhuda ya Yehova wanajibu hivi: «Ufunuo wa Kristu, aliopewa na Mungu aonyeshe watumishi wake maneno yaliyopashwa kuwa upesi» (Ufunuo 1, 1). Hapa wanasema Kitabu Ufunuo inaandika majambo na matendo, yenye watatimizwa; basi huyu «Mutoto mwanamume» hakuna namna kuwa Kristu, kwa sababu huyu alizaliwa, alisulubiwa na alipanda mbinguni, mbele ya kuandikwa Kitabu ya Ufunuo.

Sisi tunawajibu ya kama ndani ya ono moja kimungu, sawa hii ya Mutume Yoano ni ndani ma jambo ya wakati yoyote. Kwa sababu mu mustari (1, 19) anasema Kitabu: «Uandike maneno yale uliyoyaona na maneno **y a l i y o. s a s a**, na m, aneno yatakayokuja». Basi, maono ya ufunuo wekona matendo na ma jambo wa zamani, wa sasa na yatakayokuja. Hivi «Mutoto mwanamume» aliyezaliwa ni Kristu na hapana ufalme wao, iliyeumba Kristu mu mwaka. . . 1914! Kwa hivyo, mwingine ni Kristu (aliyezaliwa «mwanamume» na mwingine uso ni Mikaeli aliyefanya nvita pamoja na shetani. Iko namna kusema ya kama malaika Mikaeli ni «mutoto mwanamume» ao «mwanamuke»? !

Ku mwisho tunasema ya kama hakuna mustari moja ndani ya Madiko Takatifu yakusema ya kama Kristu ni malaika mukubwa Mikaeli. Hii sauti ya wogo waliivumbua Washuhuda ya Yehova kusudi wakatae hali kimungu ya Kristu, ya kama Kristu ni Mungu wa kweli.

# 5

# ROHO MUTAKAITFU NI MUNGU WA KWELI

## MWANZO

Washuhuda ya Yehova wanakataa hapana paka hali kimungu ya Kristu, lakini wanakataa na Roho Mutakatifu. Hawa wanasadiki ya kama Roho Mutakatifu ni paka «nguvu wa kazi na isiyo uso ya Mungu na hii nguvu inasukuma watumwa wake wafanye mapenzi yake». Hivi wanasema na wanaandika ndani ya vitabu vyao. Lakini Madiko Takatifu inaonyesha ya kama hii imani yao ni ya wogo. Roho Mutakatifu hana unyofu moja nguvu ya Mungu, lakini ni Uso sawa ma Uso wengine, baba na Mwana na Huyu Uso ni wa tatu ya Utatu Mutakatifu. Huyu Uso eko na asili moja pamoja na Baba na Mwana na hivi ni Mungu wa kweli, sawa Baba na Mwana mwake.

Washuhuda ya Yehova wanasema ya kama jina «roho» ni mara mengi maana yake: pumuzi, pepo na ingine maana. Kweli, mara mengi ni maana «pepo» sawa mu (Yoano 3, 8) na barua ya kwanza kwa waKorinto 5, 5. barua ya kwanza kwa Watesalonika 5, 23. MU mustari ya wa Ebrania 1, 14 maana ni malaika. Mu Mutayo 8, 16 na Luka 8, 29. 9, 39) maana yake ni ma shetani. Mu mustari ya Luka 1, 17 na barua ya kwanza kwa Watesalonika 5, 19 maana ni hali wa neema ya Mungu, lakini mu mustari ya Luka 8, 55, maana yake ni nafsi.

Maana yake ni tena na uso. Kwa mufano Mungu wa pekee anafananishwa sawa «Roho» (Yoano 4, 24. Vile na malaika na ma shetani na ma nafsi. Washuhuda ya Yehova, katika akili yao, inapashwa kukana na uso kimungu ya Mungu mumoja na malaika, na mashetani na ma nafsi.

Roho Mutakaitfu ni Uso moja ya kuachana, Musaidizi, katika Yoano 14, 26) na, kama sisi tutamuchabula, hakuna namna kusamehewa (Ona Matayo 12, 31-32). Ni Hule Uso anayetoa kwa waaminifu neema ya Mungu na ma zawadi wa roho ingine ya mbali mbali (Wa Galkatia 5, 22) kwa hivyo Madiko Takatifu inamufananisha ya kama anajitoa kwa waaminifu na anajaza uzima yao katika neema ya Mungu. Hii fundisho sasa tutaifafanusha kuliko nzuri:

## 1. ROHO MUTAKATIFU NI USO WA KWELI, KWA SABABU ANA MAFANANISHO YOTE YA USO MOJA NA WA AKILI

1) Anaongoza kwa fundisho ya kweli: **«Lakini wakati anapokuja yule Roho ya kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli» (Yoano 16, 13).**

2) Anafundisha na anakumbusha: **«Lakini Musaidizi, Roho Mutakatifu, Baba atakayemutuma kwa jina langu, yeye atawafundisha ninyi, na kuwakumbusha ninyi yote niliyowaambia ninyi» (Yoano 14, 26).**

3) Anashuhuda juu ya Kristu: **«Lakini wakati Musaidizi anapokuja, nitakayemutuma toka Baba, Roho ya kweli, anayetoka kwa Baba, atanishuhudia; na ninyi ni washuhuda vilevile, kwa sababu mumekuwa pamoja nami tangu mwanzo» (Yoano 15, 26-27).** Sawa vile hii neno: «ninyi ni washuhuda» inanyoloka kwa ma Uso, Mitume, vile na «Yule atashuhudia» inapashwa kunyoloka kwa Uso (Tazama na matendo 5, 32).

4) Anahamakia zambi: **«Lakini kama nikikwenda, nitamutuma kwenu. Na wakati anapokuja, atahakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu» (Yoano 16, 7-8).**

5) Anasema: «Roho akamwambia Filipo: Jongea karibu na gari hili.. . » (Matendo ya Mitume 10, 19).

6) Anasema na anaita kwa kazi ya Kanisa: «Nao walipokuwa wakitumikia Bwana na kufunga, Roho Mutakatifu akasema: Muniwekee Barnaba na Saulo kwa kazi ile niliyowaitia» (Matendo 13, 2).

7) Anazibiya: Paulo na Sila «Wakapita katika inchi ya Furigia na Galatia, wakakatazwa na Roho Mutakatifu kuhubiri Neno katika Asia. Wakati walipofika Misia, wakajaribu kwenda Bitinia, lakini Roho ya yesu hakuwapa ruhusa» (Matendo 16, 6-7).

8) Anaweka wa askofu (Wasimamishi): **«Roho Mutakatifu alilowapa ninyi kuwa wasimamishi ndani yake, mupate kulisha kanisa la Mungu.. . » (Matendo 20, 28).**

9) Anakabula zawadi katika mapenzi Yake: **«Lakini kazi hizi zote Roho huyu mumoja anatenda, akigawia kila mutu peke yake kama anavyopenda» (barua ya kwanza kwa Wa Korinto 12, 11).**

10) Anawaza na anakamata mpango sawa vile kila uso: **«Kwa maana imependeza Roho Mutakatifu na sisi, tusiweke juu yenu muzigo kuliko ule unaofaa» (Matendo 15, 28).** Kwa sababu neno: «kwa sisi» inanyoloka kwa ma uso, watu, Mitume ya kristu, basi hivi na neno: «inapendeza Roho Mutakatifu» inapashwa kuwa na namna usawa Uso.

11) Roho Mutakatifu anashuhuda: **«Roho mwenyewe anashuhuda pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu» (Wa Roma 8, 16).** Kwa sababu neno: «zetu» inanyoloka kwa ma uso (waaminifu), basi na Roho, anayeshuhuda pamoja ni Uso.

12) Anataabu: **«Wala musihuzunishe Roho Mutakatifu ya Mungu» (Wa Efeso 4, 30).** Lakini paka ma uso wanasikia huzuni ya roho yao na taabu.

13) Anasali na anaomba kwa sisi, sawa vile anasali na anaomba Kristu kwa Mungu-Baba mwake kwa saidio yetu: «Hivi Roho anasaidia uzaifu wetu; kwa maana hatujui kuomba kitu namna inavyotupasa, lakini Roho mwenyewe anatuombea kwa kuungua kusikoweza kusemwa» (Wa Roma 8, 26).

14) Anatupenda kabisa mupaka wivu: **«Roho anayekaa ndani yetu anatamani hata kuona wivu? (Yakobo 4, 5).**

15) Upekee ya Roho Mutakatifu inashuhudiwa tena na toka neno: «Y E Y E» sawa vile tuliona na ma shairi wa yulu: kwa mufano: «Yeye anawafundisha nini.. . » (Yoano 14, 26). Kama ilikuwa nguvu moja ya Mungu ilipashwa kuandika Kitabu: Hii ao hile na hapana: «YEYE ao YULE».

16) Sawa Kristu anaitwa «Musaidizi ao Mwombezi»: **«Na kama mutu akitenda zambi, tuna Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristu mwenye haki» (barua ya kwanza ya Yoano 2, 1**) kwa sababu Yesu ni Uso wa pekee; hivi na Roho Mutakatifu ni Musaidizi mwingine: Na nitaomba Baba, naye atawapa ninyi Musaidizi mwingine, akae nanyi hata milele» (Yoano 14, 16). Na huyu Roho inapashwa kuwa Uso.

17) Tena na matusi kupigana ya Roho Mutakatifu haisamehewa: **«Kila zambi na kila tukano watu watasamehewa; lakini kwa kutukana Roho hawatasamehewa» (Matayo 12, 31-32);** hii shairi inatuonyesha ya kama Roho Mutakatifu ni Uso, kwa sababu tukano na matusi paka mbele ya uso moja inanyoloka. Tena itakuwa mambo ya bure na kucheka kama tutasadiki sawa wanasadiki Washuhuda ya Yehova ya kama tukano kupigana ya uso ya Baba-Mungu na Mwana mwake inasamehewa, lakini tukano kupigana ya «mwenye nguvu Yake» (nikusema Roho Mtakaitfu, katika fundisho ya Washuhuda ya Yehova) haisamehewa.

18) Ku mwisho, namna ya Ubatizo : «Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu» (Matayo 28, 19) ni onyesho moja nguvu juu ya upekee ya Roho Mutakaitfu. Kwa sababu Mungu-Baba na Mwana ni Uso, inapashwa kuwa Uso na Roho Mutakatifu. Itakuwa mambo ya kucheka kama sisi tunabatizwa kwa jina ya ma uso wa wili na kwa «nguvu» moja ya Mungu-Baba.

Basi, Roho Mutakatifu, anayefundisha, anaongoza, anashuhuda, anahamakia, anaachana, anaita, anawaza, anahuzuni, anapenda, anasali kwa sisi na ingine matendo Yake, hakuna namna kuwa nguvu ya Mungu; ni Uso moja, kwa sababu paka Uso moja iko namna kuwa na hii ma zawadi na mafananisho.

## 2. ROHO MUTAKATIFU NI MUNGU WA KWELI

Roho Mutakatifu ni Mungu wa kweli, sawa vile na ma Uso wengine wa wili, wenye ni ndani ya Utatu Mutakatifu. Madiko Takatifu inashuhudia juu ya umungu ya Roho Mutakatifu:

1) Roho Mutakatifu **«Roho ya kweli, anayetoka kwa Baba» (Yoano 15, 26).** Hii «matokeo» ya Roho Mutakatifu toka Baba ni namna ingine, sawa namna ingine ni uzalio ya Mwana Yesu Kristu toka Mungu-Baba Mwake. Kwa hivyo Roho Mutakatifu ni wa asili moja na Baba na Mwana.

2) Kweli ukamilifu ni paka Mungu asiye na mupaka na wa milele. Halafu Madiko Takatifu inaita Roho Mtakatifu hapana paka «Roho ya kweli» (Yoano 15, 26), lakini tena inakikisha ya kama «Roho ni kweli»: (Barua ya kwanza ya Yoano 5, 6). Hii inaopnyesha ya kama ma Uso Tatu weko na asili moja, kwa sababu ila tu Baba na Roho, na Mwana ni «wa kweli» (Yoano 14, 6).

3) **«Anania-Mtume Petro anasema-kwa nini Shetani amejaza moyo wako kusema uwongo kwa Roho Mutakatifu.. . . . . Hukusema uwongo na watu, lakini na Mungu» (Matendo5, 3-4).** Basi, Roho Mutakatifu ni Mungu: «lakini na Mungu»: nikusema kwa Roho Mutakatifu. Tena, ni kweli ya kama mutu moja anasema uwongo paka mbele ya watu na hapana mbele ya nguvu moja isiyo na uso; kwa hivyo, kama Roho Mutakaitfu, haikukuwe Uso, lakini alikuwa nguvu moja ya Mungu, ilipashwa maandiko kusema: «.. . shetani amejaza moyo wako kusema uwongo kwa Mungu» na hapana kusema: «Kwa Roho Mutakatifu».

4) **«Kwani Roho anatafuta maneno yote, hata mafumbo ya Mungu.. . Hivi kwa maneno ya Mungu hakuna mutu anayeyafahamu ila Roho kwa Mungu» (barua ya kwanza**

**ya wa Korinto 2, 10-11).** Kama Roho Mutakatifu «anatafuta yote, inapahsw akuwa Uso. Kama anatafuta yote, tena na mambo yote ya Mungu: «ila Roho kwa Mungu» hii inatuonyesha ya kama Huyu Roho ni Mungu. Kwa sababu paka uso moja kimungu mukamilifu anaweza kufamia yoyote matendo na mawazo ya Mungu mukamilifu.

5) «Basi Bwana ni Roho hule» (barua ya mbili kwa wa Korintro 3, 17). Hapa Roho anasharikiwa na «Bwana», nikusema na Mungu. (tazama tena na barua ya mbili kwa Watesalonika 3, 5): «Na Bwana aongoze mioyo yenu mupate mapendo ya Mungu, na saburi» uvumilia) ya Kristu». Hapa «Bwana» (=Roho) anaachana toka Mungu-Baba na Kristu.

6) **«Basi kuna zawadi mbalimbali lakini Roho ni moja. (nikusema Huyu Roho anapatia kwa watu, mbalimbali zawadi ya Mungu ni paka moja). »**Na kuna utumishi mbalimbali, lakini Bwana ni mumoja» (Bwana ni paka moja). «Na kuna kazi mbalimbali; lakini Mungu ni mumoja, anayetenda kazi zote katika wote» (Nikusema Mungu mumoja ni Huyu anayetenda yoyote).. . . **Lakini kazi hizi zote Roho huyu mumoja anatenda, akigawia kila mutu peke yake kama anavyopenda» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 12, 4-11).** Sawa tunaona, Roho Mutakatifu anayepatia mbalimbali zawadi matakatifu, anasharikiwa na «Bwana» na «Mungu». Basi, Roho Mutakatifu ni bila mabishano, Mungu wa kweli.

## 4. ROHO MUTAKATIFU NI MUNGU-YAKHVE YA AGANO LA KALE

1) Tunarudia sasa mu sura sita ya Isaya, mistari (1-10), pale Mungu Yakhve alisema hii sauti inafwata: **«Kusikia mutasikia, lakini hamutafahamu; na kuona mutaona, lakini hamutajua» (mstari 9).** Sawa vile tuliona na Mwevangelizaji Yoano anatujulisha ya kama maneno haya yalisema Mwana wa Mungu kwa Isaya (Yoano 12, 37-41) na kwa hivi, basi, Mwana wa Mungu ni Mungu-Yakhve. Pa fasi ingine ya Madiko Takatifu, Mtume Paulo anatufunulia ya kama Mungu aliyesuburia kwa Isaya, alikuwa Roho Mutakatifu: **«.. . ya kama Roho Mutakatifu alisema vizuri na baba zenu, kwa kinywa cha nabii Isaya, akisema: Kwenda kwa watu hawa, ukawaambie: Kusikia, mutasikia wala hamutafahamu; na kuona mutaona, wala hamutapata kujua neno: kwa sababu mioyo ya watu hawa imekuwa mizito na masikio yao ni maziro ya kusikia.. . » (Matendo 28, 25-27).**

2) Mu sura 31 ya Yeremia nii hii fundisho: **«Angalia, siku zinakuja, anasema Bwana, nitakapofanya agano jipya» (shairi 31). «Lakini ili agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli, nyuma ya siku zile, anasema Bwana; nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu» (shairi 33).** Maneno haya ya Mungu-Yakhve Mtume Paulo anayanyolosha kwa watu wa Ebrania na anayatimiza Roho Mutakatifu: **«Na Roho Mutakatifu anatushuhudia vilevile, kwa maana nyuma ya kusema: Hili ni agano nitakalofanya nao nyuma ya siku zile, Bwana anasema: Nitatia sheria zangu ndani ya mioyo yao, na katika akili zao nitaziandika: » (Wa Ebrania 10, 15-16).** Huyu Yakhve aliyesema kwa Isaya, anasharikiwa huku na Roho Mutakatifu.

Kwa hivyo Mungu-Yakhve ya Madiko Takatifu hana paka Baba, lakini na Mwana wake na Roho Mutakatifu, Utatu Mutakatifu wa asili moja na asiye kuachana, Mungu moja wa kweli na wa pekee. Mu Agano Jipya hii Jina inakomboliwa paka na **Jina «Baba, Mwana na Roho Mutakatifu» (Matayo 28, 19);** hii Jina inaonyesha kamili ukweli ya Utatu Mutakatifu, lakini Huyu Mungu katika Utatu Mutakatifu anafuchikwa ndani ya maandiko ya Agano la Kale na hakuna namna kufunuliwa paka katika nuru ya Agano Jipya, katika Kristu (Barua ya mbili kwa wa Korinto 3, 14). Kwa Hii «JINA» Kristu alihamuru Wanafunzi wake kuhubiri na kubatiza na hapana kwa Jina ya Yehova (Yakhve).

# 6

## MUNGU NI MA FASI YOTE YA DUNIA

Washuhuda ya Yehova wanakataa ya kama Mungu ni ma fasi yote ya dunia. Wanasadiki ya kama Mungu anaikaa paka kwa mbingu na paka uwezo Yake ni hile inakwenda ma fasi yote. Hii fundisho yao ya uwongo inatokea kwa sababu wanachukua mafundisho ya Madiko Takatifu katika neno yao na hii maneno yanasema ya kama Mungu anaikaa kwa mbingu. Kwa mufano: **«Baba yetu uliye mbinguni.. . », ao «Mbingu ni kiti changu cha ufalme na inchi ni pahali pa kutia miguu yangu: » (Matendo 7, 49)** ao Madiko Takatifu inasema ya kama Mungu anatembea ao anashuka: **«Nitashuka pamoja nawe kwa Misri.. . . » (Mwanzo 46, 4),** anasema Mungu kwa Yakobo na ingine mifano na mafananisho ya Mungu.

Haya yote ni namna ya maandiko na ma sauti mabinadamu, kwa hivyo haipashwe kuyachukua sisi katika neno yao. Madiko Takatifu inatumia mara mengi hii ma sauti juu ya kusikia nzuri watu wa hile wakati ao juu ya kuonyesha mapendo moja kubwa ao maaguzi ya Mungu mbele ya mutu fulani ao taifa fulani, sawa kwa mufano, alisema kwa Yakobo ya kama atashuka kwa Misri.

Ya kusema na sauti moja, ma bunduki-ma sauti ya Washuhuda ya Yehova ni ya bure na mapumbafu. Kama, kwa mufano, mbingu na inchi ni ya kweli Kiti ya Mungu, sawa wanasadiki Washuhuda ya Yehova, tunapashwa kuwauliza: Mbele ya kuumbwa mbingu na inchi, Kiti ya Mungu ilikuwa wapi? Ao Mungu alikuwa bila Kiti Yake? Ao Mungu eko na mwili na miguu na hivi anatumia Kiti na kiti ya miguu yake? Hapa ni kweli ya kama Mwandishi ya hii Kitabu anatumia ma sauti ya watu juu ya kusikia watu ya hile wakati maana yake. Sauti-bunduki yao ingine upumbafu ni hii: Ya kama Mungu haipashwe kuwa pa fasi yote ya dunia, kwa sababu atakuwa ndani na ya musalani na ma fasi machafu. Mungu ni roho, ni pa fasi yote, bila kumujaza machafu viumbe vyake. Roho haiharabike toka machafu ya watu, sawa vile nuru ya jua inaingia ndani ya musalani, bila kujaza uchafu.

Ya kama Mungu ni pa fasi yote na namna ukweli na hapana paka na namna ya uwezo wake, inaonyeshwa na toka mistari haya ya Madiko Takatifu:

1) **«Mimi ni Mungu aliye karibu, anasema Bwana, mimi si Mungu aliya mbali.. . Si mimi ninayejaza mbingu na inchi? (Yeremia 23, 23-24).**

2) **«Niende wapi mbali na roho yako? ao nikimbie wapi toka uso wako? Nikipanda mbinguni, wewe ni kule: Nikipanda kitanda changu katika Hadeze, tazama, wewe ni kule. Nikitwaa mawingu ya asubui, na kukaa pande za mwisho za bahari; Hata kule mukono wako utaniongoza, na mukono wako wa kuume utanishika» (Zaburi 139, 7-10).**

3) Naye (Mungu) alifanya kila taifa la watu kuwa wa damu moja, wakae juu ya uso wa dunia yote, akaandika nyakati alizowaamuru tangu zamani, na mipaka na makao yao. ili watafute Mungu, kama wanaweza kumupapasapapasa, wamwone, lakini hayuko mbali na kila mumojawetu; kwa maana ndani yake tunaishi, tunakwenda, tuna uhai wetu» (Matendo 17, 26-28). Ni kweli juu ya kuishi ndani Yake, ni maana ya kama Huyu anajaza dunia muzina, mbingu na inchi.

4) **«Mungu mumoja, naye ni Baba ya wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote» (Wa Efeso 4, 6).** Juu ya kuwa Yeye ndani yetu, ni maana ya kama hana paka mbinguni, lakini anajaza na inchi na dunia nzima.

5) **«Naye anayeapa kwa hekalu, anaapa kwa hekalu, na kwa yeye (Mungu) anayekaa ndani yake. Naye anayeapa kwa mbingu, anaapa kwa kiti cha ufalme cha Mungu, na kwa yeye anayeketi juu yake» (Matayo 23, 21-22).** Nikusema Mungu ni kweli na ndani ya inchi, ndani ya hekalu ya Solomono na kwa mbingu mara moja, bila kuweka mupaka

pempeni Yake ndani ya haya makao: **«Tazama mbingu hazikutoshi, wala mbingu za mbingu; basi nyumba hiiniliyojenga itaweza wapi? » (Kitabu ya kwanza ya Wafalme 8, 27).**

Ku mwisho Washuhuda ya Yehova, kwani wanakana Uhai ya Mungu pa fasi yote ya dunia, walifika mu fundisho ingine ya uwongo: Ya kama Mungu «ana mwili isiyoharibika na macho na masikio na ingine ingine vintu yake.. . » Wanaita mistari haya: «Unapandwa mwili wa asili, unafufuliwa mwili wa roho. Kama ikiwa mwili wa asili uko, kuna vilevile mwili wa roho» (barua ya kwanza kwa WaKorinto 15, 44), **«Kwa maana macho ya Bwana yanakimbiakimbia katika dunia yote.. . » (2 Mambo ya Siku 16, 9), na «Jicho langu limeona vilevile wao wanaonivizia, masikio yangu yamesikia habari za waovu wanaosimama juu yangu» (Zaburi 92, 11).** Na sisi tunashangaa kwa hii fundisho yao ya uwongo na ufafanusho ya Madiko Takatifu katika akili yao ya uwongo. Hii mistari hawaonyeshe hata ya kama Mungu ana mwili na mikono na miguu. Wanaonyesha paka upumbafu na akili ugonjwa ya Washuhuda ya Yehova.

# 7

# UFUFUO WA KRISTU KATIKA MWILI MWAKE

## MWANZO

Asili ya Fundisho ya Dini wa Kristu (Kristianisme) ni ya kama «Ya kwamba Kristu alikufa kwa sababu ya zambi zetu kama maandiko yanavyosema; na ya kama alizikwa, akafufuka siku ya tatu, kama maandiko yanavyosema» (barua ya kwanza kwa waKorinto 15, 3-4). Kazi wa wokovu ya Kristu kwa mutu inatimizwa paka katika Ufufuo Wake. Kwa sababu, katika Ufufuo Wake alishinda mauti kwa ajili ya wokovu wetu, aliharabisha Hadeze na alitupatia uzima wa milele. Kwa hivyo, «Na kama Kristu hakufufuliwa, imani yenu ni bule; mungali katika zambi zenu. Na wao waliolala katika Kristu wamepotea. Kama katika maisha haya tu tuna tumaini katika Kristu, sisi ni masikini kuliko watu wote» (barua ya kwanza kwa WaKorinto 15, 17-19). Halafu utukufu kwa Mungu: «Kristu amefufuliwa toka wafu, malimbuko yao waliolala» (15, 20).

Washuhuda ya Yehova wanakataa na hii fundisho ya kweli ya Imani ya Dini ya Kristu sawa na ingine mengi. Wanafundisha ya kama mwili ya Kristu haikufufuliwe, lakini alikimbia toka kaburi Yake na Kristu alifufuka paka. . . . sawa roho!!! Wanaandika: «Mungu alikimbisha mwili ya Kristu, sawa alifanya zamani na mwili ya nabii Musa». Kama sisi tutawauliza namna gani Mungu alikimbisha Mwili ya Kristu, wanatujibu: «Ilikekea katika nguvu ya Mungu». Tena wanaandika Washuhuda ya Yehova: «Kwa sababu Kristu alitoa mwili yake kwa uzima ya dunia, hasitaweze kuchukua mara ingine mwili yake, kwa sababu aliitoa sawa sandaka mara moja»

Lakini, kama ni vile, katika mafundisho yao, kazi ya wokovu ya watu inaharabika kabisa na hawa wanafundisha Evangelio ingine. Madiko Takatifu, sawa tutaonyesha kidogo chini, inatuonyesha ya kama Kristu alifufuka kweli katika mwili Yake na katika hii mwili alipanda mbinguni na hii Mwili Yake aliichunga Kwake kwa milele, sawa Adamu wa mbili na mkubwa ya ulimwengu na ya wale watamuamini na wataokolewa. Ufufuo ya Kristu katika mwili Mwake ni onyesho safi juu ya ufufuo wetu hile wakati Kristu atakuja mara ya Mbili kwa Hukumu ya dunia.

### 1. MADIKO TAKATIFU INAANDIKA JUU YA UFUFUO WA KRISTU

1) **«Vunjeni hekalu hili, nami nitalisimamisha kwa siku tatu.. . . Lakini Yeye alisema juu ya hekalu la mwili wake. Basi alipofufuka kutoka katika wafu, wanafunzi wake wakakumbuka ya kama alisema hivi, wakaamini lile andiko na lile neno alilosema Yesu» (Yoano 2, 18-22).**

Kristu alisema juu ya Ufufuo ya mwili Yake. Imani ya Washuhuda ya Yehova ya kama «mwili» Yake ni Kanisa, haina kweli, kwa ajili ya hii mustari: «basi alipofufuka kutoka katika wafu» na kwa ajili ya hii mustari: «alisema juu ya hekalu mwili wake». Kwa hivyo Kristu anasema juu ya mwili ubinadamu yake. (barua ya kwanza kwa WaKorinto 6, 19).

2) Maneno ya malaika kwa Wanawake Wabebaji-manukato na ma «sanda» yaliyokuwa pa fasi kimoja, wanatuaambia ya kama Kristu alifufuka katika mwili Yake:

**a)** «Wakaona jiwe limefingirishwa mbali na kaburi. Wakaingia, lakini hawakuona mwili wa Bwana Yesu» Malaika wa wili «waliwaambia: **Kwa nini munatafuta yeye aliye hai katikati ya wafu? Hayuko hapa, lakini amefufuka»** (Luka 24, 2-5) na Matayo 28, 6 na Marko 16, 5-6). Wanawake Wabebaji-manukato wanatafuta mwili ya Kristu, kwa hivi neno: «amefufuka» inatuonyesha na inanyoloka kwa mwili Yake.

**b)** Mitume Petro na Yoano, wakati «kwendea kaburi», waliona **«sanda ya kitani» na «kitambaa kilichokuwa kwa kichwa chake hakikuwekwa pamoja na sanda ya kitani, lakini kimekunjwa na kimewekwa pahali peke yake» na waliamini kwa Ufufuo ya Kristu» (Yoano 20, 1-9).**

3) Mu Juma ya ufufuo, hile siku Kristu alionekana kwa Wanafunzi wake, wale

**a) «Wakafazaika, wakaogopa, wakazania ya kama waliona roho. Yesu akawaambia: Munafazaika sababu gani? Na kwa nini mashaka yanatoka katika mioyo yenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu ya kuwa ni mimi mwenyewe. Munipapase mutazame; kwani roho haina mwili na mifupa, kama munavyoniona mimi kuwa nayo. Aliposema vile akawaonyesha mikono yake na miguu yake. Walikuwa hawakuamini kwa sababu ya furaha, wakishangaa, akawaambia: Muna kitu cha kula hapa? .. . Akatwaa, akakula mbele yao» (Luka 36-43).**

**b)** Tena asubui ya hile siku ya ufufuo Wake, wakati alikuta Wanawake, wale **«Wakamukaribia, wakamushika kwa miguu, wakamwabudu» (Matayo 28, 9).**

**c)** Ku mwisho, kwa onekanao ya Tomasi, alisema: **«Leta ha[pa kidole chako, na tazama mikono yangu. Na leta hapa mukono wako uutie katika mbavu zangu; usiwer asiyeamini, lakini mwenye kuamini» (Yoano 20, 27).** Kama alikuwa «roho» hakuna namna kusema kwa Wanafunzi wake kwa kumupapasa, wala atakula pamoja nao, wala wanawake wabebaji-manukato walifanya nguvu kukamata miguu Yake, kama Kristu alikuwa bila mwili na mifupa!

Sasa, kama munataka kujua, Washuhuda ya Yehova namna gani wanafafanmusha hii ma shairi wa yulu, musikieni ya kucheka. Wanasema: Kristu alifufuka paka roho yake. Wakati aliita Tomasi kuweka mikono yake pa mbavu na mikono na miguu yake, Kristu hile saa alichukua mwili moja fulani iliyekujaza na vilonda. Alionekana sawa mutu muzima na alikuwa na lazima kula na kunywa.. . ». Nikusema, Yesu Kristu ya Washuhuda ya Yehova ni moja mudanganyifu, kwani alichukua mwili ingine na kuijaza na vilonda. Nikusema hii mwili haikukuwe yake hata vilonda hawakukuwe Yake! Sasa munaweza kucheka na hii mafundisho ya Washuhuda ya Yehova.

**4)** Ushuhuda kubwa juu ya ufufuo ya Kristu na mwili Yake tuko nayo kwa kuhubiri wa kwanza ya Mtume Petro, aliyesema ushuhuda-unabii moja ya Nabii Daudi: «Maana Daudi anasema juu yake: **Niliona Bwana mbele yangu siku zote, kwa kuwa yuko kwa mukono wangu wa kuume, nisitikisike. Kwa hili, moyo wangu ulipendezwa, ulimi wangu ukafurahi: Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini. Kwa maana hatuniacha roho yangu katika Hadeze wala hutatoa Mutakatifu wako aone uharibifu. Umenijulisha njia ya uzima; . Akitangulia kuona maneno haya, alisema habari za ufufuo wake Kristu, ya kama nafsi yake haikuachwa katika Hadeze wala mwili wake haukuona uharibifu» (Matendo 2, 25-31).**

**5)** Kristu, kama mutu, kisha Kupanda Yake mbinguni na mwili yake iliyofufuka (na sasa mwili yake haitakufa mara ingine kwa milele: Wa Roma 6, 9) aliingia kama Mwokozi na

mkubwa wetu kwa «Vitu Vitaaktifu» ya mbingu, pahali kama Kuhani na Musaidizi anaomba kwa sisi kwa Mungu) Baba mwake mukutoa wokovu kwa wale wanaomba kwa Mungu katika Kwake (Wa Ebrania 4, 14., 20, 7, 25. 8, 1-2. 9, 24-26. Wa Roma 8, 34). Ufananishwa ni sauti ya Mtume Paulo hile alisema kwa Timotheo: **«Kwa sababu Mungu ni mumoja tu, na mupatanishi katikati ya Mungu na watu ni mumoja, yule mutu Kristu Yesu» (barua ya kwanza kwa Timotheo 2, 5).** Kwa hivyo Huyu Mupatanishi anayeikaa pa «Vitu Vitakatifu» ya mbingu mwenye kuomba kwa sisi ni mutu-Yesu (nikusema eko na mwili katika nyama na mifupa) na hapana Yesu-roho.

**6)** Ma alama haya wanatuonyesha ya kama «ufufuo» ni maana ya kusimama maiti moja. Kama, basi, mwili-maiti ya Kristu «haikufufuliwa», hivi haikukuwa ufufuo na Madiko Takatifu inaandika uwongo. **«Na kama Kristu hakufufuliwa, imani yenu ni bule; mungali katika za, mbi zenu.. . Lakini sasa Kristu amefufuliwa toka wafu, malimbuko yao waliolala» (Barua ya kwanza kwa WaKorinto 15, 17-20).**

**7)** Ku mwisho, **«Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani, wasiokiri ya kuwa Yesu Kristu amekuja katika mwili; Huyu ndiye yule mudanganyifu na mupinga Kristu» (barua ya mbili ya Yoano, 7).** Kwa sababu atakuja katika mwili Yake kwa hile siku ya Hukumu dunia, hii inatuonyesha maana ya kama alifufuka katika mwili yake na alipanda mbinguni katika mwili mwake. Washuhuda ya Yehova, basi, kwani wanakataa kumuamini Kristu ya kama alikuja katika mwili Yake na alifufuka katika mwili Yake, hii mambo inatuonyesha ya kama hawa ni wadanganyifu na wapinga -Kristu.

Mwili ya Kristu, basi, haikuharabike ndani ya kaburi Yake, haikukimbie, haikuonekane, lakini alifufuka toka wafu, bila uharibifu, wa milele na mukamilifu. Huu Mwili Yake ilikuwa inje na yulu ya ma sheria ya dunia na hivi iliweza kuingia na kutoka, lakini milango na ma dirisha ilikuwa ya kufungwa na Wanafunzi wake walimuongojea ndani ya hile nyumba. Paka katika hii mwili Yake ukamilifu na isiyo uharibifu alipanda mbinguni na katika huu mwili atarudia kwetu kuhukumu wenye wanaishi na wafu.

## 2. MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA YA YEHOVA KUPINGANA UFUFUO YA KRISTU KATIKA MWILI MWAKE

**1)«Kwa maana Kristu vilevile aliteswa mara moja kwa ajili ya zambi.. . akauawa katika mwili, lakini akafufuliwa katika roho; katika roho hii alikwenda vilevile na kuhubiri kwa roho waliokaa katika kifungo» (Barua ya kwanza ya Petro 3, 18-19).**

Neno: «akafufuliwa katika roho» Washuhuda wa Yehova wanaifafanusha: «akafufuliwa kama roho». Lakini maana ya hii shairi ni ingine. Hii mustari: «akafufuliwa katika roho.. . » iko na mafafanusho wa wili: Kama inanyoloka kwa roho ya mutu-Kristu, maana yake ni ya kama «roho ya Kristu alichukua nguvu na alikwenda na alihubiri kwa roho waliokaa katika kifungo». Halafu, kama hii neno: «katika roho» inanyoloka kwa Roho wa Mungu (nikusema Roho Mutakatifu) na hii ufafanusho ni kupita wa kweli, basi mustari hii iko na maana hivi: «Akafufuliwa katika Roho na kwa ajili Yake (Roho) alikwenda na alihubiri na kwa roho waliokaa katika kifungo.. . »

2)Washuhuda wa Yehova wnasadiki ya kama Kristu, kisha Ufufuo wake, alionekana kwa Wanafunzi Wake katika ma uso ya mbali mbali na hii mambo inaonyesha, katika akili yao, ya kama alikuwa roho na alikamata mwili katika mapenzi yake. Kabisa wanasimama ya kwanza, kwa mapatano ya Kristu pamoja na Maria Magdalena, aliyemufamia mara moja na alizania ya kama alikuwa mulinzi shamba (Yoano 20, 11-16) na ya mbili kwa mapatano Yake pamoja na wanafunzi wa wili pa njia ya mukini Emaus na hawa hawakuweze kumufamia (Luka 24, 13-35 na Marko 16, 12).

a) Kwa ajili ya hii maneno ya kwanza Maria Magdalena hasikumufamie Kristu mara moja, hapana kwani Kristu aliisha kuchukua uso ingine, lakini, kwani: 1) ilikuwa giza, 2) Ma

macho ya Maria hakuna namna kutazama nzuri, kwa sababu alilia na 3) hasikuonmgojea kumuona Kristu mwenye ufufuo; alitafuta paka maiti Yake.

b) Kwa ajili ya mambo ya mbili, somo nzuri ya maandiko inatuongoza ya kama Washuhuda wa Yehova wanasema wogo. **«Nyuma ya maneno haya akatokea watu wawili, ana sura nyingine, wakishika njia kwenda mashamba» (Marko 16, 12).** Hapa Mwevangelizaji Marko anaandika na ma neno mafupi onekano ya Kristu kwa Wanafunzi Wake, mu Juma hile ya Ufufuo walikwenda kwa Mukini Emaus na Mtume Luka anaandika na maneno mengi (Luka 24, 13-35) Sawa vile anafafanusha Luka hawa Wanafunzi wawili hawakumufamie Kristu, hapana kwa sababu Kristu alionekana na sura ingine ao alikuwa na mwili ingine, lakini, kwa sababu **«macho yao yalifungwa wasipate kumutambua» (Luka 24, 16).** Nikusema Mungu alifunga macho yao juu hapana kumufamia mara moja. Kisha saa kidogo, wakati walikula pamoja **«Macho yao yakafunguliwa, wakamujua» (Luka 24, 31).**

Kwa hivyo kwa kusema kweli Kristu hasikuchukua sura ao mwili ingine, lakini alikuwa na Sura Yake hile alikuwa na mbele ya lufu Yake.

Kama, kwa mufano sisi tutawaza ya kama Kristu alichukua Sura ingine, hata na hii sauti haionyeshe imani ya Washuhuda ya Yehova, wenye wanasadiki ya kama Kristu hasikukuwe na mwili. Kwa sababu na kwa Mageuzo ya Sura yake, mbele ya usulubisho na lufu Yake, Madiko Takatifu inaandika ya kama, **«Sura ya uso yake ikageuzwa, .. . » (Luka 9, 29).** Basi, tunauliza sisi Washuhuda wa Yehova: Yesu Kristu na mbele ya lufu Yake alikuwa roho bila mwili na alikamata mwili katika mapenzi Yake; kweli ni hapana! Basi, kama Kristu alionekana ndani ya wakati kimoja na sura ingine hii haiseme ya kama Huyu hasikukuwe mwili ubinadamu.

3) **«Unapandwa mwili wa asili, unafufuliwa mwili wa roho. Kama ikiwa mwili wa asili uko, kuna vilevile mwili wa roho. Hivi iliyoandikwa: Mutu wa kwanza, Adamu, alikuwa nafsi ya uhai; Adamu wa mwisho ( Kristu) alikuwa roho yenye kupatiza uhai. Lakini ule wa roho si wa kwanza, lakini ule wa asili, kisha ule wa roho. Mutu wa kwanza alitoka katika dunia, mwenye udongo; mutu wa pili ni Bwana aliyetoka mbinguni.. . Basi, tunasema hili, ndugu zangu, ya kwamba, nyama na damu hasiwezi kuriti ufalme wa Mungu; wala kuoza kuriti kutokuoza» (Barua ya kwanza kwa WaKorinto 15, 44-50).** Namna gani, basi, wanauliza Washuhuda wa Yehova, iko namna kuwa Kristu katika mwili ubinadamu yake mu Ufalme mbinguni?

Lakini, hapa inaonekana safi ya kama, katika maneno haya: «mwili wa asili» na «mwili wa roho» Mutume Paulo anatufundisha juu ya mutu wa dunia, (sawa vile inamuzala hali kimutu), nikusema huyu mutu bado kuzaliwa katika Kristu na bado kutakaswa katika neema ya Roho Mutakatifu; lakini na neno: «mwili wa roho» Mtume Paulo anatuwaambia juu ya hule mukristu aliyezaliwa na aliokolewa katika Kristu. Kwa mufano:

a) **«Kweli, kweli, ninakuambia Mutu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho». (Yoano 3, 5-6)**

**b) Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 6, 17).**

**c) «Lakini hatukupokea roho ya dunia, lakini Roho anayetoka kwa Mungu; kusudi tupate kujua zawadi tulizopewa na Mungu.. . Lakini mwenye kufuata tabia ya asili hapokei maneno ya Roho ya Mungu: .. . lakini mwenye kufuata Roho anatambua maneno yote.. . Na mimi, ndugu, sikuweza kusema na ninyi kama na watu wa Roho, lakini kama na watu wa mwili; . . . kwa sababu hata sasa ninyi ni watu wa mwili; kwa sababu kuna wivu na ugomvi katikati yenu, ninyi si watu wa mwili mukikwenda kwa namna ya watu» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 2, 12-14 na 3, 1-3).**

d) Sisi waaminifu, anasema Mtume Paulo, «sheria ya Roho ya Uzima ulio katika Yesu Kristu imenifanyiza huru kwa sheria ya zambi na kufa.. . kwa maana wale wanaofuata maneno ya mwili, wanafikili maneno ya mwili, lakini wale wanaofuata maneno ya Roho, wanafikili maneno ya Roho. Kwa maana nia ya mwili ni kufa; lakini nia ya Roho ni uzima na salama: ..

(5). Lakini ninyi si kwa mwili, lakini kwa roho, kama Roho ya Mungu akikaa ndani yenu. Lakini kama mutu ye yote asipokuwa na Roho ya Kristu huyu si mutu wake» (barua wa Roma 8, 1-10).

Pa haya mistari wa juu Madiko Takatifu inafundisha wale watu wanaishi duniani katika mwili na mifupa. Katikati yao ni na wale wanazaliwa katika Roho Mutakatifu, lakini wale wasiyokuzaliwa katika Roho, wanafuata uzima ya mwili, ndani ya zambi zao. Kwa hivyo Madiko Takatifu wale walizaliwa katika Roho inawaita « kwa roho ao wa roho», lakini wale bado kuzaliw akatika Kristu inawaita «mwili», nikusema watu wa zambi, kwani ndani yao ni ma zoezo ya zambi, sawa tabia, kisilani, chuki, jivuno na ingine.

Kupatana na hii fundisho inaonekana safi ya kama Kristu anaitwa «Roho wa uzima» hapana kwani hana na mwili ubinadamu, lakini, kwa sababu, sawa Mutu na Huyu inakaa na ushirika ukamilifu pamoja na Roho Mutakatifu (Yoano 3, 34). Vile anaweza Kristu sawa na Mutu atupatie neema kimungu na uzima wa roho. Kwa maana ya kama «nyama na damu hasiwezi kuriti ufalme wa Mungu» inanyoloka kwa mutu wa hii dunia, mutu wa zambi, mwenye anatumika ndani ya zambi zake. Huyu, kwa sababu bado kuzaliwa katika maji (Ubatizo) na katika Roho Mutakaitfu, hana na fasi kuingia mu Ufalme Mbinguni.

Basi, haya maneno ya Washuhuda wa Yehova hakuna namna kuwasaidia kwa imani yao.

4) Kwa hii sauti ya Washuhuda wa Yehova ya kama Kristu aliingia **«wakati milango ilipofungwa pahali walipokuwa wanafunzi.. . » (Yoano 20, 19, 26),** inatuonyesha ya kama Kristu alipashwa kuwa roho. Sisi tunawajibu ya kama na mbele ya Ufufuo Wake Kristu aliisha kutembea pa bahari (matayo 14, 24-34). Basi, wakati Kristu alitembea pa bahari, alikuwa roho? Hapana, kweli! Basi, sawa Kristu alitembea katika mwili ubinadamu Yake pa bahari, vilevile aliingia mwili Wake wa ufufuo ndani ya nyumba na milango yalikuwa ya kufungwa. Tena, sawa tulisema mara ingine, Kristu mumoja alikikisha wanafunzi Wake, (wenye walizania ya kama alikywa roho) ya kama hasikukuwe roho, lakini alikuwa na mwili na mifupa (Luka 24, 36-43).

Tena, tunaisha kusema ya kama Mwili ya Kristu, kisha ufufuo yake aliisha kupata isiyo-uharibifu, isiyo mauti, ukamilifu na Mwili yake ni inje na yulu ya sheria ya hii dunia; hii tunasikia kabisa juu ya nini aliingia ndani ha nyumba, **«wakati milango ilipofungwa pahali walipokuwa wanafunzi kwa sababu ya kuogopa Wayuda.. . ».**

5) **«Hivi, tangu sasa sisi hatujui mutu kwa namna ya mwili; hata tukiwa tumejua Kristu kwa namna ya mwili, lakini sasa hatumujui hivi tena» (Barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 16).**

Katika hii shairi Washuhuda wa Yehova wanasema ya kama hatutafamia mara ingine Kristu katika mwili na mifupa yake. Lakini maneno haya wanasema juu ya unyenyekevu na ugonjwa ya Kristu sawa Mutu, kwa sababu Kristu sawa Mutu alileta pa mwili Yake mazoezo na hali ya kimutu Yake, bila zambi. Nikusema Kristu sawa mutu, asiye na zambi alisikia njaa, kihu, umivu, muchoko na ingine-ingine hali kimutu Yake. Lakini, kisha Ufufuo Wake, Mwili Yake alitosha hile yoyote ma zoezo ya hali kimutu Yake na ilikuwa isiyo uharibifu na isiyo na lufu, nikusema « hata tukiwa tumejua Kristu kwa namna ya mwili», lakini tunamujua Mutukufu na musiyekufa. «Hivi, kama mutu akiwa ndani ya Kristu, yeye ni kiumbe kipya.. . » (Barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 16).

6) Ufafanusho ni umoja na kwa ingine shairi-bunduki ya Washuhuda wa Yehova: «Yeye katika siku za mwili wake, alitolea maombi na malalamiko, pamoja na kulia sana na machozi kwake aliyeweza kumwokoa katika kufa, naye alisikilizwa kwa sababu aliogopa Mungu» (Wa Ebrania 5, 7).

«Katika siku za mwili wake» ni wakati ya uzima ya Kristu pa hii inchi, wakati tena mwili yake ilikuwa wa lufu na wa uharibifu. Haina maana ya kama sasa Kristu ni pasipo mwili Yake, sawa vile wanasadiki Washuhuda ya Yehova. Onyesho kubwa ni hii: **«Kwa sababu w a k a t i. t u l i p o k u w a. k a t i k a. m w i l i, tamaa za zambi, zilizokuwa kwa njia ya sheria,**

**zilitenda kazi katika viungo vyetu hata tukazalia kufa matunda» (wa Roma 7, 5-6).** «**w a k a t i. t u l i p o k u w a. k a t i k a. m w i l i**»: Basi, hile saa aliwaandika Mtume Paulo, wale waaminifu wa Roma walikuwa bila mwili yao? Kweli, hapana. Basi, sawa vile waaminifu wa Roma hawakukuwa «katika mwili», lakini walikuwa na mwili ubinadamu yao, vile na Kristu anafuata kuwa na mwili ubinadamu Yake, hata kama alisimama kuwa «katika siku za mwili wake».

# 8

# K A N I S A

## MWANZO

Mbele ya kuandika mafundisho ya uwogo ya Washuhuda ya Yehova, ni lazima kuandika kidogo Hadisi wa zamani ya Kanisa wa Kristu na kisha tutaendelea fundisho yetu.

Hadishi ya Kanisa yetu inaanza zamani kabisa, tangu nyakati ya watu wa kwanza. Ni kweli. Kama tutaenda ku mukongo, tutaona Adamu na Eva wanaishi na furaha na amani ndani ya Paradizo kwani walipata mapendo mingi ya Mungu. Makadaza yao ilikuwa wafike katika utii yao kwa mapenzi ya Mungu mu uzima wa Mungu, mu uzima katika neema Yake. Lakini hawa watu wa kwanza walikanyanga amri ya Mungu na walitokwa inje ya Paradizo. Matunda ya hii kosa yao yalikuwa mabaya: kwa ajili ya zambi zao walipotesha ushirika yao pamoja na Mungu. Mutu kisha alikuwa adui ya Mungu, mutumwa ya shetani na ya zambi na iliingia mu uzima yake uharibifu na lufu. Ya wakati mingi mutu alilokota mukongo yake matunda ya kosa yake na aliongojea ukombozi. Wakati fulani, hile wakati ilikuja utimilifu ya muda Mukombozi, walimuongojea watu wingi katikati ya wamilele wote, alikuja. Huyu alikuwa Mwana na Neno wa Mungu (Uso wa mbili ya Utatu Mutakatifu). Huyu bila kusimama kuwa na Mungu wa kweli, alikuwa mutu (Yoano 1, 14**), «aliyetolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki» (Wa Roma 4, 25),** «akakuwa mwenye kutii hata mauti, ndiyo mauti ya musalaba» (Wafilipi 2, 7-8). Sandaka wa musalaba na ufufuo ya Mukombozi walikuwa kwa sisi chemchem ya uzima mupya na isiyo uharibifu. Vile, Mwana wa Mungu alitakasa katika tendo Yake gali ubinadamu yetu na aliiuhuru toka utumwa ya shetani na minyororo ya lufu « (Wa Ebrania 2, 14-15 na barua ya mbili kwa Timotheo 1, 10). Yesu Kristu alikuwa Adamu wa mbili ambaye alimaliza uzalio mupya kwa hali ubinadamu, utakaso yake na ushirika yake mu uzima ya Neema Takatifu na mu ushirika pamoja na Utatu Mutakatifu. Nikusema Kristu alikuwa Muzaliwa mukubwa ya ulimwnegu moja mupya, aliiokolewa na aliitakaswa kwa ajili Yake.

Hii ulimwengu mupya haina ingienpaka Kanisa na Huu Kanisa Madiko Takatifu inaita «Mwili ya Kristu na Kristu ni Kichwa yake. Huyu Kichwa ni Muzaliwa na Mukombozi Yesu Kristu. Tangu hile wakati watu wote waliitwa ku Kristu na Mitume wakatale mutu wa zamani, nikusema mutu wa zambi, «Adamu wa kwanza» na watakuwa vipande ya Mwili mupya ya «Adamu wa mbili» nikusema Yesu Kristu, na ndani ya Huu Mwili (Kanisa) ni masaidio yote ya wokovu. Huu Mwili ni «Bibi-Arusi» ya Kristu, ni Safina ya wokovu, ni nyumba ya Neema na mulinzi ya fundisho ukweli.

Hii ushirika ya Neema wa Mungu, hali mupya ya uzima, hile Kristu alitupatia hapa duniani, nikusema Kanisa Yake, ni Ufalme wa Mungu hapa pa inchi yetu. Nikusema Kanisa ya Kristu inaanza mu Paradizo na inatandazwa mpaka huku pa inchi yetu. Vile waliiona Kanisa Wanabii na hivi aliihubiri Mtakatifu Yoano Mutangulizi, na hivi aliituonyesha Kristu.

1) Wanabii:

a) Nabii Danieli anaandika ya kama, **«na kwa siku za wafalme wale Mungu wa mbinguni atasimamisha ufalme usioharibiwa milele, . . . » (Danieli 2, 44-45**). Kupatana na Wakristu Wafafanushi hii ufalme wa milele ni Kanisa ya Mungu.

b) Ni stahili tena kutazama nzuri na unabii ya Isaya, ambaye anaita Kanisa «mulima»: **«Na itakuwa siku za mwisho, mulima wa nyumba ya Bwana utasimamamishwa juu ya milima; na utanyanyuliwa juu ya vilima, na mataifa yote wataukimbilia» (Isaya 2, 2-3).** Ma siku wa mwisho inatuonyesha ma siku hile Kristu alikuja duniani na ujengo ya Kanisa Yake (hapana ufikisho wa mbili Yake). (tena tazama na ufafanusho ya Mtume Petro juu ya ma siku wa mwisho mu Matendo wa Mitume 2, 16-21).

2) Yoano Mutangulizi:

**«Siku zile Yoano Mubatizaji alikuja akihubiri katika jangwa la Yudea, akisema: Tubuni, sababu ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyu ndiye aliyesemwa na nabii Isaya, akisema.. . » (Matayo 3, 1-2).**

3) Yesu Kristu:

a) **«Nyuma ya kufungwa kwa Yoane, yesu alipita hata Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema: Wakati umetimia, ufalme wa Mungu ni karibu. Tubuni mukaamini Habari Njeama.. . » (Marko 1, 14-15).**

**b) «Kweli ninawaambia ninyi, kuna watu katika hawa wanaosimama hapa, nao hawataonja mauti hata watakapoona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu» (Marko 9, 1).** Kweli, ufalme wa Mungu hapa duniani ni Kanisa, «umekuja kwa nguvu» hile siku ya Kushuka Roho Mutakatifu (Pentikoste). Inaonekana safi ya kama Kristu alituwaambia juu ya Kanisa Yake na hii Kanisa yake ni Ufalme wa Mungu, ambaye umekuja kwa nguvu. Basi, Washuhuda wa Yehova wanasadiki mubaya, kwani wanahubiri ya kama ufalme wa Mungu ilianza mu mwaka 1914!

Ndani ya hii Kanisa, iliyeumba Kristu wanaitwa kuingia watu wote, kwani Huu ni Safina ya wokovu na hivi watakuwa wakaaji ya ufalme wa Mungu.
Hii ni fundisho ya Kanisa Orthodokse na fundisho ya Madiko Takatifu.

Washuhuda wa Yehova, pa fasi ya Kanisa, wanasuburia juu ya.. . Kundi moja ya Yehova inayeonekana na wanatuita kuifuata na sisi. Wanaandika: **«Hii kundi ya watumwa wa Mungu iko ya kufamiwa na jina Washuhuda wa Yehova».** Tena wanaandika ndani ya vitabu yao: Huu Kundi wa Mungu inayeonekana inaongozwa na inanyolokwa toka Mungu. Centre ya Washuhuda wa Yehova ni mu muji Mbruklini ya Yorki Mupya ya inchi Amerika. Kule ni makutano moja ya wakristu wakubwa wanaume toka ma fasi ya mbali-mbali ya inchi yetu na wanatazama matendo ya taifa wa Mungu». Wanasema ya kama hii baraza yao ni «mutumwa mwaminifu na mwenye akili ya Mungu, katika mfano ya Matayo 24, 45). Hii Kundi yao ni musaidizi ya Yehova hapa duniani, ni pombe umoja pahali kati yake Yehova anatuma chakula ya roho mu dunia. Kwa hivyo waaminifu yao wanapashwa kutii bila kuona na kusikia hii kundi yao. Wanaandika: «mapenzi ya kundi (mutumwa mwaminifu na mwenye akili ya Mungu) ni mapenzi ya Mungu. Nikusema kila sauti ya Kundi yao, hile ni mu Amerika paka hii ni fundisho na mapenzi ya kweli ya Yehova-Mungu.

Tena wanasema na wanahubiri juu ya baraza wa Mungu wa dunia muzima, tena juu ya baraza pahali mkubwa ni Mungu ao wanasema juu ya baraza wa mbingu ya Mungu, ao wanaiita Baraza ya Dunia mupya.

Katika mafundisho ya Washuhuda ya Yehova hii Kundi inayeonekana ya Yehova iko nayo ma kundi ya waaminifu wa wili:

1) Kanisa ya Mungu, katika fundisho yao, iko nayo paka 144. 000 waaminifu, «watu wa Israeli wa roho», «wenye walizaliwa katika Roho Mutakatifu» na kikoma yao ni waishi kwa mbingu sawa ma roho, pahali watawala pamoja na Kristu. Mupaka ku mwaka 1931 watu wote ya hii Kundi yao walikuwa ndani ya hii Kundi; lakini wale watu waliisha kufa, walianza

kufufuliwa pasipo kuonekana ku mwaka 1918! na walitawala pamoja na Kristu, ambaye mu mwaka 1914 aliisha kuumba Ufalme kwa mbingu!

2) Kundi ya waaminifu wa wili ni taifa wote, wenye, kwani ni watumwa wa Yehova na kipimo ya pili, hawa wataishi mu paradizo wa inchi na hii paradizo itaumbwa huku! Hawa waaminifu si weko wenye kuzaliwa mara ya mbili, «katika Roho Mutakatifu» na hakuna namna kuwa «wana wa Mungu», na wataokolwa kama watafuata na wataitii bila kuona wale waaminifu wanafata kundi wa kwanza.. Yehova alianza kuwalokota tangu ku mwaka 1931 na kabisa tangu ku mwaka 1935.

Hakuna namna kupata sisi ufafanusho ukosefu sawa kwa ufafanusho yao ya Kitabu ya Madiko Takatifu. Lakini juu ya hii fundisho, utaona mingi mu sura wa tisa.

## 1. MAFANANISHO YA KANISA YA KRISTU

Kupatana na mafundisho ya Washuhuda ya Yehova, kisha lufu ya Mitume ya Kristu «ilinenepa uzulumu na zambi duniani na ilizambalala uzima ubaya wa zambi» ndani ya Kanisa; kwa hivyo Kanisa ya Kristu ilisimama kuwa kitu ya Mungu na ilikuwa kitu ya shetani (!) Wanaandika, utoaji na uzulumu na zambi ilinenepa na chongo yake ilifika mu milele wa inne, wakati Konstantino Mkubwa mufalme ya muji Konstantinopoli «aliumba» dini ya Kristu (Kristianisme). Maneno haya ya uwogo kabisa wanaandika na wanasadiki juu ya Kanisa ya Kristu.

Lakini Kanisa ya Kristu na ya Madiko Takatifu haina ushirika kimoja na mafundisho ya Washuhuda ya Yehova. Mafananisho wa kweli ya Kanisa kupatana na Madiko Takatifu ni sawa inafuata:

1) Kanisa wa kweli ya Kristu **n i M o j a**: Kanisa moja, Kundi moja na muchungaji mumoja, Mwili moja na Ufalme moja (tazama: Matayo 16, 18. Yoano 10, 16. Wa Roma 12, 5. Marko 1, 14-15 na ma fasi ingine). Kristu hasikuachana waaminifu wake ya ma kundi wa wili: wale wanzuri wa mbingu na wale wabaya wa inchi. Watu wote waliitwa waingie ndani ya Kanisa moja Yake: **«Kujeni kwangu ninyi wote.. . » (Matayo 11, 28).** Kuhubiri ya Kristu na Mitume ilinyolokwa mbele ya watu wote bila uchanisho.

Ufananisho hii: «kundi dogo» (Luka 12, 32), wanaitumia Washuhuda wa Yehova juu ya 144. 000, inanyolokwa kwa wakristu wote, kwa sababu wakristu wenye wanasikia na wanaamini nini, ni daima wadogo. Tena na hii sauti ya Kristu: «Na nina kondoo wengine, wasio wa zizi hili.. . », hii sauti wanaitumia juu ya kundi yao wa mbili, nikusema juu ya mataifa yote, lakini haina hivi. Hii sauti ya Kristu Huyu alisema hapana juu ya kuachanisha watu ndani ya ma kundi mbili, lakini kupindua juu ya kuifanyishia **u m o j a** : Na nina kondoo wengine, (wenye sanamu na wapagano) wasio wa zizi hili (nikusema lupango wa Yudea), sharti niwalete vile, na watasikia sauti yangu; na watakuwa kundi moja, na muchungaji mumoja» (Yoano 10, 16), Kweli, Kristu aliharabisha ma kundi wa wili (Wa Yuda na wapagano) na aliumba Kundi moja, Kanisa yake, «hapana Muyunani wala Muyuda, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mugeni wala mushenzi, mutumwa wala aliye huyu; lakini Kristu ni yote, na katika yote» (Wakolosayi 3, 11).

2). Kanisa ni **W a. M i t u m e (Apostoliki)**. Iliumbwa paka mara moja kwa milele, hile siku ya Kushuka Roho Mutakaitfu dunaini (Pentikosti), «mumejengwa juu ya musingi wa Mitume na manabii, naye Kristu Yesu mwenyewe ni jiwe kubwa la pempeni» (Wa Efeso 2, 20). Musingi wa Mitume ni ufananisho kubwa ya Kanisa wa kweli. Kanisa Orthodokse ni Kanisa wa Mitume (Apostoliki) na inaendelea uzima yake katika nuru ya Roho Mutakatifu katikati ya wamilele wote na inaitwa «Orthodokse», nikusema «fundisho wa kweli» juu ya kuachana na ma kanisa ya wa uwogo. Kupinduwa, «kanisa» ao kusema kupita nzuri: Kundi ya Washuhuda ya Yehova iliumbwa mu mwaka 1870 ( nikusema wa milele 19 karibu kisha Mwanzo ya Kanisa

yetu (Pentikosti) ku mkubwa yao, mtu moja mwenye biashara, toka kabila ya Ebrania na hakuna namna kusadiki watu ya kama Kundi yao ni Kanisa ya Kristu.

3) Kanisa ya Kristu ni **w a. m i l e l e. n a. i s i y o. k u h a r a b i k a,** kupatana unabii wa juu ya Nabii Danieli (2, 44-45) na ukikisho ya Kristu ya kama, «wala milango ya Hadeze haitalishinda» (Matayo 16, 18). Na hii fundisho ni wa kweli, kwani musingi yake ni Kristu na Mitume na Huu Kanisa ni Mwili wa Kristu. Basi, hakuna namna kuwa wakati, bila kuishi na kuwa Kanisa Yake, tangu siku ya Pentikoste mupaka mwisho ya wa milele. Basi, «kanisa» ao kusema kupita nzuri Kundi ya Washuhuda ya Yehova, ambaye haikukuwe ya wa milele 19, hakuna namna kusadiki ya kama hii ni Kanisa ya Kristu

**4)** Kanisa ya Kristu ni **m u l i n z i. y a. f u n d i s h o. w a. k w e l i :** Inakamata na inachunga Kanisa ya Kristu fundisho ya kweli katikati ya ma milele wote, kwani:

a) Kristu mumoja, katika malako Yake, atakuwa «pamoja nanyi siku zote hata mwisho wa dunia» (Matayo 28, 20), kwani Huyu ni Kichwa ya Kanisa Yake.

b) Kanisa itakuwa daima chini ya uongozi ya Roho Mutakatifu: «Lakini wakati anapokuja yule Roho wa kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli» (Yoano 16, 13). tena na Mtume Paulo anaandika ya kama Kanisa ni: «nguzo na musingi wa kweli» (barua ya kwanza kwa Timotheo 3, 15).

Mafundisho ya Washuhuda ya Yehova, basi, ya kama Kanisa wa Mitume iliharabika na ilikuwa kitu ya shetani na ya wogo kabisa na matusi, kwa sababu kwa ajili ya sauti yao anachabuliwa Roho Mutakatifu, lakini Roho Mutakatifu anaongoza Kanisa kwa njia ya kweli. Neno ya Mungu anatwaambia ya kama wataonekana mu wakati ya mbali mbali Wanabii wa uwogo na walimu wa uwogo na watalanda watu wingi na watahubiri mubaya na watakokota watu ku mukongo yao na watawafundisha mafundisho mabaya na ya upotevu. (Matayo 7, 15 na 24, 5, 11, 23-24. Matendo 20, 29-30. Barua ya mbili ya Petro 2, 1). Yesu Kristu mukusema kwao alisema: «Angalieni musidanganyiwe na mutu) (Matayo 24, 4). Vile anasema na leo katikati kanisa Yake: «Angalieni musidanganyiwe na Washuhuda ya Yehova, Walimu wa uwogo na wanabii wa uwogo, kwa sababu neno ya Mungu inawahukumu: (Tito 3, 10-11. Wagalatia 1, 8-9. barua ya mbili kwa WaKorinto 11, 13-15 na barua ya mbili ya Petro 3, 16).

5) K **a n i s a. n i. m w i l i. w a. m a t e n g e n e z o. n a. w a c h u n g a z i,** wenye weko na ufwasi wa Mitume. Kweli, tunatazama ndani ya Madiko Takatifu ya kama Mitume walitumika katika uongozi ya Roho Mutakatifu na walitengeneza Kanisa na walipadirisha ya kila muji na mukini Wa askofu, Wapadri na wa Shemasi (Matendo 14, 23. 20, 28. Barua ya kwanza ya Timotheo 3, 1-7 na 8-13 na Tito 1, 5-9 na Wa Efeso 4, 11-12). Hii zawadi ya uchungazi ilijitoa toka Roho Mutakatifu kwa kuweka Mitume mikono yao pa vichwa vya wale watapadirishwa (Barua ya kwanza ya Timotheo 4, 14 na barua ya mbili ya Timotheo 1, 6). Wa Mitume, ila tu zawadi ya uchungazi yao, waliwapatia kwa wale wa askofu waliwapadirisha na zawadi ya upadirisho na kwa hivi na hawa katika mustari wao, wataweza kupadirisha wachungazi wengine ( Tito 1, 5 na barua ya kwanza ya Timotheo 5, 22) na hawa watu wengine na hii mustari inafika mpaka leo.

Kanisa Orthodokse alichunga kabisa hii ufwasi wa Mitume, kw ahivyo wa askofu na wapadri yake weko na upadirisho kwa kunyoloka toka Mitume. Kupindua, wakubwa ya Washuhuda ya Yehova hawaweze kuchunga zawadi yao hata moja toka Roho Mutakatifu, kwa sababu hakuna Mtume ao mufwasi ya Mitume aliwapatia upadirisho na zawadi ya Roho Mutakatifu.

Juu ya Ufwasi wa Mitume, uwezo na uzima takatifu ya waaskofu ya Kanisa Yesu Kristu anatwaambia: **«Yeye anayesikia ninyi, anasikia mimi; naye anayewakataa ninyi anakataa mimi; naye anayekataa mimi, anakataa yeye aliyenituma» (Luka 10, 16, na «Yeye anayewapokea ninyi, ananipokea mimi naye anayenipokea mimi anamupokea yeye aliyenituma» (Matayo 19, 40).** Lakini na Mtume Paulo anaandika ya kama Mungu «alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wahubiri wa Habari Njema; na wengine kuwa wachungaji na walimu; kwa kusudi la kukamilisha watakatifu, kwa kazi ya

utumishi hata mwili wa Kristu (nikusema Kanisa) ujengwe» (Wa Efeso d, 11-12). Na pa fasi ingine, anatushauria: **«Tiini wenye kuwaongoza ninyi na kuwanyenyekea; maana wao wanaangalia kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoka hesabu, ili wapate kufanya hivi kwa furaha, wala si kwa huzuni: maana hii itakuwa kwenu pasipo faida» (wa Ebrania 13, 17).**

**6) K a n i s a. n i. M w i l i. w a. K r i s t u:** Kanisa haya wa Mitume haina paka usanyiko moja ya waaminifu, lakini ni Mwili «wa siri», na Kichwa yake ni Kristu na wafwasi waaminifu wake (Wa Roma 12, 5. Barua ya kwanza ya wa Korinto 12, 12-27 na wa Efeso 1, 22-23. 4, 15-16. 5, 23, 30 na Wakolosayi 1, 18, 24). Sawa vile vipande-vipande ya mwili moja wekona unganisho moja katikati yao, vile na waaminifu, juu ya kuwa vipande vya mwili moja wa siri, inayeitwa Kanisa, inapashwa kuunganwa pamoja na hii mwili na hivi watachukua toka uzima yake. Hii Mwili (Kanisa) inatokea toka Mungu na Mutu Yesu Kristu na ni ungano katikati ya Mungu (Kristu) na watu (waaminifu). Tunda yake ni ya kama uzima kimungu ya Kristu inajitoa na kwa Mwili ingine, nikusema kwa waaminifu, wenye katika Neema wanaishi tangu sasa mu uzima wa milele na ni tangu sasa wakaaji ya ufalme wa mbinguni na walipata wokovu hile inajitoa ku Kristu. Basi, paka lwa ungano yake pamoja na huu Mwili ya Kristu (Kanisa) anaweza kila mutu kuokolewa. Kwa hivyo Wapadri ya kanisa yetu walisema ya kama, «Inje ya Kanisa hakuna wokovu». Basi, wanapotea wakati yao Washuhuda ya yehova, kwani wanakataa na wanachabula Mwili ya Kristu, Kanisa yake na wanafata «ma kanisa ya wogo», yenye walijenga watu wa Ebrania, mbele ya miaka miya moja (100).

**7) K a n i s a. i n a c h u n g a. n d a n i. y a k e. w a t u. w a t a k a t i f u. n a. w e n y e. z a m b i:** Washuhuda ya Yehova, wenye wanakokota waaminifu orthodokse, wanakankamana kuonyesha ya kama Kanisa yetu haina kanisa ya Mungu, lakini ni Kanisa ya Shetani, kwa sababu ndani yake wanaingia na watu wenye zambi. Ssisi tunawajivu hivi ya kama ndani ya Kanisa ya Kristu watakuwa ma siku zote waaminifu wa kweli na wasiyoimani nguvu, watakuwa watakatifu na wenye zambi, watakuwa wakirtu wenye uzima na wenye kufa katika nafsi yao, lakini uchanisho yao na hukumu ya wenye zambi itafanyika hile siku ya Hukumu ya Mwisho. Hivi na Madiko Takatifu inatufundisha:

**a)** Kristu alikuwa na wanafunzi kumi nambili, lakini moja katikati yao alibaki bila toba na alikuwa mwivi na mutoaji.

**b)** **«Kwani wao wanaoitwa ni wengi, lakini wale wanaochaguliwa ni wachache» (Matayo 22, 140).**

**c)** **«Si kila mutu anayeniambia: Bwana, Bwana, atakayeingia ufalme wa** mbinguni; lakini yeye anayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni» (Matayo 7, 21).

**d)** Kupatana na mifano ya Kristu, Kanisa umefanana na shamba, iko na ngano na magugu (Matayo 13, 24-43); umefanana sawa «mukila» waliotupwa katika bahari ya kukusanya samaki «wabaya na wema (matao 13, 47-50); umefanana sawa «mulimaji» anatazama ma mbegu ya ngano ilipotea (Luka 8, 14); kisha mufano ya talanta, lakini moja asikukuwe stahili kwa mapendo ya Bwana wake (matayo 25, 14-30); kwa mufano ya ndo wa ufalme, Mufalme (Mungu) «alisanyika «waovu na wazuri» (Matayo 22, 1-13); kwa mufano ya mabikira kumi, lakini wa tano hawakukuwa wenye stahili (matayo 25, 1-13) na maana yao ni hawa waaminifu weko ndani ya kanisa bila kuwa wenye stahili.

## 2. MA FUMBO TAKATIFU YA KANISA

Ndani ya hii fundisho ya ma Fumbo ya Kanisa ya kristu haipashwe kusema masauti mengi, kwa sababu imani yao ni pamoja na imani ya fundisho ya Kanisa. Nikusema kama wanakataa mafundisho yote ya Kanisa ya Kristu, wanakataa na ma Fumbo yake yote. Washuhuda ya

Yehova, kwani wanakataa Kanisa wa kweli muzima, wanakataa na ma Fumbo matakatifu yake. Hii imani yao inatwaambia ya kama Washuhuda ya yehova wanatokea toka dini ya Protestante.

Ya kwanza Imani wa Kristu yote ni Fumbo moja kubwa. Kwa hivyo, neno ya Mungu inaiita «siri (Fumbo) ya Mungu, ndiye Kristu (Wa Kolosayi 2, 2), «siri ya Kristu» (Wa Kolosayi 1, 27. 2, 2-3 na 4, 3), «siri ya mapenzi wa Mungu» Wa Efeso 1, 9-10), «siri iliyofichwa tangu zamani ndani ya Mungu aliyeumba vitu vyote» (Wa Efeso 3, 8-10 na 14-19. «siri ya Habari Njema» (Wa Efeso 6, 19) na «sori ya utawa» (Barua ya kwanza ya Timotheo 3, 16). Lakini juu ya kusikia na kupata sisi hii «siri ya Mungu» tuko na lazima ya mwangaza ya Neema Takatifu ( Wa Efeso 1, 16-19).

Kwa hii neno, matendo wa utakaso ya Kanisa yetu, kwa ajili yao mutu anaongozwa kwa ungano na Neema takatifu, wanaitwa ma Fumbo Matakatifu. Hapa tutaandika na haraka juu ya ma Fumbo tatu: Ubatizo, Upadirisho na Komonyo Takatifu kwani, kwa ajili yao inatokea uzima wa roho ya Kanisa.

## A. UBATIZO

Kupatana na Madiko Takatifu Ubatizo inalazimishwa kwa wokovu wetu, kwani ni Fumbo na ndani yake huyu mutu anayebatizwa «anakufa» katika roho yake wa zamani kwa uwezo ya Neema Takatifu anachukua katika Kristu maondoleo ya zambi, «anafufua» mu uzima moja mupya kwa kutembea uzima mupya na mavazi ya Kristu. Ulazimisho ya hii Fumbo inaonekana kwa hii maneno ifwatayo:

1) **«Mutu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu» (Yoano 3, 5).**
2) **«Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu» (Matayo 28, 19).**
3) **«Anayeamini na kubatizwa ataokolewa» (Marko 16, 16).**
4) **«Tubuni mukabatizwe kila mumoja kwa jina lake Yesu Kristu, mupate ondoleo la zambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mutakatifu» (Matendo 2, 37-38).**
5) **«Ao hamufahamu, sisi sote tuliobatizwa katika Yesu Kristu, tulibatizwa katika kufa kwake? Hivi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika kufa: hata kama Kristu alivyofufuka toka wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo tutembee katika upya wa uzima vilevile» (Wa Roma 6, 3-4).**
6) **«Maana ninyi wote muliobatizwa na kuingizwa katika Kristu, mumevaa Kristu» (Wa Galatia 3, 27).**
7) **«Kama vile Kristu alivyopenda Kanisa, na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake; apate kulitakasa, akiwa amelisafisha kwa maji katika neno» (wa Efeso 5, 25-26).**
8) **«Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyafanya lakini kwa rehema yake alituokoa, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa mupya na kufanywa upya na Roho Mutakatifu» (Tito 3, 5).**
9) **«.. . Mufano wa maneno haya ni ubatizo unaowaokoa ninyi sasa, si kuondosha uchafu wa mwili, lakini jibu la zamiri safi mbele ya Mungu, kwa njia ya ufufuko wa Yesu Kristu» (barua ya kwanza ya Petro 3, 21). Nikusema Ubatizo sawa mufano ya maji ya hile wakati ya Noa na Safina yake, vile na maji inatuokoa katika neema ya Mungu.**

Kwa sababu, basi, Ubatizo ni amri safi ya Kristu (Matayo 28, 19, Marko 16, 16), kwa sababu ni lufu ya mutu wa zamani na uzalio umya yake (yoano 3, 5. WaRoma 6, 3-4, kwani ni «mavazi» ya Kristu (Wa Galatia 3, 27) na Utakaso ya waaminifu ( Wa Efeso 5, 25-26), kwani inatoa ondoleo ya zambi (Matendo 2, 38) na inaokoa mutu aliyeamini kwa Kristu (Tito 3, 5 na barua ya kwanza ya Petro 3, 21), inatuwaambia ya kama hii Fumbo niulazimisho kabisa kwa

wokovu wetu na katika hii Fumbo inatembea Neema Takatifu ya Mungu. Ku mwisho, Hii Fumbo ni mulango ya mutu kwa kuingia Kanisani ya Kristu. Kweli, toka Kitabu ya Matendo tunaona ya kama ninyi wote waliamini kwa kuhubiri ya Mitume, walibatizwa: Kwa mufano, tazama Matendo 2, 41. 8, 12, 36-38. 10, 48. 16, 15, 33. 18, 8). Tena na huyu Mtume Paulo «chombo ya uchuguwo» ya Mungu (Matendo 9, 18 na 22, 16).

## Ubatizo mu kipimo kidogo

Mara mengi Washuhuda ya yehova wanachukia kanisa Orthodokse kwa ajili ya Ubatizo na kipimo Kidogo na sawa bunduki yao wanaleta shairi ya Habari Njema: **«Anayeamini na kubatizwa ataokolewa» (Marko 16, 16**). Wanasema, «watoto wahaweze kuamini, na kwa hivyo paka watu wakubwa wanapashwa kubatizwa».

**1)** Ubatizo mu kipimo idogo haina kupindua mu shairi ya (Marko 16, 16). Maneno haya waliisemwa ku mwanzo kabisa ya Dini ya Kristu (Kristianisme), kwani hile wakati kuhubiri ilinyolokwa kwa watu wakubwa, wenye bado kuwa Waaminifu waorthodoksi na wenye walipashwa kuamini na kisha waliweza kubatizwa. Kisha miaka mengi, wakati waaminifu walizala watoto, waliweza kuwabatiza, kwa sababu hawa watoto walikuwa watoto ya kizazi ya waaminifu na watu wa Kristu.

**2)** Maneno ya Kristru: **«Mwache watoto wadogo waje kwangu; musiwakataze, sababu ufalme wa Mungu ni kwao wa namna hii» (Luka 18, 15-16),** wanatufundisha juu ya ubatizo ya kipimo kidogo, kwani Kristu alipokea watoto wadogo.

**3)** Mustari-Bunduki nguvu juu ya ubatizo na kipimo kidogo ni Tohara, iliyekuwa kisha ma siku mnane tangu siku ya ubatizo ya mtoto moja mwanaume mu kabisa ya WaEbrania. Hii zoezo ni mufano ya Ubatizo. Kwa sababu, basi, tuhara sawa alama, na mufano ya Ubatizo alifanyika kwa watoto, hivi na Ubatizo inafanyika kwa watoto wadogo. Juu ya nini zamani ilifanyikwa tohara kwa watoto wadogo na sasa Ubatizo haipashwe kufanyika kwa watoto wadogo?

**«Na ninyi mumetimilika katika yeye aliye kichwa cha falme zote na mamlaka. katika yeye mulitahiriwa vilevile kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuondosha mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristu, mukizikwa pamoja naye katika ubatizo, na katika huu mulifufuliwa pamoja naye kwa kuamini nguvu za Mungu, aliyemufufua toka wafu»** WaKolosayi 2, 10-12 na Mwanzo 17, 10-14). Basi, sasa, mu wakati ya dini ya Kristu tukona tohara umya, «tohara» ya Kristu, isiyofanyika kwa mikono», na inasharikiwa na Ubatizo. Itakuwa neno isiyo na akili kama mtu moja atapokea tohara wa zamani pa mwili ya watoto wanaume na Hii «tohara» wa roho wa sasa (Ubatizo) atakataa.

4) Lakini na mapito katikati ya Bahari Nyekunda inaitwa topa watu wa Ebrania «Ubatizo» na maana yake ni Ubatizo wa Kristu**: «Kwa sababu ndugu wangu, shitaki mukose kujua ya kama baba zetu walikuwa wote chini ya wingu, wote wakapita kati ya bahari: wote wakabatizwa na Musa katika wingu na katika bahari; wote wakakula chakula kile cha roho» (barua ya kwanza kwa WaKorinto 10, 1-3).** Kwa sababu, basi, taifa muzima wa Israeli, (nikusema pamoja nao walikuwa na watoto wao) «walibatizwa katika bahari», juu ya nini watoto wa sasa hawaweze kubatizwa na hawaweze kupokea Ubatizo Takatifu?

Kupatana na hii mafundisho wa juu inatosha onyesho ya kama Kanisa Orthodokse inatimiza nzuri kabisa na hii Ubatizo ya kipimo kidogo.

Ku mwisho, inaonekana safi, ya kama, kwani Ubatizo ni Fumbo na uletaji ya neema takatifu kwa wokovu, hakuna namna kuitumika kila mutu, lakini paka toka wale watu Mungu aliwapatia hii uwezo: Maneno ya Kristu: **«Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu» (Matayo 28, 19),** hasikuseme kwa watu wote, lakini kwa Mitume. Hawa kisha, katika Fumbo ya Upadirisho,

walipatia hii uwezo na zawadi ya uchungaji kwa wafwasi wao, waaaskofu na wapadri ya Kanisa: (Matendo 14, 23. Barua ya kwanza ya Timotheo 4, 14 na barua ya mbili ya Timotheo 1, 6 na Tito 1, 5). Wa askofu na wapadri ya Kanisa Orthodokse wanachunga nzima ufwasi ya Mitume na kwa hivyo wanaweza kufanya Ubatizo bila kosa. Kupindua «wa askofu» ya Washuhuda ya Yehova hawakuwana ufwasi ya Mitume, kwani kundi yao ilionekana mu milele wa kumi na tisa (19) na hawaweze kufanya Ubatizo-Fumbo Takatifu. Wanafanya paka utumishi moja unyofu, wa alama sawa mufano, lakini bila Neema Takatifu.

## B. UPADIRISHO

Washuhuda ya Yehova wanakataa Fumbo ya Upadirisho: 1) Kwa sababu ndsani ya Agano Jipya paka Kristu, wanasema, anaitwa «Padri» na «Kuhani». Na (2) kwa sababu taifa muzima ya Mungu inaitwa «ufalme wa makuhani» ao «wafalme na wapadri». (Barua ya kwanza ya Petro 2, 5, 9 na Ufufuo 5, 10) na haina kundi moja ya kuachana.

Pa mustari ya kwanza, ya kama Kristu anaitwa «padri» na «Kuhani» tunaitika na sisi. Lakini kwa hii mustari ya mbili, tunaangalia ya kama na mu Agano la Kale taifa ya Mungu aliitwa «Ufalme wa makuhani» (Kutoka 19, 6), bila kuzibiya hii Kundi na kundi ingine mara moja « (Kutoka 28, 1, 29, 4-44). Kwa hii namna umoja «Upadirisho»ya Wakristu, haizibirie Upadirisho ya Waskofu, wapadri na washemasi. Kweli, zawadi moja ingine ilijitoa kwao toka Roho Mutakatifu, katika Mitume, katika upadirisho, sawa tunaona hivi na mu Madiko Takatifu:

**1) «Mujiangalie wenyewe, na kundi lote, Roho Mutakatifu alilowapa ninyi kuwa wasimamishi ndani yake, mupate kulisha kanisa la Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe» (Matendo 20, 28).**

2) **«Usiache kutumia zawadi iliyo ndani yako uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee (wapadri) (barua ya kwanza kwa Timotheo 4, 14).**

3) **«Kwa sababu hii ninakukubusha, uamshe zawadi ya Mungu iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu» (barua ya mbili ya Timotheo 1, 6).**

4) **«Usiwekee mutu mikono kwa haraka, wala usishiriki kwa zambi za watu wengine.. . » (barua ya kwanza ya Timotheo 5, 22).**

5) **«Kwa sababu hii nilikuacha katika Krete, upate kutengeneza maneno yaliyobaki, na kuweka wazee katika kila muji, kama nilivyokuagiza» (Tito 1, 5).**

Kwa ajili ya maneno haya wa juu inaonyeshwa ya kama Mitume walipatia zawadi kwa wa askofu na wapadri na hawa na mustari yao, walipadirisha watu wengine na hawa watu wengine na hivi inafanyika sawa monyororo moja ya wa askofu wachungazi ya Kanisa yetu. Hii monyororo ni bila kupasuka katikati ya ma milele yote na iko **«U f w a s i. w a. M i t u m e».** Hii Ufwasi inafananisha wachungaji wa kweli na kundi ya wapadri ya Kanisa.

Hawa Wachungaji ya Kanisa hawakuwa na upadirisho kwa maugo yao, lakini wanachukua upadirisho ya Kristu, mwenye ni Kuhani mkubwa toka maugo Yake. Watu wachungaji weko Watumishi wa Kuhani Mkubwa Kristu na kwa mikono yao Huyu (Kristu) anafanya ma Fumbo Vitakatifu ya Kanisa. Kwa hivyo, kwa sababu hawakuwa na upadirisho yao, lakini wanachukua upadirisho toka Kristu, kwa hivyo na mu Agano Jipya hawaitwa wapadri kabisa, lakini wanaitwa pempeni wapadri.

1) Kristu anaitwa «Muchungaji Mukubwa», kwa sababu ni mkubwa ya wachungaji wote ya Kanisa Yake (barua ya kwanza ya Petro 5, 1-4). Paka na hii namna umoja, kwani anaitwa Kuhani na Muchungaji (wa Ebrania 4, 14), hii inatuonyesha ya kama weko na wapadri ya Kanisa na hawa weko watumishi Wake.

2) Kazi ya padri moja ni atoe kwa Mungu, toka taifa, ma sandaka na ma sala. Kristu kama Kuhani, alitoa maugo Yake sandaka kusudi kuungana dunia pamoja na Mungu (Wa Roma 5, 1 na pa fasi ingine). Lakini hii «kazi ya masikilizano» aliipatia kwa Mitume (barua ya mbili kwa

wa Korinto 5, 18), na hawa paka na hii namna umoja walichukua Upadirisho Yake. Vile inakuwa na kwa wafwasi ya Mitume (Wa askofu na wapadri) na Mitume waliwapatia katika Fumbo ya Upadirisho ma uwezo yote na hii «kazi ya masikilizano».

3) Ku mwisho, neno ya Mungu kwa Nabi Isaya, aliyesema ya kama mu wakati ya Mwokozi Mungu **«atasanyika ma taifa yote na lugha zote.. . Na vile vile nitatwaa wao kuwa makuhani na Walawi, Bwana anasema.. . » (Isaya 66, 18-21).**

Basi, ni muzuri sana ya kama wa askofu na wapadri na mashemasi ya Kanisa yetu Orthodokse wanaitwa wapadri.

Kikomo ya hawa wapadri ni watoe uvumba (ubani) na sandaka kwa Mungu ma fasi yote na ma siku zote: **«kwa maana tangu kucha kwa jua hata kushuka kwake jina langu ni kubwa katikati ya Mataifa, na kwa kila pahali wanatolea uvumba kwa jina langu, na toleo safi; kwa maana jina langu ni kubwa katikati ya mataifa, Bwana wa majeshi anasema» (Malaki 1, 11).**

Hii unabii ilitimizwa kabisa mu Kanisa Orthodokse, pahali uvumba na sandaka wanajitoa bila usimamisho. Kweli, tukona Mazababu na sandaka iliyefanyika juu yake, lakini hakuna namna kula wale watu wanaendelea kufata imani ya Wayuda (Wa Ebrania 13, 10). Hii sandaka haina ingine, paka Eukaristia Takatifu (Liturgia Kimungu na Komonyo Takatifu); ni Fumbo ya kubadilisha mukate na vinyo kwa Mwili na Damu ya Kristu. Halafu, wapadri ni hawa wa pekee wekona uwezo wafanye ma Fumbo yote matakatifu na matendo ya Kanisa yote. Hawa weko «wachungaji na walimu» aliwapatia Mungu **«.. . Na wengine kuwa wachungaji na walimu; kwa kusudi la kukamilisha watakatifu, kwa kazi ya utumishi hata mwili wa Kristu ujengwe» (Wa Efeso 4, 11-12).**

Washuhuda wa Yehova wanakataa hii mafundisho yote wa juu na wanatimia na ma jina mapya. Sawa wanasema ya kama Kristu ni musaidizi ya Yehova (Mungu) na wale watawala pamoja Naye wanapakaliwa.. . . . na wanaitwa Wasaidizi ya wapadri na hawa watatumika mu kanisa wa roho mu mbinguni.

## Jina ya: «Baba (Padri»

Washuhuda wa Yehova wanasimama pa shairi ya (Matayo 23, 9**): «Wala musiite mutu baba yenu duniani; kwa sababu mumoja ni Baba yenu, aliye mbinguni**» na wanasitaki wapadri waorthodoksi kwa sababu wanatimia jina «padri». Lakini mu Agano Jipya tunapata hii jina na juu ya wa baba wazazi na juu ya wa baba wa roho:

1) Wa Baba wazazi:

a) **«Baba yenu Abrahamu alifurahi.. . » (Yoano 8, 56); b) «Baba Abrahamu, unirehemu, utume Lazaro atie incha ya kidole chake. . . » (Luka 16, 24, 30).**

**c) «Kwa sababu ndugu zangu, sitaki mukose kujua ya kama baba zetu walikuwa wote chini ya wingu.. . » (barua ya kwanza kwa wa Korinto 10, 1).**

**2) Wa Baba wa roho:**

**a) «Kwa sababu hata muna walimu elfu kumi katika Kristu, lakini hamuna baba wengi; kwa sababu katika Kristu Yesuniliwazaa ninyi kwa Habari Njema» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 4, 15).**

**b) «watoto wangu wadogo, ninao tena uchungu kwa ajili yenu hata Kristu atakapoonekana ndani yenu» (wa galatia 4, 19).**

**c) «Kwa Timotheo, mwana wangu wa kweli katika imani: Neema, na rehema, na salama, kutoka kwa Mungu Baba na kwa kristu Yesu Bwana wetu» (barua ya kwanza kwa Timotheo 1, 2) (Tazama na Tito 1, 4. Filemono 10.** Barua ya mbilikwa wa Korinto 6, 13 na 12,

14. barua ya kwanza ya Yoano 2, 28 na 5, 21), pahali jina «mutoto» inatuonyesha ya kama ni ubaba wa roho.

Ni kweli ya kama Kristu anakataza utimio ya jina «Padri-Baba», kama hii jina inatimiwa na maana ukamilifu, kwa sababu Baba na maana ukamilifu ni paka moja, Mungu; lakini watu wanaweza kuwa wababa wa roho na maana hapana ukamilifu. paka na hii maana umoja Mutume Paulo anaita «Baba» maugo yake mu shairi: (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 4, 15).

## Mambo ya malipo ya wapadri ya Kanisa yetu

Washuhuda ya Yehova wanashitaki na wanachukia wapadri wetu (wa askofu, wapadri na mashemasi) kwa sababu wanachukua malipo (mushahara) kwa kazi ya kupashwa yao, lakini Kristu alisema **«Ponyesheni wagonjwa, fufuleni wafu, safisheni wakoma, toeni pepo wachafu; mulipoka bule, toeni bule» (Matayo 10, 8).** Lakini mushahara ya wachungaji ya Kanisa yetu ni katika sheria, kwa sababu (ila tu lazimisho ya kuchunga jamaa yao) neno umoja ya Mungu inaleta sheria juu ya kuishi maisha yao ku saidio ya ma hekalu:

**«Askari gani anayetumika, wakati wo wote, kwa mushahara wake mwenyewe? nani anayepanda shamba la mizabibu, pasipo kula matunda yake? ao nani anayechunga kundi, pasipo kunywa maziwa ya kundi? .. . (shairi 13):** Hamujui ya kwamba wale wanaofanya kazi ya hekalu wanakula sehemu ya vitu vya hekalu, na wale wanaotumikia kwa mazabahu wanashirikiana vitu vya mazabahu? Hivi Bwana aliagiza ya kwamba wale wanaohubiri Habari Njema wapate maisha yao kwa Habari Njema» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 9. 7-14). Na pa fasi ingine Kristu inatufundisha ya kama **«mutenda kazi anastahili kupewa mushahara wake» (Luka 10, 7).**

Pa hii fasi inaonekana kabisa roho mubaya ya washuhuda wa Yehova, kwa sababu wanashitake wachungaji wa roho zetu, lakini na hawa wanaipokea na wanafanya hivi. Kwa mufano, watu watu wenye wananunua vitabu vyao na wanaitwa «ma shemasi» ao Mahubiri» wanapewa mushahara toka kundi yao juu ya maisha yao. Paka mu mwaka 1981, kwa mufano, tulipata ujulisho ya kama walipewa malipo dollario: 22. 000. 000 juu ya watumishi wao: «wa askofu» na «mitume» ya Washuhuda wa Yehova. Kama tutawauliza juu ya nini wanaripa watumishi wao, watatujibu paka na ma shairi haya na sisi tuliandika yulu. Lakini hii hali yao iko ao haiko udanganyifu na roho kibaya? Juu ya nini, basi, wanataka kuchukia na kushitake wapadri waorthodoksi?

## C. EUKARISTIA KIMUNGU (KOMUNYO TAKATIFU)

Eukaristia Kimungu, nikusema ushirika ya Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu ni roho ya Kanisa ya kristu. Kila mara askofu na wapadri wanafanya Huu Fumbo ndani ya Liturgia Kimungu, katikati ya makusanyo ya waaminifu, tunakikiri Fumbo ya wokovu kwa Kristu na tunapewa kwa majengo ya Mwili ya Kristu, nikusema Kanisa yake: **«Kwa sababu sisi tuko wengi ni mukate mumoja na mwili mumoja: kwa sababu sisi sote tunapokea sehemu ya ule mukate mumoja» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 10, 7).** Fumbo ya Komunyo Takatifu alitupatia Yesu Kristu, hile usiku ya Karamu Kubwa, wakati Kristu mumoja alibadilisha mukate na vinyo kwa Mwili na Dama Yake, mukuwaambia wanafunji wake: **«Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi» (Luka 22, 19 na Barua ya kwanza kwa wa Korinto 11, 24-25 na Matayo 26, 26-29).**

Washuhuda wa yehova wanakataa Huu Fumbo ya Eukaristia na wanasadiki ya kama haina ya kweli Mwili na Damu ya Kristu, lakini ni alama Yake. Lakini maneno ya Kristu ni safi kabisa:

1) **«Twaeni mule; huu ni mwili wangu (hasiseme huu ni alama ya mwili yangu). Akatwaa Kikombe akashukuru, akawapa akisema: Kunyweni, ninyi wote, kwa maana hii**

**ni damu ya Agano iliyomwangika kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la zambi (Hasiseme hii ni alama ya damu yangu). (Matayo 26, 26-29).**

Kama munataka kujua namna gani Washuhuda wa Yehova wanaandika hii shairi ya Komunyo Takatifu, musomeni: «Twaeni mule.. . huu mukate inaonyesha mwili yangu, nitaipatia wakati nitakufu kwa ninyi wote.. . Kunyweni, ninyi wote, hii vinyo inaonyesha damu yangu.. . » (Mu Kitabu yao: Mukusikia Mwalimu Mukubwa).

**2). «Kweli, kweli ninawaambia ninyi, kama hamukuli mwili wa Mwana wa watu, na kunywa damu yake, hamuna uzima ndani yenu. Yeye anayekula mwili wanmgu, na kunywa damu yangu, ana uzima wa milele; nami nitamufufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinunywa cha kweli. Yeye mwenye kula mwili wangu na kunywa damu yangu anakaa ndani yangu, nami ndani yake» (Yoano 4, 53-56).**

Mwili ya Bwana Yesu ni pamoja na Roho Mutakatifu muzima (Yoano 1, 32-33 na 3, 34), kwa hivyo anaweza kuleta uzima, sawa vile analeta uzima upya katika roho na Roho Mutakatifu. Kupindua kila mwili ingine haileta faida ( Yoano 6, shairi 63). Pa hii fasi ni ufananishwa machanisho katikati ya jina «mwili yangu» ya ma shairi 53-56 na jina «mwili» ya shairi 63.

Wenye kusikia ya Kristu walisikia bila kusikia maana ya maneno ya Kristu na walikuazwa, mukusema hivi: **«Mutu huyu anaweza namna gani kutupa sisi mwili wake tule? (Yoano 6, 52). Na Kristu, hasiwapatie mafafanusho wa alama, lakini anawaambia kusikia katika herufi maana ya maneno Yake, bila kuwaza kama watakuazwa tena na wanafunji Wake. (ma shairi 60, 66, 67).**

3) Lakini na Mutume Paulo anatufundisha juu ya ukweli ya huu Fumbo Kimungu: **«Kikomba cha baraka tunachobariki, si ushirika wa damu ya Kristu? Mukate tunaovunja, si ushirika wa mwili wa Kristu? » «Basi kila mwenye kula mukate huu na kunywa kikombe cha Bwana isivyostahili atakuwa amejipatia kosa juu ya mwili na damu ya bwana. Lakini mutu ajihukumu mwenyewe, na kisha apate kula mukate na kunywa kikombe. Kwa sababu yeye anayekula na kunywa, asipostahili, anakula na kunywa hukumu kwake mwenyewe, asipotambua mwili wa Bwana» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 10, 16. na 11, 27-29).**

Ufafanisho moja wanaipatia Washuhuda wa Yehova ni ya kama katika «mwili» ni maana Kanisa. Lakini hii uwazo yao ni ya kutupa mara moja, kama tutasikia ya kama «mwili» inaingia huku pempeni ya jina «damu», kwa hivi hakuna namna kufafanusha jina «mwili» sawa Kanisa», kwa sababu Kanisa haikuitwe hata «damu» ya Kristu.

Kwa sababu Eukaristia Kitakatifu ni «ya kukata» Mwili ya Kristu na «kumwanga» Damu Yake, inatuonyesha ya kama ni ya kweli «sandaka», inayejitoa kwa Mungu Baba. Lakini, kila mara inafanyika hii Sandaka, haifanyike sandaka upya ya Kristu, kwa sababu Kristu alitoa sandaka uzima na Mwili Yake paka mara moja pa Musalaba wake kwa milele (Wa Ebrania 9, 26), lakini inaonekanana mbele ya macho yetu hile sandaka ya Golgota katika namna siri na isiyokusikiwa kwa sisi. Mutume Paulo wakati anaandika juu ya Eukaristia Kimungu sawa sandaka ni maana yake: **«Tuna mazabahu, nao wanatumikia katika hema hawana ruhusa kula vitu vyake» (Wa Ebrania 13, 10).**

Washuhuda wa Yehova wanaita tena na maneno ya Kristu: **«Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi» (Luka 22, 19)** juu ya kusema ya kama mu Komunyo Takatifu inafanyika unyofu moja ukumbusho ya Kristu na hapana Fumbo. Sisi tunawajibu ya kama «ukumbusho» inayenyoloka kwa Uso ya Kristu, iko na maana kupita mingi na wa chini na inaonyesha ungano na ushirika na Ye, ushirika mu uzima yake. Sawa onyesho tunaweza kukumbuka shauria ya Mutume Paulo aliisema kwa Timotheo: **«Mukumbuke Yesu Kristu, aliyefufuka toka wafu, wa uzao wa Daudi, kama inavyosema Habari Njema yangu» (barua ya mbili ya Timotheo 2, 8).**

«Ninakumbuka Kristu» kwa akili ya Mutume Paulo ni maana ninaishi katika Kristu, ninashirika uzima Yake: **«Nimesulubiwa pamoja na Kristu, lakini ni hai; wala si mimi, lakini Kristu ni hai ndani yangu» (wa Galatia 2, 20), «Siku zote tukichukua katika mwili kuuawa kwa Yesu, hata uzima wa Yesu vilevile uonyeshwe katika miili yetu» (barua ya mbili kwa wa Korinto 4, 10).** Ukumbusho, basi, inayenyolka kwa Kristu, ni maana ushirika mu uzima Yake. Paka na hii maana na tendo ya Eukaristia Kimungu haina paka ukumbusho unyofu ya Kristu, lakini ni ushirika wa roho pamoja na Mwili na Dama Yake.

Huu Fumbo juu ya kuwa wa kweli inapashwa kuimaliza wapadri waorthodoksi ya Kanisa Orthodokse yetu. Basi, Washuhuda wa Yehova, kweli wanatazama tendo yao sawa Karamu wa ukumbusho na wanaifanya paka mara moja kila mwaka, kwani wanatazama ya kama ni paka tendo moja wa alama na kwa ukumbusho.
Kutoka ma Fumbo hawa wa tatu inatokea na ma Fumbo ingine: Nikusema: Khrisma (Kupakaa), Maungamo, Fumbo ya Mafuta takatifu na ingine. Kwa hivyo, tunawaza ya kama ni ya bure kuendelea juu ya ma Fumbo ingine, kwani hule musomaji wa kweli ya Madiko Takatifu, kama atapokea na atasadiki haya ma Fumbo tatu, ataweza kupokea na kuamini na kwa ingine.

# 9

## MATENDO YENYE YATAKUJA - YA KUJA WA MBILI YA KRISTU DUNIANI- «UFALME WA MIAKA ELFU»

Washuhuda wa Yehova wanasadiki ya kama: 1) Ya kuja ya Kristu ilikuwa mu mwaka 1914, na 2) Wanaongojea siku kwa siku nvita munene inayeitwa Armagedoni na kisha itaanza ufalme wa Kristu ya miaka elfu moja.

Walisimamisha mu mwaka 1914, kisha mazungumuzo na makelele yao mengi. Kupatana fundisho hii yao, Kristu, aliongojea ma milele 19 na ku mwaka 1914 aliikaa-utukufu kwa Mungu- sawa mufalme kwa mbingu bila kuonekana hii ya kupanda Kwake pa Kiti yake; na hii mambo Washuhuda wa Yehova wanasadiki ya kama ni ya kuja wa Mbili ya Kristu!!

Sisi mbele ya kuandika mafundisho hii, ni lazima kuandika na ma sauti mafupi fundisho yao juu ya hii mambo toka mwanzo ya Kundi yao mpaka sasa:

Muumba ya kundi yao, Karolo Roseli, alihubiri ya kama ku mwaka 1799 ilikuwa mwanzo ya «wakati wa mwisho».

-Tena alihubiri ya kama mwaka 1872 ilikuwa mwisho ya miaka ma elfu sita (6. 000) tangu kiumba ya Adamu, na mwanzo ya elfu wa saba na hii ni wakati ya ufalme wa Kristu ya miaka elfu pa inchi yetu.

-Tena alisema ya kama ku mwaka 1874 ilikuwa mwanzo ya Kuja wa Mbili ya Kristu na wakati ya matengenezo ya dunia nzima.

-Tena alisema ya kama ku mwaka 606 mbele ya uzalio ya Kristu iliisha kuisha ufalme wa Kristu huku duniani na waliisha kuanza wakati ya ma inchi (serkali) (2520) miaka na mwisho yao itakuwa mwaka 1914, kisha uzalio ya Kristu.

-Tena alisema ya kama ku mwaka 1878 ilikuwa mwanzo ya ufalme wa Kristu ya miaka elfu, ufufuo ya wenye wafu katika Yesu na mageuzo wa haraka ya wale wataanza kufa ku mbele na utukufu wao mbinguni.

-Tena alisema ya kama ku mwaka 1914, kisha uzalio ya Kristu iliisha kuisha «wakati ya ma inchi», na «Yehova Mungu aliweka Mwana wake Yesu Kristu wa mbingu pa Kiti Yake juu ya kuwa mkubwa katikati ya ma adui wake. Kwa uzalio hii ya ufalme wa Mungu, ilianza nvita

kwa mbingu katikati Kristu (sawa malaika Mikaeli) na shetani na ku mwisho, mu mwaka 26-3-1918 (!) shetani alitupwa toka mbingu pa inchi.

Tena ndani ya hii mwaka (1918) waliongojea «kupanda» (waaminifu) ya Kundi yao mbinguni na utukufu yao, kisha ufufuo ya wenye haki ya Agano la Kale na hivi watakuwa wakubwa ya inchi.

Ku mwaka 1914, basi, wanasadiki ya kama ni mwaka ya mwisho wa dunia, Ya kuja wa Mbili ya Kristu na mwisho ya hii uzima. Tena hii mwaka ni mwanzo ya ma mbingu mapya, nikusema ni mwaka ya kutengeneza muji kubwa ya kundi yao kwa mbingu.

Lakini haya manabii yao ilionyeshwa ya kama ilikuwa ya uwogo na mufwasi ya Karolo Roseli, jina lake Yosefu Roderfonti, aliweka nyakati ingine mapya na alihubiri mafundisho mapya:

-Alisema ya kama mu mwaka 1918 Kristu «alikuja ndani ya hekalu wa roho ya mbingu sawa Mujumbe (Mwenye kutazama) ya Yehova na alianza kusafisha hekalu», ao «juu ya kusafisha na kumaliza hukumu», na mu mwaka 1919 alikuja juu ya «kuangalia nyumba Yake», nikusema kuona Kundi yake wa inchi. Hii mwaka umoja (1918) waliongojea kufanyika na ufufuo ya wenye haki ta Agano la Kale.

-Mu mwaka 1919 alihubiri mkubwa yao Yosefu ya kama «mwisho ya mwendo ya hekalu inakaribia na kisha saa kidogo waaminifu yake watapanda mbinguni». Paka hii mwaka umoja ilianza «inchi upya», nikusema «wakubwa wasaidizi ya mkubwa wa mbingu», nikusema wale waliongojea kufufuliwa wenye haki ya Agano la Kale. Tangu mwaka 1919 waaminifu ya Kundi yao wanasadiki ya kama maugo yao ni sawa «hule mutumwa mwaminifu na mwenye akili»(matayo 24, 45), tena wanasadiki ya kama hawa wenyewe ni mitume ya watu wengine na wekona kazi kupatia chakula ya roho kwa watu wote.

-Kwa sababu hii ufalme iliyejengwa mu mwaka 1914 ilikuwa isiyoonekana na macho yetu, «ilipashwa kuzambalishwa ma fasi yote». Mu mwaka 1922 walisikia amri ya mkubwa yao: Mutazameni, mutazameni, mutazameni Mufalme na ufalme wake!» Ni kweli, tangu hile mwaka watu ya Kundi hii walianza kutazama na kufundisha watu ma fasi yote ya kama «ufalme»ya Kristu ilikuja, lakini haikuonekane.

-Hile wakati Yosefu, mkubwa yao, ndani ya kitabu yake: «Watu wa milioane wenye muzima hawatakufe kwa milele» alisema ya kama mu mwaka 1925 itakuja mwisho ya hii dunia uovu!

-Mu mwaka 1925 waliweka tarehe upya juu ya kumalizwa bile matendo waliongojea tangu mwaka 1914: Nikusema mwanzo ya ufalme ya miaka elfu, Kupanda waaminifu mbinguni, ufufuo ya wenye haki ya Agano la kale, uharibifu ya ma inchi yote ya dunia na ingine.. . Hile wakati ilinunuwa na nyumba upya kubwa mu lugha kiebrania: «Mbeth-Sarim» (Nyumba ya wakubwa) mu muji Santiego ya Kalifornia ya Amerika juu ya kuikaa Abrahamu na wote wenye haki wakubwa ya Agano la Kale, wakata watafufuliwa.. . lakini ku mwisho aliikaa mkubwa Yosefu mupaka lufu yake.. . . .

Ongojeo ya mwanzo ya ufalme wa Kristu mu mwaka 1925 na hii uwogo inasema na kitabu (Kipindi) yao «Ulinzi» (Kigreki: Skopia) ya tarehe 15-6-1984.

Mu mwaka 1931 walihubiri ya kama dunia itaharibika yote. Huu mwaka mkubwa yao Yosefu alipatia kw aKundi yake jina ingine upya. Mupaka hile mwaka waliitwa «Wanafunji ya Madiko» ao «Wafwasi ya siku ya kwanza ya nyakati elfu). Tangu hile mwaka walichukua jina: «Washuhuda wa Yehova».

-Fundisho yao kubwa ni ya kama ndani ya Kanisa ya Yehova ni paka 144. 000 waaminifu, wenye watawala pamoja na Kristu mbinguni na watakuwa sawa «watu wa Israeli wa roho». Hawa watu wazuri na wema kabisa Yehova aliwalokota na pasopo mingi katikati ya wakati ya ma milele 19. Mu mwaka 1927, watu wazima ya Kundi «walisikia» ya kama hawa watu, vipande wa milele ya zamani, «walifufuka mu mwaka 1918 kwa mbingu kwa uzima moja wa milele pamoja na Yesu Kristu; ilikuwa ufufuo moja isiyoonekane, wanasema.

-Tangu mwaka 1931, «Muchungaji Muzuri alianza kusanyika na ma kondoo yake ingine», nikusema ma elfu ao ma milioane ya watu ya Kundi. Hile mwaka walisadiki hawa watu ya kama weko ndani ya kundi ingine wa mbili, kidogo chini ya ingine kundi wa kwanza kwa imani kidogo chini.

-Mu mwaka 1935 «Yehova alihubiri safi» ya kama katika kinywa ya Yosefu Roderfont, ni ma kundi wa wili ya waaminifu:

a) Ni 144. 000 «watu wa Israeli wa roho», wenye, paka hawa wa pekee ni Kanisa ya kweli na «kitumaini yao ni wa mbingu». Hawa watu wanafuata Kundi inayeonekana ya Yehova pa inchi na pombi kimoja katikati yake anapita Yehova na analeta chakula ya roho kwa watu wote.

b) Ni «taifa mengi» (Ufunuo 7, 9), ni ma milioane ya wafwasi ya Kundi yao, lakini «kitumaini yao ni wa inchi»; hawa bado kuzaliwa uzalio upya ya mbili; hakuna namna kuwa watoto wa Mungu na hawa wataikaa mu Paradizo ya hii inchi. Hawa watu wanaokolewa, kama wanatii mbele ya wakubwa wao, wenye ni ndani ya kundi wa kwanza.

Mu tarehe 8-1-1942 mkubwa yao Yosefu alikufa na alimufuata bwana Nathani Nori na huyu alimufuata mu mwaka 1977 Frenteriko Franch, wenye waliendela kazi ya manabii ya uwogo yao:

Mu mwaka 1943 walisema ya kama ni mwisho ya miaka 6. 000 ya Hadisi ya watu tangu kiumba ya Adamu na kisha miaka 6000, nikusema mu mwaka 1943 itakuwa nvita munene, inayeitwa Armagedoni. Kisha hii nvita itaanza ufalme wa Kristu pa inchi ya miaka elfu moja (1000). Mupaka ku mwaka 1943, wanaandika, ilipita miaka 5971 tangu mwanzo ya Adamu na Eva. Juu ya kutimizwa miaka 6000, ilibakia tena miaka 29 juu ya utimizo. Kwa hivi tunafika mu mwaka 1972 (1943+29=1972). Hii mwaka ni mwanzo ya ufalme wa miaka elfu ya Kristu.

Kisha na hii sauti yao ya uwogo, waliweka ma tarehe ingine mapya: Mu mwaka 1964 wanafanya matengenezo na waliweka mwaka 1975 sawa mwaka wa kweli na isiyokosa kabisa ya kama inatimizwa wakati ya miaka 6000 tangu kiumbe ya Adamu. Kisha yake itaanza nvita ya Armagedoni na kisha nvita Ufalme wa kristy ya miaka 1000 pa hii inchi yetu.

Na hii manabii yao ilikuwa ya uwongo na walikimbia waaminifu yao karibu 1. 000. 000.

-Ku mwisho, kisha ma nabii yao ya wogo, hii kazi ilikuwa ni hii: Yosefu alitengeneza manabii yake ya uwogo hivi: Alihubiri ya kama mu mwaka 1914 itakuja ufalme ya Yehova pa inchi yetu na itamusidikia na ufufuo ya watu wenye haki ya Agano la Kale. Kwani hii sauti yake ilionyeshwa ya uwogo, kisha alisema ya kama Ufalme ya Kristu ilikuwa lakini hapana huku, lakini kwa mbingu! Tena alisema ya kama wale waaminifu 144000 ni kanisa ya Yehova walipanda mbinguni katika mufano.

-Wakati ilionyeshwa ya kama na mwaka 1975 ilikuwa unabii ya uwogo, walifunga kinywa yao na wanaogopa kuweka tarehe ingine. Hii mambo sasa wanaongojea siku kwa siku akuje ni nvita ya Armagedona na hii nvita itakuwa alama ya mwisho ya hii dunia uovu. Wanaandika, kwa hii nvita wa mwisho, mataifa yote watakuja kupiga Washuhuda wa Yehova juu ya kuwaua(!), lakini atakuja Yehova na atawaua wale watu walikataa kufuata Kundi yao. Soma Kipindi yao Ulinzi Kigreki Skopia mu tarehe 1-9-1982!

-Kisha Armagedona itaanza ufalme wa miaka elfu ya Kristu pa inchi yetu. Wale wafazili ya kundi 144000, wataishi pamoja na «taifa mengi»=(kundi ya mbili) watapata furaha na shangilio, kwa sababu Yehova Mungu yao atawaua wale watu walibaki inje ya Kundi ya Washuhuda ya Yehova. Ndani ya vitabu yao wanaandika ya kama «wanataka lufu yetu (kwani sisi tunakataa kufuata Kundi yao), «wanaitika bila taabu na sikitiko kwa lufu na uuwaji wetu, na wanafurahi, kwani wanawaza ya kama watanawa miguu yao ndani ya damu yetu!!!

-Kikomo ya ufalme wa miaka elfu ya Kristu hapa duniani ni, wanasema, juu ya kutengenezwa pole-pole Paradizo pa inchi, sawa mu wakati ya Adamu, vile itakuja siku moja ubarikiwa.

Ndani ya miaka haya (1000) shetani na malaika yake watafungwa na watatupwa mu hadeze. Hile wakati watafufuliwa watu wenye haki ya Agano la Kale juu ya kufanya utawala wa

dunia nzima na wakubwa watakuwa Abrahamu, Musa, Daudi, Yovu, Danieli, Abeli, Yoano Mubatizaji na wengine

-Kisha wataanza kufufuliwa wafu ya wakati wote tangu mwanzo, ila tu wale wakibego na wasiyoimani, wenye hakuna namna kufufuliwa, sawa Adamu, Yuda, Wandishi ya Sheria ya Musa, Wafarisayo na wengine. Hii ufufuo itafanyika pole-pole: «Hawakurudie wote mara moja... Ya kurudia wafu itazala ma mambo.. . . Wenye muzima wanapashw akufanya matayarisho. Kwa ajili ya hii matayarisho ufufuo itafata mustari moja». Nikusema, wanasema, watafufuliwa kidogo-kidogo juu ya kutaguria watu wenye muzima kuwajenga ma nyumba yao na majengo ingine!!!

Juu ya mambo ya kujenga nyumba wanaandika hivi: «Mu Paradizo namna ya kujenga itakuwa muzuri sana na haitakuwa sawa hapa duniani.. . Mustari ya majengo na kutumika ma shamba itagariki miaka mengi, kwani ma nyumba italazimishwa hapana paka kwa wale wataishi kisha nvita Armagedona, lakini na kwa wale watafufuliwa pole-pole». (Kipindi Ulinzi (Skopia) ya 15-3-1984).

-Hile wakati ya miaka elfu ufalme wa Yesu pa hii inchi watu «watasafisha inchi na watarima Paradizo». Ma furaha ya hii paradizo wa hii inchi itakuwa: Ma nyumba na ma kazi ya watu wote, vitu vya kula vyote, ungano na mapendo ya kizazi ubinadamu, usimamishi ya uuaji, zambi ya usharati na uzulumi, uzambalisho ya amani mu dunia nzima, uponyesho ya magonjwa yote, ya uzee na lufu na utawala wa haki».

-Hile wakati ya ufalme na miaka elfu itakuwa desturi ya mafundisho ya watu wote na vitabu wa pumuzi wa Mungu na watakuwa na ma sheria na maongozi ya Yehova, na hii mafundisho itakuwa kupita ya mafundisho ya Madiko Takatifu yetu. Basi, Hukumu wa mwisho, itakuwa hapana kupatana na matendo yetu, hile tulifanya mu wakati ya uzima yetu, lakini kupatana na vile vitabu na tabia yetu ya hii wakati ya ufalme ya miaka elfu na hii ufalme ya miaka elfu wanaiita «Siku ya Hukumu».

-Hile waakti ya ufalme na miaka elfu Wale watu waliishi bila kutubu, watawauwa.

-Ku mwisho ya hii ufalme ya Yesu, wanasadiki, shetani atakuwa muhuru na atakokota watu wingi mukongo yake. Atafanya nvita pamoja na Kristu, lakini atashindwa, atabambwa na pamoja na wafwasi wake watalipizwa na alipizo bila kukuwa, lakini wale watabakia waaminifu kwa Mungu, wataishi ma siku zote mu paradizo wa hii inchi.

-Ndani ya hii mafundisho yao tunaona ya kama ulimwengu atapokea uhukumu hapana moja na ya Kuja Kristu ya Mbili moja, sawa vile inatufundisha Madiko Takatifu, lakini tunaona yakama itakuwa mahukumu mengi na ya Kuja Kristu mara mengi:

a) Tukona hukumu ya watu wa Kanisa;
b) Hukumu ya mataifa;
c) Hii ufalme ya miaka elfu (1000) itakuwa siku ya hukumu;
d) Hukumu wa mwisho, kisha mwisho ya ufalme wa miaka elfu

Ya Kuja Kristu tunaona:

a) Ya Kuja Kristu mara ya kwanza, hile wakati aliishi pa inchi yetu;
b) Ya Kuja Kristu mu mwaka 1914;
c) Ya Kuja Kristu hile wakati ya nvita inayeitwa Armagedona;
d) Ya Kuja Kristu wa inne ku mwisho ya ufalme wa miaka elfu.

Hii ni na masauti na haraka mafundisho ya Washuhuda wa Yehova. Jambo kubwa yao na pempeni yake wanasimama ma jambo ingine, ni jambo ya Kuja Kristu wa Mbili mu mwaka 1914 na mwanzo ya ufalme mbinguni.

Sasa tutaanza sisi kuhamakia mafundisho yao ya uwogo kabisa na tutaandika mafundisho ya kweli ya Kanisa ya Kristu.

## Namna gani walifika mu mwaka 1914?

Juu ya kufika Washuhuda wa Yehova kwa majengo ya «ufalme» wa Kristu isiyoonekane kwa mbingu mu mwaka 1914, wanaungana matendo na ma jambo ya kuachana na wanasingi pa mawazo isiyo akili na kweli.

Usingi ya mawazo yao ni ya kwanza ono moja, iliyeona mfalme wa muji Babeli jina lake Nebukadneza (Danieli sehemu 4) na ya mbili «wakati ya ma inchi» sawa vile anasema hivi Kristu (Luka 21, 24).

Kweli, mfalme Nebukadneza aliona ndani ya maono yake muti moja murefu na katika amri ya Mungu ilikatwa na gogo yake ilifungwa na minyororo ya chuma. Hii muti ilibakia pa hii hali ya «wakati saba». Danieli alifafanusha hii ono na alisema ya kama hii muti alikuwa mfalme Nebukadneza mumoja (4, 22); ya kukata kwake ni maana ya kama huyu mfalme alipotesha utawala yake ya wakati miaka saba, kwani kwa hii wakati mfalme aliisha kupotesha akili yake, alikuwa nyama na alizunguluka ma shamba na alikula mayani mubichi. Kisha miaka saba alipata mara ingine akili yake na alipanda mara ingine pa kiti ya ufalme wake.

Washuhuda wa Yehova, bila usingi, wanashariki hii muti na ufalme wa Mungu pa inchi yetu, hile ilifanyika hile wakati toka wafalme ya muji Yerusalema wa Yuda. (Kiti ya mfalme wa Yuda iliitwa «Kiti ya ufalme cha Bwana» (1 Maambo ya Siku 29, 23). Ya kukata muti ni-wanasema- uharibifu ya ufalme wa Yuda na muji Yerusalema toka taifa ya Babeli na mfalme yake Nebukadneza mu mwaka 607, mbele uzalio ya Kristu; kwa hivi, wanasema, ilisimama kuwa ufalme («Kiti») ya Mungu pa inchi. Wakati ma saba ni 7X360 ma siku=2520 miaka na hii miaka wanashariki, bila usingi, na wakati ya mainchi, nikusema haya miaka shetani atawala pa ma inchi yote na hapana Mungu. Wanaogeza mu hesabu 2520 miaka, hesabu mwaka 607 kisha uzalio ya Kristu, wanafika mu mwaka 1914 kisha uzalio ya Kristu, na hii mwaka ni wa mwisho ya wakati ya ma inchi yote ya dunia na ufalme atachukua Mungu mara ingine. Sawa usingi yao pa hii mafundisho yao wanaleta na sehemu ya Ufunuo 12, pahali «mwana» pa hile ono ni maana, katika akili yao, ya ufalme ya mwaka 1914!!

Hii mawazo na mafundisho yao ni ya bure, kama tutaangalia hii ifwatayo:

a)Nabii Danieli anafafanusha Ono yake na anasema hii muti ni maana ya mfalme Nebukadneza na paka huyu mumoja (4, 22). Basi, hakuna ungano moja pamoja na ufalme wa Mungu pa inchi yetu.

b)«Nyakati za mataifa» hile anasema Kristu Luka 21, 24, hakuna ungano moja na hii Ono ya Danieli.

c)Kupatana na Hadishi ya Waebrania, uharibifu ya ufalme wa Yuda na yerusalema ilikuwa mu mwaka 586, mbele ya uzalio ya Kristu na hapana mu mwaka 607, mbele ya uzalio ya Kristu. Basi, mawazo na sauti yao ya mwisho ilikuwa kuwa vile: 586+2520=1934 kisha uzalio ya Kristu na hapana mu mwaka 1914, kisha uzalio ya Kristu.

Kwa ajili ya mafundisho yetu wa juu inaonekana safi ya kama mawazo ya Washuhuda wa Yehova juu ya Kuja Kristu mara ya Mbili duniani na. . . jengo ya ufalme wa Kristu.. . isiyoonekana kwa mbingu, ni paka mawazo ya akili ugonjwa yao.

## YA KUJA KRISTU MARA YA MBILI- MWISHO YA DUNIA-UHUKUMU WA MWISHO-MWANZO YA UZIMA WA MILELE WANASHARIKIWA KATIKA WAKATI MOJA

Kupatana na Madiko Takatifu, ya Kuja wa Mbili, Mwisho ya dunia, Uhukumu ya mwisho na mwanzo ya uzima wa miele wanasharikiwa katika wakati moja. Washuhuda wa Yehova, kupindua, wanaachana ma jambo haya, bila uhaki, na wanaweka katikati yao wakati marefu: Ya Kuja wa Mbili ya Kristu mu mwaka 1914; tangu hii mwaka mupaka sasa inaifata kundi ya

wafwasi wao (wenye wanawafuata sawa kondoo); kisha itaifata ufalme wa miaka elfu (1000) ya Kristu huku dunaini; kisha hii utawala itakuwa nvita kupindua Shetani na kisha-ku mwisho-itakuja Uhukumu wa mwisho na mwanzo ya uzima wa milele.

Lakini neno ya Mungu inasema ya kama hii mafundisho yao ni ya uwogo kabisa:

Madiko Takatifu inatwaambia paka ya wakati wa wili ya uzima: Ni uzima wa sasa (inayeitwa «milele wa sasa») na mwisho ya hii «milele» wa sasa» itakuwa siku ya Kuja wa Mbili ya Kristu na uzima wa milele: Kwa mufano tazama mu Matayo 12, 32. Marko 10, 30 na Wa Efeso 1, 21) na pa fasi ingine. Hii wakati katikati ya Kuja wa Kwanza ya Kristu pa inchi na mpaka ya Kuja Kwake wa Mbili inaitwa mu Madiko Takatifu «ma siku wa mwisho» (Matendo 2, 14-17 na barua ya kwanza ya Yoano 2, 18) na iko muda ya Agano Jipya; Hii ni nyakati ya uzima wa sasa na itaisha hile siku ya Kuja Kristu mara ya Mbili.

Kwa sababu haitakuje wakati ingine ya Kuja na Ufalme ya Kristu hapa duniani, mbele ya mwisho ya dunia, kwa hivyo Madiko Takatifu inaita ya Kuja Kristu sawa «Siku wa mwisho» (Yoano 6, 39-44 na 12, 48), (Siku ya Bwana Yesu Kristu» (Matendo 2, 20. barua ya kwanza kwa wa Korinto 1, 8. 5, 5. barua ya mbili kwa wa Korinto 1, 14. Filipi 1, 6, 10 na 2, 16. barua ya mbili kwa Watesalonika 2, 1-2. barua ya kwanza kwa Watesalonika 5, 2), «Siku ya Mungu» (barua ya mbili ya Petro 3, 12. Ufunuo 16, 14), «Siku ya hukumu» (Matayo 11, 22. 12, 36 na barua ya mbili ya Petro 2, 9 na 3, 7. barua ya kwanza ya Yoano 4, 17), ao na namna unyofu «Hile siku» (matayo 7, 22). barua ya mbili kwa Watesalonika 1, 10 na barua ya mbili kwa Timotheo 4, 8). Tena inaiita «ya Kuja Kristu» (Matayo 24, 30), «Kwa kutokea Kwake (Kristu)» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 23. Barua ya kwanza kwa Watesalonika 2, 19. 3, 13. 4, 15 na 5, 23), «Ufunuo ya Kristu» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 1, 7 na barua ya mbili kwa Watesalonika 1, 7 na barua ya kwanza ya Petro 1, 7), «Kuonekana kwake Bwana wetu Yesu Kristu» (barua ya kwanza kwa Timotheo 6, 14 na barua ya mbili kwa Timotheo 4, 1, 8 na Tito 2, 13), «Siku kubwa» (Yuda 6), «Kwa siku ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu» (Wa Roma 2, 5).. .

Sawa vile tunaona, ma fasi yote Madiko Takatifu inatufundisha paka ya Kuja moja Kwake (Yesu Kristu) ku mbele na ya siku paka moja na hile «Siku» itakuwa ufufuo ya wafu na hukumu wa mwisho na mwanzo ya uzima wa milele ku mbele.

Sasa tutaona kabisa namna gani inatuwaambia Madiko Takatifu fundisho ya Kuja wa Mbili ya Kristu hapa duniani:

**1)** Mitume walisema kwa Kristu: «Utuambie, maneno haya yote yatakuwa wakati gani? na nini alama ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia? Yesu akajibu, akawaambia: Angalieni musidanganyiwe na mutu. Kwa sababu.. . Na wakati mutu atakapowaambia ninyi: tazama, Kristu ni hapa, ao kule; musiamini (23).. . kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaonekana hata mangaribi; hivi kuja kwa Mungu wa watu kutakavyokuwa vile (27).. . Na wakati ule wataona Mwana wa watu akikuja katika wingu pamoja na uwezo na utukufu mukubwa. (Matayo 24, 3-31. Marko 14, 62 na Luka 17, 34 na 21, 27).

**2) «Tazama anakuja na mawingu; na kila jicho litamwona, na wale waliomuchoma; na mataifa yote ya dunia wataomboleza kwa ajili yake. Ndiyo. Amina» (Ufunuo 1, 7).**

**3) «Lakini wakati Mwana wa watru atakapokuja katika utukufu wake, na malaika yote pamoja naye,, halafu ataketi juu ya kiti cha utukufu wake; na mbele yake mataifa yote watakusanyika; naye atawatenga kama muchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi; na ataweka.. . Halafu Mufalme atawaambia wale kwa mukono wake wa kuume: Kujeni, ninyi muliobarikiwa na Baba yangu, muriti ufalme muliotengenezewa.. . . Kisha atawaambia wale kwa mukono wake wa kushoto: Ondokeni kwangu, ninyi muliolaaniwa, mwende katika moto wa milele uliotengenezewa kwa shetani na malaika zake.. . Na hawa**

**wote watakwenda kuingia katika azabu ya milele; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele» (Matayo 25, 31-46 na 16, 27).** Basi, ya Kuja Kristu, ufufuo ya wafu na Hukumu wa mwisho wanasharikiwa.

**4) «Ninyi watu wa galilaya, kwa sababu gani mumesimama mukitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomuona akikwenda zake mbinguni» (Matendo 1, 11).**

**5) «Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, na sauti kubwa, na sauti ya malaika mukubwa, na pamoja na baragumu ya Mungu: nao waliokufa katika Kristu watafufuliwa kwanza; Kisha sisi tulio hai, tuliobaki, tutanyanyuliwa pamoja nao katika mawingu, kukutana na Bwana katika hewa,, na hivi tutakuwa pamoja na Bwana milele» (barua ya kwanza kwa Wa Tesalonika 4, 16). «Tazameni, ninawaambia ninyi siri: Ssisi sote hatutalala, lakini sisi sote tutabadilika, kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho, kwa baragumu ya mwisho: sababu baragumu italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na kuoza, natutabadilika» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 51-52).** Tunaona huku ya kama ufufuo ya wafu na ubadilisho ya wenye muzima itakuwa mara moja, hile siku ya Kuja wa Mbili ya Bwana Yesu Kristu.

**6)** « (Mungu atawapatia) ninyi munaoteswa pumziko pamoja na sisi, wakati wa ufunuo wa Bwana Yesu kutoka mbingu pamoja na malaika za uwezo wake. Katika moto wa kuwaka akiwalipa kisasi wao wasiojua Mungu, na wao wasiotii Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristu» (Barua ya mbili kwa Watesalonika 1, 7-8). Siku ya Kuja wa Mbili ya Kristu na hukumu ya wasiyokutubu inasharikiwa na itafanyikwa mu wakati umoja.

**7) «Ninakuagiza mbele ya Mungu, na ya Bwana Yesu Kristu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, na kwa kuonekana kwake, nakwa ufalme wake; uhubiri neno.. . » (barua ya mbili kwa Timotheo 4, 1).** Hapa inasharikiwa kabisa onekana ya Kristu pamoja na Hukumu wa mwisho na Ufame.

**8) «Ndugu, vumilieni basi, hata kuja kwake Bwana.. . mutie mioyo yenu nguvu, kwa sababu kuja kwake Bwana kunakaribia. Ndugu musinungunikiane ninyi kwa ninyi, musipate kuhukumiwa; tazameni mwamuzi amesimama mbele ya milango» (barua ya Yakobo 5, 7-9).** Na hapa siku ya Kuja wa Mbili ya Kristu inasharikiwa na Hukumu wa mwisho na itafanyika mu wakati umoja.

**9)** Ku mwisho, Mtume Paulo anatukikiri ya kama: **«Na sawasawa watu wanavyowekwa kufa mara moja, na nyuma ya kufa hukumu.. » (Wa Ebrania 9, 27).**

Ma shairi haya yote inatwaambia ya kama Siku ya Kuja Kristu wa Mbili, Ufufuo ya wafu, Hukumu wa mwisho, Mwisho ya dunia watafanyika wakati umoja. Nikusema hakuna namna kuja ufalme wa Kristu ya miaka 1000, sawa vile wanafundisha Washuhuda wa Yehova.

Sawa vile inaonekana safi ku shairi wa juu, hile wakati Kristu atakuja ataonekana ku watu wote. Kupindua, Washuhuda wa Yehova wanafundisha ya kama Siku ya Kuja wa Mbili ya kristu ni. . . «isiyoonekana» (!) Hii imani yao inaisingi pa hii shairi:

**1)** Kwa hile maneno alisema Kristu kwa Wanafunji Wake, saa kidogo mbele ya Mateso Yake: **«Angali wakati mudogo, na dunia hainioni tena; lakini munaniona» (Yoano 14, 19).** Nikusema: Kisha saa kidogo watu wa dunia hakuna namna wanione mara ingine, lakini mweye mutaniona.

**2)** Kwani Kupanda kwake ilikuwa bila makelele na wingu moja ilikuja na ilimufunisha Kristu. Na tena, kwa sababu malaika amewaambia Mitume ya kama Kristu atakuja mara ingine. Tena, kwani paka Wanafunji walimuona ya kupanda mbinguni na kwani paka kwao aliisha kuwaambia saa kidogo ku mbele: **«nanyi mutakuwa washuhuda wangu katika.. . » (Matendo 1, 8-11).**

Katika hii ma shairi haya Washuhuda wa yehova wanataka kusadiki ya kama Kristu hasitaonekane kwa wenye kibego na wqenye zambi, lakini ataonekana paka kwa wafazili na watu wazuri. Lakini ma shairi haya tuliandika juu wanatwaambia, bila shaka, ya kama, hile wakati atakuja Kristu atakuwa ya kuonekana ku watu wote, na wenye zambi na wenye haki na wote watamutazama akuje pa mawingu ya mbingu pamoja na malaika wake na katika utukufu Yake yote. Basi, ni ya bure ya kuandika mara ingine hii fundisho. Tunakumbusha paka kwa Washuhuda wa Yehova maneno haya: **«Nanyi mutaona Mwana wa watu ameketi mukono wa kuumw wa nguvu akikuja na mawingu ya mbingu» (Marko 14, 62**) na Kristu alisema maneno haya kwa Kuhani kayafa na wakuhani wengine, wenye walimuhukumu. Basi, watamuona na wadui wabaya kabisa wake, wakata atakuja na tena **«na wale walimuchoma» (Ufunuo 1, 7).**

Kama tunajua hii mafundisho yote, shairi hii: **«Na dunia hainioni tena» (Yoano 14, 19)** inatwaambia ya kama watu hawaweze kumuona tena mu uzima Wake pa inchi yetu, nikusema tangu wakati ya lufu yake mpaka Kupande Kwake mbinguni, sawa vile ilifanyika: Ndani ya hile wakati ya ma siku makumi inne (40) alibakia pa inchi, kisha Ufufuo Wake, hasikuonekane Kristu mu dunia, lakini paka kwa Wanafunji wake. Tena, sauti ingine umoja amewaambia Kristu kwa Wanafunji wake: **«Kwa sababu ninakwenda kwa Baba na hamunioni tena» (Yoano 16, 10**) na maana yake ni ya kama kisha Kupanda Kwake kwa baba Wake mbinguni, hakuna namna kuonekana ku Wanafunji wake pa hii inchi. Sawa vile: «na hamunioni tena» iliyesema kwa Wanafunji wake, hakuna namna kuwaza ya kama Wanafunji wake hawataweze kumuona mara ingine, vile vile na «dunia hainioni tena» hakuna namna kuwaza ya kama hawaweze kumuona mara ingine.

Kwa ajili ya shairi yao wa mbili ni kweli ya kama: **« (Kristu) atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni» (Matendo 1, 11).** Nikusema malaika walisema kwa Wanafunji ya Kristu ya kama Huyu (Kristu) atakuja mara ingine toka mbingu, sawa vile alipanda mbinguni.

## 2. NI NANI UFALME WA MIAKA ELFU (1000) UFUNUO, SEHEMU 20

Imani yao ya kama, mbele ya Hukumu wa mwisho itakuja ufalme na miaka elfu (1000) pa inchi yetu ni ndani ya sehemu 20 ya Ufunuo ya Yoano. Katika hii sehemu malaika toka mbingu alifunga shetani na alimuweka ndani ya shimo (hadeze) ya wakati miaka elfu (1000). Ndani ya hii wakati watu wa Mungu waliishi na walitawala pamoja na Kristu. Hii, ni «ufufuo wa kwanza»; na inaendelea Kitabu ya Ufunuo: «Heri na Mutakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuko wa kwanza; juu ya hawa mauti ya pili haina nguvu; » Ufalme wa miaka 1000 Washuhuda wa Yehova wanaiongojea kuja tena. Lakini, bahati mubaya kuwao, fundisho ya kweli ni ingine na hapana imani yao.

## A. UFALME WA MUNGU ILIKUJA TANGU HILE WAKATI ALIKUJA KRISTU DUNIANI

Yoano mu Kitabu Ufunuo anatimia ma neno na mifano lakini sisi tusiweze kuyasikia katika herufi yao. Mu sehemu 20 kwa mufano, pahali inaandikwa ufalme wa miaka elfu maana yake ni wa siri. Haiandikwe hata fasi moja ya Madiko Takatifu ya kama itatengenezwa Utawala wa dunia muzima na watakuwa wakumbwa Abrahamu na wengine wanaume ya Agano la Kale, hata ma furaha ya mwili na chakula ya mbali-mbali sawa hivi wanasadiki Washuhuda wa Yehova. Kupindua na imani yao, Madiko Takatifu inatufundisha juu ya ufalme wa roho wa Mungu moja, itawala pa inchi hile wakati aliishi tena Kristu duniani. Huu Ufalme haina ingine

ya Kanisa wa Kristu na Huu ni Ufalme wa Mungu pa inchi na Kanisa yake ni endeleo ya Ufalme wa mbingu pa inchi:

**1)** «Siku zile Yoane Mubatizaji alikuja, akihubiri katika jangwa la Yudea, akisema: Tubuni, sababu ufalme wa mbinguni umekaribia». Nyuma ya kufungwa kwa Yoane, Yesu alipita hata galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema: Wakati umetimia, ufalme wa Mungu ni karibu. Tubuni mukaamini Habari Njema» (Matayo 3, 1-2 na Marko 1, 14-15).

**2) «Na kama mimi kwa Roho ya Mungu nikitoa pepo wachafu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwafikia ninyi» (Matayo 12, 28),** alisema Kristu kwa watu wa Yudea. Basi, Ufalme wa inchi ilifika tangu hile masiku.

**3) «Lakini ole wenu, waandishi na wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munafungia watu ufalme wa mbinguni. Kwa maana ninyi hamwingi ninyi wenyewe, wala wale wanaoingia, hamuwaachi kuingia» (Matayo 23, 14).** Ufalme umoja ya Kristu kwa mbingu na inchi, basi, ilikuwa tangu hile wakati; kwa hivyo na ninyi wote walitaka kuingia tangu hile muda, waliweza waingie.

**4) «Kwa sababu ya neno hili ninawaambia ninyi: Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu na taifa lingine watapewa, wenye kuzaa matunda yake» (Matayo 21, 43).** Kristu hapa anasema juu ya Ufalme iliyekuwa tangu hile wakati wake na ilikuwa mambo ya kupoteshwa kwa ajili ya taifa wa Israeli, asiye na imani na itajitoa kwa «taifa» ya wakristu, wenye walimuamini Kristu.

**5) «Basi Pilato akaingia nyumba ya hukumu tena, akaita Yesu, akmwaambia: Wewe ni mufalme wa Wayuda? Yesu akajibu: Wewe unasema hivi wewe mwenyewe, ao watu wengine walikuambia habari zangu? .. . Yesu akajibu: Ufalme wangu si wa dunia hii; kama ufalme wangu ungekuwa wa dunia hii, watumishi wangu wangenipoigania nisitolewe kwa Wayuda» (Yoano 18, 33-37).** Hapa Kristu anasema ya kama ufalme wake si wa dunia hii na hapana «sitakuwa» ku mbele.

**6)** Ufalme wa Mungu wa hii inchi iko na ufananisho wa roho: **«Na alipoulizwa na Wafarisayo: Ufalme wa Mungu utakuja wakati gani? Akawajibu, akasema: Ufalme wa Mungu haufiki kwa kutazamia. wala hawatasema, tazama hapa, ao tazama kule. Kwa maana tazama ufalme wa Mungu ni ndani yenu» (Luka 17, 20-21).** Basi, Ufalme wa Mungu pa inchi haina katika vitu vya hii dunia, sawa vile waliwaza watu wa Yuda na sawa vile wanasadiki leo Washuhuda wa Yehova, lakini ni hali wa roho na uzima katika Kristu. Ndani ya hii uzima katika Kristu, hile inapashwa kutawala ndani yetu inatufundisha na sala ya Kristu: «Baba yetu uliye mbinguni.. . ». Ni hii neno: «Ufalme wako uje».

**7)** «Akawaambia: Kweli ninawaambia ninyi, kuna watu katika hawa wanaosimama hapa, nao hawataonja mauti hata watakapoona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu» (Marko 9, 1). Kweli, Kanisa ni ufalme wa roho wa Kristu, umeonekana katika nguvu, hile siku ya Pentikosti, mbele Wanafunji ya Kristu «wapime lufu». Lakini ufalme ya uwogo ya Washuhuda wa Yehova ilikuja mu mwaka 1914, kisha uzalio ya Kristu, wakati wale waliyomusikia Kristu waliisha kufa. Huu ufalme wa uwogo ya Washuhuda ya Yehova hana hata ungano na ufamio na Ufalme wa Kristu wa kweli.

**8)** Basi, tangu wakati ya Mitume Waaminifu walikuwa ndani ya Ufalme wa Mungu: «Na ye (Mungu Baba) alitutoa katika uwezo wa giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa mapendo yake» (Wa Kolosayi 1, 13).

## B. KRISTU ALIKUWA MUFALME TANGU HILE WAKATI ALIISHI

1) **«Yuko wapi yeye, aliyezaliwa Mufalme wa Wayuda? » waliuliza watu wenye akili wa tatu, wakati walifika mu Yerusalema. (Matayo 2, 1-2).**

2) **«Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu, wewe ni Mufalme wa Israeli», alimuliza Natanaeli Kristu (Yoano 1, 50).**

3) **«Mumwambie binti ya Sayuni, tazama, mufalme wako anakuja kwako, mupole, naye amepanda punda, na mwana-punda, mutoto wa punda» (Matayo 21, 5**) alisema Nabii kwa sayuni, nikusema kwa Yerusalema, juu ya kuingia Kristu kwake, mu Juma ya Matawi. Mara moja na watu wa taifa walipaza sauti wakasema: **«Hosana! Amebarikiwa Mufalme wa Israeli anayekuja kwa jina la Bwana» (Yoano 12, 13) na «Mubarikiwa Mufalme anayekuja kwa jina la Bwana, salama katika mbingu, na utukufu pahali pa juu» (Luka 19, 38) Na Marko 11, 9-10).**

4) **«Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani» (Matayo 28, 18). Kristu «kwa mikono wa kuuma wa Mungu, akiwa amekwenda mbinguni; malaika na mamlaka na nguvu zikikwisha kutiishwa chini yake» barua ya kwanza ya Petro 3, 22).**

5) **«Maana sharti atawale hata atakapoweka adui zote chini ya miguu yake. Adui ya mwisho ya kuondoshwa ni mauti. Sababu vitu vyote viliwekwa chini ya miguu yake, imeonekana wazi ya kwamba vyote viliwekwa ila yeye aliyeviweka» (barua ya kwanza kwa waKorinto 15, 25-27).**

Basi, Kristu alikuwa Mufalme tangu hile wakati ya kuja yake duniani. Basi, mufalme wa uwogo ya mwaka 1914 na ufalme wake ya miaka 1000 katika mafundisho ya Washuhuda ya Yehova hakuna namna kuwa mumoja na Kristu ya Agano Jipya.

## C. «KWA KUFUNGWA» SHETANI ILIKUWA TANGU HILE WAKATI ALIISHI KRISTU DUNIANI

Kama tunajua hii mafundisho yote ya Kanisa yetu ni kwlei ya kama wakati ya miaka elfu (1000) inayeandika Ufunuo ni mustari na maana ingine. Nikusema inatuwaambia hii wakati iliyoanza tangu mwanzo ya Kristu hapa duniani: Ni uzima ya Kanisa yetu. Kristu katika sandaka wake pa Musalaba na Ufufuo Wake, «alivunja kichwa ya nyoka», nikusema shetani na aliharabisha mamlaka yake pa vichwa vya watu na hivi ilitimizwa unabii wa zamani, aliisema Mungu kwa watu wa kwanza Adamu na Eva, wakati aliwafukuza ku Paradizo: Ya kama, siku fulani atatuma Mukombozi, aliye ataokolewa uzazi ubinadamu kwa kuvunja kichwa ya nyoka (shetani) (Mwanzo 3, 15). Kweli, wakati ilikuja utimilifu ya wakati (Wagalatia 4, 4) Mukombozi alikuja: Alikuwa Mwana na Neno wa Mungu, aliyechukua hali kimutu (Yoano 1, 14) na katika lufu Yake pa Musalaba, «alivunja kichwa ya nyoka: nikusema ya Shetani na aliuhuru mutu. Kwa kusema sisi uvunjo ya kichwa ya Shetani, tusiwaze lufu ya shetani, lakini uharibifu ya uwezo wake na mamlaka yake pa uzima ya watu. Sandaka wa Usulubio na Ufufuo wa Kristu walikuwa monyororo urefu na munene na hii alifungwa shetani na aliharabisha uwezo wake, sawa inatuwaambia andiko ya Ufunuo. Basi, ufalme wa Kristu ya miaka 1000 na kufungwa ya shetani walianza tangu hile siku alikuja Kristu duniani. Kama Washuhuda wa Yehova wanakataa utimizo ya unabii ya Kitabu Mwanzo 3, 15, iliyetimizwa katika Usulubio na Ufufuo wa Kristu, ni sawa kufundisha ya kama Kristu alisulubiwa na alikufa kwa bure na isiyo haki.
Tena fundisho ya kufungwa shetani inatwaambia Madiko Takatifu safi kabisa:

1) **«Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alionekana ili avunje kazi za Shetani» (barua ya kwanza ya Yoano 3, 8).** Na kweli hii tendo aliifanya, kwani alikamata na «alimufunga» shetani.

**2)** **«Na kama mimi kwa Roho ya Mungu nikitoa pepo wachafu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwafikia ninyi- anasema Kristu hile wakati ya uponyesho ya hule mutu wa pepo uchafu- Ao namna gani mutu anaweza kuingia nyumbani mwa mwenye nguvu (shetani) na kuteka vitu vyake, (nikusema wenye wapate pepo wachafu) asipofunga kwanza yule mwenye nguvu? Na halafu atateka nyumba yake. (matayo 12, 28-29) «Mutu hawezi kuingia ndani ya nyumba ya mwenye nguvu, na kunyanganya mali yake pasipo kufunga kwanza yule mwenye nguvu, na nyuma kunyaganya vitu vya nyumba yake» (Marko 3, 27).**

**3)** **«Niliona shetani akianguka kama umeme toka mbingu» (Luka 10, 18),** alisema Kristu kwa kufafanusha matunda ya Tendo kitakatifu Yake. Basi, tangu hile wakati shetani alifukuzwa toka mbingu na hapana mu mwaka 1918, sawa vile wanahubiri Washuhuda wa Yehova.

**4)** **«Sasa ni hukumu ya dunia hii; sasa mukubwa wa dunia hii atatupwa inje»; nikusema atafukuzwa, atatupwa ku uwezo na mamlaka yake (Yoano 12, 31)** alisema Kristu saa kidogo mbele ya Usulubisho Yake.

**5)** **«Lakini kama nikikwenda (kwa Mungu Baba) nitamutuma (Roho Mutakatifu) kwenu. Na waakti anapokuja, atahakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu.. . Kwa maneno ya zambi, kwa sababu.. . kwa maneno ya hukumu, kwa sababu mukubwa wa dunia hii amehukumiwa»; nikusema aliisha kuhukumiwa, alihukumiwa shetani (Yoano 16, 7-11).**

**6)** **«Basi, kwa sababu watoto (sisi watoto wa Mungu, sisi watu) wameshiriki damu na mwili (tukona mwili kimutu) yeye mwenyewe (Kristu) aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye Shetani, na kuwafungua wale wote waliokuwa maisha yao yote katika hali ya utumwa, kwa woga wa mauti» (Wa Ebrania 14, 15).** Basi, mauti ya Kristu «alifunga» nguvu ya Shetani na aliuhuru wale walikuwa kwa utumwa wake (shetani).

**7)** **«Nanyi muliokuwa wafu kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, ninyi aliwafanya hai pamoja naye, akiwa ametusamehe makosa yetu yote; akikwisha kuzima hati ile iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondosha na kuifunga kwa musalaba na misumari. Akikwisha kuondosha falme na mamlaka (nikusema ma shetani) akazionyesha waziwazi akizishangilia katika musalaba huu» (Wa Kolosayi 2, 13-15).**

**8)** «Kwa hivi anasema: **Wakati alipopanda juu, alifunga kifungo, akawapa watu zawadi» (Wa Efeso 4, 8).** Nikusema, Kristu tangu hile wakati alipanda Musalabani (Wafafanushi wengine wanasema, wakati alipanda mbinguni) alimufunga Shetani na kwa watu, wenye zamani walikuwa watumwa ya shetani, aliwapatia zawadi ya mbalimbali.

Sawa vile tunaona «kichwa ya nyoka» ilivunjwa kweli kwa sandaka ya Kristu pa Musalaba na Ufufuo Wake. Tangu hile wakati, Shetani alipotesha mamlaka yake pa watu. Kama tena anaitwa «mungu ya hii milele», (barua ya mbili kwa Wa Korinto 4, 4), «mukubwa ya giza» (Wa Efeso 6, 12) hii inakuwa, kwa sababu watu wingi wanakataa wokofu iliyetokea ya Bwana Yesu na wanabaki katika mapenzi yao watumwa ya Shetani. Kristu hasiokoe mutu moja, bila mapenzi yake: Alisema: «Mutu anayetaka kunifuata.. . » (Marko 8, 34). Hwa watu wanakataa, basi, Kristu sawa Muhuru yao, wekona «mungu» yao Shetani katika mapenzi yao. Shetani, hata kisha uvunji wake, anawauzi watu wa dunia, lakini hii tendo yake inakuwa katika uvumilia ya Mungu, anayetuacha sisi kupata majaribu juu ya kufunda ushindani ya roho kupindua ya zambi na hivi tutapata «taji ya uhaki» (Barua ya mbili kwa Timotheo 4, 8). Apizo wa mwisho ya shetani itakuwa kwa Kuja ya Mbili ya Bwana Yesu, na hile wakati Kristu atamutupa mu Gehena pahali «watateswa mushana na usiku hata milele na milele» (Ufunuo 20, 10). Diavolo (shetani) anajua hii malipizo yake, kwa hivyo, wakati Kristu aliponyesha watu wa wili wale walikuwa na pepo machafu ya mukioni Wagerase, ma shetani walipaza sauti, walimwaambia: **« Tuna nini nawe, wewe Mwana wa Mungu? Wewe umekuja hapa kututesa mbele ya wakati? (Matayo 8,**

**29).** Mupaka hile siku ya apizo yake, watu wasiyoamini na wasiyoutawa watamufuata na mapenzi yao na shetani atakuwa mukubwa yao na atawalanda. Lakini shetani hasitaweze kuwa na nguvu yake pa vichwa ya wakristu wa kweli.

Basi, hii wakati ya miaka elfu (1000) ni maana yao ya waakti moja urefu, hile ilianza tangu mwanzo ya Kuja ya Kristu hapa duniani na itaisha kidogo ku mbele ya Kuja ya Mbili Yake. Nikusema ni hii wakati sisi tunaipita. Ndani ya hii wakati anatawala Kristu na wale wanataka kumufuata, wanamuamini na wanamufuata. Ndani ya hii wakati nguvu ya shetani iliisha kuharabika, lakini kama wakristu na mapenzi yao watakataa matendo yake na watafuata matendo ya Kristu.

Hii wakati urefu, ni wakati ya Kanisa wa Kristu, ni Ufalme wa Mungu hapa duniani na inakuwa **«U f u f u o w a. k w a n z a»** inayeandikwa mu sehemu 20 ya Kitabu Ufunuo. Kupatana na Madiko Takatifu, Ufufuo wetu wa kwanza ni uzalio wetu wa mbili katika Roho Mutakatifu; ni wokovu wetu katika Kristu, kama sisi tutaamini na tutabatizwa. Hii wakati tuko mbali ya Kristu na Kanisa Yake, tuko «wafu» katika roho. Angalia kwa mufano baba wa mwana mupotevu, aliyemuita mwana wake: «mufu», ao kumbuka Kristu aliyeita «wafu» wa ndugu ya Mwanafunzi Yake moja, kwani wale waliishi mbali ya sheria yake, lakini hule (mwanafunzi yake) alitaka aende kuzika maiti ya baba yake (Luka 15, 24, 32 Na Matayo 8, 22).

Hii sauti ya kweli anatwaambia na Mutume Paulo: «Hata wakati tulipokuwa wafu, kwa sababu ya makosa yetu, alitupatiza uzima pamoja na Kristu (mumeokolewa kwa neema), na alitufufua pamoja naye na kutukalisha pamoja naye katika pahali pa mbingu, katika Kristu Yesu» (Wa Efeso 2, 5-6. Wa Kolosayi 2, 12-13 na Wa Roma 6, 4). Nikusema Mungu, hata kama sisi tuko wafu, kwa ajili ya zambi zetu, alitupatia uzima upya pamoja na Kristu, alitufufua pamoja na Kristu. Sawa anaweza kusikia kila mutu, hii sauti inanyoloka kwa watu, wenye walikuwa wafu katika roho (waliishi bila imani na uzima upya katika roho) na kisha «walifufua», nikusema wakati waliishi ndani ya hii uzima walifufua katika roho yao (walitubu, walimuamini Kristu na walifanya matendo mazuri); hii ni maana na haiseme ya watu wenye watafufuka katika mwili yao hile wakati ya miaka elfu sawa wanasadiki Washuhuda wa Yehova.

Basi, ufufuo wetu wa kwanza ni ufufuo wetu katika roho, ni uzalio upya yetu katika Kristu na Roho Mutakatifu. Ufufuo wa mbili ni ufufuo wa mwili, itayekuwa hile wakati ya ufufuo muzima ya wafu wote, hile wakati ya Kuja Kristu wa Mbili hapa duniani.

Kristu anatufundisha juu ya «Maufufuo» wa wili» kama anaszema**: «Kweli, kweli ninawaambia ninyi, yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye aliyenituma ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima. Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Saa inakuja, n a. i k o. s a s a, wakati wafu watakaposikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale wanaosikia watakuwa hai»(Yoano 5, 24-25).** Neno: «n a. i k o. s a s a» inaonyesha ya kama alisikia watu, wenye wafu katika roho, waliyeishi mu wakati Mwake na wenye walisadiki mu Kuhubiri Yake na waliokolewa. Na kisha anaendelea: **«Kwa sababu saa itakuja na watu wote walio katika makaburi, watasikia sauti yake (Mungu), nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuko wa uzima, na wale waliofanya mabaya, kwa ufufuko wa hukumu» (Yoano 5, 28-29).**

## 3. UFALME WA MUNGU NI UMOJA

Sawa tulisema juu, Washuhuda wa Yehova, wanafata sehemu saba ya Kitabu Ufunuo na wanaachana watu ya ma kundi wa wili:

1) Kundi wa kwanza ni wenye fazila 144. 000, wenye paka haw ani watu wazuri na waaminifu ya Kanisa: Paka hawa walizaliwa katika roho na wekona ndani yao Roho Mutakatifu na kitumaini yao ni wa mbingu, nikusema mwisho yao ni ya kuishi kwa mbingu sawa ma roho na watawala pamoja na Kristu kwa milele na watakuwa «wana wa Mungu».

2) Kundi ya mbili ni «watu wingi», nikusema ma milioane ya waaminifu, wenye walibaki bila kuzaliwa mara ya mbili katika roho yao na wanaishi bila kuwa ndani yao Roho Mutakaitfu na «kitumaini yao ni wa inchi»: Nikusema wataishi paradizo moja huku pa inchi chini ya utawala wa mbingu ya Kristu pahali watakuwa wale 144. 000 watu wazuri. Hawa watu wingi hawataweze kuwa wana wa Mungu na wanaokolewa, kama wanafuata, bila kuona na kusikia ma amri ya Kundi wa kwanza.

Kwa kusema na ma sauti madogo, Washuhuda wa Yehova wanasema juu ya namna ya wokovu pili na matumaini pili: Moja ni «wa mbingu» ya watu 144. 000 wenye fazila, na moja «wa inchi» juu ya watu wengine. Uchanisho hii inaendelea hivi: Ma zawadi, mabariki yote hile inatokea ya Tendo ukombozi ya Kristu ni paka ya wale 144. 000 waaminifu. Kristu alisulubiwa paka ya wokovu na utakaso ya hawa watu (144. 000). Ma milioane ya watu wengine wanaokolewa hapana kwa ajili ya ushirika wao pamoja na Kristu, lakini kwa ajili ya utii wao kwa wale 144. 000 wenye fazila na utawala wao ni Kundi yao mu fasi Mbruklini ya muji Yorki Mupya ya Amerika. Nikusema hawa 144. 000 wanaokolewa sawa watoto wa Mungu, lakini watu wengine milioane mingi si weko watoto wa Mungu lakini ni watoto ya Kundi yao!

Lakini, utukufu kwa Mungu, kwa sababu hii Habari Njema ya Washuhuda wa Yehova haina hata ushirika na ungano moja na Habari Njema ya Kristu, hile ni ndani ya Agano Jipya. Hii «Habari Njema» yao haina Evangelio ya Kristu, lakini inatokea ya roho muovu na inaleta mafigo ya Mutume Paulo: «Lakini, ama malaika ya mbinguni, tukiwahubiri ninyi Hasbari Njema ya mbalimbali na ile tuliyowahubiri ninyi, alaaniwe. Kama tulivyosema kwanza, sasa tena ninasema mara ya pili. Mutu ye yote akiwahubiri ninyi habari Njema ya mbalimabli na ile muliyopokea, alaaniwe» (Wa Galatia 1, 8-9).

Evangelio (Habari Njema) ya Kristu inahubiri matendo ingine: Inahubiri juu ya wokovu ya watu wote wa dunia, juu ya «kitumaini» moja ya watu wote, juu ya mwito moja ya watu wote, juu ya ma «zawadi» na mabariki ya watu wote. Kabisa inatufundisha hivi:

**1) «Kitumaini»** ni moja: «Mwili ni mumoja, na Roho mumoja kama vilevile mulivyoitwa katika t u m a i n i. moja la mwito wenu» ( Wa Efeso 4, 4). Kitumaini, basi ni moja na hii ni wa mbingu na hapana wa inchi, sawa vile tutaona kidogo chini.

**2) Ma zawadi ni ya watu wote:**

**a)** Watu wenye waliamini na walibatizwa wanachukua wote Roho Mutakatifu (Yoano 3, 5. 7, 38-39. Wa Roma 8, 5-9. 14-17) na pa fasi ingine.

**b)** Waaminifu wote wanachukua zawadi kuwa wana na watoto wa Mungu (Yoano 1, 12, wa Roma 8, 16 na Wa Galatia 3, 26 na 4, 4-5 na barua ya kwanza ya Yoano 3, 2).

**N**a inakuwa hivi, kwa sababu «Mungu hana upendeleo kwa mutu» (Matendo 10, 34).

**3)** Ni wa nani hawa 144. 000 watu wenye fazila na kundi ya mbili «Watu wingi? » Namna gani inaelejewa fundisho hii ya uwogo ya Washuhuda wa Yehova, kwa hii kundi wa wili? Maandiko ya Ufunuo inatwaambia hivi:

**a)** «Nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri katika kila kabila la wana wa Israeli elfu mia moja makumi ine na ine. Wa kabila la Yuda elfu kumi na mbili waliotiwa muhuri. Wa kabila la Rubeni elfu kumi na mbili. Wa kabila la Gadi elfu kumi na mbili. Wa kabila wa Aseri elfu kumi na mbili. Wa kabila la Nafutali elfu kumi na mbili. Wa kabila na Manase elfu kumi na mbili. Wa kabila na Simeoni elfu kumi na mbili. Wa kabila la Lawi elfu kumi na mbili. Wa kabila la Isakari elfu kumi na mbili. Wa kabila la Zebuluni elfu kumi na mbili. Wa kabila la Yosefu elfu kumi na mbili. Wa kabila la Benyamina elfu kumi na mbili waliotiwa muhuri» (Ufunuo 7, 4-8). «Ila wale elfu mia moja makumi ine na ine, walionunuliwa katika dunia. Hawa ndio wasiotiwa uchafu pamoja na wanawake; kwa maana ni mabikira. wanaofuata Mwana -Kondoo kila pahali

anapokwenda. Hawa wamenunuliwa katika watu, malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo» (Ufunuo 14, 3-4).

**b) «Nyuma ya maneno haya nikaona, na tazama, makutano makubwa sana asiyeweza mutu kuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha wamesimama mbele ya kile kiti (wa Mungu) cha ufalme, na mbele ya Mwana-Kondoo (Kristu) wamevikwa mavazi meupe, na matawi na mitende katika mikono yao; wakilia na sauti kubwa wakisema: Wokovu kwa Mungu wetu anayeketi juu ya kiti cha ufalme, na Mwana-Kondoo.. . Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni nani? Nao walitoka wapi? .. . Hawa ndio wanaotoka katika mateso haya makubwa, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya mwana-Kondoo. (15)Vile wako mbele ya kiti cha ufalme cha Mungu, na wanamutumikia mushana na usiku katika hekalu lake.. . » (Ufunuo 7, 9-16 na 19, 1).**

Imani ya Washuhuda wa Yehova ya kama ndani ya Ufalme wa mbingu wataingia paka 144. 000 waaminifu ni wa bure, ya kucheka na upumbafu. Kwa sababu inaonekana sadi ya kama hii maandiko ya Kitabu Ufunuo inatwaambia na namna kwa mufano: 144. 000 wana wa Israeli (nikusema 12. 000) watu ya kila kabila ya watoto wa Yakobo, «Hawa ndio wasiotiwa uchafu pamoja na wanawake; kwa maana ni mabikira». Kama tutapokea hesabu 144. 000 katika hesabu yake na hapana katika mufano na alama yake, tutafika pa hii mawazo: Ndani ya Ufalme wa Mungu wataingia:
Paka watu wa Ebrania,
paka wanaume,
paka wasiyo ndoa
na paka mabikira.
Kwa hivi hakuna namna kuwa ndani Mutume Petro, kwa sababu yeye alikuwa na ndoa. Mtume Luka inapashwa kumufukuza, kwani hasikukuwe mutu wa Ebrania. Tena inapashwa kutosha na Mzazi-Mungu Bikira Maria, kwa sababu alikuwa mwanamuke. Hivi, kama tutaelejea hesabu 144. 000, tunapashwa kutosha inje ya Ufalme ya Mungu watakatifu milioane.

Basi inaonekana safi, ya kama hii hesabu ya 144. 000 ni mufano ya watumwa (watoto) wa Mungu wenye muhuri. Ni alama na inatwaambia waaminifu wote ya ma wakati wote ya dunia wote, wenye walimufurahisha Mungu, mbele na kisha uzalio ya Kristu, katika uzima takatifu yao. Hesabu wa kweli ya wale wataingia mu Ufalme wa Mungu hakuna namna kujua sisi. Paka Mungu anajua watu wa ngapi wataenda mu Paradizo.

Juu ya kuelejea mambo ya Kundi ya mbili, nikusema «watu wingi», Washuhuda wa Yehova, wanasadiki ya kama hii Kundi ya watu itaikaa kwa milele pa inchi, lakini andiko ya Ufunuo haiseme hata fasi moja hii sauti na imani yao. Kupindua inaandika: «Hekalu la Mungu likafunguliwa katika mbingu na sanduku ya agano lake ilionekana ndani ya hekalu lake» (Ufunuo 11, 19) na: «na nyuma ya maneno haya nikaona, na tazama, hekalu la hema ya ushuhuda katika mbingu lilifunguliwa» (Ufunuo 15, 5) na «Sauti kubwa ikatoka katika hekalu, katika kiti cha ufalme, ikisema: Imefanyika.. . » (Ufunuo 16, 17). Nikusema ndani ya ma shairi wa juu tunasoma ya kama watasimama mbele ya kiti ya Mungu na Kristu kwa mbingu na watamuabudu Mungu siku na usiku ndani ya hekalu, nikusema ndani ya hekalu wa mbingu.

Ila tu, mu sehemu 19, 1 tunasoma: «Nyuma ya maneno haya nikasikia sauti kama sauti ya makutano makubwa, sauti kubwa mbinguni, ikisema: Haleluya» (Ufunuo 19, 1). Basi, makutano makubwa ya watu itakuwa kwa mbingu na hapana pa inchi yetu. Inchi yetu itaharabikwa, sawa vile tutaandika kidogo chini.

Basi, ma kundi wa wili watakuwa pamoja na watabaki ndani ya Ufalme moja wa Mungu, kwa mbingu na hapana pa inchi yetu.

## 4. UFALME WA MUNGU NI WA MBINGU

Ufalme wa Mungu, basi, ni wa mbingu na moja na ndani kwake wataingia hawa wataokolewa. Keli, Kristu na Mitume hawakuaachana Ufalme wa Mungu na Vipande wa wili: Ufalme wa mbingu na wa inchi. Ma siku zote mu uzima yao hapa duniani walihubiri paka ya Ufalme M o j a (Matayo 16, 28. 25, 34); walisema juu ya Kanisa M o j a (Matayo 16, 18), juu ya Mwili ya Kristu M o j a ( Wa Roma 12, 4-5), juu ya Kundi (ya waaminifu) M o j a (Yoano 10, 16). Huu Ufalme Moja na wa pekee haina wa inchi na wa mbingu, lakini ni paka wa mbingu. Hii inatufundisha na Madiko Takatifu na inafundisha hapana waaminifu ya kundi moja, sawa vile wanasadiki Washuhuda wa Yehova, lakini inanyoloka ma sauti yake (Madiko Takatifu) mbele ya watu wote:

**1)** **«Tubuni, sababu ufalme wa mbinguni umekaribia», walihubiri hivi Kristu, Mitume na Yoano Mubatizaji mbele ya taifa yote (Matayo 3, 1-2. 4, 17 na 10, 7. Marko 1, 14-15 na ma fasi ingine)**

**2)** Kristu alihubiri paka ya Ufalme mbinguni: «Furahini, shangilieni; kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni» (Matayo 5, 11-12). **«.. . Lakini mutu atakayezitenda na kuzifundisha, huyu ataitwa mukubwa katika ufalme wa mbinguni» (Matayo 5, 19-20)** na ingine mistari pa fasi ingine.

**3)** Mutume paulo tena anatufunua ya kama Paradizo haitakuwa pa hii inchi yetu, lakini itakuwa kwa Mbingu wa tatu. Kule pa «mbingu wa tatu», pahali ni Paradizo **«.. . Alichukuliwa juu hata mbingu ya tatu. Nami ninajua mutu huyu (kama katika mwili, kama inje ya mwili, sijui: Mungu anajua), ya kama alichukuliwa juu hata Paradiso, akasikia maneno yasiyoweza kusemwa.. . » (Barua ya mbili kwa wa Korinto 12, 2-4).** Pa fasi ingine anaandika: «Lakini kama ilivyoandikwa: Jicho halikuona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mutu» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 2, 9). Paradizo, basi, haitakuwa pa inchi, lakini kwa «mbingu ya tatu», nikusema mu Paradizo na vitu vyake hayatakuwa usawa na vitu vya hii inchi yetu.

**4)** **«Kwa maana sisi ni wenyeji wa mbingu; kutoka pale tunangoja Mwokozi, Bwana Yesu Kristu» (Wa Filipi 3, 20).**

**5)** **«Maana hapa (pa inchi hii) hatuna muji unaodumu, lakini tunatafuta ule unaokuja» (Wa Ebrania 13, 14).**

**6)** **«Tunashukuru Mungu.. . . kwa sababu ya tumaini mulilowekewa akiba mbinguni, habari zake mulizosikia zamani katika neno la kweli ya habari Njema» (Wa Kolosayi 1, 3-5)** anaandika hivi Mutume Pauli na anaendelea: **«Basi mukiwa mumefufuliwa pamoja na Kristu, tafuteni maneno yaliyo juu, pahali Kristu yuko, akiketi mukono wa kuume wa Mungu. Tieni mafikili yenu juu ya maneno ya juu, wala si juu ya maneno yaliyo duniani» (Wa Kolosayi 3, 1-2).**

**7)** **«Maana mulihurumia wale waliokuwa katika kifungo, na mulikubali kwa furaha kunyanganya kwa mali zenu, mukijua ndani yenu na kuwa muna mali mbinguni, iliyo njema zaidi, inayodumu», anaandika Mutume Paulo kwa watoto wa roho yake ( Wa Ebrania 10, 34).**

**8)** Mungu alituzala sisi mara ya mbili katika roho **«tupate uriti usioharibika, usio na uchafu wala usiopunguka, muliowekewa akiba mbinguni» (Barua ya kwanza ya Petro 1, 4).**

**9)** Huu Ufalme mbinguni na Mutume Paulo anaitakia kufa na hivi atakutana na Yesu Kristu: **«Lakini ninasongwa katika mambo wa wili, (niishi hapa ao nikufe) nikitamani kwenda zangu nikae pamoja na Kristu; maana ni vizuri zaidi sana» (Wa Filipi 1, 23).** Anaitakia kufa, kwani anajua ya kama: **«kwa maana tunajua ya kama nyumba ya dunia ya hema yetu ikibomolewa (nikusema mwili yetu itakufa) tuna jengo linalotoka kwa Mungu,**

**nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele katika mbingu» (Barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 1).**

**10)** Basi, kwa sababu inchi yetu wa kweli ni mbinguni na hapana pa inchi yetu, kwa hivyo andiko ya ma jina yetu inakuwa kwa mbingu: **a) «.. . Lakini furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa katika mbingu» (Luka 10, 20). b) «lakini minyi mumefikia mulima Sayuniu, na muji wa Mungu aliye hai, Yerusalema wa mbinguni, na mjeshi ya malaika elfu nyingi, na makutano makubwa, na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa katika mbingu.. . » (Wa Ebrania 12, 22-23).**

**11)** Ku mwisho, kwa hii fundisho ya Washuhuda wa Yehova ya kama watafufuliwa watu wenye haki ya Agano la kale (kwa mufano Abrahamu, Isaka, Yakobo na wengine) juu ya kuchukua utawala ya inchi yetu na hii itakuwa ufalme wa Mungu(!) tunatazama ya kama hawa watu wenye haki ya Agano la Kale, wanasema ya kama maneno haya ya Washuhuda wa Yehova ni ya uwogo zaidi:

**«**Hawa wote walikufa katika imani, pasipo kupokea zile ahadi, lakini waliziona tokea mbali na kuzisalimu, na kukiri ya kwamba **walikuwa wageni, na wasafiri juu ya inchi.** Maana wenye kusema maneno kama haya wanaonyesha wazi ya kuwa wanatafuta inchi yao wenyewe. Na kama wangalikumbuka ile waliyotoka, wangalipata nafasi kurudi. Lakini sasa wanatamani inchi iliyo nzuri zaidi, ndiyo ya mbinguni. Kwa sababu hii Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea muji». **«Kwa imani alikaa katika inchi ya ahadi kama katika inchi isiyo yake, akakaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, wariti pamoja naye wa ahadi ile ile. Maana alitazamia muji wenye misingi, ndiyo mwenye kuujenga na kuufanya ni Mungu» (Wa Ebrania 11, 13-16 na 9-10).**

Hii sauti ya kweli anaikikiri na Yesu Kristu: **«.. . ya kama wengi watakuja toka mashariki na toka mangaribi, na wataketi pamoja na Abrahamu na Isaka na yakobo katika ufalme wa mbinguni, lakini wana wa ufalme watatupwa katika giza la inje; » (Matayo 8, 11-12).**

Basi, Washuhuda wa Yehova wanaongojea ya bule kufika Ufalme wa Mungu na utawala na mkubwa Abrahamu na wengine wenye haki ya Agano la Kale. Maneno ya Kristu: **«Lakini ole wenu.. . kwa sababu munafungia watu ufalme wa mbinguni. Kwa maana ninyi hamwingii ninyi wenyewe, wala wale wanaoingia, hamuwaachi kuingia» (Matayo 23, 14);** hii sauti ya Kristu inatimizwa kabisa kwa hawa Washuhuda wa Yehova.

## 5. UFALME WA MUNGU NI WA ROHO NA HAPANA WA MWILI

Sawa vile sisi tulisikia na tulisoma nyumba wa milele ya wale wataokolewa itakuwa Ufalme mbinguni na hapana hii inchi; hivi na vitu wa hii inchi itakuwa kwa bure. Paradizo wa hii inchi wanasema na wanasadiki Washuhuda wa Yehova (na chakula na kinywaji na zambi wa mwili) ni umoja na Paradizo ya dini ya Umuslimani (wenye wanasadiki ya kama paradizo yao itakuwa na chakula ya muchele, sali na zambi katika mwili); lakini hii paradizo yao hana na hata ushirika kimoja na Ufalme Mbinguni wa Mungu wetu, kwa sabahu Ufalme wa Mungu ni hali wa roho kw ambingu.

**1)** «Kwa maana tazama, ufalme wa Mungu ni ndani yenu» (Luka 17, 21), alisema Kristu na alisikia uzima katika sheria ya Mungu, inayepashwa kutawala ndani ya roho ya watu.

**2) «Kwa maana ufalme wa Mungu si kula na kunywa, lakini haki, na salama, na furaha katika Roho Mutakatifu» (Wa Roma 14, 17).** Basi, Ufalme wa Mungu ni kupata Neema ya Roho Mutakatifu na hapana kula na kunywa.

**3)** «Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula, lakini Mungu ataharibu vyote viwili, tumbo na vyakula» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 6, 13).

4) **«Lakini Yesu akajibu, akawaambia: Munakosa kwa sababu hamujui maandiko wala uwezo wa Mungu. Kwa maana katika ufufuko hawaoi wala hawaolewi, lakini watakuwa kama malaika mbinguni» (Matayo 22, 29-30).** Hii jibu umoja Kristu ananyoloka leo na kwa Washuhuda wa Yehova, wenye wanafundisha ya kama mu Ufalme wa Mungu wataendelea zambi wa mwili yao.

**5)** Ku mwisho, mu Ufalme wa Mungu miili wetu watafufuliwa makamilifu na wasiyoharabika, watabadilika na kisha mafuraha katika mwili na mali ya hii uzima itakuwa vitu wa bure: **«Ufufuo wa wafu ni hivi vilevile. Unapandwa katika kuoza, unafufuliwa katika kutokuoza: . . . (shairi 51-53): «Sisi sote hatutalala, lakini sisi sote tutabadilika, kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho, kwa baragumu ya mwisho: sababu baragumu italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na kuoza, na tutabadilika. Maana sharti ule wenye kuoza uvae kutokuoza, na huu wa mauti uvae kutokufa». Barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 42, 51-53).** Mali ya hii inchi inalazimishwa paka ya maisha ya miili yetu inayaharabika na hapana ya miili isiyaharabika

Washuhuda wa Yehova wanaleta maandiko ya mbali mbali toka Agano la kale, kabisa maandiko ya Isaya: 11, 6-9. 35, 36, 3. 65, 17-25. 25, 6-8 ; maandiko haya wanasema juu ya paradizo moja wa inchi, pahali mume imbwa atakula mayani pamoja na mwana-kondoo, simba pamoja na mbuzi na ingine sauti na ndani ya huu paradizo watu watapata, bila muchoko, vitu vyote vya hii dunia.

Sawa sisi wote tunasikia hii maandiko yote ni mifano. Kwa mufano andiko ya kuishi imbwa pamoja na mwana-kondoo (11, 6-9) inatimizwa mu wakati ya Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa sababu mbele Yake watu waliishi sawa nyama ya pori, lakini kwa Kuja Kristu duniani watu walikuwa wenye amani na wa haki. Washuhuda wa Yehova, lakini wanapokea na hii ufafanusho yetu.

Tena unabii mu mustari (Isaya 35) ni kweli ya kama utimizo yake ni wa roho.. » Unabii ya mustari (65, 17-23) wanatimizwa kabisa mu hii wakati ya uzima yetu. Unabii ya mustari (25, 6-8) Washuhuda wa Yehova wanasema ya kama inatimizwa leo na namna wa roho.

Lakini, wanasadiki zaidi na wanaongojea paradizo wa mwili na wa inchi pahali wataendelea ma furaha na zambi zao. Kwa hawa inatimizwa neno ya Mutume Paulo: «mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao ni haya yao, wanaofikili maneno ya dunia» (Wa Filipi 3, 18-20).

## 6. UHARIBIFU YA INCHI NA MBINGU

Washuhuda wa Yehova wanafundisha tena ya kama hii inchi sisi tunaikaa itakuwa kwa milele, sawa tulisema kidogo yulu, kwani ndani ya hii inchi itakuwa paradizo yao. Lakini neno ya Mungu inatufunua ya kama hapana paka inchi, lakini ulimwengu muzima, hii sisi tunaiona, itaharabika hile wakati ya Kuja wa Mbili ya Kristu na itachukua uso ingine:

**1) «Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kabisa». (29) «jua litatiwa giza, wala mwezi hautatoa nuru yake, na nyota zitaanguka toka mbinguni, na nguvu za mbingu zitatikisika» (Matayo 24, 35, 29). «Kwa maana kweli ninawaambia ninyi, Hata mbingu na inchi zitakapoondoka, yodi moa wala nukta moja haitaondoka, hata yote yatimie» (Matayo 5, 18).**

Lakini Washuhuda wa Yehova wanafafanusha hii mistari wa juu na namna ingine. Wanasema: «Jua» ya utajiri ubinadamu itajaza na giza kwa ajili ya sikitiko ya feza». Mwezi, wanasema, ni «mwezi» ya utawala wa watu iliyejaza na mwangaza na itakuwa ukali na watu chini ya hii utawala watateswa». Ku mwisho, «na nyota zitaanguka toka mbinguni.. . », wanasema, ni hekima ya wenye akli watu wa hii dunia, lakini hii hekima yao itaharabika»!!!

**2) «Wewe Bwana, katika mwanzo umeweka misingi ya inchi, na mbingu ni kazi za mikono yako. Hizi zitaharabika, lakini wewe unabaki; Na hizi zote (wa mbingu) zitachakaa kama nguo, na kama mavazi itazikunja, nazo zitabadilika; lakini wewe ni sawasawa saa zote, na miaka yako haitakoma» (Wa Ebrania 1, 10-12).**

**3) «Lakini mbingu zilizo sasa, na dunia, zimewekwa akiba kwa moto kwa neno hili, zikilindwa hata siku ya hukumu na uharibifu wao wasiogopa Mungu» (barua ya mbili ya Petro 3, 7).** Nikusema mbingu na inchi wa sasa wanabakia hivi katika uwezo na neno ya Mungu kwa moto na watabakia hivi mpaka hile siku ya hukumu na uharibifu ya watu wasiyoimani.

**-«Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwizi; katika siku hii mbingu zitatoweka na sauti kubwa, na viumbe vya asili vitayeyushwa kwa moto mukali, na inchi na kazi zilizo ndani yake zitateketezwa» (barua ya mbili ya Petro 3, 10).**

**-«Basi kwa kuwa vitu hivi vyote vitayeyushwa hivi, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mutakatifu na utawa, mukitazamia na kutaka sana kuja kwa siku ya Mungu, kwa sababu yake, mbingu zikiungua zitayeyushwa, na viumbe vya asili vitayeyuka kwa moto mukali? » (barua ya mbili ya Petro 3, 11-12).**

**4)** «ndiyo sauti yake ilitetemesha dunia wakati ule (pa mulima Sinaya); lakini sasa ameahidi akisema: Mara moja tena nitatetemesha dunia, wala si dunia tu, lakini na mbingu pia. Neno lile, Mama moja tena, linaonyesha kuhamishwa kwa vitu vinavyoweza kutetemeshwa kama vitu vilivyoumbwa, kusudi vitu visivyoweza kutetemeshwa vikae» ( Wa Ebrania 12, 26-27). Nikusema inchi na mbingu, kama viumbe, yatatemeshwa ku Mungu, yatatoka, yataharabika na yatabakia paka vile vitu visivyoweza kutetemeshwa (nikusema Ufalme wa Mungu).

**5) «Nikaona kiti cha ufalme, kikumbwa, cheupe, naye anayeketi juu yake, dunia na mbingu zikakimbia uso wake; na pahali pao hapakuonekana» (nikusema hata alama yao haikuonekana) (Ufunuo 20, 11-12).**

**6)** Kisha uharibifu ya hii ulimwengu Mungu ataleta mbingu na inchi mapya: **«Lakini kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na inchi mpya, pahali haki inapokaa» (barua ya mbili ya Petro 3, 13). «Nikaona mbingu mupya na dunia mupya; kwa maana mbingu za kwanza na dunia ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena» (Ufunuo 21, 1).**

Neno ya Mungu kwa uharibifu ya mbingu na inchi, sawa sisi wote tunaona, ni usadi kabisa, hata kama Washuhuda wa Yehova, wanataka kufunga ma macho yao na hawaweze kutazamia fundisho hii wa kweli ya Madiko Takatifu. Na hawa walipata mafafanuisho ingine katika akili yao. Wanasema ya kama hii inchi na mbingu toka mustari ya (barua ya mbili ya Petro 3, 7-12), haina mbingu wetu na ulimwengu wetu, lakini ni mataifa ya dunia; vile wanafafanusha «inchi»; lakini Matawala wa watu ni «wa mbingu». Tena wanaleta na mistari yao juu ya kusema ya kama inchi ni maana ya watu. Kwa mufano Zakaria 1, 11), Matayo 6, 10). Ndani ya mistari haya tunatazamia ya kama katika neno «inchi» ni maana ya watu. Lakini tusitaweze kupata hata fasi moja ya kama neno «mbingu» inaonyesha maana «matawala ya watu. Kwa hivyo mustari ya Petro hakuna namna kuifafanusha katika mufano.

Tena, kama ufafanusho ya neno: «wa mbingu» niko na maana= matawala ilikuwa wa kweli; sauti yao itakuwa kupindua ya Washuhuda wa Yehova. Hivi ilipashwa kila utawala ubinadamu kuwa (hapana wa zambi na washetani, sawa hawa wanasema, lakini ilipaswa ) kuwa matakatifu na wa Mungu, kwani: **«Na anga zinaonyesha kazi ya mikono yake». Tena: «Mbingu (watawala) zinatangaza utukufu wa Mungu; (zaburi 19, 1).** Iko namna kusadiki sisi ya kama «wa mbingu» ni matawala wa watu na haya matawala wanaelejea utukufu wa Mungu?

Tena na ingine neno: Kwa sababu Washuhuda wa Yehova wanataka kufafanusha neno «Wa mbingu» sawa matawala ya dunia hii, sisi tunawauliza: « Basi, na «jua» inaonyesha maana ya waongozi (wakubwa) ya matawala, «mwezi» wakubwa ya Makutano yao na «ma nyota» wakubwa ya ma serkali yao? Hawa watu wakubwa, sisi tunajua, ni watu ya matawala ya inchi kimoja, sawa jua, mwezi na nyota ni vitu vya mbingu. Hii haina katika uwazo ya akili ya mutu moja? Basi, tunaona, ufafanusho kimoja ukosefu, mafafanusho ma ngapi iko namna kuzala na itaongoza wapi!

Ndani ya vitabu vyao wanaandika ya kama «wa mbingu wapya» ni Kristu pamoja na 144. 000 «warafiki ya mufalme» na pamoja nao Kristu atawala mu Ufalme wa mbingu, lakini «wa mbingu na inchi wa sasa» ni «Kundi isiyoonekana ya shetani». «Ma nyota», yenye utaanguka chini toka mbingu, katika akili yao, itakuwa, «mashemasi ya dini wa uwogo ya shetani»!!! Ninazania, ya kama haina lazima kufafanusha maana ya akili yao!

Washuhuda wa Yehova wanasingi imani yao juu ya uzima wa milele pa hii inchi ndani ya mistari ya Madiko Takatifu na hii mistari wanapatia maana ya kama uzima wa milele itakuwa pa hii inchi, sawa vile ni haya:

1) **«Kizazi kimoja kinakwenda, na kizazi kingine kinakuja; na dunia inadumu milele» (Muhubiri 1, 4).**
2) **«Aliyeweka miningi ya inchi, isitikisike milele» (Zaburi 104, 5).**
3) **«Na kiti chake cha ufalme kama jua mbele yangu. Kitasimamishwa milele kama mwezi» (Zaburi 89, 36-37).**
4) **«Mungu yeye mwenyewe aliyeumba dunia na kuifanya, yeye aliyeisimamisha, hakuiumba ukiwa.. . » (Isaya 45, 18); kwa hivyo alibariki uzazi ubinadamu juu ya kuongezeka na kujaza inchi (Mwanzo 1, 28). Na kwani anachunga malako Yake na hasibadilika (Malaki 3, 6), kwa hivyo hasiweze kugeuza uwazo na hasipenda kuharabisha inchi, wanasema Washuhuda wa Yehova. Tena, wanaongeza, Huyu mumoja «ataharabisha wala watu wataharabisha inchi» (Ufunuo 11, 18).** Basi, Mungu anaonyesha mafaa Yake ya kubaki inchi kwa milele. Vile wanasema Washuhuda wa Yehova.
5) **«Heri wenye upole: maana wao watariti inchi» (Matayo 5, 5). «Lakini wapole watariti inchi, na kukaa ndani yake milele» (Zaburi 37, 11, 22, 29)**

Sawa anaweza kuona kila musomaji mistari haya wa juu walichukuliwa toka Agano la Kale.

Mbele ya kufafanusha ma shairi-bunduki yao, tunamikumbuka sauti moja tuliisema ku mwanzo ya hii Kitabu: Ya kama Agano la Kale haiandike ufunuo muzima ya fundisho ya Mungu, haina nikusema ukamilifu na wa safi kabisa. Paka tunapata ndani ya Kitabu ya Agano la Kale mifano na maandiko wa zamani sawa mifano na ma alama ya sauti wa kweli. Lakini fundishi ukamilifu na muzima kabisa ilionekana na Bwana Yesu Kristu duniani. Kwa hivyo Agano la Kale iko namna kuisikiwa maana yake, paka chini ya ufafanusho ya Agano Jipya. «Basi kwa kuwa torati (ya Agano la Kale) ni kivuli cha yale mema yatakayokuwa, wala si sura yao yenyewe, haiwezi hata mara moja kwa zabihu wanazozitoa kila mwaka daima, kukamilisha wenye kukaribia» (wa Ebrania 10, 1) na (Kolosayi 2, 16-17). Neno ya Mungu ilikuwa siri iliyekuwa kwa siri mbele ya miaka wa milele. Kwa hivyo, hapana Agano la Kale, lakini Agano Jipya ni Kitabu ya kupata yeyuko ya machanisho yote katikati ya Agano la Kale na Agano Jipya.

Kama tunajua maneno haya yote, hii machanisho ni katikati ya Agano la Kale, (pahali inaandika juu ya uzima wa milele ya inchi hii) na Agano Jipya (pahali inaandika juu ya uharibifu nzima ya inchi na mbingu) itapashwa kupatana maana ya Agani Jipya na hapana ya Agano la Kale. Kwa hivyo, mafundisho toka Agano la kale juu ya uzima wa milele pa inchi yetu tunapashwa kuipokea sisi na maana hapana ukamilifu, kwa sababu, kama sisi tutayaona katika nuru ya Agano Jipya hakuna namna kusadiki ya kama hii inchi itabakia kwa milele.

Ila tu, mustari: «kwa milele», mara mengi ni maana hapana milele, masiku zote, lakini wakati ya hii dunia» Kwa mufano Matayo 13, 39. 28, 20.

Pa hii fundishso bunduki yetu ingine ni hii: Neno» «kwa milele» mu Agano la Kale, mu lugha kiebrania ni «O-LAM» nikusema nyakati isiyokuchakuliwa. Basi, ufafanusho ilipashwa kuwa hivi:

1) **«Kizazi kimoja kinakwenda, na kizazi kingine kinakuja; na dunia inadumu nyakati isiyokuchakuliwa» (Muhubiri 1, 4).**
2) **«Aliyeweka miningi ya inchi, isitikisike nyakati isiyokuchakuliwa» (Zaburi 104, 5).**
3) **«Na kiti chake cha ufalme kama jua mbele yangu. Kitasimamishwa nyakati isiyokuchakuliwa kama mwezi» (Zaburi 89, 36-37).**

Sisi tulipata hii ufafanusho ndani ya vitabu yao. Basi, hatunana lazima ya ma bunduki ingine. Ma bunduki yetu wanatupatia hawa Washuhuda wa Yehova. Tena mara ingine inatimizwa sauti ya Kristu: **«Kwa kinywa chako nitakuhukumu, wewe mutumwa mubaya» (Luka 19, 22).**

Hii misteri wa juu wanafafanusha nzuri kabisa mambo ya uzima wa milele pa inchi hii; lakini sisi tutajibu pa mistari yao ya hesabu **4), 5).**

Kwa fundisho yao na hesabu **4)** tunajibu ya kama, kweli Mungu aliumba inchi kwa inadumu ya watu. Lakini, wakati Mungu alipatia kwa Wazazi wetu wa kwanza amri wagezeka na wajaze inchi, kiumba (mbingu, inchi na mutu) hayakukuwa sawa sisi leo tunayaona, lakini na namna ingine. Lakini zambi na kosa ya wazazi wa kwanza walibadilisha yote wa hii dunia:

a) Watu walifata sheria ya uharibifu, mauti na zambi (Mwanzo 2, 17. 3, 16, 19. Wa Roma 5, 12, 14, 6, 23, 7, 14-23. Barua ya kwanza ya Petro 1, 24).

b) Kiumbe isiyo na mioyo iliingia na hii ndani ya uharibifu, badilisho na **«viumbe vyote pia vinaugua, na vina uchungu pamoja hata sasa» (Wa Roma 8, 20-22 na Mwanzo 3, 17).**

Basi, malako, ya Mungu na baraka Yake yalikuwa kwa hali kimutu ya wazazi wa kwanza mbele ya kosa yao. Wakati, lakini, Adamu na kiumbe yote walianguka pamoja naye, kisha ilibadilishwa namna ya maisha. Hii inchi na hii mbingu haina hii kiumba aliitaka Mungu kujaza na watu. Inakuwa namna umoja sawa itafanyika na kwa mwili wa mutu. Sawa vile inatufundisha Madiko Takatifu huu mwili yetu wa uharibifu na ubinadamu na ugonjwa na isiyoutukufu inapashwa kuvaa utukufu na nguvu na uzima isiyo kufa na isiyokuharabika (barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 42-53), lakini juu ya kuwa hii tendo inapashwa mbele kuwa uharibifu yake ndani ya bulongo. (Sawa vile mbegu, inakufa ndani ya bulongo ya inchi, na kisha inaota sawa chipukizi, vile zaidi na mwili yetu, inapashwa kufa, na kisha itafufuliwa isiyoharibifu na isiyo mauti, kwa utukufu na wa nguvu (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 35-44). Basi, juu ya nini inaonekana kwa sisi hii mambo wa ajabu, kwani na ulimwengu mzima inayeiko chini ya kiumba wa uharibifu (wa Roma 8, 20) itauhuruwa toka utumwa ya uharibifu (Wa Roma 8, 21), lakini itafanyika ku mbele uharibifu yake kwa moto (barua ya mbili ya Petro 3, 10-13)? Toka hii uharibifu kwa moto itaumbuwa «inchi upya» na «ma mbingu mapya», lakini «mbingu wa kwanza na dunia ya kwanza zimekwisha kupita»( Ufunuo 21, 1).

Kwa ajili ya shairi yao mu hesabu **5)** ni usafi ya kama, kwa sababu hii inchi itaharabika na hii «inchi» watariti «wenye upole» na «wenye njaa na kiu kwa haki», ni «inchi upya», itayeonekana Mungu, kisha uharibifu ya hii inchi. Hile «inchi upya» ni Inchi wa kweli ya malako», ni Paradizo, ni Ufalme wa mbingu. Mustari yao ya hesabu **(5)** ilitokea toka Heri (Matayo 5, 3-12), pahali anahubiri Kristu juu ya malipo wa roho ya wenye haki: «maana ufalme wa mbinguni ni wao», «wao watariti inchi», «wao watapata rehema», «wao wataona Mungu».. . Lakini, sawa vile tuliona, Ufalme wa Mungu itakuwa umoja na wa mbingu. Basi, mashahara ya

wa Heri wanatwaambia juu ya Ufalme wa Mungu Umoja. Basi, «inchi ya wenye upole» (Matayo 5, 5), inapashwa kusharikiwa na «ufalme wa mbingu» na «walio masikini wa roho». (5, 3).

Basi, uharibifu ya inchi na mbingu kwa moto haitarudie kwa sifuru, lakini kwa iumba upya yatakwa mbingu na inchi mapya. Hii kiumba upya, itayekuwa uhuru toka uharibifu itakuwa ya kuachana ya hii kiumba wa sasa, kwani haitakuwa lazima kula, wala kuwa zambi wa mwili, lakini watu wataishi kama malaika» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 6, 13 na Matayo 22, 30) na watakuwa na ushirika pamoja na Mungu. Hii «inchi» watairiti «wenye upole», na itakuwa isiyo haribifu na isiyo uchafu toka zambi na itabakia kwa milele.

Tena, tunaweza kuandika sasa na Agano la Kale inatufundisha juu ya uharibifu ya mbingu na inchi na kiumba ya «ma mbingu mapya» na «inchi upya»:

**«Tazama Bwana anafanya dunia kuwa utupu, na anaiharibu, na anaipindua, na kusambaza wenye kukaa ndani yake.. ». «Inchi itafanya kuwa utupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; kwa maana Bwana amesema neno hili». «Na itakuwa kila mutu anayekimbia sauti ya woga ataanguka katika shimo; na kila mutu anayepanda toka katikati ya shimo atanaswa kwa mutego; .. . Dunia inavunjika kabisa, dunia inayeyuka kabisa, dunia imetikisika sana.. . na zambi yake itakuwa nzito juu yake; na itaanguka na haitasimama tena» (Isaya 24, 1, 3, 18-20).**

**-«Nyanyueni macho yenu mbinguni, na tazameni dunia chini: maana mbingu zitatoweka kama moshi, na dunia itachokaa kama vazi, nao wanaokaa ndani yake watakufa vivyo hivyo; lakini wokovu wangu utakuwa kwa milele, na haki yangu haitavunjika» (Isaya 51, 6).**

**-«Maana, tazama, mimi ninaumba mbingu mpya na dunia mpya, na maneno ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni» (Isaya 65, 17 na 66, 22).**

Sauti ya mwisho: Haipashwe kuwa hata shaka moja juu ya uharibifu nzima ya inchi na mbingu, kwa sababu yanatuwaambia na namna usafi Washuhuda tano toka Madiko Takatifu:

-Kristu mumoja (Matayo 5, 18. 24, 35, 29).
-Mutume Paulo (Wa Ebrania 1, 10-12).
-Mutume Petro «barua ya mbili ya Petro 3, 7, 10-13).
-Mutume Yoano (Ufunuo 20, 11 na 21, 1).
-Nabii Isaya (24, 1, 3, 18-20. 51, 6. 65, 17. 66, 22).

## 7. MA NENO YA WAKATI

Washuhuda wa Yehova walichakua mara mengi ma tarehe ya mbali mbali juu ya mwisho ya dunia, lakini ma sauti-manabii yao hayakutimizwa na hawa walichekelewa. Madiko Takatifu inatwaambia ya kama hata mtu moja hasijue nyakati ya kweli ya mwisho ya hii dunia na KUja wa Mbili ya Kristu, ila tu Mungu:

1) **«Lakini hakuna mutu anayejua habari za siku ile na saa ile, hata malaika walio mbinguni wala Mwana, ila Baba peke yake» (Matayo 24, 36).**

2) **«Kwa hivi muwe tayari; kwa sababu kwa saa musiyozani Mwana wa watu anakuja. Angalieni basi; kwa sababu hamujui siku Bwana yenu atakapokuja». Angalieni basi, kwa sababu hamujui siku wala saa» (Matayo 24, 44, 42. 25, 13 na Luka 12, 40).**

3) **«Si maneno yenu kujua nyakati wala majira Baba aliyoweka katika mamlaka yake mwenyewe» (Matendo 1, 7).**

4) **«Lakini juu ya nyakati na majira, ndugu, hamuhitaji niwaandike ninyi. Maana ninyi wenyewe munajua sana ya kwamba siku ya Bwana inakuja kama mwizi katika usiku» (barua ya kwanza kwa Watesalonika 5, 1-2)** na **«Lakini siku ya Bwana itakuja**

**kama mwizi; katika siku hii mbingu zitatoweka na sauti kubwa, na viumbe vya asili vitayeyushwa kwa moto mukali, na inchi na kazi zilizo ndani yake zitateketezwa» (barua ya mbili ya Petro 3, 10).**

Mbele ya mistari yetu wa juu Washuhuda wa Yehova wanasema hii shairi: **«lakini ninyi ndugu, si katika giza, hata siku ile iwapate ninyi kama mwizi» (Barua ya kwanza kwa waresalonika 5, 4)** juu ya kusema ya kama majira (nyakati) itakuwa kwa kuifamia. lakini hapa Mtume Paulo na maneno haya anasema ya kama waaminifu hawatakuwa bila matayarisho, hile wakati watasimama mbele ya Kristu Muhukumu kwa hile Siku Ya Kuja Kwake. Sawa vile inasema kisha: «Sababu ninyi wote ni wana wa nuru, na wana wa muchana: sisi hatuko wana wa usiku wala wa giza. Basi tusilale usingizi, kama wengine, lakini tuangalie na kuwa na kiasi» (5, 5-6). Kwa sababu, basi, sisi tuko wana wa muchana na hapana wana wa giza, hakuna namna sisi kuwa pasipo matayarisho ya roho hile siku ya Hukumu ya Kuja wa Mbili ya Kristu.

Tena Washuhuda wa Yehova wanatimia maneno ya Kristu, wakati anafundisha ma jambo hile itakuwa mbele ya Kuja Kwake (Matayo 24). tena wanaweka na nyakati ya ma jambo 39, yenye yote pamoja yanatwaambia «alama» ya Kuja wa Mbili ya Kristu.

Lakini tunazania ya kama ni ya bule ya kuendelea kusema ma fundisho ingine juu ya hii mambo. Paka tunasema sauti ya Kristu: **«Angalieni, musidanganyike,, kwani wengi watakuja kwa jina langu, wakisema: Mimi ndiye, na, wakati umekaribia: musiwafuate wale» (Luka 21, 8).**

# 10

# ISIYO KUFA YA NAFSI

## KUINGIA

Kuumba ya mutu inaonekana na namna ingine mbele ya kuumba ya vitu vingine ndani ya Madiko Takatifu. Mungu kwa kuumba ya mutu hasitimie neno wa mamlaka Wake kwa kumuumba mutu, sawa vile alifanya kwa kuumba ingine (nikusema hasiseme, «iwe mutu»), lakini alimuumba na namna ingine ya kuachana. Madiko Takatifu inatimia ma neno ya maisha ya watu na mifano mukusema ya kama aliumba mutu «katika mikono wake» (zaburi 119, 73). Mutu aliyeumbwa toka Mungu anakaa na vitu vya wili: mwili wa bulongo na nafsi wa roho. Kabisa Kitabu ya Mwanzo inaandika ya kama: **«Bwana Mungu akafanya mutu wa mavumbi ya inchi, akapuliza pumuzi ya uzima ndani ya pua yake; na mutu alikuwa nafsi ya uhai» (Mwanzo 2, 7).**

Kila mutu katika nafsi wa roho yake anaingia mu dunia wa roho na anaungana maugo yake na dunia wa mwili na wa roho na huyu anakuwa chongo ya kuumba. Pumuzi ya Mungu aliumba kwa mutu nafsi isiyo kufa na wa roho yake. Huu nafsi yake hana na ungano kimoja mbele ya vitu vya hii uzima, lakini hana hali wa roho. Inafananishwa tena huu pumuzi ya Mungu sawa pumuzi ya uzima, kwa sababu nafsi ni chemchem ya uzima ya mwili na huu (nafsi) anatenda juu ya kupumuzi na kuishi mwili. Pumuzi ya Mungu haina tunda ya Mungu, lakini inaonyeshwa ya kama nafsi haikuumbwa sawa mwili toka mavumbi, lakini ilitokea mara moja toka uwezo kimungu ya Mungu toka sifuru na iliunganwa na mwili.

Haya vitu vya wili ya mutu (mwili na nafsi) weko na ungano nguvu na nzima. Nafsi inaleta uzima, inaongeza na inachunga mwili, kwa hivyo, wakatri nafsi itatoka ku mwili, mwili inalekea na inapotea. Kupindua, nafsi inabakia kwa milele na inaendelea kuishi na kisha lufu ya mwili na mafananisho yote na uso ubinadamu, nikusema mioyo, zamiri, sikio, mapenzi.. . Hii zawadi ya nafsi ya kuwa isiyo kufa, haina katika hali yake, kwa sababu paka Mungu ni musiyekufa katika hali Yake (barua ya kwanza kwa Timotheo 16, 16), lakini ni hali yake katika neema ya Mungu.

Hii ni ya kweli, kwa sababu nafsi ni kiumbe ya Mungu na sawa kiumbe, haikuwe toka maugo yake na iko mu uzima kwa ajili ya neema ya Mungu.

Vile vitu vya wili, mwili na nafsi pamoja, wanafanya mutu moja muzima. Hata mwili hii wa pekee, wala nafsi wa pekee inaweza kuitwa «mutu», kwani «mutu» ni ungano ya vile vitu vya wili. Kwa hivyo, lufu ni adui wa kwanza ya mutu, kwa sababu inavunja hii ungano na inaharabisha «mutu». Kwa hivyo lufu ni jambo inje ya hali ya uzima ya mutu, ni kuanguka, ni «matunda ya zambi» (Wa Roma 6, 23). Kristu katika tendo Yake wa ukombozi alituokoa toka huu adui mukali (lufu), kwani aliharabisha uwezo yake (Wa Ebrania 2, 14-15) na alilaka Ufufuo ya wafu hile siku ya Kuja wa Mbili Kristu (Yoano 5, 28-29). Basi, kwa sababu «Mutu» ni kiumbe moja wa vitu vya wili (mwili na nafsi), uchanisho ya nafsi ku mwili ni lufu ya mutu sawa «Mutu». Hata, kama nafsi anaishi, kisha hii uchanisho, hii kiumbe haiitwa tena «Mutu», lakini anaitwa «nafsi» (Ufunuo 6, 9) ao «roho» (Wa Ebrania 12, 23). Sawa nafsi inaendelea kuishi (kwani ni katika neema ya Mungu isiyokufa) na inaongojea ungano yake mara ingine pamoja na mwili yake, hile nyakati ya ufufuo ya wafu, kwa Kuja wa Mbili ya Kristu na hivi itakuwa mara ingine kiumba wa vitu vya wili (nafsi na mwili). Kwa sababu Mungu alipenda kuumba kiumba Yake aishi kwa uzima wa milele na hapana paka sawa «roho». Washuhuda wa Yehova wanakataa hii mafundisho yote na wanafundisha ya kama nafsi inakufa pamoja na mwili. Nafsi katika fundisho yao, haina kintu kinene, paka kupashwa ya uzima hile iko nayo kila mutu. Lakini, mbele ya kuhamakia sisi makosa yao, twende sasa kuona inatufundisha nini Madiko Takatifu juu ya nafsi ya mutu.

## 1. MAANA YA NENO «NAFSI»

Neno ya «nafsi» inapatana mu Madiko Takatifu na maana ya mbalimbali. Kwa mufano:

**1)** Na maana munene neno «nafsi» inaonyesha uzima ya viumbe vya hii uzima, yenye waliumbwa toka Mungu na wanaitwa «Ma nafsi wa uzima», Paka na hii maana, wakati mutu ao nyama anasimama kuishi, tunasema ya kama huu nafsi alikufa. Kwa mufano: «na mutu alikuwa nafsi ya uhai» (Mwanzo 2, 7) na barua ya kwanza kwa wa korinto 15, 45). «Na kwa kila nyama ya dunia, na kwa kila ndege ya anga na kwa kila mutambazi juu ya inchi uliyo hai; nimewapa majani yote ya mboga kwa chakula; na ilikuwa hivi» (Mwanzo 1, 30). «na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikakufa» (Ufunuo 16, 3). Ona na (Hesabu 9, 13 na Walawi 23, 30. Yosua 10, 28-39) na pa fasi ingine. Na hii maana ya maisha wa hii uzima nafsi»inakula», ana damu, inakufa (Walawi 7, 18).

**2)** Wakati ingine neno «nafsi» inaonyesha uzima wa hii inchi ya watu: Kwa mufano Kristu «kwa sababu alimwanga nafsi yake hata kufa» (Isaya 53, 12). **«Kwa hivi tumefahamu mapendo kwa kuwa yeye alitoa uzima wake kwa ajli yetu, imetupasa sisi kutoa uzima wetu kwa ajili ya ndugu» (barua ya kwanza ya Yoano 3, 16). «Maye anayeona uzima (nafsi) wake ataupoteza; naye anayepoteza uzima (nafsi) wake kwa ajili yangu, atauona» (Matayo 10. 39. Ona na Yoano 10, 15 na 15, 13).**

**3)** Wakati ingine neno «nafsi» inaonyesha mahasa ya watu: Kwa mufano: **«Upende Bwana Mungu wako na moyo wako wote, na kwa roho (nafsi) yako yote, na kwa akili zako zote.. . » (Matayo 22, 37). «Hana akajibu akamwambia: Sivyo, Bwana wangu, mimi mwanamuke mwenye roho (nafsi) ya huzuni; Sikunywa mvinyo wala kileo cha nguvu, lakini nimemwanga roho (nafsi) ya huzuni» (! Samweli 1, 15). «Tazama mutumishi wangu niliyemuchagua; Mupendwa wangu nafsi yangu inayependezwa naye; nitatia roho yangu juu yake» (Matayo 12, 18). «Sasa roho (nafsi) yangu inafazaika» (Yoano 12, 27). Matayo 26, 38 na Isaya 1, 14. Hesabu 21, 5 na ! Samweli 30, 6).**

**4)** Wakati ingine maana yake ni ya hule mutu bado kuzaliwa katika Roho Mutakatifu (mutu wa mwili), kupindua ya hule mutu alizaliwa katika Roho ya Mungu na anaitwa mutu wa roho: Kwa mufano **«Lakini mwenye kufuata tabia ya asili hapokei maneno ya Roho ya**

**Mungu: kwa sababu maneno haya ni upumbafu kwake; wala hawezi kuyafahamu, kwa sababu yanatambulikana na Roho» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 2, 14); «Akili hii haitoki juu, lakini ni ya dunia, na ya tamaa, na ya shetani» (Yakobo 3, 15).**

**6)** Ku mwisho, maana wa kwanza ya neno «nafsi» ni maana ya hile kitu isiyokufa ya mutu, inaipatia Mungu katika pumuzi yake kwa kila mutu.

## 2. NAFSI UBINADAMU NI ISIYO KUFA

Sasa nitaandika mashuhuda ya Madiko Takatifu yanatuonyesha ya kama nafsi ni kitu kimoja isiyo kufa na wa roho katika neema ya Mungu. Ya kwanza tutaandika mashuhuda toka Agano la Kale:

**1)** **«Bwana Mungu akafanya mutu wa mavumbi ya inchi, akapuliza pumuzi ya uzima ndani ya pua yake; na mutu alikuwa nafsi wa uhai» (Mwanzo 2, 7).** Mutu alikuwa «nafsi wa uhai» na pumuzi ya uzima ya Mungu, aliyepumuzi ndani ya mwili wa mavumbi ya inchi ya mutu wa kwanza. Nikusema, pumuzi ya Mungu ilipatia pa mwili iyokufa uzima, uso ya kuachana, mioyo, mahasa, akili na ma zawadi ingine. Nikusema hii pumuzi ya Mungu ilikuwa kitu ingine inje ya mwili, iliyeumbwa katika pumuzi ya Mungu, na huu nafsi aliungana Mungu pamoja na mwili wa inchi na hivi aliumba «mutu» muzima. Mu lugha kiebrania inajitimia neno: NEFES= nafsi na RUAH= (roho) juu ya «pumuzi ya uzima». Sawa tutaona kidogo chini, nafsi na roho inasharikiwa.

**2)** Ufananisho munene ya Madiko Takatifu kwa fundisho ya nafsi isiyo kufa ni ya kama inasema juu ya wale walikufa, hapana ya kama walirudia kwa sifuru, lakini ya kama waliongezwa kwa watu ya kizazi yao wa zamani. Kwa mufano: **«Abrahamu akakata roho, mwenye uzee wema.. akakusanyika kwa watu wake» (Mwanzo 25, 8 na 17).**

**3)** Imani ya watu mu wakati ya Madiko Takatifu ya kama nafsi haikufe inaonyeshwa na toka makankamana ya mufalme Sauli, aliyeita roho (nafsi) ya aliyokufa nabii Samweli (1 Samweli 28, 8-25). Kweli, roho ya Samweli alikuja na alimufokea nguvu kabisa Sauli na alimwaambia na mwisho mubaya yake ku mikono ya taifa wa Filisteni. Mapokeo wa Ebrania inasadiki ya kama Mungu aliacha nafsi ya nabii Samweli kuonekana, hata inje ya namna kizuri, juu ya amuhamakie na amufokee Sauli na anaishe hukumu nzima yake toka Mungu, sawa inaandikwa mu shairi 15, 23. Katika uwazo ingine, haikukuwe roho ya Samweli, iliyesuburia, lakini ilikuwa roho ya shetani.

**4)** **«Kisha alijonyesha mwenyewe juu ya mutoto mara tatu, akalilia huyu irudie ndani yake tena. na Bwana alisikiliza sauti ya Elia; na roho ya mutoto ilimurudia, akafufuka». (1 Wafalme 17, 21-22).** Juu ya kurudia roho (nafsi) ya mutoto, inatuonyesha ya kama ilikuwa muzima, pa fasi moja, inje ya maiti-mwili yake.

**5)** «Kwa sababu hutaachia Hadeze nafsi yangu; wala hutaacha mutakatifu wako kuona uharibifu» (Zaburi 16, 10) na Matendo 2, 27), anasema Kristu Mwokozi kwa Mungu-Baba ndani ya unabii moja ya Daudi. Ndani ya hii shairi inaonekana safi ya kama nafsi ilitembea mu Hadeze (fasi ya kuikaa ma nafsi), lakini mwili «iliharabikwa: ndani nya kaburi. Pa jambo ya Mwokozi, wala nafsi yake ilibakia mu Hadeze, wala mwili Yake iliharabika, kwa sababu kisha ma siku tatu alifufuka toka wafu.

**6)** «.. . Bwana anasema hivi anayetanda mbingu na kuweka musingi wa inchi, na kuumba roho ya mutu ndani yake» (Zakaria 12, 1). «Roho ya mutu», nikusema nafsi yake ni kitu kingine ndani ya mutu.

**7)** Ku mwisho, Ushuhuda kubwa katikati ya mashuhuda yote ya Agano la Kale juu ya nafsi ni hii: **«.. . kwa sababu mutu anakwenda kwa nyumba yake ya milele, na waombezi wanazunguka kwa birika.. . na mavumbi yanarudi kwa inchi kama yalivyokuwa, na roho**

**inarudi kwa Mungu aliyeitoa» (Muhubiri 12, 5-7).** Basi, ni usafi ya kama paka mwili yetu wa mavumbi ya hii inchi inarudi kw ainchi, lakini nafsi (roho) inarudi kwa Mungu.

Sasa tutaandika mashuhuda toka Agano Jipya, inayetupatia ufunuo muzima ya mapenzi na mafundisho ya Mungu. Tutatazamia inafundisha nini juu ya nafsi ya mutu:

**1) «Mimi ni Mungu wa Abrahamu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Mungu si Mungu wa wafu, lakini wa walio hai» (Matayo 22, 32). Mtume Luka anaongeza: «Kwani yeye si Mungu wa wafu lakini wa walio hai» (Luka 20, 38). Nikusema, wote ni wazima na «wote ni walio uhai».**

**2) «Musiwaogope wale wanaoua mwili lakini hawawezi kuua nafsi» (Matayo 10, 28).** Kama nafsi ilikuwa «kupashwa ya uzima» sawa vile wanahubiri Washuhuda wa Yehova, kisha lufu ya mwili na nafsi haipashwe kuwa. Kwani, hakuna namna kuua nafsi, hii inatuonyesha ya kama nafsi ni kitu ingine ya kuachana ya mwili na isiyokufa na iko wa roho.

**3) «Kijana, amka. Roho yake ikarudi, akasimama mara moja» (Luka 8, 54-55).** Inatwaambia Madiko Takatifu juu ya ufufuo ya binti ya Yairo toka Kristu. Kwa sababu nafsi yake ilirudi, inatuonyesha ya kama ilikuwa inje ya mwili-maiti na kisha ufufuo ya mwili ilirudi na nafsi yake.

**4) «Akamwambia yesu: Bwana unikumbuke wakati unapokuja katika ufalme wako. Yesu akamwambia: Kweli ninakuambia, leo utakuwa nami katika Paradiso» (Luka 23, 42-43).** Nikusema, mara moja, kisha lufu yake hule munyanganyi alikuwa ndani ya Paradizo. Namna gani? Kweli pamoja na nafsi yake, kwa sababu mwili yake ilikufa pa musalaba na ilibaki chini ya inchi.

-Washuhuda wa Yehova juu ya kuharabisha maana ya hii ushuhuda ya Madiko Takatifu, waliweka hii, kisha neno: «leo», na hivi waligeuza maana yake: Nikusema: «kweli ninakwambia leo, utakuwa (wakati fulani, kisha mwaka 1914 nikusema) pamoja nami katika Paradiso».

**5) «Baba, katika mikono yako ninaweka roho yangu», alisema Kristu, wakati alikufa pa Musalaba (Luka 23, 46). Hii mambo umoja inaonekana kwa lufu ya shahidi kubwa wa kwanza Stefano: «Bwana Yesu, pokea roho yangu» (Matendo 7, 59).**

**6)** Hile wakati ya Mageuzo Sura ya Kristu pa Mulima Tabori walionekana pempeni ya Kristu Wanabii Musa na Elia, wenye wamekufa miaka mengi zamani, mbele ya uzalio ya Kristu. Kwa sababu alikuja kule Musa pamoja na Kristu, inatuwaambia ya kama Musa, kisha lufu yake hasikurudie kwa sifuru, sawa vile wanasadiki Washuhuda wa Yehova. Musa aliendelea kuishi katika mioyo nzima yake na alisuburia na Kristu. (Nabii Elia aliisha kupanda mbinguni katika mwili muzima yake). (Matayo 17, 2-8. Marko 8. 2-9 na Luka 9, 28-36).

Washuhuda wa Yehova wanasema sawa bunduki yao maneno ya Mwevangelizaji Luka ya kama, **«Petro nao waliokuwa pamoja naye, walikuwa na macho mazito na usingizi» (Luka 9, 32),** na kwa hivyo Mitume walisema maneno haya na vile vitu waliona kwa.. . . . ndoto yao. Lakini, haina vile, kwani endeleo ya maandiko inatuonyesha ya kama roho yao ya Yehova ni mubaya sana, kwa sababu anasema kisha Mwevangelizaji: **«lakini walipokwisha kuamka, wakaona utukufu wake, na wale watu wa wili waliosimama pamoja naye» (shairi 32).** Basi, Mitume ya Kristu hakuna namna kusadiki sisi ya kama waliona. . . ndoto yao.

**7) «Hadishi ya hule mutajiri na Lazaro masikini ni ushuhuda munene kabisa juu ya kajua sisi ya kama nafsi inabaki kwa milele (Luka 16, 19-31).** Ndani ya hii hadisi tunaona safi ya kama, kisha lufu, nafsi ya mutu mwaminifu (sawa alikuwa Lazaro masikini) inaongozwa ku malaika pa hile fasi ni na ma nafsi ya wenye haki, lakini nafsi ya wasiyo haki na wasiyo

kutubu (sawa alikuwa mutajiri) yanateswa ndani ya Hadeze. Ndani ya hii hadisi tunaona tena ya kama ma nafsi wekona mioyo, wanabaki na mufano ya roho yao na wanafamiana katikati yao.

Washuhuda wa Yehova wanakataa mashuhuda haya mukusema ya kama iko.. . . «mufano». Tunajibu sisi ya kama haiandikwe ya kama ni mufano. Tunaweze kupokea sisi ya kama hii hadisi ilikuwa wa kweli, kwani tena na Kristu anasema na ma jina ya wale watu wa wili (Abrahamu na Lazaro), kwani Kristu hasiseme na jina, wakati alisema mifano. Lakini, kama tutapokea ya kama hii hadisi ni mufano, ushuhuda ya kama nafsi inabaki kwa milele ni ya kweli na haitengwa. Kwa sababu mufano moja inaonyesha fundisho moja ya kweli na maneno ingine. Hapa, fundisho ya kama nafsi ni wa milele ni usafi kabisa na paka wale wanataka na mapenzi yao kufunga macho yao, hawataweze kuona hii sauti ya kweli.

**8)** **«Na wakati walipofungua muhuru wa tano, nikaona chini ya mazabahu nafsi zao waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. Wakalia kwa sauti kubwa, wakisema: Ee Bwana, Mutakatifu, mwenye kweli, hata wakati gani huhukumu, wala kupatia haki damu yetu kwao wanaokaa juu ya dunia? Wakapewa kila mumoja nguo ndefu nyeupe wakaambiwa wastarehe muda mudogo, hata itakapotimia hesabu ya watumishi wenzao na ndugu zao watakaouawa kama wao» (Ufunuo 6, 9-11).** Na paka hii kipande inenea juu ya kuonyesha ya kama nafsi itabaki kwa milele.

**9)** **«Kwa maana tunajua ya kama nyumba ya dunia ya hema yetu (mwili yetu) ikibomolewa, tuna jengo linalotoka kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele katika mbingu.. . . kwa sababu kweli sisi tulio katika hema (mwili) hii tunaugua kwa kulemewa; si kwa sababu tunataka mavazi haya kuondolewa, lakini tunataka kuvikwa, kusudi iliyo ya mauti imezwe na iliyo ya uzima.. . lakini tuna uhodari, nasi tunapenda zaidi kutoka katika mwili, na kukaa pamoja na Bwana» (barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 1-8).** Basi, lufu ya mwili hana na maana ya kama nafsi inaenda kwa sifuru, lakini inaenda karibu ya Kristu. Kwa hii mambo na Mutume Paulo anapenda kufa juu ya kuwa karibu ya Kristu: **«Kwa maana kwangu kuishi ni Kristu, na kufa ni faida. Lakini ikiwa kama kuishi katika mwili, -haya ni matunda ya kazi yangu, sijui nitakalolichagua» (Wa Filipi 1, 21-23).**

**10)** Mutume Paulo anasema kwa Waaminifu ya Agano Jipya: **«Maana hamukufikia mulima ulioweza kuguswa, ikiwaka moto, wala wingu jeusi, na giza, na tufani, .. . lakini ninyi mumefikia mulima Sayuni, na muji wa Mungu aliye hai, Yerusalema wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, na makutano makubwa, na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa katika mbingu, na Mungu, muhukumu wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, na Yesu Mupatanishi wa Agano Jipya, na damu ya kunyunyizwa inayosema mema kuliko ile ya Abeli» (Wa Ebrania 12, 18, 22-24).** Basi, nafsi ya wenye haki ni wa milele, wanaishi karibu ya Mungu na malaika wake na ni makamilifu.

**11)** **«Nafsi, kisha lufu ya mwili, yanaishi na yanachunga mioyo na upekeo yao. Hivyo inaonekana hapana paka kwa Mageuzo Sura ya Kristu, pahali alikuja Nabii Musa pamoja na Nabii Elia, hapana paka kwa hadisi ya Mutajiri na Lazaro Masikini, hapana paka mu mazabahu ya mbingu (Ufunuo 6, 9-11),** lakini tena na kwa maneno haya ifwatayo ya Kristu: «Baba yenu Abrahamu alifurahi kuona siku yangu; (siku ya kufika duniani sawa Mwokozi na Mukombozi) akaiona, akafurahi» (Yoano 8, 56). Kwa kuona Abrahamu, aliyekufa 2000 miaka mbele ya uzalio ya Kristu, jambo ya Kuja kwake sawa mwokozi ya dunia na alifurahi, inatuwaambia ya kama nafsi yake aliishi na alikuwa na mioyo na upekeo yake.

Vile iko namna kusema sisi juu ya nabii Musa alisema Kristu juu ya kwake mbele ya watu wa Yudea: **«Musizanie ya kama nitawashitaki ninyi kwa Baba; yuko mumoja anayeshitaki ninyi, hata Musa, taraja lenu» (Yoano 5, 45).** Neno: «Yuko mumoja anayeshitaki ninyi» inatwaambia ya kama Musa anaishi sasa na anashitaki sasa watu wa Yudea mbele ya Mungu Mungu.

**12)** **«Fanyeni kwenu wenyewe rafiki kwa mali za uzalimu, ili, wakati zinapopunguka, (wakati mutakufa) waweze kuwapokea ninyi katika makao ya milele» (Luka 16, 9),** alisema Kristu kwa Wanafunji wake kwa kuwaonyesha nguvu ya rehema. Nikusema anasema Kristu, kama tutafanya huruma kwa watu wamaskini, hawa watakuwa rafiki yewtu na watatupokelea katika makao ya milele, mu Paradiso. Basi, kisha lufu ya mwili yetu tutaishi na sisi na hawa wa rafiki wetu.

**13)** **«Hamujui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mutakatifu aliye ndani yenu, muliyepewa na Mungu? Na ninyi si mali yenu wenyewe; kwa sababu mulinunuliwa kwa bei; basi tukuzeni Mungu katika mwili wenu na katika roho yenu, maana ni ya Mungu» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 6, 19-20).** Kwani Madiko Takatifu inatushauria kumutukuza Mungu katika mwili yetu na katika roho yetu ni kweli ya kama mwili na roho (nafsi) ni vitu vya wili ya kuachana.

**14)** Onyesho ya uhai ya nafsi ni na matakio ya mutu, anayependa kuwa «inje ya mwili», kwa mufano hile saa ya ono, iliyeona Mtume Paulo, anayeandika hivi: **«Ninajua mutu katika Kristu tangu miaka kumi na mine (kama katika mwili, sijui; kama inje ya mwili, sijui, Mungu anajua), mutu huyu alichukuliwa juu hata mbingu ya tatu. Nami ninajua mutu huyu (kama katika mwili, kama inje ya mwili, sijui: Mungu anajua), ya kama alichukuliwa juu hata paradiso, akasikia maneno yasiyoweza kusemwa na yasiyofaa mutu kuyasema» (barua ya mbili kwa wa Korinto 12, 1-4).** Hii mambo ya kama mutu moja alikuwa inje ya mwili yake na alipanda ya saa kidogo kwa mbingu ya tatu na kisha alirudi mara ingine mwilini yake, ilifanyikwa hivi, kama paka tutasadiki sisi ya kama nafsi iliishi.

## 3. HADEZE NI FASI YA NAFSI YASIYOOKOLEWA NA KUSHUKA KULE KRISTU

Ushuhuda munene juu ya nafsi isiyokufa ni imani na usabiti hapana paka taifa ya Ebrania, lakini mataifa yote ya dunia. Hadeze ilikuwa fasi pahali walienda ma nafsi ya wafu na, walisadiki ya kama ilikuwa (hadeze) ndani ya hii inchi. Kule yalikuwa ma nafsi yote ya wale wafu walikufa mbele ya Kristu na waliongojea ufikisho ya Mukombozi. Kweli, wakati Kristu alikufa pa Musalaba, nafsi Yake (inayekuwa na ungano pamoja na hali kimungu Yake) alishuka mu Hadeze na alihubiri mbele ya ma nafsi haya. Ma nafsi haya walipokea kuhubiri ukombozi, walitoka inje ya Hadeze, waliokolewa na walipelekwa mu Yerusalema wa mbingu, pahali pamoja na malaika na Mungu ni mu **«Kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa katika mbingu, na Mungu, muhukumu wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika» (Wa Ebrania 12, 22-23).** Kisha Kuja ya Mukombozi duniani ma nafsi ya waaminifu wakristu hawaende tena mu Hadeze, lakini mu Yerusalema wa mbingu, lakini ma nafsi ya wasiyookolewa wanaendelea kufungwa kule. Kushuka ya Mukombozi-Kristu kule mu Hadeze, inatushuhuda Madiko Takatifu, hivi:

**1)** **«Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini (kaburi). Kwa maana hutaniacha roho yangu katika Hadeze, wala hutatoa Mutakatifu wako aone uharibifu» (Matendo 2, 27)** anasema Mwokozi Kristu kwa Mungu Baba Mwake, anayetolewa sawa sandaka pa Musalaba mwake. Mtume Petro anafafanusha unabii hii na anasema: **«Akitangulia (daudi) kuona maneno haya, alisema habari za ufufuko wake Kristu, ya kama nafsi yake haikuachwa katika Hadeze wala mwili wake haukuona uharibifu» (Matendo 2, 31).** Hapa inakuwa machanisho safi katikati ya Hadeze, pahali yalifungwa ma nafsi na kaburi pahali, «iliharabikwa» mwili ya mufu.

**2)** **«Kwa maana Kristu vile vile aliteswa mara moja kwa ajili ya zambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; akauawa katika mwili, lakini**

**akafufuliwa katika roho, katika roho hii alikwenda vilevile na kuhubiri kwa roho waliokuwa katika kifungo; wasiotii zamani, wakati uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja kwa siku za Noa, wakati safina ilipokuwa ikitengenezwa, ndani yake wachache, watu wanane waliokolewa kwa maji» (barua ya kwanza ya Petro 3, 18-20).**

Washuhuda wa Yehova wanakataa hii shairi wa juu: (barua ya kwanza ya Petro 3, 18-20) ya kama inase, a juu ya ma nafsi yasiyokufa ya watu. Kupindua, wanasadiki ya kama hawa «wana wa Mungu» mu sehemu 6 ya Kitabu Mwanzo, «wenye waliona ma binti ya watu ya kama walikuwa na ma uso mazuri, waliwachukua ma bibi yao»; hawa walikuwa malaika, wenye walitakia kufanya zambi ya mwili pamoja na wanawake ya inchi yetu. Hawa malaika, waliyoanguka kwa hii zambi ya usharati ni «roho waliokuwa katika kifungo», mbele yao alihubiri Kristu!!!

Hii fundisho yao ni ukosefu kabisa kama tutawaza ya kama malaika ni roho na yasiyo mwili na hakuna namna wafanye zambi ya mwili na wanawake. Tena tunamikumbusha na maneno ya Kristu: **«Kwa maana katika ufufuko hawaoi wala hawaolewi, lakini watakuwa kama malaika mbinguni» (Matayo 22, 30).** Tena, katikati ya malaika hakuna uchanisho ya mume na muke na kwa hivyo tusiweze kusema ya kama huyu malaika fulani ni mume na anaweza kufanya zambi katika mwili.

Tena, hata fasi moja ndani ya Madiko Takatifu, haiseme ya kama «wana wa Mungu» ya sehemu 6 ya Kitabu Mwanzo walikuwa malaika. Ni kweli ya kama hawa «wana wa Mungu» ni wafwasi wenye fazila ya Semu, wenye waliishi ya kuachana na wafwasi wenye kibego ya Kaina. (Watoto wanawake ya watu» walikuwa wanawake ya kizazi isiyoutawa ya Kaina. Mwisho ya uzima kuchanga toka vizazi vya wili ilikuwa ya kuharabika kizazi ya Semu, iliongezeka uzulumu kabisa na Mungu alileta Uharibifu ya dunia. Ku mwisho, uvumilia na mapendo ya Mungu iliongojea watu watubu na hapana malaika, hile wakati ya Noa.

**3) «Maana kwa ajili hii hata wafu walihubiriwa Habari Njema, ili wahukumiwe, kama watu katika mwili, lakini wawe hai katika roho kama Mungu alivyo hai» (Barua ya kwanza ya Petro 4, 6).** Nikusema, kwa hivyo Kristu alihubiri Habari Njema (Evangelio) na kwa wafu, kwani, walihukumiwa sawa watu katika mwili yao na walikufa katika mwili, wataishi kisha katika Mungu kwa roho yao.

Mutume Paulo anatwaambia juu ya Hadeze, sawa fasi pahali walikwenda nafsi ya wale watu walikufaka, mbele ya Kuja Kristu Duniani na aliyoleta wokovu:

**4)** «Lakini haki iliyo kwa imani inasema hivi: Usiseme katika moyo wako: Nani atakayepanda katika mbingu? (maana ni kuleta Kristu chini; ) ao: Nani atakayeshuka kwa kuzimu (Hadeze)? (maana ni kuleta Kristu juu kutoka kwa wafu). «Kuzimu» hakuna namna kuwa unyofu kaburi, sawa vile wanataka kusadiki Washuhuda wa Yehova.

**5) «Kwa hivi anasema: Wakati alipopanda juu, alifunga kifungo, akawapa watu zawadi. (basi neno hili: Alipanda maana yake nini kama si kusema kwamba yeye alishuka vile vile mupaka pande za chini za inchi? » (Wa Efeso 4, 8-9).** Washuhuda wa Yehova wanafafanusha «chini za inchi» sawa kaburi, lakini chini ya inchi ni Hadeze. Ona na Zaburi: 86, 13 na Ezekieli 32, 17-21).

**6)** Mungu alinyanyua Kristu «kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia» (Wa Filipi 2, 10). «Chini ya dunia» ni wale wanaishi chini ya inchi. Tena ni na ingine shairi: «Nikaona katika mukono wa kuuma wake aliyekaa juu ya kiti cha ufalme kitabu kilichoandikwa ndani ya nyuma kimetiwa mihuri saba.. . Wala hakuna mutu mumoja mbinguni wala juu ya dunia, wala chini ya dunia aliyeweza kufungua kitabu wala kukitazama» (Ufunuo 5, 1-3). Hapana anasema mtume Yoano juu ya wale wanaishi mbinguni, pa hii inchi na chini ya hii inchi.

**7)** Tena na Kristu alisema kwa watu wa Yuda na mufano moja juu ya kushuka Kwake ndani ya Hadeze na atabakia pale ma siku tatu: «**Kwani kama Yona alivyokuwa siku tatu muchana na usiku katika tumbo la samaki mukubwa, vivyo hivyo Mwana wa watu atakuwa siku tatu muchana na usiku katika moyo wa inchi» (Matayo 12, 39-40).** Tena ukikiri yake ya kama, **«Wewe ni Petro, na juu ya mwamba huu nitajenga kanisa langu; wala milango ya Hadeze haitalishinda» (Matayo 16, 18)** alionyesha kweli ushindi Wake pa Hadeze, wakati aliuhuru na alikombozi wale nafsi wafungwa na aliwapeleka mu «Yerusalema wa mbingu». Kweli, tangu hile wakati «milango ya Hadeze» hayataweze kuchunga nafsi, yenye yaliokolewa, ndani yao.

Mashuhuda ingine juu ya uhai ya Hadeze inatupatia na Agano la Kale:

**8)** Tazama mashuhuda toka Zaburi:

a) **«Kwa sababu hutaachia Hadeze nafsi yangu» (Zaburi 16, 10).**

b) **«Kama kondoo wamemekwa kwenda kwa Hadeze». «Lakini Mungu atakomboa nafsi yangu toka mukononi mwa Hadeze, maana yeye atanipokea. «Zaburi 49, 14-15).**

c) **«Maana rehema yako ni kubwa kwangu, na umeponyesha nafsi yangu toka Hadeze ya chini kabisa» (Zaburi 86, 13).**

Basi, inaonekana safi ya kama hadeze hakuna namna kuwa kaburi, sawa vile wanasadiki Washuhuda wa Yehova, kwa sababu kule ni paka mwili isiyouzima na wala maumivu anasikia, wala mahuzuni.

**9)** Imani ya kama Hadeze ni chini kabisa ya inchi inatushuhuda na ma shairi haya: **a)** «Maana rehema yako ni kubwa kwangu, na umeponyesha nafsi yangu toka Hadeze ya chini kabisa» (Zaburi 86, 13)**. b) «Akasema: kwa sababu ya mateso yangu nimeomba Bwana, akanitikia; Toka tumboni mwa Hadeze nimelia, ukasikia sauti yangu. Kwa maana umenitupa vilindini, katika moyo wa bahari, Garika imenizunguka; » (Yona 2, 1-3). c)** Mustari murefu hile ni katikati ya mbingu mpaka chini kabisa, sawa anasema hivi Mungu kwa Amosi: **«Hata wanachimba katika Hadeze, toka kule mukono wangu utawatwaa; na hata wanapanda mbinguni, toka kule nitawashusha» (Amosi 9, 2). Tena: «Nawe Kapernaumu, unayepandishwa hata mbingu, utashushwa hata Hadeze» (Luka 10, 15).**

**10) «Hadeze toka chini imetikisikwa kwa ajili yako, kukutana na wewe kwa kuja kwako, ikiamsha wafu kwa ajili yako, hata walio wakubwa wote wa dunia; ikinyanyua wafalme wote wa mataifa kuondoka kwa viti vyao vya ufalme. Hawa wote watajibu na kukuambia, wewe, umekuwa zaifu kama sisi! Wewe umekuwa kama sisi!» (Isaya 14, 9-10).** Maneno haya anasema Isaya kwa mufalme ya Babeli, kwa amuwambie mwisho isioyoutukufu yake. Watu wote wa wafu wanaonekana wenye muzima ndani chini ya Hadeze. Tazama na Iezekieli 32, 21).

Mashuhuda haya yote na ingine mengi yanatuonyesha, bila shaka, ya kama iko Hadeze sawa makao ya ma nafsi yasiyookolewa na fasi yake ni kwa siri ndani na chini ya inchi. Ndani ya hii makao, basi, alishuka Kristu, hile saa alipanda pa Musalaba mwake na alihubiri kule kwa nafsi yasiyookolewa. Hii fundisho inatushuhuda Mapokeo wa Mitume katika uzima wa Ibada ya Kanisa (Tazama Ibada ya siku Mu Kazi Tano Mkubwa na Muposho Mukubwa); hivi wanatufundisha na Wapadri wa Mitume, Wafwasi wao, sawa Ignatio wa muji Antiokhia, aliyekuwa mwanafunji ya Mtume Yoano, aliyesema: «Alishuka ndani ya Hadeze paka Kristu wa pekee, lakini alipanda na ma nafsi mengi na alibomoa kibabashi iliyekuwa katikati yao». Vile wanatufundisha na wapadri wengine ya Kanisa wa zamani na kwanza, na hii inatwaambia ya kama ilikuwa imani ya Kanisa wa kwanza yetu uhai ya Hadeze na ya kama nafsi isiyokufa.

Imani ya Washuhuda wa Yehova ya kama Hadeze ni kaburi, pahali yoyote inazimishwa na yanarudi kwa sifuru ni pasipo misingi na mashuhuda ya Madiko Takatifu.

Tena ma fasi ingine ndani ya Madiko Takatifu tunapata mistari, pahali lufu inaitwa musingizi, kwa sababu lufu haiongoze kwa sifuru, sawa vile wanasadiki Washuhuda wa Yehova. Kwa mufano (Yoano 11, 11. Matayo 27, 52. Matendo 7, 6). Barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 51) na ma fasi ingine.

## 4. «NAFSI» NA «ROHO» YANASHARIKIWA

Neno «roho» tuliikuta mara mengi na maana ya neno «nafsi», iko na maana ingine. Lakini maana yake kabisa ni ya mbili:

**1)** Maana yake ni kabisa «nafsi». kwa mufano: **«Baba, katika mikono yako ninaweka roho yangu» (Luka 23, 46 na Matendo 7, 59 na Luka 8, 54-55).**

**2)** Mara mengi niko na maana paka manguvu ya roho minene, kwa ajili yao mutu moja anapata maarifa ya Neema Takatifu na anatakashwa na kwa ajili yao anamwabudu Mungu. Kwa mufano: **«Kwa maana Mungu ni mushuhuda wangu, ninayemutumikia kwa roho yangu.. . » (Wa Roma 1, 9).**

Tena neno «nafsi» niko na maana juu ya kutuwambia ya wale watu bado kuzaliwa mara ya mbili katika roho; nikusema bado kuishi katika neema ya Roho Mutakatifu. Hawa watu Mtume Paulo anawaita watu wa nafsi. Hawa watu, hawakuwana nuru ya Mungu na hawapokelee sauti ya Roho wa Mungu. Lakini hawa watu walichukua neema ya Roho Mutakatifu Mutume Paulo anawaita watu wa roho, kwnai walipokelea nguvu ya utakaso ya Roho Mutakatifu.

Kwa hii ufafanusho ya mistari haya wa juu ni teketeke kusikia mistari ya mbili toka Agano Jipya, pahali inaonekana uchanisho moja katikati ya ma neno: «nafsi» na «roho» kwa mutu:

a) «Mungu wa salama mwenyewe awatakase ninyi kabisa; roho yenu na nafsi yenu na mwili wenu ichungwe mizima, pasipo laumu mupaka wakati Bwana wetu Yesu Kristu atakaporudi» (Barua ya kwanza kwa Watesalonika 5, 23).

b) Maana Neno la Mungu ni hai, lenye nguvu na ukali kupita ukali wa upanga unaokata ngambo mbili, likitoboa hata kutenga nafsi na roho, na viungo na mafuta ndani ya mifupa; nalo ni jepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo"»(Wa Ebrania 4, 12). Sawa vile "viungo na mafuta ndani ya mifupa» ya mutu moja haina vipande na uhuru yao ya mwili yake, vile na «nafsi» na «roho» haina vipande ya wili ya kuachana, lakini ni ma sura mbili ya kipande kimoja.

Ya kama «nafsi» na «roho» yanasharikiwa kweli, inatuonyesha na mistari ingine ya Madiko Takatifu, pahali maneno haya ya mbili yanasharikiwa na yanageuzwa; Kwa mufano:

**1) «Roho yangu ina huzuni sana hata kufa» (Matayo 26, 38) anasema Kristu, lakini mu fasi ingine anasema: «Wakati Yesu alipokwisha kusema haya, alifazaika katika roho» (Yoano 13, 21).**

**2) «Ee Bwana, Mungu wangu, ninakuomba, roho ya mutoto huyu irudie ndani yake tena.. . na roho ya mutoto ilimurudia, akafufuka» (1 Wafalme 17, 21-22)** inatwaambia Madiko Takatifu juu ya hii muujiza ya Nabii Elia. Lakini mu jabo ya ufufuo ya binti ya Yairo, Kristu alisema: **«Kijana, amka. Roho yake ikarudi, akasimama mara moja: akaagiza apewe chakula» (Luka 8, 54-55).**

**3)** Mu kiumba ya ma nyama (Mwanzo 1, 20-25) haiseme hata fasi moja ya kama ma nyama wekona «roho». Inaandikwa paka ya kama weko na «nafsi wa uzima». Ndani ya maandiko ingine ya Madiko Takatifu ma nyama yanaandikwa sawa weko na «roho» badala ya neno «nafsi». Kwa mufano: «Nani anayejua kama roho ya mutu inapanda juu, na roho ya nyama, kama inashuka katika inchi? (Muhubiri 3, 21). Inaenekana hapa safi ya kama Muhubiri ya kusema «roho» anawaza nafsi ya mutu na nyama. Ni mifano mengi, lakini hii ninazania ya kama inenea.

Washuhuda wa Yehova wanakataa kushariki nafsi na roho na wanafundisha ya kama «roho» ni «mwanzo ao nguvu ya uzima inayetumikia nafsi». Kama hii sauti yao ni ya kweli, roho yao ilipashwa kuwa kitu kimoja isiyo uso na mahasa. Lakini Madiko Takatifu inaandika mafananisho yote ya kitu kimoja inayeikaa na mioyo na uso. Kwa mufano: **Inatetemeka:** «alifazaika katika roho» (Yoano 13, 21). **Iko tayari:** «Roho ni tayari lakini mwili ni zaifu» (Matayo 26, 41). **Inajua maneno ya mutu:** «Kwa sababu nani katika ya watu anayejua maneno ya mutu, ila roho ya mutu iliyo ndani yake? » (barua ya kwanza kwa wa Korinto, 2, 11), **Anamwabudu Mungu:** «Kwa maana Mungu ni mushuhuda wangu, ninayemutumikia kwa roho yangu.. . » (Wa Roma 1, 9). **Inatakashwa:** «Kuna tofauti katikati ya muke na bikira. Mwanamuke asiyeolewa anasumbuka juu ya maneno ya Bwana, awe mutakatifu katika mwili na roho: lakini yeye anayeolewa anasumbuka juu ya maneno ya dunia, apate kupendeza mume wake» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 7, 34). **Inakamilikwa:** «Na makutano makubwa, na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa katika mbingu, na Mungu, muhukumu wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika» ( Wa Ebrania 12, 23).

Maneno haya yote yanashuhuda ya kama roho ya mutu haina nguvu moja ya uzima, lakini ni maugo yake wa roho, nikusema nafsi yake.

Roho na pumuzi:

Washuhuda wa Yehova wanasadiki tena ya kama «roho» kwa mutu ni pumuzi yake, hile kisha lufu yake, inatokea. Lakini haina hivi, sawa vile inatuonyesha Madiko Takatifu: **«Kama aliwekea mutu moyo wake, kama akijikusanyia roho yake na pumuzi yake.. . » (Yobu 34, 14-15). Madiko Takatifu inaachana roho na pumuzi.**

Kweli, hakuna namna kukombola sisi neno «roho « na neno «pumuzi», kwani maana itakuwa mubaya. Kwa mufano: a) **«.. . Tujisafishe kwa uchafu wote wa mwili na wa roho (pumuzi); iko namna? ).. . » (barua ya mbili kwa wa Koritno 7, 1). b) «Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu Yesu Kristu iwe pamoja na roho (pumuzi) (!) zenu» (Wa Galatia 6, 18). c). «Kwa maana Wasadukayo wanasema ya kwamba hakuna ufufuko, wala malaika wala roho (pumuzi)(!), lakini Wafarisayo wanakiri yote» (Matendo 23, 8).**

## 5. MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA

Washuhuda wa Yehova wanasadiki ya kama nafsi haina ya milele, lakini ni wa kufa. Wanasema nafsi haina kitu kingine ya mwili, lakini ni nguvu ya mwili na inakufa mwili, inakufa na nafsi pamoja!

Wanakataa ya kama nafsi ni kitu isiyokufa na wa roho ya kila mutu. Kwa hivyo, katika imani yao, wakati mwili inakufa, inakufa na nafsi, kwnai nafsi ni nguvu ya uzima ya mwili.. Hii kosa yao inatokea kwa sababu wanachanga maana ya neno «nafsi» na maana ya neno «roho» sawa vile tulisema kidogo yulu. Juu ya kusingi mafundisho yao ya uwogo wanaleta mistari filani toka Madiko Takatifu. Tazama:

**1)** Alisema Mungu kwa wazazi wa kwanza Adamu na Eva: **«Wa kila muti wa shamba unaweza kula; lakini wa muti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa» (Mwanzo 2, 16-17).** Kisha kosa ya utii alisema Mungu kwake: **«kwa jasho ya uso wako utakula mukate, hata utakaporudi kwa udongo, kwa maana umetwaliwa katikati yake; kwa sababu mavumbi wewe, na utarudi kwa mavumbi» (Mwanzo 3, 19).**

Lakini, «lufu» mu Madiko Takatifu haina maana ya kurudi mu sifuru na uharibifu. Madiko Takatifu inatwaambia ya maana vya wili ya neno «lufu»:

a) Lufu wa mwili, kwa ajili yake inaisha uzima wa hii inchi ya mutu na tunda ya hii lufu ni uchanisho katikati ya mwili na nafsi na elekeo ya mwili. Hile nyakati nafsi, inachunga mafananisho yake yote, inaendela kuishi na mioyo yake, sawa hivi tulisema, ao mu Yerusalema wa mbingu (Wa Ebrania 12, 22-23) ao mu Hadeze (Luka 16, 23). Huu ni lufu ya mutu sawa

«Mutu», anayekuwa vitu vya wili: Mwili na nafsi. Kisha lufu katika mwili, basi, mutu anakufa sawa Mutu= mwenye kuwa na mwili na nafsi na sawa nafsi anaishi anaongojea ufufuo ya mwili yake kwa siku ya Kuja Kristu mara ya Mbili. Sauti ya Mungu: **«Lakini wa muti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa» (Mwanzo 2, 16-17)** anawaza Mungu mutu muzima sawa «Mutu», kwa sababu sawa «Mutu» alikufa. Lakini nafsi yake kwani ni wa milele, anaishi.

**b)** «Lufu wa roho», lufu ya nafsi, nikusema kama nafsi itatoka mbali ya ushirika ya Mungu na ushirika ya Neema Takaitfu. Mutu anayeishi mbali ya Mungu, ndani ya Madiko Takatifu, anaitwa mufu, hata kama huyu ni muzima: Kwa mufano:

1) **«Kwani huyu mwana wangu alikufa, naye ameishi tena, alipotea, naye anaonekana» (Luka 15, 24).**
2) **«Lakini Yesu alimwambia: Unifuate, na acha wafu wazike wafu wao» (Matayo 8, 22).**
3) **«Nanyi mulikuwa wafu kwa sababu ya makosa yenu na zambi zenu.. . alitupatiza uzima pamoja na Kristu (mumeokolewa kwa neema). (Wa Efeso 2, 1-5).**
4) **«Kwa hivi anasema: Amka, wewe unayelala, na ufufuke katika wafu, na Kristu atakuangaza» (Wa Efeso 5, 14).**
5) **«Wala musitoe viungu vyenu kuwa silaha za uzalimu kwa zambi, lakini mujitoe wenyewe kwa Mungu kama wenye uhai nyuma ya kufa, na viungu vyenu kwa MUngu kuwa silaha za haki» (Wa Roma 6, 13).**
6) **«Lakini yeye anayefuata tamaa zake amekwisha kufa angali yeye ni hai» (barua ya kwanza kwa Timotheo 5, 6).**

**Lakini kosa ya Adamu, ilileta, wa huzuni mingi wetu, yote mbili vipande ya «lufu».**

**Mustari hii: «Hata utakaporudi kwa udongo» (Mwanzo 3, 19**) inanyoloka paka kwa mwili, kwa sbabau paka huu ilichukuwa toka udongo. Nafsi, sawa tuliona, iliumbwa kwa kunyoloka mara moja toka Mungu kwa pumuzi Mwake ndani ya mwili isiyopumuzi ya Adamu, na kwa hivi mutu alikuwa «nafsi ya uhai» (Mwanzo 2, 7).

Basi, lufu, kwa maana ya mwili ni uchanisho ya nafsi (roho) toka mwili, pahali na pamoja naye anaikaa na inamupatia uzima. **«Hakuna mutu aliye na uwezo juu ya roho ili azuize roho; wala hana mamlaka juu ya siku ya mauti; wala hakuna kuondosha katika vita ile: wala uovu hautamwokoa yeye aliyejitoa kwake» (Muhubiri 8, 8).** Maana na maneno manyofu ni ya kama hata mutu moja hasiweze kuzibiya roho atoke hile saa ya lufu. Na kweli sawa ilielejewa, **«Na mavumbi yanarudi kwa inchi kama yalivyokuwa, na roho inarudi kwa Mungu aliyeitoa» (Muhubiri 12, 7).**

Basi, lufu na maana wa mwisho ni kurudi mwili hii wa bulongo ndani ya hii inchi toka yake ilichukuwa na kurudi roho (nafsi) kwa Mungu.

**2)** Washuhuda wa Yehova wanafanana nafsi ya mutu pamoja na nafsi ya nyama na wanasadiki ya kama katika lufu inarudi kwa sifuru, sawa vile inarudi na nafsi ya ma nyama. Wanaita ya a) jabo ya kama Madiko Takatifu inaita ma nyama «ma nafsiya uhai» sawa inaita hivi na mutu na b) wanaita maneno ya kitabu ya Agano la kale: (Muhubiuri, sehemu 3, 18-21)

Kwa ajili ya mambo yao wa kwanza tulisema mafundisho mengi ku mukongo na ni nani uchanisho ya kiumba ya mutu na ma nyama. Sasa mara ingine tunakumbuka hapa ya kama ma nafsi ya nyama yaliumbwa katika neno ya Mungu toka bulongo: **«Mungu akasema: Maji yajae kwa wingi na viuymbe vilivyo hai.. Inchi itoe kila kiumbe kilicho hai kwa namna yake.. . » (Mwanzo 1, 20, 24).** Ya kusema na maneno ingine maji na inchi walileta nafsi ya nyama, kw ahivyo kw alufu yao nafsi yao inaharabika pamoja na mwili yao, kwa sababu hali ya nafsi yao inasharikiwa na hali ya mwili yao. Lalini nafsi ya mutu haikuumbwa toka inchi, sawa imeumbwa mwili ubinadamu (onyesho ni ya kama mwili ilikuwa bila uzima, mbele ya kupumuzi Mungu

«pumuzi ya uzima» ndani yake), lakini katika pumuzi ya Mungu. Huu namna ya kuumba ya kuachana inatuwaambia ya kama nafsi ya mutu iko na makadara (kikomo) ingine. Kama, kwa mufano, nafsi ya mutu ilikuwa na kikomo umoja na kikomo ya watu, Mungu aliupashwa kuiumba sawa aliumba na nafsi ya nyama. Kwa hivi, basi, wakati mutu atakufa, nafsi yake haikufe pamoja na mwili ndani ya bulongo, kwa sababu haikuumbwa toka bulongo, lakini anaenda kwa Mungu, kwani aliuumbwa toka pumuzi ya Mungu.

Kwa ajili ya mambo yao ya mbili, tunaona ya kama kweli mu Kitabu Muhubiri inaandikwa hivi: **«Nikasema moyoni mwangu: Ni kwa sababu ya wana wa watu, ili Mungu apate kuwajaribu nao waone ya kuwa wao wenyewe ni nyama tu. Maana neno linalopata wana wa watu linapata nyama; neno moja linawapata: kama mumoja anavyokufa, vivyo hivyo mwingine anakufa, ndivyo, wao wote wana pumuzi moja; wala mutu hana kitu cha kupita nyama: maana yote ni ya bule. Wote wanakwenda kwa pahali pamoja; wote wanatoka katika mavumbi, na wote watarudi kwa mavumbi tena. Nani anayejua kama roho ya mutu inapanda juu, na roho ya nyama, kama inashuka katika inchi? » (Muhubiri 3, 18-21).**

Lakini hapa mwandishi Solomono anawaza ndani ya roho yake, kwani anasema: «Nikasema moyoni mwangu.. . ». Jibu ya mawazo haya mabaya inatupatia ku mwisho hii Kitabu: **«Na mavumbi yanarudi kwa inchi kama yalivyokuwa, na roho inarudi kwa Mungu aliyeitoa» (Muhubiri 12, 7).** Hii shairi ni jibu nguvu kabisa, inayefunga kinywa ya Washuhuda wa Yehova.

**3) «Nafsi inayofanya zambi, itakufa» (Ezekieli 18, 4).** Lakini hapa: **«Nafsi inayofanya zambi» ni maana ya mutu anayefanya zambi. Ndani ya hii sehemu ya Ezekieli Mungu anaita na jina yao zambi mazito ya kuachana, yenye yalipizwa na lufu na anaandika safi ya kama malipizo ni paka kwa mukosefu na hapana na watoto wake. Sababu ya kusema hii sauti Ezekieli ilikuwa uwazo hile wakati yalikuwa Watu wa Ebrania, wenye waliteswa kwa ajili ya nvita, mateso ya utumwa na mateso ingine na walisadiki ya kama walipizwa kwa ajili ya vizazi vyao wa zamani. Mungu anafundisha huku na anasema ya kama kila mutu analipizwa kwa zambi zake. Mu shairi kidogo chini (18, 9)** anaandika: **«Yeye ni mwenye haki, hakika ataishi, Bwana Mungu anasema».** Hata kama tutapokelea maana ya «nafsi» sawa vile wanataka huku Washuhuda wa Yehova, lakini hakuna namna kuonyeshwa ya kama inatokea toka mavumbi, kwa sababu ma «nafsi» ya wenye haki hayatakufe, lakini yataishi.

**4)** « Na itakuwa kila mutu (ndani ya Vitabu vingine ni neno nafsi) asiyesikia nabii yule (Kristu) atapotea na kuharibiwa na watu wake» (Matendo 3, 23). Na hapa «nafsi» ni maana kila mutu, lakini neno «atapotea» ni maana ya malipizo na hapana ya uharibifu. Hii onaonyeshwa hivi kama tutachukua hii unabi ku Agano la Kale, kwani toka huu Kitabu aliichukua Mtume Petro: **«Na itakuwa mutu ye yote asiyetaka kusikiliza maneno yangu atakayosema kwa jina langu, nitalitaka kwake» (Kumbukumbu Torati 18, 19).** Lakini na hapa, haionyeshwa ya kama nafsi inakufa.

**5) «Jueni ya kuwa mwenye kumurudisha mwenye zambi hata atoke kwa njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa zambi» (Yakobo 5, 20).** Hapa inaonekana safi ya kama hii shairi inatwaambia juu ya lufu wa roho, nikusema uchanisho katikati ya nafsi na Mungu, inayeitwa mu Kitabu Ufunuo 21, 8 **«Lile ziwa linalowaka moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili». Pale «watateswa muchana na usiku hata milele na milele» (Ufunuo 20, 10).**

**6)** Kwa ufufuo ya Lazaro, wanasema Washuhuda wa Yehova, ya kama Kristu alisema mbele ya maiti yake na namna unyofu hivi: **«Lazaro, toka inje. Na yule aliyekufa akatoka inje.. . » (Yoano 11, 43-44).**

Hapa Mwandishi Mtume Yoano alisahau kuandika ya kama «alirudi nafsi yake». Onyesho umoja ni jabo ya ufufuo ya binti ya Yairo, pahali Marko anasema maneno ya Kristu: **«Talita kumi, maana yake: Musichana, ninakuambia: Simama. Mara moja Musichana akasimama, akatembea.. » (Marko 5, 41-42), lakini Luka mu Evangelio yake anatimiza hivi: «Roho yake ikarudi, akasimama mara moja.. . » (Luka 8, 55).**

**7)** Kwa sababu Washuhuda wa Yehova wanasadiki ya kama nafsi ya mutu inakufa, tena wanasadiki ya kama lufu inarudi nafsi kwa sifuru na uharibifu ya uso ya hule mutu. tena wanaita kwa hii fundisho yao na hii ma shairi:

a) **«Maana katika mauti hapana ukumbusho juu yako, katika Hadeze nani atakayekupa sante? (Zaburi 6, 5) na**

b) «**Wafu hawasifu Bwana, wala wo wote wanaoshuka kimya; »** Lakini shairi moja chini anasema Nabii Daudi: **«Lakini sisi tutabariki Bwana tangu sasa hata milele».** Kama sisi sote tutakufa na nafsi yetu, namna gani, hapa ansema Nabii Daudi ya kama sisi tutabariki Bwana hata milele? Hapa Nabii Daudi anakikiri ya kama ma nafsi yenye haki yataweza kumutukuza Mungu na kisha lufu ya mwili. (Zaburi 115, 17-18).

c) **«.. . lakini wafu hawajui kitu, wala hawana zawabu tena; .. . maana ukumbuko wao umesahauliwa.. . Kitu cho chote mukono wako unachopata kufanya, ukifanye kwa nguvu zako zote; maana hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima ndani ya kaburi, pahali unapokwenda» (Muhubiri 9, 4-6, 10).** Ndani ya hii shairi Mwandishi Muhubiri anasema juu ya jabo yanafanyika pa inchi katika ya wenye uzima na katikati ya ma jabo haya wafu hawawezi kuwa pamoja.

d) **«Kwa kuwa Hadeze haiwezi kukusifu, wala kufa hakuwezi kukutukuza; wala wenye kushuka kwa shimo hawawezi kutaraja kweli yako». (Isaya 38, 18).** Hii shairi inatwaambia juu ya kaburi pahali itaingia mwili isiyouzima na kweli haina mioyo. Haiseme kitu juu ya nafsi.

Maneno haya yalitokea toka uwazo na maarifa walikuwa na watu wa Ebrania hile wakati mbele ya Kuja Kristu duniani, juu ya giza na taabu mu Hadeze, sawa makao ya kifungo ya ma nafsi yao. Lakini tulisema mara mengi ku mukongo ya kama ufunuo ya fundisho ya Agano la Kale haina ukamilifu na inaangazwa paka katika nuru ya Agano Jipya. Kwa sababu, basi, Agano Jipya inatwaambia safi kabisa juu ya uzima ya nafsi na mioyo yake, kisha lufu ya mwili, ma shairi yanatokea toka Agano la Kale hayaseme fundisho ya Mungu, lakini yanasema mawazo na imani ya watu wa Ebrania hile wakati waliishi.

# 11
# UFUFUO YA WAFU WOTE

## MWANZO

Ufufuo ya miili ya watu wafu wote ni fundisho munene ya Kanisa Orthodokse. Sawa tulisema ku mukongo, Mungu aliumba mutu hapana paka sawa nafsi (roho), lakini sawa uso moja na vitu vya wili ndani yake: Mwili na nafsi. Basi, makadaza (kikomo) yake kuingia kwa uzima wa milele na hali muzima yake na hapaka paka katika roho yake. Kwa hivyo, fundisho kubwa ya Dini wa Kristu ni ma siku zote Ufufuo ya miili yetu yenye yalikufa, yenye, kwa ajili ya zambi ya Wazazi wa kwanza, wanaachana toka nafsi yao ya nyakati kidogo. Watu wa Ebrania mu wakati yao, mbele ya Kuja Kristu duniani, walisadiki sana kwa ufufuo ya wafu. Kupindua mataifa wengine, sawa kwa mufano Wayunani (WaGreki) walikataa ufufuo ya wafu, kwa sababu

kwao «mutu» alikuwa paka nafsi, lakini mwili ilikuwa, katika imani yao, kifungo ya nafsi, na ilipashwa kuuhuru na hivi itapata okombozi. Hapa tunaona hii uchanisho munene ni katikati ya nyakati mbele ya Kristu na nyakati kisha Uzalio ya Kristu.

Kwa hii ufufuo ya wafu miili yatafufuliwa yasipouharibifu, yatakuwa yakamilifu na ya milele. Itarudi ndani yao na nafsi yao na hivi yatakuwa «watu» wazima kwa waishi kwa milele. Miili haya makamilifu hayatakuwa mara ingine ndani ya uharibifu na lufu, wala ulazimisho ya vitu ya maisha ao kufata ma sheria ya hii dunia, lakini yatakuwa sawa Mwili iliyefufuka ya Kristu. Huu Ufufuo ya watu wote itakuwa na Tendo wa mwisho ya Kazi ya Kristu. Kwa hivyo HULE KRISTU alifufuka katika mwili Yake toka wafu juu ya kuwa mwanzo na ukikiri ya ufufuo wetu: **«na kama Kristu hakufufuliwa, imani yenu ni bule; mungali katika zambi zenu.. . Lakini sasa Kristu amefufuliwa toka wafu, malimbuko yao waliolala.. . » (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 17, 20).**

Washuhuda wa Yehova wanakataa hii fundisho wa kweli ya Dini wa Kristu, sawa vile wanakataa na mafundisho ingine na wanasema hivi: «Hile kitu itafufuliwa ni nafsi, nikusema alama ya uzima ao upekee ya mutu na hapana mwili umoja. Kisha ufufuo moja, kiumbe inarudi ao inaumbwa mara ya pili ama katika mwili ubinadamu ama mwili wa roho, lakini huu mwili haina ubinadamu na haisharikiwa hata kidogo na mwili wa kwanza ya hule mufu. Kwa wale 144. 000 wenye wataenda mbinguni, Mungu anawapatia mwili mupya wa roho. Kwa wale wanafufuliwa pa hii inchi, anawapatia mwili wa bulongo. Hii mwili, bila shaka, itakuwa umoja na mwili hile alikuwa hule mutu na zamani pa hii inchi, kwa hivi itaifamiwa na ku watu wenye walimufamia». Hii ni imani ya Washuhuda wa Yehova!

Tena, ila tu, wanakataa ufufuo nzima ya wafu wote, wenye haki na wasiyo haki, na wanasadiki paka ufufuo ya wenye haki na wale watu mu uzima yao hawakupate nyakati kusikia mafundisho ya Mungu. Wanasema: «Wenye kibego hakuna namna Mungu awakumbuke kwa ufufuo. watu sawa Adamu, Yuda, Wandishi ya Sheria na Wafarisayo na wengine hawatafufuliwa. Hawa wasiyo imani hawatarudia kwa kuhukumiwa, kwa sababu wamehukumiwa na ni wenye stahili ya uharibifu». Lakini Madiko Takatifu mara ingine inafunusha mafundisho yao ya kama ni ya uwogo na inatufundisha ufufuo itakuwa ya wafu wote tangu mwanzo ya hii muzima.

## 1. MADIKO TAKATIFU INAANDIKA JUU YA UFUFUO YA WAFU

**1)** a) **«Kwa sababu kama katika Adamu wote wanakufa, hivyo wote katika Kristu watapatizwa uhai» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 22).**

**b) Kwa sababu sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.. . » (Wa Roma 14, 10).**

**c) «Nina tumaini kwa Mungu kamaao wenyewe wanalotazamia ya kwamba utakuwa ufufuko wa wafu, wenye haki na wasio haki pia» (Matendo 24, 15).**

**d) «kwa sababu imetupasa sisi sote kuonekana mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu; hata kila mutu apokee maneno aliyotenda kwa mwili, kwa kadiri alivyotenda, kama ni mazuri ao mabaya» (barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 10).**

Kwa hivyo, Ufufuo itakuwa ya wafu wote.

**2)** Ufufuo huu haina ufufuo moja «wa roho» ya nafsi, *(sawa vile wanasadiki Washuhuda wa Yehova na itafanyika ndani ya kaburi),* lakini itakuwa ufufuo ya mwili muzima, inayeiko ndani ya kaburi bila uzima na bila nyama yake: **«Kwa sababu saa itakuja na watu wote walio katika makaburi watasikia sauti yake (ya Kristu), nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuko wa uzima, na wale waliofanya mabaya, kwa ufufuko wa hukumu» (Yoano 5, 28-29).** Hii imani ya kufufuka maiti ya ndugu zake alisema na dada ya Lazaro, Marata, wakati

alisemaka kwa Kristu: **«Ninajua ya kama atafufuka katika ufufuko wa siku ya mwihso» (Yoano 11, 24).**

**3)** Hii sauti alisemaka na Mtume Paulo kwa Wakristu ya Roma: **«Lakini kama roho yake yeye aliyefufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyefufua Kristu katika wafu, atawapa uzima kwa miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa sababu ya Roho yake anayekaa ndani yenu» (Wa Roma 8, 11).**

**4) «Lakini sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi vilevile tunaugua ndani ya roho zetu, tukitazamia kuwekwa kama wana, ndiyo ukombozi wa mwili wetu» (Wa Roma 8, 23).** Hapana «ukombozi toka mwili», lakini ukombozi wa mwili umoja toka uharibifu, sawa vile inasema shairi (8, 20-21).

**5)** Tena safi kabisa inaandikwa hii ukombozi wa mwili toka uharibifu na kwa wa Korinto: «Basi, kama ikiwa Kristu amehubiriwa ya kama alifufuliwa toka wafu, namna gani wengine wenu wanasema ya kuwa hakuna ufufuko wa wafu? . . . Lakini mutu fulani atasema: Wafu wanafufuliwa namna gani, nao wanakuja kwa mwili gani? Mupumbafu wewe, mbegu unayopanda haipati uhai ila ife.. . . Ufufuko wa wafu ni hivi vilevile. Unapandwa katika kuoza, unafufuliwa katika kutokuoza: unapandwa katika haya; unafufuliwa katika utukufu: unapandwa katika uzaifu, unafufuliwa katika uwezo; unapandwa mwili wa asili, unafufuliwa mwili wa roho. Kama ikiwa mwili wa asili uko, kuna vilevile mwili wa roho.. . Na kama tulivyochukua sura ya yule wa udongo, vivyo hivyo tutachukua sura ya yule wa mbinguni» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 12, 35-36, 42-44, 49). « Ukombozi» hii na geuzo ya mwili wa mavumbi yetu itakuwa kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho, kwa baragumu ya mwisho: sababu baragumu italia na wafu watafufuliwa wasiwe na kuoza, na (sisi wenye muzima) tutabadilika. Maana sharti (mwili inayekufa) ule wenye kuoza uvae kutokuoza, na huu wa mauti uvae kutokufa» (15, 52-53).

**6)** Hii mwili wetu itayekuwa katika ubadilisho na ukamilifu, itakuwa mutukufu na inafanana na mwili wa ufufuo wa Bwana Yesu Kristu: **«Atakayebadilisha mwili wetu wa haya upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uwezo ule anaoweza kutiisha vitu vyote viwe chini yake» (Wa Filipi 3, 21).**

**7)** Kwani anajua maneno haya yote Mutume Paulo anasema ya kama Wakristu wanaomboleza chini ya uzito mwili yao wa bulongo, hapana kwani wanataka kufukuza, lakini, kwani wanataka kuivala uvazi ya isiyoharabika kwa uzima wa milele: **«Kwa sababu kweli sisi tulio katika hema hii tunaugua kwa kulemewa; si kwa sababu tunataka mavazi haya kuondolewa, lakini tunataka kuvikwa, kusudi iliyo ya mauti imezwe na iliyo ya uzima» (barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 4).**

Hapana paka Agano Jipya, lakini na Agano la kale inashuhuda juu ya ufufuo ya wafu katika miili yao:

**8) «Lakini ninajua ya kuwa mukombozi wangu ni hai, na ya kuwa katika mwisho atasimama juu ya inchi: na nyuma ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini pasipo mwili wangu nitaona Mungu: Na mimi mwenyewe nitamwona na macho yangu yatamutazama, wala si mwingine. Mutima wangu unazimia ndani yangu» (Yobu 19, 25-27).** Basi, Yobu alijua ya kama, siku moja (ma siku wa mwisho) ataona Mungu katika mwili wa ufufuo yake, tena alijua ya kama mwili yake itaingia na itaharabika ndani ya kaburi.

**9)** «Wafu wako wataishi, maiti zangu zitafufuka. Amkeni na kuimba, ninyi munaokaa katika mavumbi; kwa maana umande wako ni kama wa asubui, na dunia itatoa wafu» (Isaya 26, 19).

**10) «Kwa wakati ule Mikaeli atasimama yule mukubwa anayesimama kwa ajili ya wana wa watu wako: na kutakuwa na wakati wa taabu kama usivyokuwa mbele tangu wakati taifa lilipokuwa hata wakati ule: Na kwa wakati ule watu wako wataponyeshwa,**

**kila mutu atakayeonekana ameandikwa katika kitabu. Na wengi wao wanaolala mavumbini mwa inchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, na wengine kwa haya na kuzarauliwa kwa milele» (Danieli 12, 1-2).** Nabii Danieli hapa ku mwanzo anaandika juu ya wakati ya mfalme Antiokos Mukubwa (hile nyakati ilikuwa nyakati ya mafukuzo na ma taabu ya watu wa Ebrania). Huyu mufalme alionekana sawa mufano ya Mupinga wa Kristu, mwenye atakuja ku mwisho ya dunia. Hapa Nabii Danieli anaandika juu ya nyakati wa mwisho, wakati atakuja Mupinga ya Kristu (Antikristi) na ya kama hawa wenye haki watapata uzima wa milele, lakini wengine watazarauliwa kwa milele. Hivi anataka kuwasaidia mbele ya mafukuzo alifanya mufalme Antiokos kupindua yao.

**11)** Ku mwisho kwa Nabii Ezekieli ni unabii ingine, pahali Nabii aliona kwa maono yake mifupa nyingi ya watu wafu, na yenye katika amri ya Mungu walipata mara ingine nyama, mizizi na ngozi na pumuzi ya uzima yao na waliishi mara ingine (37, 1-14). Mifupa haya yenye kufufuliwa yanaleta maana ya kama siku fulani taifa wa Israeli itatengenezwa mara ingine, lakini hile nyakati ilikuwa kwa kutumwa na kuzambalishwa pa fasi ya kuachana. Lakini maana ingine wa chini kabisa ni Ufufuo ya wafu wote wa dunia, hiule siku ya Kuja wa Mbili ya Kristu hapa duniani.

## 2. MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA

Sawa vile tulisema mara nyngi Washuhuda wa Yehova wanaachana Ufalme wa Mungu kwa ufalme wa mbungu pahali wataikaa 144. 000 watu wenye fazila na kwa ufalme wa inchi juu ya kuikaa watu wingi. Hawa 144. 000 watafufuliwa na miili yao wa roho, lakini wengine na mwili wa mauti. Tena tulisema ya kama wenye kibego, katika imani ya Washuhuda wa Yehova, hawatafufuliwa kwani walihukumwa wenye stahili ya uharibifu. Kupindwa «wasiyo haki» na watu wengine milioane, kwani hawakupate wakati wafamie mapenzi ya Mungu, watafufuliwa, lakini kwa hukumu pa hii inchi»: Nikusema, kama watafata mafundisho na watabaki waaminifu, wataishi kwa milele pa hii inchi. Hii imani yao ya kama wasiyoimani hawatafufuliwa, wanaisingi pa ma shairi haya:

1) **«Kwa hivi waovu (wasiyoimani) hawatasimama (hawatafufuliwa) katika hukumu (Zaburi 1, 5).**
2) **«Wakati waovu wanapochipuka kama majani, na wakati watenda uovu wote wanapositawi: ni kwa kusudi waharibiwe milele» (Zaburi 92, 7).**

**3) «Nami nitafanya wakubwa wake kulewa na mvinyo, na watu wake wenye akili watawala wake, na wakubwa wa jeshi lake, nawenye uhodari wake wa vita; nao watawala usingizi wa milele, wasiamke, anasema Mufalme, Bwana wa majeshi, jina lake ni Bwana» (Yeremia 51, 57);** vile anasema Nabii juu ya wakubwa wenye zambi ya muji Babeli.

**4) «Wamekufa, hawataishi; wamefariki, hawatafufuka; kwa sababu hii umewaangalia na kuwaharibu na kupoteza ukumbusho wao» (Isaye 26, 14), anasema hivi Nabii juu ya watu wa adui ya Mungu.**

5) **«Na watakuwa kama hawakuwa mbele» (Obadia 16),** anasema Nabii juu ya mataifa, yenye ni ma adui ya Mungu.

Ndani ya ma sehemu uya Nafsi na Hegena wa Milele tumefanya mafundisho juu ya lufu wa mwili na wa roho, inayeitwa mu Kitabu Ufunuo «mauti wa mbili» na huu ni uchanisho wa milele ya hule mutu mwenye zambi toka Mungu. Kila musomaji ataweza aende kusoma pale pa sehemu. Hapa tunaona ya kama ma shairi yote ya Agano la Kale yanapata maana yao ndani ya nuru ya Agano Jipya. Mafundisho muzima wa kweli inaonekana kabisa ndani ya Agano Jipya na watu wasiyo imani watapata lufu wa milele, nikusema uchanisho na maepuko mbali ya Mungu.

Tena, ya kama wenye wasiyo imani watafufuliwa kwa hukumu, inatukikiri na Kristu mumoja, mwenye mu sehemu ya Evangelio ya Hukumu anawafanana sawa mbuzi na atawaweka pa fasi ya kushoto Yake (Matayo 25, 31-46). Pa fasi ingine anasema ya kama **«wote walikuwa mu kaburi» watafufuliwa na wenye kibego watatembea kwa ufufuo ya hukumu (Yoano 5, 28-29).** Mtume Paulo tena anasema ya kama «ufufuo itakuwa ya wafu, wenye haki, na wasiyo haki (ndani ya kundi ya wasiyo haki ni na watu wasiyo imani) (Matendo 24, 15). **«Kwa sababu imetupasa sisi sote kuonekana mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu; hata kila mutu apokee maneno aliyotenda kwa mwili, kwa kadiri alivyotenda, kama na mazuri ao mabaya» (bartua ya mbili kwa wa Korinto 5, 10 na wa Roma 14, 10).** Lakini na Kristu alielejea safi ya kama watu wenye zambi na wasiyo toba watatupwa mu gehena ya moto na miili yao, nikusema mbele ya gehena na miili yao itakuwa ufufuo ya miili yao (Matayo 5, 29-30. 18, 8-9 na Matayo 10, 28).

Ushuhuda munene juu ya ufufuo na hukumu na wenye kibego (wasiyoimani) ni maneno ya mwenye hekima Nabii Solomono: **«Mungu atahukumu wenye haki na waovu» (Muhubiri 3, 17)** na unabii wa zamani ya Enoka, hile inaandika Mutume Yuda mu Agano Jipya: **«Na Enoka mutu wa saba tangu Adamu, alitabiri juu ya hawa, akisema: Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, elfu elfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuazibisha wote wasioogopa Mungu, kwa ajili ya matendo yao yote ya upotevu waliyotenda pasipo kuogopa Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote wakosayi hawa wasioogopa Mungu waliyosema juu yake» (Yuda 14-15).** Hapa Mutume Yuda ansema juu ya Hukumu wa mwisho itayekuwa kwa Kuja ya Mbili ya Kristu; na hii inaonekana safi katika hii mustari yake**: «Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, elfu elfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote.. . »;** hii mustari inasharikiwa na maneno ya Kristu na Mitume wengine juu ya Hukumu wa mwisho (Matayo 25, 31-32 na barua ya mbili kwa wa Tesalonika 1, 7).

# 12

## UZIMA WA MILELE MU GEHENA

### MWANZO

Washuhuda wa Yehova wanakataa tena na uzima wa milele ya Gehena. Katika fundisho yao, hawa watu wenye zambi na wasiyokutubu watarudi kwa sifuru, kisha Hukumu wa mwisho. Lakini Madiko Takatifu inaandika kupindua: Na Gehena na Ufalme mbinguni yatakuwa kwa milele. Na Ufalme mbinguni itakuwa shangilio wa furaha ya waaminifu wakristu (Wa Ebrania 13, 23), wenye wataishi ndani ya ushirika moja pamoja na Utatu Mutakatifu na watapata uzima wa heri pamoja Naye. Kupindua, Gehena itakuwa uchanisho wa milele ha watu wenye zambi toka Mungu (Luka 13, 28), pahali pa hii fasi haitaingie ndani nuru ya Jua-Kristu na baraka ya Mungu. Wenye heri mara tatu watakuwa hawa watastahiliwa waingie mu Ufalme mbinguni. Lakini, wenye taabu na sikitiko mingi watakuwa hawa watafungwa mu gehena na watakuwa ndani ya giza kwa milele (Matayo 8, 12), kwnai katika mapenzi yao walichagua hii fasi ya giza: **«Na hii ndiyo hukumu, ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni na watu wamependa giza kupita nuru, kwa sababu matendo yao yalikuwa mabaya» (Yoano 3, 19).** Mufano ya ma Bikira kumi inatupatia hii ufananisho safi: Wakati alikuja Bwana-Arusi Kristu, «nao walikuwa tayari waliingia pamoja naye kwa arusi; mulango ukafungwa. Halafu mabikira wale wengine wakakuja vilevile wakisema: Bwana, Bwana, utufungulie. Lakini akajibu, akisema: **Kweli ninawaambia ninyi, siwajui, ninyi» (Matayo 25, 10-12).** Hii mambo ya kama wale ma Bikira tano walibaki inje ya arusi-makao ni maana ya gehena. Na hii gehena ni wa milele. Na ndani ya gehena wale watu wataingia watapata mapendo ya Mungu, lakini hii mapendo ya Mungu itakuwa

mbele ya wenye haki chemchem ya duraha na uzima wa heri, lakini kwa wale wa gehena itakuwa pingilio na moto, itayelungua mioyo yao.

## MADIKO TAKATIFU INASEMA NINI JUU YA GEHENA WA MILELE

**1)** Evangelio (Kipande) ya Hukumu wa Mwisho inatukikisha ya kama: **«Na hawa wote watakwenda kuingia katika azabu ya milele; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele» (Matayo 25, 31-46).** Kwa sababu uzima wa milele itakuwa kweli kwa milele (na hii fundishso wanaipokea na Washuhuda wa Yehova), katika namna umoja na gehena wa milele, inapashwa kuwa ya kweli kwa milele.

Washuhuda wa Yehova, juu ya kukimbia toka hii shairi ya Madiko Takatifu, wanafafanusha neno: «katika azabu (gehena) ya milele» hivi: «katika kukata ya milele».

**2)** Ya kama gehena ni ya milele inatushuhuda na maneno haya, sawa: **«Ni afazali kuingia katika uzima mwenye kilema, kuliko kuwa na mikono miwili na kwenda katika gehena katika, moto usiozimika. (pahali pasipokoma funza lao, wala moto hauzimiki.. . na miguu miwili na kutupwa katika gehena.. . » (Marko 9, 43-48), tena inaitwa sawa: «Moto wa milele» (Matayo 18, 8 na 25, 41), tena sawa: «hukumu ya moto wa milele» (Yuda 6-7).**

**3)** Ya kama Gehena haina kurudi kwa sifuru, lakini ni malipizo ya kweli inatukikiri hii sauti Kristu, wakati anasema ya kama: «Lakini wana wa ufalme watatupwa katika giza la inje; kutakuwa kulia na kusaga meno» (Matayo 8, 12. 13, 42, 49-50. 22, 13. 25, 30), inaitwa : «gehena ya moto ao kutupwa katika gehena» (Matayo 5, 22, 29-30. 13, 42, 50. 18, 9).

**4)** Tena stahili ya kuisopoka ni hii mustari: **«Musiwaogope wale wanaoua mwili, na nyuma hawawezi kufanya neno lingine. Lakini nitawaonya ninyi ninyi ni nani mutakayeogopa. Mumwogope yeye aliye na uwezo, nyuma ya kuua mutu, kumutupa katika Gehena» (Luka 12, 4-5).** Kama : «nyuma ya kuua mutu» nikusema kisha uuaji ya mutu moja, nafsi yake haiishi na yoyote yanarudi mu bulongo, sawa vile wanasema Washuhuda wa Yehova, basi, ni nini maana kisha: «Kumutupa katika gehena? » Nikusema itatupwa nini ndani ya gehena, kama na nafsi na mwili yatarudi kwa sifuru, sawa vile wanasema Washuhuda wa Yehova?

**5)** Kwa sababu gehena itakuwa malipizo wa kweli, hii apizo itakuwa ya mbali-mbali: **«Na mutumwa yule aliyejua mapenzi ya bwana yake, lakini hakufanya tayari, wala kutenda mapenzi yake, atapigwa mapigo mengi. Lakini yeye asiyejua, akifanya matendo yanayofaa mapigo, atapigwa mapigo machache, kwani kila mutu aliyepewa mengi, kwake mengi yatatafutiwa; naye watu wanayemuwekea vitu vingi, kwake wataombe vitu vingi zaidi» (Luka 12, 47-48). Tazama na Matayo 10, 15 na 26, 24).**

**6)** Ku mwisho uzima ya milele ya Gehena inatukikisha na Ufunuo:

**a) «.. . Mutu akiabudu nyama na sanamu yake, na kupokea chapa katika kipaji cha uso wake, ao katika mukono wake, yeye atakunywa mvinyo ya gazabu ya Mungu.. . naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele ya Mwana-Kondoo. Na moshi wa mateso yao ulipanda juu hata milele na milele, wala hawana raha muchana wala usiku, hawa wanaoabudu nyama na sanamu yake, na kila mutu anayepokea chapa ya jina lake» (Ufunuo 14, 9-11).**

**b)** «Yule nyama akakamatwa na yule nabii wa uwongo pamoja naye, yeye aliyefanya mastaajabu mbele yake, kwa haya alidanganya watu wale waliopokea ile chapa ya nyama, nao walioabudu sanamu yake; hawa wawili walitupwa wangali hai katika lile ziwa la moto linalowaka kwa kiberiti» (Ufunuo 19, 20).

c) «Na yule Diabolo, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moro na kiberiti, pahali wanapokaa yule nyama na yule nabii wa uwongo. Na watateswa muchana na usiku hata milele na milele» (Ufunuo 20, 10).

## 2. MAFUNDISHO-MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA

Sawa vile tulisema, Washuhuda wa Yehova wanakataa ya kama Gehena ni ya milele na wanahubiri ya kama watu wenye zambi watarudi kwa sifuru na watakufa kwa milele. Hii fundisho yao yanaisingi pa mistari haya:

1) **«Lakini wenye woga na wasioamini, na wenye machukio na wauaji, na wazini, na washawi, na waanaoabudu sanamu, na wawongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa linalawaka moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili» (ufunuo 21, 8).** Ndani ya vitabu yao wanahubiri hivi: **«Hakuna ufufuo kisha mauti ya pili, lakini mauti ni mwisho ya uhai na usimamisho ya mioyo na akili na maarifa»**.

Lakini sawa vile tulifunza mu Sehgemu ya Nafsi, «mauti» ndani ya Madiko Takatifu hana maana ya kurudi mutu kwa sifuru. Sawa kila mutu anatazama, tuna mauti viwili: Ni mauti ya mwili, kwa ajili yake inaachana nafsi na mwili na ya pili tuna mauti ya roho, maana yake wakati mutu moja anatoka mbali toka Mungu. Tunakumbuka huku mifano ya watu wenye waliishi tena ndani ya hii uzima, lakini wanaitwa mu Madiko Takatifu «wafu: (Matayo 8, 22. Luka 12, 24. Waefeso 2, 1, 5. 5, 14 na Waroma 6, 13 na barua ya kwanza kwa Timotheo 5, 6). Basi, «mauti ya pili» hana ya kurudi mutu moja kwa sifuru, lakini ni uchanisho ya wasiyokutubu watu wenye zambi toka Mungu; huu ni «mauti wa roho».

Lakini na Ufunuo umoja inatwaambia maana ya mauti ya pili na kiziwa ya moto: **«Na yule Diabolo.. . akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, pahali wanapokaa yule nyama na yule nabii wa uwongo. Na watateswa muchana na usiku hata milele na milele» (Ufunuo 20, 10).** Basi kiziwa ya moto ni maana ya mateso wa milele.

Hii jabo yanajua muzuri sana ma Diabolo. Ni ufananishwa ya kama kwa uponyesho moja ku Kristu kwa mutu moja aliyekuwa na pepo uchafu, diabolo alisema: **«Ee, Yesu wa Nazareti, tuna nini nawe? Umekuja hapa kutuangamiza sisi? Marko 1, 24) na Luka 4, 34).** Lakini pa fasi ingine mu Gerasa ma Diabolo walisema: **«Tuna nini nawe, wewe Mwana wa Mungu? Wewe umekuja hapa kututesa mbele ya wakati? (Matayo 8, 29).** Basi maneno: «kutuangamiza sisi» na «kututesa» hakuna namna kuwa maana yake ya kurudi kwa sifuru.

Ku mwisho, ushuhuda munene ni ya kama mauti ya pili haina kwa kurudi kwa sifuru, lakini uchanisho ya milele toka Mungu katika maneno ya Mtume Yuda: **«Wata hawa ni miamba yenye hatari katika karamu zenu za mapendo wakati wanapokula karamu pamoja nanyi, wachungaji wanaoijikulisha wenyewe pasipo woga, na mawingu yasiyo na maji, yanayochukuliwa na upepo, ni miti isiyo na mayani, pasipo matunda, iliyokufa mara mbili na kungolewa kabisa» (Yuda, 12).** Walikuwa wenye muzima, lakini wanaitawa ya kama walikufa mara mbili.

2) **«Nafsi, inavyofanya zambi, itakufa» (Ezekieli 18, 4).** Sawa vile tulifunza mu sehemu ya Nafsi «nafsi» hapa ni maana ya kila mutu aliyekosa. Mungu anatufundisha ya kama kila mutu analipizwa kwa zambi zake na hapana kwa zambi za watu ya vizizi vyake. Hii mustari, basi, hakuna namna kuisema ya kama nafsi ya mutu moja itarudi kwa sifuru.

3) **«Bwana anachunga wote wanaomupenda; lakini waovu wote atawaharibu» (Zaburi 145, 20).**

4) **«.. . ndivyo mataifa yote watakavyokunywa daima, ndiyo watakunywa na watameza, na watakuwa kama hawakuwa mbele» (Obadia 16).**

5) **«.. . nao watalala usingizi wa milele wasiamke, anasema Mufalme, Bwana wa majeshi, jina lake ni Bwana» (Yeremia 51, 57). Lakini Nabii na Mwimbaji Daudi anasema: «kwa hivi waovu hawatasimama katika hukumu» (zaburi 1, 5).**

**6) «kuna zambi iliyo ya mauti» (barua ya kwanza ya Yoano 5, 16).**

Mistari haya (3-6) hakuna namna sisi kusadiki ya kama maana yao ni yakurudi nafsi kwa sifuru (0). Mistari haya yalichukuliwa toka Agano la kale na tulisema ya kama Agano la kale inapata maana yake wa kweli paka chini ya nuru ya Agano Jipya.

Mu mustari 5) maana yake haina ya kama wenye zambi hawatafufuliwa kwa Hukumu wa mwisho, sawa wanasadiki Washuhuda wa Yehova, lakini watafufuliwa na wale wenye zambi na wasiyoamini sawa vile inatukikisha Agano Jipya: (Yoano 5, 28-29. Matendoi 24, 15 na barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 10 na Waroma 14, 10 na Yuda 14-15).

**1)** Maana wa kweli ya shairi: ««kwa hivi waovu hawatasimama katika hukumu» (zaburi 1, 5), ni ya kama watu waovu hawataweza wasimame mbele ya Muhukumu Kristu. Hii ufafanusho wanaipokea na Washuhuda wa Yehova.

# 13

# MUZAZI-MUNGU MARIA

## MWANZO

Sisi Waorthodoksi, kisha Mungu (Baba, Mwana na Roho Mutakatifu) sawa na ma dini wote wa zamani tunasifu Bikira Maria sawa «uliye wadamani kuashinda Wakheruvi, uliye na utukufu kuapita bila kiasi Waserafi.. .  », sawa» umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza». Tunasifu Muzazi-Mungu kwani alikuwa stahili kuwa Mama wa Bwana wetu. « Kwani tazama,  tangu leo vizazi vyote wataniita heri» (Luka 1, 48), anasema mumoja ndani ya Habari Njema.

Washuhuda wa Yehova wanakataa sifa hile tunaitoa sisi wa Orthodoksi kwa Mutakatifu kamili Mzazi-Mungu Maria na wanafundisha ya kama alikuwa mwanamuke moja wa bure, sawa vile  ni na wanawake wengine. Tena wanakataa ya kama Huyu ni bikira ma siku zote na wanafundisha tena ya kama, ila uzalio ya Kristu, alizala na watoto wengine pamoja na mulinzi yake Yosefu. Kwa sababu hawaamini Yesu Kristu sawa Mungu, ni teketeke kukataa na jina lake: «Muzazi-Mungu»

Ni kweli ya kama Madiko Takatifu haiandike ma hadishi mengi juu ya Mzazi-Mungu Maria. Ninazania, kwani, hile wakati yaliandikwa Evangelia ya inne, Bikira Maria aliishi tena na alikuwa pamoja na Mitume. Tena, kwa sababu fundisho wa kwanza ndani ya Agano Jipya alikuwa Uso ya Bwana Yesu Kristu, sawa Mwokozi na dunia muzima. Tena, wakriastiani wale wa kwanza walijua Mzazi-Mungu Maria na haikukuwe lazima kuandika Waevangelizaji juu ya Uso na Hadishi yake. Ufamio hii juu ya Mzazi-Mungu ilikuwa kitu kimoja ya imani inayekwenda kizazi kwa kizazi sawa maarifa ya Kanisa, sawa imani ya waamnifu sawa Mapokeo Takatifu.

Tulisema kidogo yulu ya kama Agano Jipya haiandike mambo mengi ya uzima ya Mzazi-Mungu. Lakini Agano la kale kama tunaisoma katika nuru ya Agano Jipya, tunaweza kupata ma alama na mifano mengi juu ya Uso ya Mzazi-Mungu. Sawa:

**1)** Mugazi iliyeona kwa ndoto yake Yakobo ilisimama pa inchi na chogo yake ilifika mbinguni na pa hii mugazi malaika wa Mungu walipanda na walishuka. (Mwanzo 28, 10-13).

2) «Lango hili litafungwa, halitafunguliwa, wala mutu ye yote hataingia kwa njia yake, kwa maana Bwana Mungu wa Isareli ameingia kwa njia yake; kwa hivi litafungwa» (Ezekieli 44, 1-2). Hii unabii inatuonyesha ubikira ya Mzazi-Mungu.

3) «Binti za wafalme ni kati ya wanawake wako wenye heshima; kwa mukono wako wa kuuma anasimama malkia amevaa zahabu ya Ofiri» (zaburi 45, 9). Huyu Binti ni Mzazi-Mungu.

## 1. MADIKO TAKATIFU JUU YA MUTAKATIFU KAMILI MUZAZI-MUNGU

**1)** Bikira Maria ni Muzazi-Mungu: Kwa sababu Huyu aliyemuzala asikukuwe Mwingine paka Emanueli, nikusema: **«Mungu pamoja nasi» (Matayo 1, 23**). Basi, hii jina ya Bikira Maria ni ya kweli, kwa sababu kweli alizala Mungu katika mwili.

Tunakumbuka sasa maneno ya Elisabeti**: «Neno hili limetoka wapi, mama ya Bwana yangu anakuja kwangu? (Luka 1, 41-43).** Mu akili ya mwanamuke moja wa Israeli jina «Bwana» haikukuwe ingine paka Mungu. Basi, «mama ya Bwana yangu»= mama ya Mungu wangu, Muzazi-Mungu.

**2)** Heshima munene ya Kanisa yetu mbele Kwake: Kwnai yeye alikuwa katika kimutu, Mama wa Mungu na Kanisa anamusifu na anamutukuza na haki. Hii inatufundisha na Madiko Takatifu: **«Malaika alikuja kwake, akasema: Salamu, uliyepewa neema, Bwana yuko pamoja nawe; wewe umebarikiwa katika ya wanawake.. . Na roho yangu imefurahia Mungu, Mwokozi wangu. Maana ametazama unyenyekevu wa mujukazi wake; kwani tazama, t a n g u. l e o. v i z a z i. v y o t e. w a t a n i i t a. h e r i» (Luka 1, 28, 47-48**).

**3)** Bikira Daima: Ya kama Mzazi-Mungu anabaki bikira ma siku zote inaonyeshwa hii fundisho hapana paka toka Mapokeo Takatifu, lakini tena toka mistari haya:

**a)** Uchumba yake pamoja na Yosefu (mwenye katika Mapokeo Takatifu alikuwa kuliko mukubwa kwa kipimo yake) haikukuwe kikomo ndoa, lakini uchumba yake ilikuwa kwa ulinzi yake na utimizo ya tendo ya Mungu. Kwa hivyo, wakati malaika alimuwaambia ya kama atazala mwana, huyu Binti alishangaa na alisema: «Neno hili litakuwa nam, na gani, kwani sijui mume? » (Luka 1, 31-34). Kama uchumba yake ilikuwa kikomo ndoa, haikukuwe lazima kushangaa.

**b)** Ndani ya Madiko Takatifu haiandikwe hata fasi moja ndoa ya Mzazi-Mungu pamoja na Yosefu. Kupindua, na kisha uzalio ya Kristu mu mukini Betlehemu, anaendelea kuitwa tena «Muchumba» ya Yosefu na hapana muke yake (Luka 2, 5). Tena kisha uzalio ya Kristu hasiitwa tena wala «muchumba, lakini paka «Mama ya mutoto» (matayo 2, 11. 13, 14. 20, 21 na Luka 2, 33, 43).

**c)** Hata pa fasi moja Madiko Takatifu haiandike ya kama Mzazi-Mungu Maria alizala na watoto wengine. Kwa sababu hasikuzale watoto wengine, kwa hivyo Kristu, Mwana wake, wakati alikuwa pa Musalaba Wake, alimuacha mama yake kwa mwanafunzi wake Yoano: «Basi wakati Yesu alipoona mama yake, na yule mwanafunzi mupendwa akisimama karibu, akamwambia mama yake: Mwanamuke, tazama mwana wako! Halafu akamwambia yule mwanafunzi: Tazama mama yako. Na kutoka saa ile mwanafunzi yule alimupeleka kwake» (Yoano 19, 26-27). Kama wale waliyeitwa sawa ndugu na dada ya Kristu (Matayo 12, 46 na 13, 55) walikuwa watoto ya Mzazi-Mungu Maria, hakuna namna wamuache mama yao aende mu nyumba ugeni na mikono ya mwanafunzi ya Kristu Yoano.

**d)** Nabii Solomono mukusema kwa jina ya Mwokozi, anasema: «Maana nimekuwa mwana kwa baba yangu, mupole, mupenzi pekee wa mama yangu» (Mezali 4, 3). Hasinyoloka sauti yake kwa maugo yake, kwa sababu huyu hasikukuwe «wa pekee» ya mama yake, lakini alikuwa mwana wa mbili ya Daudi na Birsavee (2 Wafalme 12, 15).

**e)** Tena mafundisho mengi ya Agano la kale, kama itafafanushwa katika nuru ya Mapokeo Takatifu, yanaonyesha ubikira daima ya Mzazi-Mungu. Unabii moja ni hii, iliyeandikwa ku mwanzo: «Lango hili litafungwa, halitafunguliwa, wala mutu ye yote hataingia kwa njia yake, kwa maana Bwana Mungu wa Isareli ameingia kwa njia yake; kwa hivi

litafungwa» (Ezekieli 44, 1-2). Hii unabii inatuonyesha ubikira ya Mzazi-Mungu. Hii Lango litafungwa, ndani yake atapita paka Mungu wa Israeli na hii Lango haina ingine paka tumbo ya Mzazi-Mungu.

## 2. MA SHAIRI- MA BUNDUKI YA WASHUHUDA WA YEHOVA

Washuhuda wa Yehova wanaita mistari yafuata yo juu ya kukataa uzima ubikira ya Mzazi-Mungu:

**1) «Na wakati Yosefu alipoamka toka usingizi, alifanya kama malaika ya Bwana alivyomwagiza: Akachukua muke wake; lakini hakumujua hata alipozaa mwana wake; aliita jina lake Yersu» (Matayo 1, 24-25).**

**2)** Agano Jipya inaandika juu ya ndugu na dada ya Kristu (Matayo 12, 46. 13, 55. Marko 3, 31-32. 6, 3. Luka 8, 19-21. Yoano 2, 12. 7, 3, 5, 10. Matendo 1, 14. Barua ya kwanza kwa wa Korinto 9, 5. Wagalatia 1, 19).

Tunajibu mbele ya ma shairi-bunduki yao:

**a)** «.. . . Muke yake». Mwevangelizaji mukuandika «muke» anasikia na anawaza «muchumba» na hapana «muke». Hii inaonyeshwa ya kama, ku mwanzo ya kupata mimba yake anamuita «muke» ya Yosefu (matayo 1, 24), ku mwisho, wakati alikuwa karibu ya kuzala Kristu anamuita «muchumba» (Luka 2, 5).

**b)** «.. . hata alipozaa mwana wake.. . »; hii neno «hata» haiko maana yake geuzo ya hali kimoja, lakini inaonyesha hali hii itabaki ma siku zote. Kwa mufano:

**a) «Na tazama, mimi ni pamoja nawe na nitakulinda pahali gani unapokwenda, na nitakurudisha tena kwa inchi hii; kwa sababu sitakuacha, hata nitakapokwisha kufanya yale niliyokuambia» (Mwanzo 28, 15).** Lakini Mungu alimuacha Yakobo, kisha ya bile aliyefanya, haya yote alimusema?

**b)** «Na Mikali binti ya Saulo hakuwa na mutoto hata siku ya kufa kwake» (2 Samweli 6, 23). Ni kweli hapa ya kama neno: «hata» inaonyesha hali ya ma siku zote na hapana geuzo ya hali ya binti Mikali. Mikali hasikuzale kisha lufu yake!

**c) «Tazama mutumishi wangu (anasema Mungu Baba juu ya Mwokozi)ninayemushika, muchaguliwa wangu, na nafsi yangu inapendezwa naye; .. . Hatazimia roho wala hatakata tamaa, hata ameweka hukumu ya haki duniani: na visanga vitangojea sheria yake» (Isaya 42, 1-4).** Basi, Mwokozi atazimia roho yake, kisha ya kuweka hukumu duniani?

**d) « Na tazama, mimi ni pamoja nanyi siku zote hata mwisho wa dunia», anasema Kristu kwa Wanafunzi wake, m, bele ya Kupanda kwake mbinguni (Matayo 28, 20).** Lakini atasimama Kristu kuwa pamoja na wanafunzi wake na kisha mwisho ya hii dunia? Kweli hapana. Kupindua atakuwa pamoja nao: (Yoano 14, 3, 17, 24).

Katika hii namna umoja na neno «hata» kwa mustari ya Mzazi-Mungu inatuonmyesha hali ya ma siku zote zake nikusema hali ya ubikira yake na Yosefu hasikumufamie sawa muke yake. Tena Mwevangelizaji anataka kabisa kukikisha ya kama Kristu alizaliwa toka Binti Bikira na huyu hasikufamie bwana-mume mupaka hile wakati, kwnai alitaka kuonyesha ya kama Kristu alikuwa «Mwana» yake sawa inatwaambia unabii ya Isaya 7, 14 na Matayo 1, 23).

**c) «Muzaliwa wa kwanza»:** Nikusema huyu anayezaliwa, bila kumufuata mutoto mwingine wa mbili, wa tatu.. . Mwevangelizaji anamuita Kristu «Muzaliwa wa kwanza» juu ya kutwaambia ya kama alizaliwa toka Bikira, aliyezala mara ya kwanza na, basi, alikuwa mama usiolewa na Bikira sawa vile aliisha kusema juu yake Nabii Isaya (7, 14) na tena huyu Mwana wake «muzaliwa wa kwanza» alikuwa Mwokozi walimuongojea mataifa yote.

Kwa sababu «muzaliwa wa kwanza» mwana wa Bikira Maria ni na Mwana wake wa pekee, inaonyeshwa kwa ajili ya kama Kristu anaitwa «muzaliwa wa kwanza» mwana wa Mungu Baba (Wa Ebrania 1, 6), lakini sisi tunajua ya kama Huyu ni : mwana wake wa pekee» (Yoano 1, 18. 3, 16) Basi, jina: «Muzaliwa wa kwanza» na «wa pekee» yanasharikiwa kwa Uso ya Kristu.

Ila tu, jina «muzaliwa wa kwanza» mu Madiko Takatifu inaikaa na maana ya mbali-mbali:

a) **Maana yake ni huyu aliyezaliwa ya kwanza, aliyefungula mimba (Kutoka 13, 2**), ama watamufuata watoto wengine ama hapana.

b) Maana ingine ni ya muriti ya malako ya Mungu, huyu anayechukua baraka wa roho ya Mungu: Kwa mufano:

**-«Na makutano makubwa, na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa katika mbingu, na Mungu, muhukumu wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika» (Wa Ebrania 12, 23),** nikusema inaitwa kundi ya wameokolewa.

**-«Israeli ni mwana wangu, muzaliwa wangu wa kwanza» (Kutoka 4, 22).**

**-«Kwa hivyo ilikuwa namna kwa Esau, muzaliwa mutoto wa kwanza kuuzisha haki yake ya muzaliwa wa kwanza kwa ndugu yake Yakobo, aliyezaliwa mu nyuma yake (Mwanzo 25, 29-34).**

**c) Ku mwisho, ni maana ya hule ni kupita yulu mbele ya watu wengine. Kwa mufano: «Nami nitamufanya kuwa muzaliwa wangu wa kwanza, juu sana kuliko wafalme wote wa dunia» (Zaburi 89, 27)** anasema Mungu juu ya Daudi, aliyekuwa mutoto kupita mudogo katikati ya watoto ya baba yake Yese. Maneno haya yananyoloka kwa Mwokozi ya dunia, lakini Daudi alikuwa alama na Mwokozi.

d) Wa «ndugu» (Yakobo, Yosia, Simoni na Yuda na wa «dada» ya Kristu:

a) Mu lugha ya Madiko Takaitfu neno «ndugu» iko na maana ya kuachana na iko namna kuwa na maana ya: jirani, semeki, muviala, muyomba, mwipwa na maana ingine. (tazama kwa mufano mu: Mwanzo 13, 8. 29, 15. 31, 23, 25, 32, 37. Walawi 10, 4. 1Mambo ya siku 9, 6, 13. 15, 3-10, 26, 30, 32. Nehemia 11, 13-14, 19).

b) Kanisa tangu wakati wa kwanza haikusadiki hata kidogo ya kama hawa wa «ndugu» na wa «dada» ya Kristu walikuwa wa kweli ndugu Yake. Mafafanusho yalikuwa ya wili: Ao walikuwa watoto ya Yosefu toka bibi yake wa zamani, ao walikuwa watoto ya Klopa na bibi yake Maria. Ufafanusho wa mbili ni kuliko wa kweli kama tutaangalia maonyesho ya Madiko Takatifu kwa kusimama wanawake filani chini ya Musalaba ya Kristu.

**-«Na wanawake wengi walikuwa pale wakitazama kwa mbali, wao waliofuata Yesu toka Galilaya wakimutumikia; katikati yao alikuwa Maria Magdalene, na Maria mama ya Yakobo na Yose, na mama wa Zebedayo» (Matayo 27, 55-56).**

**-«Wanawake walikuwa pale vilevile wakitazama kwa mbali; katika hawa walikuwa Maria Magdalene, na mama Maria ya Yakobo mudogo, na Yose na Salome» (Marko 15, 40).**

**-«Lakini karibu ya musalaba wa Yesu alisimama mama yake, na ndugu muke ya mama yake, Maria mwanamuke wa Kleopa, na Maria Magdalene» (Yoano 19, 25).**

Hapa tunaona ya kama, ila tu ya Muzazi-Mungu, anayemuandika paka Mutume Yoano, yanandikwa na kwa Waevangelizaji tatu na wanawake wengine:

-Maria Magdalene.

-Maria (muke) ya Klopa, mwenye ndani ya Waevangelizaji wa wili wa kwanza anaitwa : mama ya Yakobo na Yose», nikusema, ni «ndugu» ya Kristu. (Hapa hawawaandikwa wa ndugu wa ine ao kwa ajili ya kuandikwa na maneno madogo ao kwani wanasikiwa na wengine).

-Mwanamuke wa tatu anaandikwa sawa «mama ya wana wa Zebedayo», sawa Salome, na sawa «dada ya mama» wa Kristu.

Basi, katika mashuhuda ya Mapokeo Takatifu maonyesho yote ya Madiko Takatifu, sawa inaonekana yulu, yanashuhuda ya kama Yakobo na Yose na «ndugu» wengine na wa «dada» ya Kristu hakuna namna kuwa watoto ya Mzazi-Mungu Maria, lakini walikuwa watoto ya Maria wa Kleopa (ao iko namna kupokea na ufafanusho ingine ya kama walikuwa na watoto ya Yosefu toka bibi wake wa zamani).

Washuhuda wa Yehova wanataka kushariki Muzazi-Mungu Maria pamoja na Maria «ya Yakobo na Yose». Lakini hii fundisho na uwazo yao inatupwa kabisa, kama tutaangalia ya kama Muzazi-Mungu Mtakatifu kamili Maria anaitwa ma siku zote «mama ya Yesu» (Matayo 2, 11, 13, 14, 20-21. Luka 2, 43, 48, 51. Yoano 2, 1, 3, 5, 12) Na Matendo 1, 14). Tena, kama alikuwa na watoto wengine, hakuna namna kufamiwa sawa mama na watoto wengine (wenye walikuwa watu wanyofu) na hapana mama ya Kristu.

Basi, Mama ya Kristu Mutakatifu kamili ni Muzazi-Mungu na Bikira daima na mwenye stahili aimidiwe na atukuzwe kwani ni Uso kabisa kitakatifu, kisha Utatu Mutakatifu, Mungu wetu.

# 14

## WATAKATIFU YA KANISA YETU NA MAOMBEZI YAO

### WATAKATIFU NI WATUMISHI WA KWELI YA MUNGU

1) Washuhuda wa Yehova wanakataa, hapana paka Muzazi-Mungu Bikira Maria, lakini na Watakatifu wote ya Kanisa yetu Orthodokse. Sababu inaonekana safi. Watakatifu ya Imani wa Kristu hawakukuwe «Washuhuda ya Yehova», lakini walikuwa «Washuhuda» ya Mwokozi wa pekee (Matendo 4, 12), Washuhuda ya Bwana wetu Yesu kristu (Matendo 1, 8, 2, 32 na 3, 15) na washuhuda ya ya Mungu wa kweli katika Uso wa Tatu (matayo 28, 19. Barua ya mbili kwa wa Korinto 13, 13). Kama tunasema «Watakatifu», tunasikia watu wenye walimufurahisha Mungu katika uzima yao na walikuwa ya kujaza na neema ya Roho Mutakatifu. Hawa watu ya Mungu weko na fasi moja kabaila ndani ya Kanisa, na Mungu anaonyesha mapendo na wema wake na namna ya mbali-mbali. Hii fasi ya sifa yao anatukikisha na Yesu Kristu mumoja:

a) **«Basi mutu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kufundisha watu hivyo, ataitwa mudogo kabisa katika ufalme wa mbinguni: lakini mutu atakayezitenda na kuzifundisha, huyu ataitwa mukubwa katika ufalme wa mbinguni» (Matayo 5, 19).**

b) **«na utukufu ulionipa (ee Baba) nimewapa, wakae mumoja kama sisi tulivyo mumoja; », anasema Kristu kwa wanafunzi wake (Yoano 17, 22).**

c) **«Yeye anayeshinda, nitamupa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha ufalme, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha ufalme»(Ufunuo 3, 21)**

d) **«Nimepiga vita vizuri-anasema Mutume Paulo-nimemaliza mwendo wangu, nimelinda imani; nyuma ya haya nimewekewa taji ya haki, Bwana muhukumu wa haki atakayonipa siku ile; wala si mimi tu, lakini watu wote pia waliopenda kuonekana kwake» (barua ya mbili kwa Timotheo 4, 7-8).**

e) **«Lakini ninyi mumefikia mulima Sayuni, na muji wa Mungu aliye hai, Yerusalema wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, na makutano makubwa, na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa katika mbingu, na Mungu muhukumu wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika» (Wa Ebrania 12, 22-23),**

**f) «Halafu wenye haki watangaa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio ya kusikia, asikie» (Matayo 13, 43). Kwa hivyo, watakatifu wanaonekana pa picha yao na taji wa mwangaza.**

**2)** Kwani wanajua hii mafundisho Wakristiani wetu, wanasifu na wanaheshimiwa wale watu watakatifu Mungu aliwatukuza na namna ya mbali-mbali, mu uzima yao pa hhi inchi wala kisha lufu ya mwili yao katika ma shairi haya:

**a) «.. . kwa maana wenye kuniheshimu nitawaheshimu, na wenye kunizarau watazarauliwa» (1 Samweli 2, 30).**

**b) «Ukumbusho wa wenye haki una baraka» (Mezali 10, 7).**

**c) «Lakini utukufu na heshima, na salama kwa kila mutu anayetenda mema, . . . » (Wa Roma 2, 10).**

**d) Kabisa juu ya Mzazi-Mungu tukona ma sauti yake, yaliosema katika pumuzi ya Mungu: «Kwani tazama, tangu leo vizazi vyote wataniita heri» (Luka 1, 48).**

**3)** Shangilio ya ukumbusho ya Watakatifu iko na kikomo juu ya kuweka mifano ya uzima yao mbele ya macho ya roho yetu, kupatana na sauti ya watakatifu: «Ukumbusho ya mtakatifu ni kufuata mwendo yake» na ingine: **«Kumbukeni waongozi wenu waliowaambia ninyi Neno la Mungu; na kwa kuangalia mwisho wa mienendo yao fuateni imani yao» (Wa Ebrania 13, 7).** Hii shauria haionyesha paka sifa kwa wenye muzima walimu ya imani, lakini na kwa wale waliisha kufa. Hivi ni maana ya neno: «waliowaambia ninyi Neno la Mungu.. . ».

**4)** Washuhuda wa Yehova wanazarau Watakatifu wetu na kwa sababu ingine: Sawa tuliisha kusema, hawasadiki ya kama ma nafsi yanaishi kisha lufu ya mwili, na kwa hivi hawasadiki ya kama watakatifu iko namna kusikia maombi yetu. Sisi fundisho ya kama nafsi haikufe kwa milele tuliisha kufanya. Hapa tutasema paka ya kama watakatifu hapana paka wanaishi kisha mauti, lakini wanasikia matendo yote yanafanyika huku duniani na mbinguni na kwa hivi iko namna wasikie na maombi yetu:

**a) «Baba yenu Abrahamu alifurahi kuona siku yangu; akaiona akafurahi» (Yoano 8, 56).** Abrahamu alikufa mbele ya miaka ma elfu mbili (2000) mbele ya uzalio ya Kristu. Kwani, basi, aliona Kuja ya Kristu hapa duniani na alifurahi, hii jabo inatuonyesha ya kama huyu Abrahamu aliona ilifanyika nini mu dunia na alikuwa na mioyo yake usafi na muzima.

**b)** Mu hadishi ya hule mutajiri na Lazaro tunaona ya kama Abrahamu, aliyeisha kufa mbele ya miaka 2000 mbele ya uzalio ya Kristu, alijua muzuri sana hapana paka namna gani waliishi mutajiri na Lazaro pa hii inchi («Mwana, kumbuka ya kuwa ulipokea vitu vizuri katika maisha yako kama vile Lazaro alivyopokea vitu vibaya.. . »), anasema kwa hule mutajiri), lakini alijua muzuri sana juu ya Nabii Musa na Manabii na vitabu ya Agano la Kale, yalioandika, lakini Musa na Manabii waliishi miaka mengi ku mukongo na kisha lufu ya Abrahamu («Wana Musa na manabii, wawasikilize wao») anajibu mbele ya ombi ya mutajiri atume Lazaro mukongo pa hii inchi kwa kufundisha ndugu wenye zambi yake. (Luka 16, 19-31). Kwa hivi Abrahamu, miaka 2000 kisha lufu yake, anaonekana sasa ya kuhua matendo yote yanakuwa na pa inchi katika milele mengi. Washuhuda wa yehova wanasema ya kama hii kipande ya Evangelio ya Luka ni mufano na haina ya kweli. Sisi tunawajibu ya kama hakuna hata mustari moja inatuwaambia ya kama hii Kipande ya Evangelio ni mufano (Parabole). Kupindua, ni hadishi wa kweli, kwa sababu yanaandikwa na ma jina ya watu.

**c) Mu Kitabu Ufunuo ya Yoano tunaona ya kama ma nafsi ya washuhuda ya Kristu wanaishi na wanasuburia na Mungu (Ufunuo 6, 9-11).**

**d) Mutume Paulo alitakia kutoka ya mwili yake (nikusema alipenda kufa) juu ya kusafiri kwa Bwana (barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 1-8).** Itakuwa upumbafu, kama

alipenda aende mu uzima moja bila mioyo na zamiri (kama nafsi kweli anakufa) na alipenda kukimbia toka hii uzima!!

**5)** Basi, watakatifu wetu hapana paka wanaishi, lakini wanaishi na mioyo muzima (sawa watu wote) tena ni na ushirika muzima katikati Kanisa wa mbinguni na Kanisa wa hii inchi.

**a) «Itakuwa furaha katika mbingu juu ya mwenye zambi mumoja anayetubu.. . » (Luka 15, 7).**

**b) « Mapendo hayapunguki hata kidogo.. . »(barua ya kwanza kwa wa Korinto 13, 8),** nikusema wala na kisha lufu.

**c) «Na wakati alipofungua muhuri wa tano, nikaona chini ya mazabahu nafsi zao waliouawa kwa ajili ya Neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. Wakalia kwa sauti kubwa, wakisema: .. . » wenye wanaomba toka Mungu uhaki, kwa ajili ya wafukuzo ya Wakristu pa hii inchi (Ufunuo 6, 9-11).** Ni tena kweli ma nafsi haya ya washuhuda watakatifu wamuombe kwa Mungu juu ya hawa Wakristu wanaishi tena pa hii inchi.

**d) «Na malaika mwingine alikuja akasimama mbele ya mazabahu, mwenye chungu cha zahabu; akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya mazabahu ya zahabu iliyo mbele ya kiti cha ufalme. Na moshi wa ule uvumba ukapanda mbele ya Mungu pamoja na maombi ya wataaktifu toka mukono wa malaika» (Ufunuo 8, 3-4).** Hii maandiko inatwaambia ya kama maombi ya «wataaktifu wote», nikusema ya waaminifu, wenye muzima na wenye kufa, yanapanda pamoja mbele ya Mungu.

## 2. MAOMBEZI YA WATAKATIFU

Kwani, basi, watu watakatifu ni marafiki ya Mungu na wanaishi karibu ya Mungu na wanachunga moyo na zamiri yao, kiisha lufu yao, kwa hivyo Kanisa yetu Takatifu inaomba sala yao. Washuhuda wa Yehova wanatuchukia pa hii fasi ya fundisho mukusema ya kama «Mupatanishi katikati ya Mungu na watu ni mumoja, yule mutu Kristu Yesu»(barua ya kwanza kwa Timotheo 2, 5); kwa hivi, katika akili yao, sisi tusipashwe kuomba saidio ya Watakatifu kwa sala yetu, (kwa sababu hivi tunazarau na tunasimamisha upatanishi ya Kristu).

Mukujibu kwao, tunasema ya kama, kama tunaomba saidio ya watakatifu wetu, hatutupe upatanishi ya Kristu, kwani watakatifu wetu wanaomba kwa jina ya Kristu mbele Yake na kwa saidio na wokovu wetu. Sala yao (upatanishi) inatumika paka hii upatanishi umoja na wa pekee ya Kristu. Kama sala ya watakatifu mbele ya Mungu kwa saidio yetu inazarau na inatosha upatanishi ya Kristu, basi, hii umoja itakuwa kufanyika na wakati Mukristu moja anaomba masalio ya mukristu mwingine. Lakini Madiko Takatifu inajaza na mifano ya watu watakatifu, wenye, ila tu sala yao kunyoloka kwa Mungu, waliomba na watu wengine waombe kwa saidio yao, bila kuogopa ya kama na hii namna wanazarau na wanafukuza upatanishi ya Kristu:

**1) «Kuomba kwake mwenye haki kuna faida sana.. . » (Yakobo 5, 16).**

**2) «Kirini zambi ninyi kwa ninyi na kuombeana, mupate kuponyeshwa.. . », «Ndugu, mutuombee» (Yakobo 5, 16) (barua ya kwanza kwa wa tesalonika 5, 25 na ya mbili kwa wa Tesalonika 3, 1)**

**3) «Na ninawasihi ninyi, ndugu kwa Bwana wetu Yesu Kristu, na kwa mapendo ya Roho, mudumu pamoja nami kwa maombi yenu kwa Mungu kwa ajili yangu. niokolewe kwa watu wasioamini katika Yudea; na utumishi wangu nilio nao katika Yerusalema ukubaliwe kwa watakatifu; » (Wa Roma 15, 30-31).**

**4) «Siachi kuleta asante kwa ajili yenu, nikiwataja ninyi katika maombi yangu; » (Wa Efeso 1, 16).**

5) **«Mutu akiona ndugu yake anatenda zambi isiyo ya mauti, ataomba, na Mungu atamupa uzima kwa ajili ya hawa wanaotenda zambi isiyo ya mauti» (barua ya kwanza ya Yoano 5, 16).**

6) **«Basi, Petro alilindwa katika kifungo; lakini kanisa walimwombea kwa Mungu pasipo kuchoka» (Matendo 12, 5-12).**

7) **«Lakini pamoja na maneno haya, unitengenezee pahali pa kukaa, -anasema Mutume Paulo kwa Filemono- maana ninatumaini ya kuwa kwa maombi yenu mutanipata kwenu» (Filemono, 22).**

8) **«Basi sisi ni wajumbe kwa ajili ya Kristu, ni kama Mungu anasihi kwa vinywa vyetu, tunawasihi ninyi kwa ajili ya Kristu, mupatanishwe na Mungu) (Barua ya mbili kwa wa Korinto 5, 20).**

-Paka na hii maana Mutume Paulo anapatia kwa maugo yake hali yake sawa «mwokozi»: **«Kwa wenye zaifu nilikuwa zaifu, nipate wazaifu. Nimekuwa vitu vyote kwa watu wote, hata kwa njia zote nipate kuokoa wengine» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 9, 22).** Lakini kwa sababu anaita maugo yake sawa «mwokozi» anasimama na anazarau hali ya Kristu sawa Mwokozi? Hapana; anaokoa Mtume Paulo paka na maana ya kama anaongoza watu kwa Kristu Mwokozi wa pekee. Hii kazi wanafanya na watakatifu katika maombezi yao.

Sawa vile maombi ya Wakristiani kwa wakriatiani wengine hayazarau na hayasimamisha upatanishi ya Kristu, vile na maombezi ya watakatifu hayasimamisha upatanishi ya Kristu, lakini yanafanyika kwa Jina ya Kristu na katika uwezo ya upatanishi Yake.

Mifano mengi ni ndani kabisa mu Kitabu ya Agano la Kale. Kule, katikati ya matendo ingine wanaomba na malaika (Zakaria 1, 12-13), tena na Nabii Yeremia anafananishwa ku Mungu sawa «mupatanishi» (Yeremia 7, 16).

## 3. MIUJIZA YA WATAKATIFU

Washuhuda wa Yehova wanakataa ya kama yanafanyika miujiza kisha lufu ya Mitume. Ndani ya Vitabu vyao wanaandika hivi: «Sawa vile iliisha andiko ya vitabu ya Madiko Takatifu, vile vile iliisha ya kushuka uwezo kwa kumaliza alama na miujiza. Ma alama na miujiza haya yalijipatia juu ya kuonyeshwa ya kama huu Dini wa Kristu ilitokea toka Mungu. Mitume kumi na wili walikuwa na hii uwezo wafanye matendo wa ajabu, na tena waliweza kuipatia hii uwezo wao na kwa watu wengine kwa kuweka mikono yao pa kichwa ya wale watu walipokea hii neema ya Mungu. Wakati walikufa Mitume na wafwasi wao, ilipotea na hii uwezo kimungu ya kufanya miujiza. Ndiyo, sasa hakuna tena zawadi ya uponyesho, ya kufufuka wafu.. . matendo haya yaliondoshwa katika mustari ya barua ya kwanza kwa wa Korinto 13, 8, 10).

Fundisho ya mustari ya barua ya kwanza kwa wa Korinto 13, 8, 10) haiseme «yaliondoshwa» lakini inasema: «yataondoshwa» nikusema nyakati ya ku mbele. Toka hii mustari inaonekana safi ya kama hii kazi itakuwa mu zima ingine, mu uzima wa milele, hile wakati itakuja «ukamilifu» na hile wakati tutaona utukufu wa Mungu «uso kwa uso» (13, 9-12). Tena mara ingine Washuhuda wa Yehova wanaonyeshwa ya kama hawaogope ya kuharabisha mafundisho ya Madiko Takatifu.

Bwana Yesu Kristu anatwaambia ya kama iko namna kumaliza miujiza watu watakatifu mupaka mwisho ya hii dunia:

1) «Kweli, kweli, ninawaambia ninyi, Yeye anayeniamini mimi, kazi ninazofanya yeye atazifanya vilevile; na atafanya kazi kubwa kuliko hizi; kwa sababu ninakwenda kwa Baba yangu» (Yoano 14, 12). katika neno: «kazi» tunapashwa sisi kuwaza kila tendo na miujiza inayefanyika katika uwezo ya Mungu. (Tazama na Yoano 7, 21-23 na 15, 24).

2) «Na alama hizi zitafuatana nao wanaoamini; kwa jina langu watatokeza pepo; watasema kwa lugha mpya. Watasikia nyoka; kama wakikunywa kitu cha kufa hakitawazuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya» (Marko 16, 17-18). Hii mustari

inatwaambia ya kama miujiza yatakuwa ma siku zote, kama weko waaminifu, nikusema mupaka mwisho ya milele.

# 15

# MA PICHA (IKONE) MATAKATIFU NA USUJUDU KATIKA SIFA YAO

## 1. NI KWELI YA KUFATULA MA USO YAO

Ufundi ya kufatula ma picha (ikone) ya Watakatifu ni kazi kimoja upendwa kabisa ndani ya Kanisa Orthodokse. Katika ma Ikone haya tunafatula Kristu na ma Uso ingine ya watakatifu tena na ma hema toka Madiko Takatifu. Ma Ikone weko na kikomo katika ragi ya kuachana kutujulisha kila fundisho Madiko Takatifu inatupatia na maandiko. Kwa mufano kufatula Uso ya Kristu ni kuhubiri wa kwanza ya fundisho wa kweli ya Dini wa Kristu: Ya kama **« Na Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, tukatazama utukufu wake.. . » (Yoano 1, 14).** Kama tunakataa kufatula Uso ya Kristu ni umoja ya kukataa fundisho hii ya Uso ya Kristu sawa Mutu na Mungu pamoja.

Washuhuda wa Yehova wanatimia ndani ya vitabu vyao ma hema wa dini, bila hata ushirika kimoja na ma ikone ya Kanisa yetu na bila ma hema haya yatupatia tangazo moja wa Mungu na Dini ya Kristu. Hawa wenyewe wanasema ya kama ikone moja inatuwaambia maneno elfu na tena ma Ikone «yanatusaidia kwa kutufundisha matendo filani». Lakini wanakataa utimio yao na usujudu yao na wanachukia waorthodoksi ya kama weko wapagano!

Kosa yao inatokea ya kama hawaweze kuachanisha alama ya Ikone na sanamu (nikusema mungu moja wa uwongo katika mbau ao njiwe ao na chuma). Shairi-bunduki yao ni amri ya mbili toka Dekaloge ya Mungu toka Agano la Kale:

**«Usijifanye sanamu mingine ya kuchonga, wala wa kitu kilicho mbinguni juu, wala duniani chini wala ndani ya maji chini ya dunia; usijiiname mbele yao kuzitumikia; kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu; nikipatiliza wana uovu wa baba zao, hata kizazi cha tatu ao cha ine cha wale wanaonichukia» (Kutoka 20, 4-5).**

**1)** Toka amri ya Dekaloge inaonekana safi ya kama inakatazwa kuabudu ma sanamu, nikusema ma uso na miili ya wa mungu wa uwongo, yenye waliiabudu sawa wa mungu watu wapagano. Kwa hivyo, kidogo chini iko ufafanusho hii: **«Musifanye pamoja nami miungu mingine; musijifanyize miungu ya feza, wala miungu ya zahabu» (Kutoka 20, 23).** Kupindua, ma Ikone (Picha) ya Kanisa wa Kristu si wana ushirika kimoja na ma sanamu. Nikusema haiko sanamu ya miungu, lakini paka ni ma Picha ya watu watakatifu, wenye walitumika kwa Mungu na sisi tunawasujudu na hapana kuwabudu.

**2**) Mu Kitabu ya Agano la Kale: Kumbukumbu ya Torati Mungu mumoja anaelejea ya kama hii amri iko na kikomo ya kuzibiya watu wa Ebrania juu hapana kufanya ikone ao sanamu ya Mungu wa kweli, kwa sababu hawakumuone Uso yake hata mara moja. Paka waliisha kusikia sauti Yake pa Mulima Sinaya. Basi, kila ikone ao sanamu walipenda kuifanya, itakuwa moja «sanamu», uso moja wa uwongo ya Mungu na katika uwazo ya akili yao, lakini hii tendo yao itakuwa umoja na dini ya kuabudu ma sanamu: «Bwana akasema nanyi kutoka kati ya moto: Mukasikia sauti ya maneno, lakini hamukuona sura yo yote: Lakini mukasikia sauti tu. Akawajulisha ninyi agano lake alilowaamuru ninyi kulitenda, hata zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe. Bwana akaniamuru waakti ule niwafundishe ninyi amri na hukumu, ili muzitende katika inchi munayoivukia ili mwiriti. Basi, mwangalie sana nafsi zenu, maana hamukuona sura ya namna yo yuote kwa siku Bwana aliyosema nanyi kutoka kati ya moto;

Musiharibu nafsi zenu na kujifanyia sanamu ya kuchonga, mufano wa sura yo yote, mufano wa mwanamume ao mwanamuke» Kumbukumbu 4. 12-16)

**3)** Neno ingine kwa ajili yake ilikatazwa hii amri, ilikuwa ya kama watu wa Ebrania waliishi pempoeni na mataifa wenye pagano na ilikuwa namna teketeke kutelemuka kwa dini ya wa sanamu, kwani ilifanyika hii mambo na zamani mara mengi. Kwa hivyo Mungu alikuwa mukali sana ya hii mambo ya dini na alikataza kila tendo inayefanana na sanamu, nikusema sanamu ya mungu wa uwongo. Kupindua, kama haikukuwe hatari ya dini wa sanamu, Mungu alibariki tena alihamuru kufanya watu ma picha ya kufatula. Kwa mufano:

**a)** Wakati Mungu alimupatia kwa Nabii Musa hii amri wa yulu ya kukataza kujenga ma sanamu ya miungu, alimupatia na amri ingine juu ya kufanya ma Kheruvim wa wili katika miili yao toka zahabu na atawaweka pa Altari Takatifu, ndani ya Matakatifu ya Watakatifu ya «Sanduku ya Agano» (nikusema hekalu wa kwanza ya taifa wa Israeli, mbele ya majengo ya hekalu ya Solomono (Tazama Kutoka 25, 17-22).

**b)** Wakati ilikuwa lazima kuweka «Mapazia ya hema Takatifu» juu ya kuachana hekalu ku «Matakatifu ya Watakatifu» Mungu alihamuru mara ingine Nabii Musa ya kuweka pa hii fasi miili ya Wakheruvim (Tazama 26, 1, 31).

**c)** Tena Mungu alimuhamuru Nabii Musa kufanya nyoka moja ya shaba na hu nyoka alikuwa na uwezo wa muujiza na alipona watu wa Israeli toka kulumiza ya ma nyoka waliyokuwa na sumu (Tazama Hesabu 21, 8-9).

**d)** Kisha wakati ingine ku mbele, wakati Solomono alijenga Hakalu kubwa mu Yerusalema, aliijaza na miili ya wa Kerubi wa wili ya muzeituni, na ma picha ingine, bila amri ya Mungu (Tazama 1 Wafalme 6, 23-35). Mungu hasikusikitike kwa hii kazi ya Solomono, lakini alionyesha furaha na shukrani Yake (! Wafalme 9, 3).

Kwa ajili ya mafundisho haya yote wa yulu tunakikiri ya kama ukatazo hile ya Dekaloge ilikuwa paka ya ma sanamu ya miugu wa uwongo na kazi ya kuwabudu yao. Basi, kama haikukuwe mambo ya «sanamu» lakini paka mambo ya ma hema ya kufatula, bila yakuabudu, paka yaliisifu, amri ya Dekaloge haikukuwe na nguvu.

**4)** Washuhuda wa Yehova halafu, ma fasi ingine wanakataa ao ma fasi ya mafundisho yao, ndani ya vitabu yao vingine wanaitika na sisi. Kwa mufano, mu Kipindi yao: Ulinzi (Skopia) ya 1-2-1981 wanaandika: «Ma ikone yote si weko ma sanamu: Sanamu moja ni ikone moja, ao hema ya hadishi moja ao alama moja ile ni kitu ya kuiabudu.. . Lakini sheria ya Mungu juu ya ukatazo ya kujenga ma ikone, haikukataze kufanya na ma hema na ma sanamu.. . »

**5)** Tena wanaita shairi ya Nabii (Isaya 44, 9-20), pahali inasemwa ya kama toka muti umoja mutu anapata moto, anafanya mukate yake na anafanya na ma «sanamu» na «miungu»: «Wao wanatengeneza sanamu za kuchonga, wote ni ubatili; na maneno yao yote hayafai kitu; nao ni washuhuda wao wenyewe: Hawaoni wala hawajui, hata wapate haya.. . . . . Nimechoma sehemu yake kwa moto, na nimepika mukate vile juu ya makaa yake, nimeoka nyama, na nimeikula, na sehemu iliyobaki nitafanya kuwa chukizo? nitaanguka mbele ya kipande cha muti? Anakula majivu; moyo wa kudanganya umemugeuza kando, asiweze kuokoa roho yake, wala kusema: Uwongo si katika mukono wangu wa kuume? »

Vile tunafika mu wakati ya Agano Jipya. Hapa Kanisa wa Kristu katika ma hema na ma alama na ma Ikone haifanye kitu kingine, paka hile kazi aliifanya zamani Nabii Musa na ma Kerubi wa zahabu ao Solomono aliyejaza Hekalu yake mu muji Yerusalema na ma hema na ma Kerubi.

**1)** Mu Kanisa wa Kristu ma Ikone (ma Picha) hayajiabudu, sawa ilikuwa hii mambo zamani katika ma sanamu, kwani ma Ikone si weko ma sanamu ya miungu wa uwongo, lakini ni ma uso ya watu watakaitfu, wenye walimufurahisha Mungu katika maisha yao na sisi tunawasifu

sawa warafiki ya Mungu na hapana tunawaabudu sawa miungu. Kanisa yetu, katika fundisho ya kweli ya Makutano Mkubwa wa Saba inatufundisha hivi: «Sifa inatembea toka ikone kwa hule Mutakatifu ni uso yake pa hii ikone». Uhai na usujudu ya ma Ikone mu Kanisa Orthodokse haina hata ushirika kimoja na ma sanamu na dini ya wapagano wa zamani. Tena hii amri ya Dekaloge hana na nguvu kimoja mbele ya usujudu ya ma Ikone yetu mu Kanisa Orthodokse, kwani wa Ortodoksi wanasifu ma Uso ya watakatifu katika ma Ikone yao, kwa ajili ya heshima na mapendo na hapana kuwaabudu ma ikone yao.

**2)** Katika mafundisho haya inazeonekana kufatula miili na ma uso ya watakaitu wetu, tena na Uso ya Bwana Yesu Kristu, aliyekuwa mutu na Mungu na alitimiza tendo ya wokovu ya watu. Kwani alichukua mwili na uso sawa mutu, sawa sisi, bila zambi, sisi tunaweza kumufatula uso na mwili yake ma nguo moja ao mbau, kwani na yeye alikuwa mutu na tuliona sura yake. Kama tunafatula uso Yake, hatufatule hali kimungu yake, lakini paka hali kimutu Yake, kwani alichukua hali ubinadamu na «Neno lililokuwa tangu mwanzo, tulilosikia, tulioliona kwa macho yetu, tulilolitazama na kulipapasa kwa mikono yetu, kwa habari za Neno la uzima» (barua ya kwanza ya Yoano1, 1). Basi, kama tunafatula Kristu, tusikanyanga amri ya Mungu, lakini tunakikiri ya kama Kristu ya kweli alikuja sawa Mutu hapa duniani na Huyu ni Mwana na Neno wa Mungu.

**3)** Tena Washuhuda wa yehova wanatushitaki ya kama tunasema ya kama ma Ikone mengi yanafanya miujiza na tunayasifu sawa vitu vitakatifu, lakini ma Ikone ni paka mbao na ragi. Tunawajibu: Vitu vyote yenye ni ndani ya Kanisa ya Mungu inapashwa kuyaona sisi sawa vitakatifu na yatakaswa. Kristu mumoja alisema ya kama hekalu ya Solomono alitakasa zahabu hile ilikuwa ndani yake (Matayo 23, 15-17). Basi, kama hule hekalu isiyokamilifu ya Agano la kale alitakasa vitu vyake visiyouzima, ngapi kupita mingi hekalu ya Agano Jipya inapashwa kutakasa vile vitu ni ndani yake!

**4)** Juu ya hii mambo ya kama ma Ikone ya kuachana Mungu aliyapatia uwezo yafanye miujiza hii inatuonyesha ya kama Mungu anafanya miujiza Yake na katika ma Ikone ya Watakatifu na vitu ya kuachana. Kwa mufano: Fimbo ya Musa (Kutoka 4, 2-3), Nyoka wa shaba (Hesabu 21, 8, Fimbo ya Haruni (Hesabu 17, 1-11), «Vitambaa na nguo zilizogusa mwili wake.. »ya Mutume Paulo (matendo 19, 11-12), kimvuli ya Mtume Petro (Matendo 5, 12-16). Basi, juu ya nini tunapashwa kukataa ya kama Mungu, kama anataka, anaweza kufanya miujiza na katika Ikone (picha) kimoja? Ufamio na maarifa ya wakristiani wetu wote wa Orthodoksi katika milele yote mpaka sasa inatupatia haki na hapana kwa washuhuda wa Yehova, kwani kwa ajili ya imani yao Mungu na Watakatifu wetu waliwafanyisia miujiza mengi.

**5)** Washuhuda wa Yehova wasasema tena, hata kama ma Ikone si weko ma sanamu na paka ma alama manyofu, yanakatazwa kwani mu Agano Jipya Mungu anajiabudu paka «katika roho na ukweli» (Yoano 4, 24). Tunawajibu: Kuabudu ya Mungu katika roho na ukweli haifanye kitu kwa ajili ya uhai ya ma Ikone, wala kwa ajili ya uhai ya Madiko Takatifu. Kwa sababu Madiko Takatifu haina na huu alama moja ya neno ya Mungu? Nikusema ma herufi ya Alfabeti haina ma alama ya ma sauti ya ulimi ya kila mutu. Basi, Washuhuda wa Yehova, kama wanataka kufuata fundisho yao, wanapashwa kukataa ya kwanza kila alama, ama ni ma herufi ya Alfabeti, ama ni ma ikone. Lakini Mungu alilaka katika ma Nabii Yake ya kama Agano Jipya Yake katika Mwokozi Kristu haitaandikwa na ma herufi yas Alfabeti, sawa zamani Agano la kale katika nabii Musa, lakini itaandikwa ndani ya roho ya waaminifu katika Roho Mutakatifu (Wa Ebrania 8, 10. 10, 16. Yoano 6, 45. 14, 26. Barua ya kwanza ya Yoano 2, 20, 27 na barua ya mbili kwa wa Korinto 3, 6).

Sawa vile katika ma herufi ya Alfabeti inakuwa neno ya kuandikwa ya Mungu (Madiko Takatifu) na katika ma herufi haya inaonekana neno ya Mungu «ni hai, lenye nguvu na ukali kupita ukali wa upanga unaokata ngambo mbili.. . » (Wa Ebrania 4, 12) na haina kitabu isiyo pumuzi; hivi na ma Ikone matakatifu yanatuonyesha neno ya Mungu, lakini hapana na ma herufi ya Alfabeti, lakini katika ma ragi na ma uso ya watu watakatifu.

## 2. USUJUDU HESHIMIWA YA MA IKONE (MA PICHA)

Washuhuda wa yehova na Waprotestante wanatushitaki ya kama sisi Waorthodoksi kwa kusujudu ma Ikone tunaabudu vitu yasiyoroho na vile tunakuwa wenye pagano, lakini sisi tunawajibu ya kama tukona masujudu wa mbili: Ni Usujudu ya kuabudu na inajitoa paka kwa Mungu na usujudu heshimiwa, wa sifu inayejitoa kwa kila mutu na mutakatifu. Kwa kubusu sisi waorthodoksi ma Ikone, tusisujudu na namna ya kuabudu (kwani hivi tutakuwa wa pagano), lakini tunaonyesha sifa na heshima mbele ya ma Uso ya Watakatifu wetu. Madiko Takatifu ni ya kujaza na mifano ya hii sifa na usujudu ya watu mbele ya watu wa Mungu. Kwa mufano:

**1) Abrahamu akasimama, akajinama kwa watu wa inchi, hata kwa wana wa Heti» (Mwanzo 23, 7-12).**

**2) Naye (Yakobo) mwenyewe alivuka mbele yao, akajiinama kwa udongo mara saba, mupaka alikaribia ndugu yake». Vile walifanya na wanawake wake Lia na Lakeli pamoja na watoto wao (Mwanzo 33, 3-7).**

**3) Wakati Yesua wa Navi alikuwa mu muji Yeriko, aliona mbele yake malaika ya Bwana, aliyemwaambia: «Sasa nimefika kama kapiteni ya jeshi la Bwana. Yosua akaanguka kwa uso wake kwa udongo, a k a a b u d u, akamwambia: Bwana yangu anasema nini kwa mutumishi wake? Kapiteni ya jeshi la Bwana akamwambia Yosua: Ondosha viatu vyako kwa miguu yako, kwa kuwa pahali unaposimama ni patakatifu, Yosua akafanya hivi» (Yosua wa Navi 5, 13-15). 4) «Daudi akamwambia Saulo: Kwa nini unasikiliza maneno ya watu wanaosema: Tazama Daudi anatafuta kukuumiza? » (1 Samweli 24, 9).**

**5) Nabii Natana, wakati alipoingia ndani mbele ya mufalme, akaanguka kifudifudi mbele yake.. . » (1 Wafalme 1, 23).**

**6) «Na kusanyiko lote ((taifa) wakabariki Bwana, Mungu wa baba zao, wakainamisha vichwa vyao, na kuabudu Bwana, na mufalme (Daudi)» (1 Mambo ya siku 29, 20). Wanamuabudu Mungu katika namna ya kwanza: (kwa kuabudu) na mufalme Daudi katika namna ya mbili: katika heshima na sifa mbele yake.**

**7) «Basi mutumishi mwenzake akaanguka na kumusihi akisema: Univumilie, na nitakulipa yote» (Matayo 18, 23-29).**

**8)** Kristu anasema kwa «malaika» (askofu) ya Kanisa ya Filadelfia: **«Tazama nitakupa wale wa sunagogi la shetani wanaosema wao ni Wayuda, nao sio, lakini wanasema uwongo. Tazama, nitawafanya waje kuabudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda wewe» (Ufunuo 3, 9).**

Ni mifano na ma hadishi mengi ndani ya Madiko Takatifu yanatuonyesha usujudu katika sifa, lakini inenea maneno haya wa yulu na wale watu wekona akili nzuri na mapenzi nzuri watasikia na wataona ya kama ni kitu ingine ya kuabudu Mungu na namna ingine ni ya kusifu Watakatifu.

Pa hii fundisho Washuhuda wa Yehova wanaita mistari yao ingine: Ni mistari haya:

**1) Mweshimiwa Mordekayi alikataa kusujudu Hamani mutu wa pagano, mukubwa ya mufalme wa inchi Persia jina lake Ahasuero. (Esiteri 3, 1-2).**

**2) Mutume Petro alikataa kupokea usujudu ya Kornilios, akiba wa Roma (Matendo 10, 25-26). Na**

**3) Malaika ya Ufunuo, aliyekataa kupokea usujudu ya Mtume Yoano, aliyemuonyesha vitu vyote yatakuwa ku mbele (19, 10).**

Pa mistari wa tatu wa yulu yanaita Washuhuda wa Yehova sisi tunajibu hivi:

a) Hii usujudu anaomba Hamani ilikuwa umoja na usujudu ya kuabudu, iliikuwa hile wakati, kwani ma taifa walikuwa na zoezo kutoa kuabudu mbele ya wafalme na wakubwa wao. Kwa hii mambo na Mordekayi alikataa kumuabudu Hamani. (Esiteri 4, 17e).

b) Hii usujudu alifanya Kornilio mbele ya Mtume Petro ilikuwa umoja ya namna ya kuabudu, kwani Kornilio alikuja toka watu wa pagano na alimuona Petro, kupatana na ono kimungu hile aliiona, sawa uhai kimungu. Kwa hivyo Petro alienda na haraka amuwaambie na amuelejee ya kama «Simama, mimi vile mutu tu» (Matendo 10, 26).

c) Ku mwisho, pa hile mustari ya Ufunuo inaonekana ya kama Yoano alizania ya kama malaika alikuwa Kristu, aliyesuburia na ye ku mwanzo ya ono kimungu (1, 17). Kwa hivyo zaidi malaika anakwenda mbio amuelejee ya kama «Angalia usifanye hivi; mimi ni mutumishi mwenzako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu.. . » (Ufunuo 19, 10).

## 3. MIFUPA MATAKATIFU YA WATAKATIFU

Juu ya mafundisho ya Mifupa Matakatifu tunasema ya kama, kwa sababu mwili yetu ni hekalu ya Roho Mutakatifu (barua ya kwanza kwa waKorinto 6, 19), ni kweli ya kama Neema Kimungu inaendelea kuikaa na kisha lufu ndani ya Mifupa ya wale wakritu waliyekuwa wenye kujaza na Roho Mutakatifu. Sasa tunaweza kuandika juu ya Mifupa Matakatifu ya nabii Elisa, yenye yalifufulia mufu moja (2 ya Wafalme 13, 20-21): «Elisa akakufa, nao wakamuzika. Basi vikosi vya Wamoabu wakaingia katika inchi mwanzo wa mwaka. Na ilikuwa, waakti walipokuwa wakizika mutu, tazama, waliona kikosi; wakatupa yule mutu katika kaburi la Elisa; na wakati yule maiti alipogusa mifupa ya Elisa, alifufuka, akasimama kwa miguu» (2 Wafalme 13, 20-21).

Sawa vile, basi, mu wakati ya Agano la Kale, vile na leo, mu nyakati ya Kristu, Mifupa ya Watakatifu wa Mungu yanaendelea kuwa na Neema Kimungu na mara mengi katika mapenzi ya Mungu, yanakuwa miujiza kwa wale waaminifu weko na imani nguvu na wanaomba saidio yao.

Hapana paka Mifupa ya watu watakatifu, lakini na vitu vyao, yaliyojaza na Neema kimungu iko namna kufanya miujiza. Kwa mufano:

1) **Fimbo ya Nabii Musa, iliyekuwa nyoka (Kutoka 4, 2-3) na kisha ilikata katikati bahari Nyekunda (14, 16).**
2) **Ngozi ya Nabii Elia, aliyepika naye maji ya mutoni Yordani na maji ilisimama na ngambo moja na ngambo ingine na walipita kati Elia na Elisa (2 Wafalme 2, 8).**
3) **Waaminifu wengine waligusu manguo ya Kristu na waliponyeshwa (Matayo 9, 20. 14, 36 na Marko 5, 27. 6, 56 na Luka 8, 44).**
4) **«KItambaa na manguo ya Mutume Paulo watu waliyaweka yulu yao na waliponyeshwa (Matendo 19, 11-12).**
5) **Tena na kivuli ya Mtume Petro ilipona wagonjwa (Matendo 5, 12-16).**

# 16
# MUSALABA MWESHIMIWA

Washuhuda wa Yehova wanakataa Musalaba Mweshimiwa. Wanasema ya kama hii alama tunaitimia sisi wa Kristiani ni alama wa pagano na mufalme mkubwa mtakatifu Konstantinos aliileta sawa alama ya dini wa Kristu mu milele wa ine. Tena wanasema ya kama Kristu hasisulubiwe pa alama ya musalaba, lakini pa muti moja. Lakini kwa hii fundisho Washuhuda wa Yehova zamani walisadiki fundisho ingine na kisha wakati fulani wanasadiki fundisho ingine.

Nikusema mpaka ku mwaka 1931 Musalaba ilikuwa alama ya Kundi yao na yule yake ilikuwa na taji moja. Lakini huu mwaka (1931), wanasema, ilikuja nuru mupya, nuru mingi toka Yehova ndani ya vichwa ya wakubwa wao na walikamata mpango kufundisha kwa waaminifu wao ya kama Kristu hasisulubiwe pa Musalaba, lakini pa muti moja. Tangu hile mwaka wanagombana sana alama ya Musalaba.

Lakini na Yosefu Roderfont, mukubwa ya kundi yao, mu mwaka 1931 aliandika: «Musalaba ya Kristu ni kitu kikumbwa ya ukweli na ya vitu vitakatifu na kwa huu musalaba inatokea matumaini ya watu wote».

Sasa tunajibu mbele ya machukizo ya Washuhuda wa Yehova:

**1)** Hile wakati aliishi Kristu taifa wa Roma walikuwana namna ya kuua watu wakosefu usulubisho na walitimia sawa musalaba alama hii: **+** ao alama ya namna **T.** Kwani Kristu alisulubiwa pa musalaba na namna **+** inashuhuda Mapokeo Takatifu na Madiko Takatifu: Inasema nikusema, Madiko Takatifu ya kama, wakati walisulubisha Kristu, «Wakaweka juu ya kichwa yake mashitaki yake yaliyoandikwa: HUYU NI YESU MUFALME WA WAYUDA» (Matayo 27, 37). Ni kweli ya kama juu ya kuwekwa mbau na maneno ya usulubisho Yake pa kichwa chake, hii inatuonyesha ya kama Kristu alisulubiwa pa Musalaba na namna **+.** Lakini, kama Kristu alisulubiwa pa muti na namna hii: T mbau na maneno ya usulubio yake ilipashwa kuwekwa yulu ya mikono yake, lakini Agano Jipya inaandika ya kama iliwekwa pa kichwa chake, sawa vile inaonekana muzuri na pa picha ya mwisho mu ukurasa:

**2)** Kama Kristu alipingiliwa pa muti moja, basi, mikono Yake wa wili yalipashwa kupingiliwa pamoja na musumari moja, nikusema mukono moja pa mukono ingine. Lakini, Mutume Thomasi, kisha Ufufuo ya Kristu, anaomba kuona mikono ya Kristu «alama ya misumari) na hapana «alama ya musumari-(moja)»; hii inatuonyesha ya kama mikono ya Kristu yalipingiliwa kimoja ya kuachana na kingine na hii mambo inawezekana kufanyika paka pa musalaba (Yoano 20, 25).

**3)** Lakini na ma Kamusi ya mbali-mbali yanatukikiri ya kama alama wa zoezo ya musalaba ni hii sisi Wakristiani tunaitimia: Kwa mufano Kamusi ya lugha Kigreki: Papiros Larus inaelejea ya kama ni nini Musalaba: **«Musalaba ni alama na ma mbao wa wili wanaungana katika yao; ni namna ya kuua watu wakosefu na huyu mukosefu walimuweka juu yake na mikono yake ya kuwa kufunguliwa».**

**4)** Mbele ya imani ya Washuhuda wa Yehova, wenye wanasadiki ya kama, mbele ya milele wa inne huu alama ya musalaba isikufamiwa mu Kanisa, sisi tunajibu ya kama ndani ya ma nyumba chini ya inchi-bulongo, mu muji Roma (hawa ma nyumba yanaitwa katakombe) na ma fasi ingine ni musalaba pa kibabashi yao tangu miaka wa Kwanza ya Dini ya Kristu. Tena na Wandishi wa Kanisa wanakikiri ya kama musalaba ilitimiwa tangu miaka wa kwanza ya Kanisa ya Kristu. Kwa mufano Mwandishi ya Kanisa jina lake Tertilianos (150-200) kisha uzalio ya Kristu anaandika hivi: «Sisi wa Kristiani kwa kila safari na matembeo yetu, kwa kila ondoko na urudisho, wakati tunavaa manguo na vilato vyetu, waakti tunaenda kunawaao pa meza ya kula, wakati tunawaka moto ya nyumba yetu, wakti tunaikaa ao tunalaria na kwa kila kazi na matendo ya uzima yetu tunafanya alama ya Musalaba.. . Hii Kutimi iko na mwanzo yake mu Mapokeo Takatifu ya Kanisa, ilikuwa nguvu katika zoezo na inapashwa kuichungwa na imani». Na Wandishi wengine ya Kanisa wa Kridtu wa zamani, sawa Kiprianos, Laktantios, Klimis wa muji Aleksandria, Origenis na «Matendo wa siri ya Mtume Yoano» na ingine yanatukikiri ya kama ilikuwa zoezo Wakristiani wafanye alama ya Musalaba pa sura yao na huu zoezo ilikuwa ya kufamiwa tangu milele wa mbili (tangu ku mwaka 150, kisha uzalio ya Kristu).

**5)** Mbele ya mashitaki ya Washuhuda wa Yehova ya kama sisi wa Orthodoksi tunaheshimiwa alama moja wa pagano, tunawajibu ya kama sisi hatuna na mafaa, wala ni kikomo wa nani waliitimia musalaba, mbele ya Kristu. Kikomo na jabo wa kwanza ni ya kama juu yake alisulubiwa Kristu kwa ajili ya wokovu wetu: Basi, huu ni kitu hile aliitimia Mungu kwa kutuokoa (Wa Efeso 2, 16 na Wakolosayi 1, 20). Hii ni alama ya wokovu wetu na sawa vile ni alama ya wokovu sisi tunaieshimiwa.

**6)** Tena Washuhuda wa yehova wanatushitaki ya kama haipashwe kusifu musalaba, kwani ilikuwa alama ya laana na hukumu na juu yake walitundika watu wenye zambi na wanyanganyi (Wa Galatia 3, 13). Sisi tunawajibu ya kama, tangu hile saa alisulubiwa juu yake Kristu, Mwana wa Mungu na alimwanga Damu Samani yake kwa wokovu wa dunia (Wa Efeso 2, 16), musalaba alitakaswa na ku alama ya mafigo ilikuwa alama ya baraka na wokovu. Vile, tangu hile wakati kila mwaminifu wa kweli anahubiri pamoja na Mtume Paulo: «Lakini mimi nisijisifu hata kidogo juu ya kitu ila musalaba wa Bwana wetu Yesu Kristu; kwa yeye dunia hii imesulibiwa kwangu, na mimi kwa dunia» (Wa Galatia 6, 14). Pa fasi ingine anasema ya kama Kristu alimutuma «kuhubiri Habari Njema: si kwa akili ya maneno, musalaba wa Kristu usifanyizwe kuwa bule. Kwa sababu neno la musalaba kwao wanaopotea ni upumbafu; lakini kwetu sisi tunaookolewa ni uwezo wa Mungu» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 1, 17-18). Hii sauti yetu na mustari ya Mtume Paulo, kama wanapenda washuhuda wa Yehova, waangalie muzuri, juu hapana kuhesabiwa katikati ya wenye kupotea ma adui ya musalaba wa Kristu, kwani mwisho yao ni uharibifu (Wa Filipi 3, 18-19).

Chuki ya Washuhuda wa Yehova ni hata munene mbele ya Musalaba ya Kristu, na ndani ya Madiko Takatifu yao pa hii fasi iliandikwa jina ya «musalaba», hawa waliikombola hii jina na jina: «muti ya mateso» (ao muti), na neno: «Kusulimbia» waliikombola na neno: «kutundika pa muti». Tunaandika kidogo chini mifano haya juu ya kusoma kila musomaji mupaka fasi gani inafika mambo ya kucheka mbele ya akili upumfafu yao:

**1) «Naye asiyechukua musalaba wake na kunifuata hanistahili» (Matayo 10, 38). Mu Madiko yao inaandikwa: «Naye asiyepokea m u t i. y a m a t e s o yake na asiyenifuata.. . ».**

**2) «.. . Wakamuchukua inje ili wamusulibishe. Walishurutisha mutu aliyepita akitoka mashamba, Simoni Mukurene.. . ili achukue musalaba wake.. . Wakamusulibisha.. . Pamoja naye wakasulibisha wanyanganyi wawili.. . » (Marko 15, 20-32).**

Hawa ndani ya Madiko yao wanaandika: «Na walimuongoza inje juu ya k u m u t u n d i k a. pa muti. Na walishurutisha.. . Simoni Mukurene.. . , kwa kunyanya m u t i. y a. m a t e s o. . . Na, wakati walimutundika.. . Pamoja naye walitundika pa muti na wanyanganyi wa wili.. . ».

**3) «Naye (malaika) aliwaambia: Musishangae, munatafuta Yesu wa nazareti aliyesulibiwa; . . . » (Marko 16, 6).** Mu Madiko yao wanaandika: **«.. . Munatafuta Yesu wa Nazareti aliyetundikwa pa muti; »**

**4)** Mutume Paulo anasema: **« Kwa sababu Kristu hakunituma kubatiza, lakini kuhubiri Habari Njema: si kwa akili ya maneno, musalaba wa Kristu usifanyizwe kuwa bule» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 1, 17).** Hawa mu Madiko yao wanaandika: «Kwa sababu Kristu alinituma, hapana nibatize, lakini kuhubiri habari njema hapana katika akili ya maneno, muti ya mateso wa Kristu usifanyizwe kwa bure».

**5)** «Kwa sababu neno la musalaba kwao wanaopotea ni upumbafu; lakini kwetu sisi tunaookolewa ni uwezo wa Mungu.. . Lakini tunahubiri Kristu aliyesulibiwa.. . » (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 1, 18-23). Mu Madiko yao wanaandika: **«Kwa sababu neno la muti ya mateso ni upumbafu kwa wenye wanapotea, lakini kwa sisi tunaookolewa ni uwezo wa Mungu». «Lakini sisi tunahubiri Kristu aliyetundikwa pa muti.. . »**

**6)** Mutume Paulo anaandika: **«Lakini mimi nisijisifu hata kidogo juu ya kitu ila musalaba wa Bwana wetu Yesu Kristu; kwa yeye dunia hii imesulibiwa kwangu, na mimi kwa dunia» (Wa Galatia 6, 14).** Washuhuda wa Yehova wanaandika: «lakini mimi nisijisifu hata kidogo juu ya kitu ila ila muti ya mateso wa bwana wetu Yesu Kristu; kwa kila kitu kwa mimi na mimi mbele ya kila kitu wa dunia».

**7)** Mutume Paulo analia juu ya adui ya musalaba wa Kristu, kwani mwisho yao ni uharibifu (Wa Filipi 3, 18-19). Hawa wanaandika mu Madiko «Takatifu» yao: «.. . wenye wanatembea sawa adui ya muti wa mateso ya Kristu na mwisho yao ni uharibifu».

Tunazania ya kama mistari haya ni yakuenea. Ila ya Kitabu Madiko «Takatifu» yao mafafanusho katika hii roho inaonekana na ndani ya vipindi na vitabu vyao, lakini ndani wanapenda kuandika pahali pa neno: «muti ya mateso» wanaweka: «fimbo wa mateso». Kisha iko shaka katikati yetu ya kama adui wa Kristu ni wa nani? Si weko Washuhuda wa Yehova?

# 17

## FUNDISHO YA MAKUMBUSHO

Makumbusho ni onyesho ya mapendo yewtu watu wenye muzima mbele ya ndugu wenye kulala. Kupatana na hadishi ya mutajiri na Lazaro maskini (Luka 16, 19-31), nafsi ya wenye haki hile saa ya lufu inachukuliwa ku malaika na inaongozwa pa makao ya furaha: Mu Kifuo ya Abrahamu (katika Luka 16, 22, ao mu Yerusalem wa mbingu, pahali ma roho-nafsi ya wale waliisha uzima yao katika uhaki wanafanya shangilio na kanisa wa wenye kuzaliwa wa kwanza katika (wa Ebrania 12, 22-23). Kupindua, ma nafsi ya wasiyookolewa wanaingia mu Hadeze kwa kuwa katika mateso, (katika Luka 16, 23). Toka hii hadishi kila mutu anasikia ya kama, na pa fasi moja na pa fasi (makao) ingine nafsi inaishi, iko na mioyo na mahasa ya uzima wa huku na uzima wa milele.

Washuhuda wa Yehova wanakata kabisa Makumbusho, sawa vile wanafanya hivi na ma dini ya uwongo wote, yenye yalitokea toka Kundi ya Protestante. Lakini:

1) Hakuna shairi moja ndani ya Madiko Takatifu inayezibiya mukristu moja afanye sala juu ya nafsi ya waliyolala majirani na marafiki yake.
2) **Ukumbusho ni sala kwa wokovu na kwa hivi ni onyesho ya mapendo. Na mapendo wa kweli haionyeshwa paka kwa wenye muzima, lakini na kwa waliyokufa, kwani «mapendo hayapunguki hata kidogo» (barua ya kwanza kwa wa Korinto 13, 8).**
3) Hii kazi umoja anafanya na Mutume Paulo, hile wakati alisali juu ya mwenye kufa Onisiforo, mukuandika hivi: **«Bwana amupe kuona rehema kwa Bwana siku ile» (Barua ya mbili kwa Timotheo 1, 18).**
4) Hii kazi kimoja alifanya na Kanisa na ma nyakati yote tangu wakati ya Mitume, nikusema alisali kwa wenye kufa.
5) Tena hii kazi ya kusali walifanya na Wabrania hile wakati ya Agano la Kale:

**-«Wana wa Israeli walikuwa wamekusanyika wakifunga chakula, na wakivaa gunia.. . wakakiri zambi na kuabudu Bwana Mungu wao» (Nehemia 9, 1-3).** Hii neno: «wakakiri» ni umoja na maana ya kama waliungama na walisikia makosa yao na waliomba rehema toka Mungu.

Tena, haikukuwe Hukumu wa mwisho na malipo ya kila mutu, hile itafanyika kwa Kuja ya Mbili ya Kristu (Matayo 16, 27, 25, 31-46. Yoano 5, 28-29. Wa Ebrania 11, 39 na ma shairi ingine. Na, kwa sababu Kristu alitufundisha safi ya kama paka matukano mbele ya Roho Mutakatifu haisamehewa «wala ulimwengu wa sasa, wala katika ule unayokuja» (Matayo 12, 31-

32), inawezekana ya kama katika ma asili filani, usameha ya zambi ingine katika ule milele unayokuja, lakini mbele ya Kuja ya Mbili ya Kristu na Hukumu wa mwisho.

Usamehe ya zambi ya wafu katika maombi ya Kanisa inafanyika katika ma namna filani: Namna wa kwanza ni kama huyu mufu alikuwa mwaminifu na hasikukuwe adui ya Mungu na alipokea rehema kimungu. Lakini, kama hule mufu alikuwa mu uzima yake adui ya Mungu, alikufa bila toba, hata sala moja haitaweze kumusaidia. Tunafanya makumbusho sisi ya wafu wote na wenye uzima yote kwa sababu hatujue ma roho ya watu sawa anawafamia Mungu na kwa hivyo hatujue nani eko na roho muzuri na anapokea rehema ya Mungu na nani hapana.

Washuhuda wa Yehova wanakataa na wanaandika ma shairi-bunduki yao kupingana ya sisi:

**1)** Mu hadisi ya huler mutajiri na Lazaro maskini inaandikwa zaidi ya kama katikati ya wenye kuokolewa na wenye kwenda mu Gehena ni shimo kubwa na hakuna namna kwenda wala hawa mu fasi ingine na kupindua (Luka 16, 26).

Sisi tunwajibu ya kama ma nafsi hawaweze yenye wa pekee kutambuka hii shimo kubwa. kama Mungu anataka asikie masali yetu wenye muzima juu ya wale waliokufa, kwani HULE KRISTU ni Bwana mkubwa ya ma fasi yote na Huyu anakamata mafungulo ya lufu na hadeze (Ufunuo 1, 18) na Yeye eko na uwezo kurehema na ma nafsi haya.

**2) «Na sawasawa watu wanavyowekwa kufa mara moja, na nyuma ya kufa hukumu» (Wa Ebrania 9, 27).** Maneno haya ya Mtume Paulo yanatuwaambia ya kama wakati anakufa mutu moja, anahukumwa toka Mungu katika matendo yake ya hii uzima yake, anataguria kipimo matunda ya uzima yake mu Ufalme wa mbingu, sawa Lazaro maskini, ao anapima taabu na sikitiko ya Gehena, sawa hule mutajiri ya hadisi ya Mtume Luka. Lakini hii mambo, haitoke namna, kama Mungu anataka, kwa ajili ya maombi yetu, amupatie kwa hule mwenye kulala (mufu) rehema, kwa sababu bado kufanyika Hukumu wa mwisho ya Kuja yake wa Mbili.

**3)** Neno ingine kwa ajili yake Wahuhuda wa Yehova wanakataa Makumbusho ni fundisho yao ya kama tusihukumwa juu ya matendo hile tulifanya pa hii maisha yetu, lakini tutafanya matendo gani kwa ufalme wa miaka elfu (1000) ile itakuja ku mbele, katika imani yao. Na hile wakati ya Ufalme wa miaka 1000 Yehova, wanasema, atatufundisha ma sheria mapya ku vitabu mapya na ingine ya Kitabu ya Madiko Takatifu.

Kwa sababu, basi, wanasadiki ya kama, kisha lufu yao, hawatahukumiwa katika matendo ya uzima yao wa hii inchi, ni teketeke kusikia sisi juu ya nini wanakata ma sali na maombi yetu yote ya pumuziko na rahati ya wenye kufa.

**4)** Sababu kubwa kwa ajili yake Washuhuda wa Yehova wanakataa Makumbusho ya Kanisa yetu ni neno ya kama hawa wanakataa ya kama nafsi itabaki kwa milele. Ni kweli, kama nafsi haiishi kisha lufu, kwa hivi kila sala kwa saidio ya wenye kufa ni kwa bure. Lakini nafsi inabaki kwa milele kwa hivyo na Makumbusho yas Kanisa yetu yanachunga stahili yao na fasi yao sawa onyesho ya mapendo na saidio mbele ya wenye kufa ndugu wetu.

# 18

## JUU YA NVITA

Washuhuda wa Yehova wanatuchukia na wanatushitaki tena, kwa sababu tunachukua ma bunduki na tunaenda tufanye nvita lakini amri ya Mungu inasema: «Usiue». Hii shitaki isiyo na haki. Isiyo na haki kwa sababu hatupende sisi wa kwanza kufanya nvita. Sisi wa Orthodoksi

hatufanye nvita ya kuiba vipande ya inchi ya mataifa ingine. Ma nvita yetu yalikuwa daima paka ya kuchunga ma inchi na mali na ma jamaa yetu. Tena shitaki yao ni kibaya kwa sababu na hawa Washuhuda wa Yehova, kama ni lazima, wanakimbilia kwa nyumba ya hukumu na kwa nyumba ya ma jemadari, nikusema mamlaka wa inchi, «hile inavaa kisu» (wa Roma 13, 4) na wanaomba haki yao. Lakini, kama walikuwa wenye kweli katika imani yao, ilipashwa kukataa saidio ya mamlaka ya serkali na waliongojea uhaki yao katika miujiza ya Yehova (sawa vile, hivi wanasema kufanya sisi, kama tukona ma jabo umoja).

Hii mambo inapata yeyuko yake kama tutafanya hii uchanisho: Kitu ingine ni uuaji upekee, inayekuwa katika akili na tamaa ao kisasi na kitu ingine ni uuaji isiyo upekee inayekuwa mu wakati ya nvita. Hata akili moa, hata uhaki moja haiweze kushariki na kuweka pa mustari kimoja uuaji upekee na uuaji isiyo upekee. Amri ya Mungu ya Agano la Kale inatuonyesha uuaji upekee; huu uuaji inakatazwa kabisa toka Mungu na ni zambi munene wa lufu. Kupindua, uuaji mu wakati ya nvita ni isiyo upekee, hainyoloke kwa uso na mutu moja upekee na inatokeas inje ya inchi yetu, kwani sisi wa Orthodoksi tunachunga inchi yetu na hatufanye nvita ya kunyanganya ma inchi ya wageni. Kama ni jukumu moja, hii yanaileta wakubwa wetu, mamlaka ya serkali, iliyeweka pa vichwa yetu Mungu na sisi mbele yake tunapashwa utii, kama wanatembea na wanatumika katika sheria ya Mungu. (wa Roma 13, 17).

Hii ushanisho ya uuaji wa mbili inatuonyesha na Madiko Takatifu na kabisa mu uzima ya wa Israeli: Kwa mufano, Mungu anahamuru «usiue», mara moja anabariki ma nvita ya taifa yake na anawapatia saidio na shauriaYake. Kana hii tendo ya Mungu itahukumwa katika akili ya Washuhuda wa Yehova, ilikuwa namna kusadiki sisi ya kama Mungu anasema wakati ingine sauti ya wongo na wakati ingine sauti ya kweli. Lakini akili ya Mungu inaachana ya akili ya watu na kabisa ya Washuhuda wa Yehova, kwa hivyo Mungu hasiweke uuaji upekee na uuaji isiyo upekee pa mustari kimoja.

Mifano toka Madiko Takatifu iko lazima ya kuandika kwa kuona ufananisho ya hii fundisho:

1) **«Na mutafukuza adui zenu, nao wataanguka mbele yenu kwa upanga.. . », anasmea Mungu kwa Watu wa Israeli (Walawi 26, 7).**
2) **Mungu anahamuru Nabii Musa ahesabu wanaume wote wenye wanaweza wafanye nvita (Hesabu 1, 1-46).**
3) **Mungu anahamuru Munsa na wa Israeli wafanye nvita na kuua taifa wa Midiani. (Hesabu 31, 1-10).**
4) **Musa anashauria watu wa Israeli ya kabila Gadi na Ruvimi kwa kutembea na silaha yao mbele ya Bwana kwa nvita. (Hesabu 32, 20-32).**
5) **Mungu anahamuru watu wa Israeli ya kuua wanaume wote ya muji moja, kwani unakataa kujitoa na amani kwa mikono yao. ((Kumbukumbu la Torati 20, 13).**
6) **Ma bunduki wa nvita ya Daudi sawa: mikuki, na ngabo, na vigabo, vilivyokuwa vya mufalme Daudi, vilivyokuwa katika nyumba ya Mungu» (2 Mambo ya siku 23, 9).**

7) Watu wa Israeli, kisha kwa kurudia toka utumwa ya muji Babeli walijenga mara ingine muji Yerusalema mukukombana ma siku zote kupinganaya adui yao, lakini mkubwa yao Neyemie aliwamabia: «Musiwaogopeni; mukumbukeni Bwana, mkubwa na mwenyezi na mukombaneni juu ya ndugu wenu, wana wenu na wa binti wenu na wa bibi wenu na ma nyumba wenu. (Nehemia 4, 14-18). Vile na sisi Wa Orthodoksi tunasema, wakati tunakombana kwa imani na inchi na jamaa yetu.

**8)** Nabii Daudi anasema: Mungu anafundisha mikono yangu kupiga nvita» (Zaburi 18, 34).

**9)** Mungu analaka kulipiza mataifa walikombana na waliwabamba wa Israeli na anasema kwao (watu wa Israeli): **«Tangazeni maneno haya katikati ya mataifa; tengenezeni vita; amsheni watu hodari; watu wote wa vita wakaribie, wapande. Fueni majembe yenu kuwa**

**panga, na miundu yenu kuwa mikuki, muzaifu aseme: mwenye nguvu mimi» (Yoeli 3, 9-10).**

**10)** Tena ni na maaji ya pekee, yenye yalifanya watu wa Mungu kwa maneno ya imani, kwa hivyo Mungu hasiwahukumu, . Kwa mufano:

a) **Nabii Musa anaua hule mutu mwenye Misri, aliyepiga mtu moja wa Ebrania (Kutoka 2, 11-12).**

b) **Mukubwa Finehasi alipata baraka ya Mungu mukuua mutu moja wa Ebrania, mwenye zambi aliyefanya zambi ya usharati pamoja na mwanamuke moja (Hesabu 25, 6-16).**

c) **Nabii Elia «alichinja» na mukono umoja yake 450 ma nabii wa uwongo ya mungu Baali. (I Wafalme 18, 40).**

**11)** Lakini na mu Agano Jipya tunaona ya kama wakubwa wa askari walimukaribia Kristu ao Yoano Mutangulizi ao Mitume, lakini hawa hawakuwaambie kuacha hii kazi yao. Kwa mufano:

a) **Yoano Mutangulizi aliwashauria hivi wakubwa ya waaskari: «Musifanye jeuri, hata kwa mutu mumoja; musishitaki mwingine kwa uwongo; tena mufurahi na mishahara yenu» (Luka 3, 14).**

b) **Kristu anamutukuza Akida ya Kapernaumu mukusema: «Sikukuta imani kubwa namna hii, hata katika Israeli» (Matayo 8, 10).**

c) **Akida Kornilio anatukuzwa sawa «Mwenye kuabudu na kuogopa Mungu pamoja na nyumba yake yote, aliyewapa watu sadaka nyingi, na kuomba Mungu siku zote» (Matendo 10, 2).**

Katika maneno haya yetu sisi tusipende nvita. Hakuna namna! Nvita ni kitu kibaya kabisa ma siku zote. Kwa hivyo kanisa yetu inaomba kwa ajili ya amani ya ulimwengu muzima». Lakini, wakati ma taifa nyingine wanatupiga na sisi inalazimishwa kuchukua ma silaha yetu juu ya kuchunga inchi yetu, imani na jamaa yetu.

Basi, Washuhuda wa Yehova, kama wanataka kuwa watu wa kweli mbele ya masauti yao, walipashwa kuhukumu na taifa ya Waisraeli wa zamani, wenye walikombana na mapendo kimungu na Mungu aliwabariki ao aliwashauria kukombana ma adui wao, waliyofuata imani ingine.

Lakini, sisi wakristiani wa Orthodoksi, kupindua na ma sauti ya Washuhuda wa yehova, tunatakia ma fasi yote na waakti yote amani ya ulimwengu muzima. Tunasema kupindua na ma sauti ya Washuhuda wa yehova, kwani wale wanafurahi kama inakuwa nvita na wanakataa kuomba kwa Mungu juu ya amani ya ulimwengu. Wanafurahi, kwani katika hii nvita, mataifa, wenye si weko Washuhuda wa Yehova, wanarabika hawa wenyewe. Na, kama watafanya sala kwa Mungu na Mungu atawasikia, itakuwa hatari juu ya kupotesha hii zawadi kubwa: (nikusema kwa kufa wale watu hawapende kufuata Kundi yao).

# 19

## UBADILISHO YA MADIKO TAKATIFU KU WASHUHUDA WA YEHOVA

Sawa vile inafamiwa, Washuhuda wa Yehova waliandika na walikabula Madiko yao Takatifu, inayeitwa: «Ufasiri ya Dunia Mupya». Pa hii mafundisho yetu tukona mafaa kujua ufasiri hile walifanya mu Agano Jipya, kwa sababu walibadilisha ma fasi mengi ya hii Kitabu, kupita ya ma dini yote tangu mwanzo ya Dini wa Kristu mpaka sasa.

Hii ufasiri ya kitabu yao «Agano Jipya» waliandika ya kwanza mu lugha ya kiingereza na kisha waliifasiri hii kitabu na ma lugha ingine. Juu ya kuandiuka hii Kitabu mu lugha kigreki, hawakuchukua Kitabu wa Kwanza ya Agano Jipya, lakini walifanya ufasiri yao ingine na mafasiri wageni yetu.

Sasa tutaandika mifano madogo juu ya kuona na kushangaa kila musomaji kibego gani walifanya kwa ufasiri yao mu Kitabu ya Agano Jipya.

**1)** Pa fasi mengi ya Agano jipya neno ya «Bwana» waliikombola na neno: «Yehova». Lakini, bahati yao mubaya, kwa sababu ma shairi mengi pahali anaandikwa jina ya Kristu na hapana jina ya Mungu-Baba, hawa wanaweka jina paka Yehova. Kwa mufano, unabii ya Yoeli, iko na andika na Mtume Paulo: «Kwa sababu kila mutu anayeita jina la Bwana ataokolewa» (wa Roma 10, 13); unapata utimizi yake hii unabii kwa uso ya Kristu, sawa vile tulisema mu Sehemu wa 4. Kwa hivi, bila kusikia ma kosa yao wanachanga maana ya hii Kitabu na manabii.

**2)** Pa kila fasi ni neno: «musalaba» waliandika neno: «muti ya mateso» ao «fimbo ya mateso», lakini pa neno «kusulibia» waliikombola na neno: «Kutundika pa muti».

**3)** Pa hile fasi ni neno: «milele», kwa mufano, milele wa sasa, ao milele uliyekuja, ao mamilele (matayo 12, 32. 24, 3 na 28, 20). na Waebrania 1, 2 na pa fasi ingine waliikombola na jina: «matengenezo ya vitu: «huu tengenezo ya vitu= (milele wa sasa).

**4)** Mustari hii: «gehena (azabu) ya milele (Matayo 25, 46) waliikombola na mustari: «kwa kukata wa milele» juu ya kupatana na imani yao, kwani wanasadiki ya kama hakuna gehena na malipizo.

**5)** Pa hile fasi Kristu anaitwa «Mukubwa ya uzima» (Matendo 3, 15), ao «Mkubwa ya wokovu» (Wa Ebrania 2, 10) ao paka: «Mkubwa» Wa Matendo 5, 31) waliikombola na neno: musaidizi wa kwanza ya uzima na hivi wanashusha hali na tendo ya Kristu sawa Mwokozi ya dunia na Mungu wa kweli.

**6)** Pa hile fasi inaandikwa ya kama Mwana wa Mungu aliumba vitu vyote» (hii mambo inaonyesha ya kama Huyu hana kiumbe), sawa kwa mufano kwa (Wa Kolosayi 1, 16) hawa waliongeza na neno: «na vitu vingine, juu ya kupatana katika imani yao, ya kama Mungu Baba aliumba ya kwanza Mwana wake na kisha katika Yake na vitu vingine vyote.

**7)** Pa hile fasi inaandikwa sauti ya Mungu Baba kwa Mwana wake**: «Wewe ndiwe mwana wangu, siku hii ya leo nimekuzaa» (matendo 13, 33**) na ( Wa Ebrania 1, 5. 5, 5) inayeonyesha uzalio isiyomwanzo na isiyowakati ya Mwana toka asili ya Mungu Baba na hivi inaonyeshwa asili moja la Mungu Baba na Mwana wake, hawa waligeuza na pa hii fasi waliandika: «Mimi leo nimekuwa baba yako», na hii mustari hivi haionyesha ya kama Yesu alikuwa Mwana wake toka asili yake. Kwa hivyo, wanataka kukataa asili moja la Baba, la Mwana na ya Roho Mutakaitfu na hivi wanakataa hali kimungu ya Kristu.

**8)** Mustari hii: «Hosana kwa Mwana wa Daudi; mubarikiwa yeye anayekuja kwa jina la Bwana; hosana juu mbinguni» (Matayo 21, 9), nikusema utukufu kwa mufwasi ya Daudi (Mwokozi) wanaibadilisha kabisa na wanafasiri hivi: **«Ee (Yehova) okoa, tunakuomba Mwana**

**wa Daudi; mubarikiwa ni yeye anayekuja kwa jina ya Yehova; tunakuomba umuokoe, pale juu mbinguni». Hivi Kristu Mwokozi wa dunia anaonekana sawa mutu wa bure, anayelazimishwa amuokoe Yehova.**

**9)** Pa hile fasi ni neno: «Rabi», nikusema Bwana inaandikwa juu ya Mungu Baba, Washuhuda wa Yehova wanaifasiri kweli: «Bwana mukubwa» (Luka 2, 29. Matendo 4, 24. Ufunuo 6, 10). Lakini pa hii fasi inaandikwa neno: «Rabi» juu ya Kristu (kwa mufano mu barua ya mbili ya Petro 2, 1 na Yuda 4) wanaikombola na neno.. .. «mwenye kuchunga» na hii neno wanaitimia na kwa wa «rabi» wa inchi. Kwa mufano mu barua ya Timotheo 6, 1. barua ya mbili ya Timotheo 2, 21. Tito 2, 9. barua ya kwanza ya Petro 2, 18) na hivi wanashusha Kristu mu daraja ya viumbe vya dunia.

**10)** Pahali inaandikwa neno ya: «Roho Mutakatifu» wanaandika na ma heruvu madogo, hivi: «roho mutakatifu» juu ya kushusha hali kimungu yake na hivi kukataa Uso kimungu Yake. Kwa mufano: Matayo 12, 31-32. 28, 19. Yoano 14, 26. Matendo 13, 2. 20, 28). Kupindua, juu ya neno: «diabolo» na «shetani» wanaoandika na herufu munene, nikusema: Diabolo, Shetani!!!

**11)** Pahali ni neno: «kuwachangulia» (Matendo 14, 23. Tito 1, 5), inayeandikwa juu ya Upadirisho ya wapadri na wa askofu na wa shemasi Washuhuda wa Yehova wanaikombola hii neno na hii: «kuhamuru» na hivi wanashusha Fumbo ya upadirisho sawa kwa kuchangua mutu moha wa bule.

Mifano haya, tunazania ni ya kuenea juu ya kujua kila musomaji wanaeshimiwa ngapi Washuhuda ya Yehova Madiko Takatifu. Tuliandika miafani madogo kwa ubadilisho yao na hapana mabadilisho yote, kwani ilipashwa kuandika kitabu moja muzima.

Washuda wa Yehova ni kweli ya kama wanaandika kitabu ingine ya Habari Njema (Evangelio) ya hile sisi tulichukua toka Kanisa ya Kristu tangu milele wa kwanza. Kwani ni matata sauti ya Mutume Paulo, mwenye anasema ma sauti haya juu yao: «Lakini sisi, ama malaika ya mbinguni, tukiwahubiri ninyi Habari Njema ya mbalimbali na ile tuliyowahubiri ninyi, alaaniwe. Kama tulivyosema kwanza, sasa tena ninasema mara ya pili. Mutu ye yote akiwahubiri ninyi Habari Njema ya mbalimbali na ile muliyopokea, alaaniwe» (wa Galatia 1, 8-9).

## MONASTERI YA MUTAKATIFU GRIGORIO
## KILIMA TAKATIFU
## GREKIA (HELLAS)
## 2000

**Τό παρόν βιβλίο: <’Ορθοδοξία καί Μάρτυρες το□ ’Ιεχωβ@> το□ Αρχιμ. tερομονάχου π. Σωφρονίου Μιχαηλίδου, ‘Ι. Μητροπόλεως Κιτίου Κύπρου 1997, μεταφράσθηκε τόν ’Ιούλιο το□ Vτους 2000 στήν Αφρικανική γλ™σσα σουαχίλι γιά τόν Αντιαιρετικό Αγ™να τ™ν Αφρικαν™ν Κληρικ™ν τ\ς ’Ορθοδόξου ’Εκκλησίας το□ Κογκό, κατόπιν Tπιμόνου Tπιθυμίας τ™ν sδίων.**

**Γνωρίζω …τι □πάρχουν παντός ευδους λάθη στήν μετάφρασι, Αλλά ζητ™ τήν Tπιείκια τ™ν κογκολλέζων ’Αδελφ™ν. ’Επιθυμία μου εyναι νά μεταφέρω, …σον εyναι δυνατόν, □ρθά τά νοήματα καί μελλοντικά οt uδιοι θά προβο□ν στήν διόρθωσι τ™ν λαθ™ν καί τήν σωστή Αποκατάστσι το□ κειμένου.**

**‘Ο μεταφραστής Tλάχιστος μοναχός Δαμασκηνός Γρηγοριάτης.**